# WATOTO KWA KRISTU

## KITABU YA KWANZA KU MASOMO YA KANISA

## (JUU YA WATOTO KU MASOMO YA MBILI (SECONTAIR)
## MUSTARI YA MBILI

**CENTRE MISSION ORTHODOXE**
**KOLWEZI KONGO**
**1998**

# YALIYOMO

FUNDISHO YA KWANZA
MUTAKATIFU MUSHAHINDI DIMITRIOS. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .3
FUNDISHO YA MBILI
KUUMBA YA MUTU (Mwanzo 1, 26-28 na 2, 7). . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 7
FUNDISHO YA TATU
KAINA NA ABELI. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .11
FUNDISHO YA INE
MUFANO YA MUPANDAJI MBEGU. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .15
FUNDISHO YA TANO
EFTIHOS. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .. 18
FUNDISHO YA SITA
SAMWELI NABII NA MWAMUZI. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .22
FUNDISHO YA SABA
MTAKATIFU YOANE MURAHIMU. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .26
FUNDISHO YA MNANE
MUTAKATIFU EKATERINI. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .30
FUNDISHO YA TISA
MUTAKATIFU SPIRIDON. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .35
FUNDISHO YA KUMI
MUTAKATIFU ELEFTHERIOS. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .38
FUNDISHO KUMI NA MOJA
NDANI YA SADUKU MOJA YA KULISHA NYAMA. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .40
FUNDISHO KUMI NA MBILI
MUTAKATIFU YOANE MUTANGULIZI. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .44
FUNDISHO KUMI NA TATU
YESU KRISTU ANATEMBELEA ZAKAYO MU NYUMBA YAKE. . . . . . . . . . . . . . . . . . 49.
FUNDISHO KUMI NA INE
WA MITUME YA WILI. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .52
FUNDISHO KUMI NA TANO
MWIVI AHARI. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .57
FUNDISHO KUMI NA SITA
ANANIAS NA SAFIRA. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 61
FUNDISHO KUMI NA SABA
WASHAHINDI WATAKATIFU MAKUMI INE. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .64
FUNDISHO KUMI NA MNANE
MUFANO YA MWANA MUPOTEVU. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 68
FUNDISHO KUMI NA TISA
MUTAKATIFU TIMOTHEO. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 73
FUNDISHO MAKUMI MBILI
MUSHAHINDI YA KWANZA STEFANO. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 76
FUNDISHO MAKUMI MBILI YA MOJA
WATOTO YA SABA WENYE WANAITWA MAKAVEI. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .80
FUNDISHO MAKUMI MBILI NA MBILI
MUTAKATIFU FILOTHEI. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 84
FUNDISHO MAKUMI MBILI NA TATU

ALAMA YA WAKRISTIANI. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .87
FUNDISHO MAKUMI MBILI NA INE
WIMBO AKATHISTE. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 92
FUNDISHO MAKUMI MBILI NA TANO
MEZA UKUBWA NA TAKATIFU. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .95
FUNDISHO MAKUMI MBILI NA SITA
YESU KRISTU ALITESWA KWA SISI. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .100
FUNDISHO MAKUMI MBILI NA SABA
MWENDO KU MUKINI EMAU. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 104

# FUNDISHO YA KWANZA
# MUTAKATIFU MUSHAHINDI DIMITRIOS

Wafu wako, ee Watoto, ku hii Masomo yetu. Kisha wakati ya pumuziko tulifika hapa mara ingine. Masomo ya Inchi yetu ilianza mara ingine. Lakini na Masomo yetu inapaswa kuanza mafundisho yetu. Hii ni Masomo ya zamani kabisa. Masomo yetu ikona urefu Historia.

Watoto ngapi mulikuja leo? Iko muzuri sasa kubalula mweye. Tuko makumi (fulani)? Ni kweli ya kama ku masomo yenu ya Inchi yetu muko watoto wa mingi kupita. Watoto, wenye wanaikala karibu yenu ku masomo yenu, leo abakukuje hapa. Mara ingine watakuja mu Juma itayefika. Mara ingine watalofa pamoja na wazazi ao wanduku wao. Ao, abajue kintu ninyi iko Masomo ya Kanisa yetu.

Na mweye na wale, watakuja juma ingine, wote mutaoana ya kama hapa ku hii masomo yetu tunasikia Mashindano wazuri ya roho na tunafunda na sisi namna gani tutakombana kufata na kufanya moja uzima takatifu. Leo mutasikia moja mashindano nguvu. Ilifanyikwa ku muji ya Grece iliyeitwa Thessaloniki.

HISTORIA. Muji Thesaloniki ikona bintu ya muzuri wa mingi. Mukubwa na muzuri ni Kanisa ya Mtakatifu Dimitrios, mwenye ni mulinzi yake.

Kila mwaka ku tarehe 26 mwezi ya Kumi ndani ya hii muji inafanyikwa mashangilio na Siku Kuu ukubwa kwa makumbusho ya yule Mtakatifu. Juu ya ninyi? Kwa sababu huyu Mtakatifu alizaliwa mu Thessaloniki na amefanya miujiza wa mingi ku muji yake.

Moja ukubwa muujiza katikati ya ingine ni, ya kama hii siku ya makumbusho yake ku mwaka 1912 aliuhuru muji na njimbo yake toka utumwa ya waTurki. Wa askari wagreki waliingia ndani ya hii muji, iliyekuwa utumuwa miaka 500 kwa waTurki. Nani alifanya hii muujiza kuuhuru hii muji? Nani mwingine, paka Mt. Dimitrios.

Lakini ni nani huyu Mutakatifu? Moja mushindani nguvu. Aliishi ku miaka ya zamani, ile wakati Thessaloniki ilikuwa utumwa kwa unguvu ya wafalme ya Roma. Nikusema, aliishi ku mwaka 300, kisha ya kuzaliwa Bwana Yesu Kristu.

Alizaliwa ku hii muji na alionyesha ya kipimo kuliko yake ya kama atafanyika moja mukubwa mushindani. Alikuwa na mwili nguvu na roho kujaza na nguvu ya Mungu. Watu wote walimutukuza juu ya ma zawandi wake.

Wakati tena alikuwa kijana na alikomea ndani ya Kanisa ya Kristu, alienda na mu Kundi ya wa askari. Hasikupitishe mingi wakati na wakubwa yake walisikia ya kama yeye alikuwa moja askari kuliko mukubwa ya beingine. Alienda ya kwanza ku kila nvita na matendo yake walikuwa ya utukufu. Mfalme ya Roma, kwa sababu aliona ma zawandi wake mu kazi yake kama askari, alimupatia cheo ya yulu. Alimuweka mukubwa ya muji Thessaloniki na yote njimbo pembeni yake.

Alikuwa kijana, lakini mustahili mu kazi yake kama mukubwa ya moja munene muji. Na sisi tunamuajaabu, hapana paka juu ya cheo na nguvu yake, lakini kuliko tunamuajaabu juu ya moja kintu ingine. Yeye alikuwa mwalimu ya mafundisho ya Kristu.

Namna gani moja mukubwa ya wa askari alikuwa na mwalimu ya Masomo ya Kanisa yetu? Watoto wangu, sasa mukujeni na pasopo ya akili yenu juu ya kusikia huyu Mt. Dimitrios alifanya ninyi kila siku ku muji yake Thessaloniki.

Dimitrios yulu ya kila zawandi alikuwa mukristu ile wakati wafalme ya Roma walikuwa Dioklitianos na Maksiminos, wenye walifukuza sana waKristiani wetu. Ma elfu wa mingi

walimwanga ma damu yao juu ya kuchunga Jina ya Kristu. Na wale wafalme walizania ya kama na hii mafukozo wao watazimisha imani ya Kristu. Lakini habakujue ya kama ile wakati walifukuza wakristiani, beingine waKristiani walipanda ma cheo ya yulu kabisa ndani ya ufalme yao. Habakujue ya kama mukubwa jemadari ya muji Thesaloniki alikuwa mukristu.

Mukristu Dimitrios, wakati aliisha kazi yake kama mukubwa kila siku, alitosha manguo ya cheo yake na alivaa ingine manguo wapole. Aliziuguluka muji yake na alitafuta watu, wenye walipenda kusikia fundisho ya Mungu. Kazi yake ya kila siku ilikuwa hii: Kusaidia kila siku hata mutu moja kufata imani ya Kristu. Asikupate kimya na asikulale, kama kila siku asikupeleke moja mutu mu Kanisa ya Kristu.

Na neema ya Mungu aliweza kufanya muzuri hii kazi yake. Alipenda kabisa watoto na wakijana. Moja picha (Ikona) yake, iliyeokolewa na iko ndani ya Kanisa yake mu Thesaloniki inaonekana Mt. Dimitrios na pembeni yake watoto wa mbili. Hii Ikona inatuonyesha sana hii kazi alifanya Mt. Dimitrios kama mwalimu ya mafundisho ya Mungu.

Na mapendo ngapi alifundisha Dimitriios wale watoto kwa Kristu! Aliikala

kwa siri ndani ya katakombe ma saa wa mingi kila busiku na alisuburia

mafundisho ya Kristu. Alifundisha watoto na nguvu, na imani na mapendo. Na

kila siku alisaidia kufata imani ya Kristu, hapana paka moja, lakini wa

mingi watoto. Matakio yake ilikuwa ndani ya muji yake watu wote kumuamini Kristu

Lakini hii tendo ya Kristu, hakuna namna kubakia kwa siri, watoto wangu. Kisha wakati kiloko walisikia wakubwa ya Roma ya kama jemadari Dimitrios ni mukristu. Lakini nani atamuhukumu? Ilipaswa kukuja mumoja mfalme ya Roma. Na wakati moja alikuja mfalme mu Thessaloniki. Aliita Dimitrios na alimwambia:

Ee Dimitrie, miye milikusifu na hii cheo yako ukubwa. Milikufanyisia jemadari, kwa sababu milistaajabu ma fazila yako na ma zawandi yako. Basi, ni kweli, ya kama ulikanyanga hii sifa yangu na unahabudu Kristu?

Ee Mfalme, alimujibu Dimitrios, minakushukuru ya hii sifa yako.

Minakupenda na minakusifu. Na milionyesha hii mapendo na sifa yangu ku kila nvita, pahali milikombana juu ya sifa yako. Lakini inapaswa kujua, ee mfalme wangu, ya kama yulu yako ni moja mwingine mfalme. Huyu minamupenda na minamusifu kuliko ya weye. Na huyu mfalme ni Mungu.

Na miye minasandiki kwa wamungu, ee Dimitrie. Kwa wale wa mungu wangu inapaswa kusandiki na weye, sawa vile wanafanye na weingine wakubwa jemadari wangu. . .

Hapana, mfalme wangu, hawa wa mungu, unahabudu weye ni wa wongo. Miye minasandiki kwa Mungu Yesu Kristu, mwenye ni ukweli Mungu.

Ee Dimitrie, hauwaze muzuri, kwa sababu utapotesha yote ma cheo na utukufu yako na utalipizwa sana.

Misiogope, ee mfalme. Niko tayari kuvumilia kila mateso kwa Kristu wangu. Fanya kila kazi unawaza.

Mfalme alishirika kwa ile ma jibu ya Dimitrios mukristu. Mara moja anahamuru kumukamata na kumutupa mu buloko. Jemadari Dimitrios sasa anatowa kwa mikono ya wa askari wake. Na wale walimukamata, walimutosha manguo ya cheo yake na kama mutu munyanganyi walimuongoza mu buloko ya muji yake Thessaloniki.

Dimitrios mu buloko. Lakini hana paka huyu mumoja. Pamoja na yeye ni Bwana wake, Yesu Kristu, anayemupenda na yote nguvu ya roho kijana yake.

Moja busiku ilionekana moja nuru kuliko nguvu ya hii nuru ya dunia, iliyeangaza chumba yake. Moja Malaika na mabawa mweupe alikuja na moja taji ku mukono yake. Alikuja na aliweka hii taji pa kichwa ya Mushindani. Ngapi nguvu alimupatia hii matembeleo ya Malaika!

Kisha ma siku wadogo Dimitrios alipokelea na moja ingine matembeleo.

Hii mara huyu Dimitrios alipatia nguvu kwa moja mutu mwingine.

Moja asubui aliona Dimitrios kukuja moja mwanafunji yake, moja mtoto ya Masomo ya Kanisa yake. Alikuwa Nestoras.

Namna gani ulikuja hapa, ee Nestora? Alimuuliza mwalimu yake Dimitrios.

Ee Mwalimu wangu, milikuja kubeba baraka yako. Mitaenda kukombana.

Na mutu nani?

Inje mu kiwanja iko makelele mingi. Waliisha kusanyika watu wa mingi na mfalme. Katikati ya hii kiwanja ni moja mutu munene, aliyemuletea mfalme. Yeye aliitwa Lieos. Yeye ni murefu na ekona nguvu kabisa. Anataka kukombana na moja mutu mwingine. Miliwaza ya kama inapaswa kukombana na yeye mimi, mwalimu wangu. Mimi niko mutu mudogo, lakini nikona karibu yangu Yesu Kristu, mwenye eko kupita nguvu ya Lieos na ya kila ma nguvu ya hii dunia. Minataka kukombana na Lieos, kumushinda juu ya kutukuzwa Mungu wetu. Basi, unipe baraka yako. . .

Mtoto wangu, Nestora, alimujibu Dimitrios, « Utamushinda Lieos na utakufa kwa jina ya Mungu». Uende na baraka ya Mungu.

Ndani ya kiwanja watu wote walilalamika hivi: Li-eos, Li-eos, Li-eos!

Hii ma sauti ya watu walisikia watu wote na muji na wa askari ya

kiwanja. Na huyu Lieos alitembea na majivuno na aliongolea nani atakuja kukombana na ye. Yeye alitukuza nguvu yake. Nani, basi, atapata nguvu kukombana na huyu mukubwa askari? Ilipaswa mbele kukufa na kisha atakamata mupango kukombana na yeye.

Kisha saa kiloko ndani ya hii kiwanja ilisikiwa moja sauti: Ee Lieos, milikuja kukombana na weye.

Alipindula Lieos na watu wote na mfalme na waliona kukaribia moja mutu mufupi mukijana. Alikuwa Nestoras. Aliisha kukamata mupango kukombana na Lieos.

Lakini, weye, mtoto wangu, alimwambia mfalme, weye utakombana na huyu mukubwa na mwenye nguvu askari? Juu ya ninyi unataka kufa? Haupende kuishi wakati ingine?

Hapana, minataka kukombana na huyu, kwa sababu minasandiki ya kama mitamushinda. . . .

Ha, ha, ha, . . . alicheka na udanganyifu Lieos. Huyu atanishinda!

Lakini mbele ya mupango ya Nestoras mbukomvi katikati yao ilianza. Watu wote, wenye waliona hii mbukomvi walikamata pumuzi yao. Moja mtoto kijana atakombana na moja mukubwa askari. Asitaweze kumushinda. Habakujue watu ya sanamu ya kama na moja wakati ingine zamani na moja mwingine kijana, aliyeitwa Daudi alishinda mukubwa askari Goliathi.

Saa ya mbukomvi ilifika. Mtoto Nestoras alifanya alama ya musalaba na midomo yake alisema moja sala na haraka: « Ee Mungu ya Dimitrios, unisaidie». Na wakati alifanya hii sala alikuja kontre ya Lieos. Watu wote waliongolea kuona Nestora kuanguka mufu chini.

Lakini wanaona ninyi? Chini ya mbulongo alianguka mukubwa Lieos. Lieos?

Ndivyo! Nestoras alipanda yulu yake na moja kisu kiloko yake alimupika na alimuacha mufu chini.

Lieos mufu! Nestoras mushindi! Watu wote walishangaa. Mfalme aliuliza roho yake: Namna gani ilifanyikwa hii haya ya Lieos? Watu beingine walimwambia ya kama Nestoras wakati alianza kumupika Lieos alimuomba kwa Mungu ya Dimitrios mwalimu yake. Aliomba saidio ya Mungu ukweli yake.

Basi, mukosefu ni Dimitrios! Nestoras ni na huyu mukristu na mwanafunji ya Dimitrios. Bila kuchelewa alitosha moja mupya hamuri yake. Wa askari ya Roma waliingia ndani ya kiwanja na walimukamata Nestoras na walikata kichwa yake.

Sasa inakuja na mustari ya mwalimu yake. Dimitrios ndani ya buloko yake anapokelea matembeleo ya wakubwa wa askari ya mfalme. Na ma mukuki wao walipingilia mwili yake. Damu inatoka na inatelemuka mingi. Kisha ma dakina wadogo lufu inaleta mwisho ku uzima ya Dimitrios, moja uzima kujaza na mapendo ya Mungu na ya watu. Sasa Dimitrios na Nestoras, mwanafunji na mwalimu weko pamoja mbinguni.

Kanisa yetu inakumbuka makumbusho yao: Ya Mt. Dimitrios mu tarehe 26 mwezi ya Kuma na Nestoras mu tarehe 27 ya hii umoja mwezi. MAELEZEO. Ulizo: Minasandiki ya kama muliangalia hii mbukomvi nguvu toka muji Tsessaloniki. Munaweza kuniambia nani alikuwa matakio ukubwa ya Mt. Dimitrios? Jibu: Kuongoza watu wote ya muji yake kwa Kristu.

Ulizo: Matakio gani aliisha kuweka ku uzima yake?

Jibu: Hasikupitishe hata siku moja, bila kukokota hata moja mutu kwa imani ya Kristu.

Ulizo: Makila mabarikikwa yake fasi ngani aliitupa?

Jibu: Kwa watoto na wakijana. Alipenda kabisa makijana. Ulizo: Mtoto nani yake leo tuliona kwa hii sindano?

Jibu: Nestoras. Yeye alimuamini Kwa Kristu nguvu na alimupenda mpaka kutoa na uzima yake Kwake na tena kumwanga damu yake kwa mapendu ya Kristu. Ulizo: Mt. Dimitrios kila siku alikombana kuleta hata mutu moja kwa Kristu. Sisi tunaweza kufanya ninyi?

Jibu: Kusema na kwa watu weingine juu ya Imani na fundisho ya Kristu.

Ulizo: Nani inapaswa kuwa kazi yetu kila siku kabisa?

Jibu: Kuleta kwa Kristu warafiki, wanafunji na wote watoto kwa imani ya Kristu na Kanisa wetu.

FUNDISHO: Tutatumika kupeleka na weingine watoto ku Masomo yetu. SAUTI YA MAPOKEO TAKATIFU: : Mutu moja kwa Yesu Kristu, Mwana wa Mungu, Mwokozi wetu.

MATENDO KU UZIMA WETU. Hii sauti ya Mapokeo takatifu ikona Historia yake. Iliandikwa ndani ya kibabashi ya Katakombe, ile wakati walifukuza waKristiani wafalme ya Roma. Na, kwani walitaka waKristiani kuishi na kupata nguvu ya Mungu kwa sisi waliandika na alama pa kibabashi ma sauti fulani. Kwa mufanmo walifatula moja samaki na waliandika jina yake kigreki ni IHSOYS. Hii samaki ilikuwa alama ya Yesu Kristu. Kila neno ya hii jina Samaki inatuelezea hivi: Yesu Kristu, Mwana wa Mungu, Mwokozi.

Kila busiku habakuende paka wenye wenyewe mu Katakombe. Waliongoza na watu weingine kwa hii makusanyo ya Kristu. Ni kweli, ya kama hii kazi waliifanya ilikuwa ya hatari. Walicheza na uzima yao, vile tunaweza kusema. Nikusema chini ya kinywa ya imbwa (mfalme ya Roma) walifanya utumwa. Kama waliwakamata, mara moja ilipaswa kuwawua. Na hii mambo ilifanyikwa mara wa mingi. Lakini ni ninyi lufu mbele ya wokovu ya moja nafsi?

Leo hata mutu moja hasifukuzwe. Tuko wauhuru kusema sauti ya Kristu, kufanya Masomo ya Kanisa yetu, kufundisha watu weingine ku imani yetu. Basi, haina muzuri kuzaifu juu ya wa nduku wetu na weingine watoto, wenye abakuje ku hii Masomo yetu. Na hawa weko watoto ya Mungu. Na hawa walimuamini Kristu. Na Kanisa ni juu ya wokovu na kwa hawa watoto. Kama watakuja mara moja, watapata furaha na butamu kwa roho yao, na kisha habatapende kutoka.

Mweye, munasema ninyi, watoto wangu? Mutafanya ninyi hii juma na kila juma kisha? Muniambia beingine ma kazi mutaweza kuifanya:

Kwa mufano: Miye, iko namna kusema moja mtoto, nikona huyu mtoto minaikala naye ku masomo ya Inchi yetu. Juma iliyefika mitafanya nguvu kumuletea ku Masomo ya Kanisa yetu.

Mtoto mwingine: - Nikona moja murafiki. Kama ataisha somo ya ma kitabu yake anakuja kucheza pamoja. Miye mitamwambia kufika ku hii masomo yetu.

Na kama asitakuje?

Ma, juu ya ninyi asitakuje?

Tazama, kwani, iko namna kumwambia ya kama haina lazima kufata watoto hii Kitabu. Ao, hasipende kuingia mu Misa.

Lakini mimi mitakombana kumwambia ya kukuja. Mitamwambia kukuja hata mara moja. Atafanya ninyi? Minawaza, atakuja. Tena mitafanya na sala kwa Mungu juu ya kumuangaza akili yake.

Basi, hata mutoto moja haipaswe kuwa muvuvi na muzaifu. Mungu alimipatia mikulu, lunrimi na roho. Na mikulu juu ya kutembea ma fasi yote. Na lunrimi juu ya kusuburia ma sauti wazuri kwa watu weingine sauti ya Mungu. Na ma roho yenu juu ya kupenda watu weingine. Na hii fazila ya mapendo ni moja zawandi ukubwa, ile mutaweza kuwapatia kwa wa nduku wenu.

Leo tunaanza. Na saidio ya hii Masomo yetu tutafanyika watoto ya Kanisa. Kama iko namna mufanye nguvu musilofe ya hii mafundisho yetu. Mbele tutaenda mu Kanisa na kisha tutafanya na mafundisho yetu.

Mitamilaka na ma zawandi kwa wale watoto wataleta hata moja mtoto mwingine ku hii Masomo yetu? Itafika na wakati na mutabeba na ma zawandi yenu. Lakini kuliko zawandi ukubwa itakuwa hii furaha mutasikia kwa sababu mulileta mtoto moja mu Kanisa na ku Masomo yetu juu ya wokovu ya nafsi yake.

Basi, leo, mbele ya kutoka wote pamoja tutasema mara ingine hii fundisho

yetu ya leo: «Tutaleta na weingine watoto ku hii Masomo yetu»

## FUNDISHO YA MBILI
## KUUMBA YA MUTU (Mwanzo 1, 26-28 na 2, 7)

***NAMNA YA KUKARIBIA***

Watoto wangu, mukona nyumba yenu? Hii ulizo yangu inamishangaa kiloko?

Ni kweli ya kama, sisi hatupende kujua kama hii nyumba munaikala ni yenu ao munaikala ya kuripa makuta fulani. Minamiuliza na moja ingine maana kama mukona nyumba yenu ao hii nyumba ile munaikala ni ugeni. Kila mutu ngapi anasopoka nyumba yake! Na ngapi sikitiko anasikia kama atatoka ya nyumba yake, kwa sababu hakuna makuta ya kuripa!

Tena mitamiuliza na moja mambo ingine ku mwanzo ya hii fundisho yetu leo. Mukona ma Picha (Ikona) mu nyumba yenu? Hakuna namna kuwa nyumba moja ya Kristu bila ma Ikona ya Kristu na ya Watakatifu wetu na kabisa wale watakatifu tukona na ma jina yao.

Iko ma nyumba bila ma Ikona?

Ndivyo, iko beingine ma nyumba, pahali hakuna ma Ikona ndani yao. Ku fasi ya ma Ikona ya Watakatifu wetu wekona bintu beingine pa kibabashi yao.

Lakini leo, watoto wangu, mitamielezea ya kama hakuna hata nyumba moja bila ma Ikona. Ndani ya kila nyumba iko moja ao ma mingi ma Ikona.

HISTORIA. Na hii fundisho yangu ya leo, mitamionyesha watoto wangu, nani eko mufundi mukubwa na nani eko mwenye kufatula mukubwa.

Wakati moja, mwalimu moja aliuliza wanafunji wake: Munajua, watoto wangu, nani alijenga hii nyumba ya Masomo yetu?

Na moja mtoto, bila kuwaza mingi, alisema: - Ee Bwana, hii nyumba ilifanyikwa hii wenyewe. . . Watoto weingine walicheka sana. Walicheka kwa sababu walisikia hii jibu ya nduku wao, iliyekuwa umbafu; joo vile huyu mtoto alikimbia mbio kufuchamwa, kwa sababu alisikia kosa yake.

Ni kweli, watoto, aliwaambia huyu mwalimu, hakuna namna nyumba moja kufanyika hii wenyewe. Kila nyumba ni lazima ya kutegeneza picha. Iko lazima kuangalia hii kazi ya kujenga moja arhitekti na micanishe. Iko lazima kutumia watumishi wamingi. Kila nyumba haina moja buyoka, kuotesha hii wenyewe toka inchi yetu.

Munajua juu ya ninyi milimisema hii yote ma sauti yangu?

Ni moja nyumba munene kabisa na ndani yake iko namna kuingia ma nyumba yetu yote. Hii ni ulimwengu, ile ni pembeni yetu. Hii ulimwengu ni kama moja kanisa bila mupaka na ndani yake inatukuzwa Mungu. Munatupa moja richo yenu ndani ya hii dunia yetu na inchi yetu, pahali bintu ya kuachana weko vizuri sana. Nani alifanya hii nyumba-ulimwengu, inayeitwa na dunia?

Kama atajibu moja mtoto ya kama hii dunia ilifanyikwa hii wenyewe, ni kweli ya kama tutacheka sana. Lakini kama mutu moja mwenye akili atasema hii sauti, hii mambo itakuwa hapana ya kucheka, lakini ya kuria.

Moja nyumba hasikufanyike hii wenyewe. Lakini namna gani hii dunia iko karibu na pembeni yetu itafanyikwa hii wenyewe? Moja nyumba, hata kama iko nguvu, wakati moja, itaharabika na itapomona. Na sisi hatuseme ya kama ilifanyikwa hii wenyewe. Na hii ulimwengu inayeionekona uzima ya miaka wa elfu na wa milione, bila kuharabika, namna gani tutasema ya kama ilifanyikwa hii wenyewe?

Hapana, watoto wangu. Mutume Paulo anatujibu hivi: « Maana kila nyumba imejengwa na mutu; lakini yeye aliyejenga vitu vyote ni Mungu» (WaEbrania 3, 4). Nikusema kila nyumba inajenga mutu moja, na yule alijenga dunia muzima ni mufundi mukubwa, Mungu wetu.

Wakati moja hasikukuwe dunia. Alikuwa paka Mungu. Yeye alitegeneza kuumba ya dunia. Ndani ya akili ya Mungu ni ma picha yote wazuri, sawa vile na ndani ya akili ya shetani ni yoyote ma picha ya uovu na giza. Mungu alitegeneza kuumba ya dunia. Mungu alitegeneza na wokovu ya dunia.

Hakuna kintu moja, ile hasiweze kuitegeneza Mungu.

Mungu ni mufundi. Na ma bintu gani alijenga dunia? Paka na sauti ile wenyezi yake. Munajua namna gani ilifanyikwa? Tutasema moja mufano. Wakati uko ndani ya moja nyumba ya giza, unaenda mbio kutafuta fasi gani ni interrupteur juu ya kuifungula. Na mara moja nyumba inajaza na moto ilectrice. Ngapi teketeke ni kwa sisi kufungula hii interrupteur, na hii teketeke na Mungu anafungula kinywa yake na neno yake anafanya hii kintu anapenda. Kwa mufano alisema: Nuru iwe!

Sawa vile mawingo wanakimbia kwa ajili ya mwangaza ya Jua, vile na ma giza wanaepuka mbele ya hii nuru iliyekuja toka Mungu, mwenye ni Nuru ya milele.

Kila neno ya Mungu ni moja tendo, moja kuumba. Na hii ma neno na ma sauti ya Mungu ilijengwa yoyote viti vizuri inaonekana ya sisi, nikusema inchi yetu, bahari, ma nyota, ma nyama, mayani na yote bintu ya inchi yetu.

Dunia muzima inajaza na miujiza ya kuachana. Musopokeni bintu wa tatu na mutabakia na ma kinywa yenu wazi kwa ajili ya ushangao wenu kwa hekima na fundi ya Mungu.

Kintu ya kwanza ni mawa. Muangalieni moja uwa, ngapi ragi na harufu kizuri na mufano kizuri ikona yo. Wale watu ya wakili wanaweza kufanya hata moja uwa? Hapana. Wanafanya mawa artifice, bila faida. Mawa fisice habakuweze kufanya.

Kintu ya mbili ni ma ndeke. Mubebe moja mudogo ndeke. Ni mudogo, lakini inaimba muzuri. Namna gani ndani ya sigo yake alifuchama hii corde. Na nani alimufundisha kutenge na fundi musique hii ma corde yake? Anaweza technocratie yetu kufanya moja ndeke mudogo? Hapana!

Na kintu ingine ni ma nyota. Ma nyota wa mingi wanatengwa mu mbingu na kilometre wa mingi. Lakini moja nyota hasipike ingine, na kila moja inafata mustari ya kiviringo yake ku mwendo yake na sisi watu tunashangaa sana. Moja mukono ya moja mukubwa Mufundi alitegeneza ma mwendo wao na hasikupike moja ingine. Hii mukono ni mukono ya Mungu.

Mungu aliumba bintu bote vema sana. Tena kupita wazuri weko ma sheria ya hii ulimwengu. Mara ingine mutaniuliza: Juu ya ninyi aliumba hii yote bintu Mungu?

Tazama, moja nyumba juu ya ninyi tanaijenga? Juu ya kuikala ndani mutu moja. Moja motoka juu ya ninyi inatembea? Juu ya kupeleka watu mu kazi yao. Juu ya ninyi tunafanya moja nyumba kiloko ya ndeke? Juu ya kuishi ndani moja ndeke mudogo.

Hii nyumba kizuri, inayeitwa ulimwengu aliijenga Mungu juu ya kuikala moja ndeke mwenye mbingu. Na huyu ndeke mwenye mbingu ni mutu. Dunia muzima alijenga Mungu juu ya kuikala ndani yake mutu. Ulimwengu muzima inatengwa na inatembea juu ya kupeleka musafiri mu kazi yake ya mwisho. Na yule musafiri ni kila mutu.

Bintu vyote ilijengwa kwa kila mutu. Ni ma zawandi ya Mungu. Mungu vyote vitu alijenga ndani ya ma siku wa tano. Hii ma siku walikuwa ma wakati warefu, na ku mwisho alijenga mutu kwa siku ya sita. Wakati tunasema Mungu mu Kanisa yetu inapaswa kuuwaza ya kama Mungu wetu eko ma Uso wa tatu. Nikusema eko Mungu-Baba, Mungu Yesu Kristu na Mungu Roho Mtakatifu. Hatusandiki kwa wa mungu wa tatu lakini kwa Mungu moja, mwenye ekona ma Uso wa tatu; joo vile mu Kitabu Mwanzo, Sehemu ya kwanza, mustari 26 (1, 26) tunasoma hivi: «Tufanye mutu kwa mufano wetu, mwenye sura yetu, . . . «. Nikusema tutafanya sisi, nikusema Utatu Mutakatifu, mutu, mwenye atakuwa katika sura wetu.

Ku mwanzo ya hii fundisho milimiambia ya kama mitamionyesha moja mufundi na moja mutu mwenye kufatula. Sasa mulisikia ya kama nani eko Huyu Mufundi? Mungu ni Mufundi ya hii dunia muzima, aliyefanya yoyote bintu na hekima. Mungu ni mutu, mwenye kufatula, kwa sababu Yeye alifanya picha-Sura (ikona) ya kwanza, na hii picha ni mutu.

Ekona kadiri ukubwa juu ya kuumba Mungu pamoja na Uso yake wa tatu mutu moja? Tena kadiri ya mutu inaonekana na toka hii namna Mungu alimuumba. Juu ya beingine vyumbe Mungu akasema na waliumbwa, lakini juu ya kuumba mutu alifanya moja tendo kimungu, moja tendo ya Mungu kabisa. Mukona ona moja mutu, anayefanya chupa moja ao vase ya fleurs na bulongo? Ya kwanza anabeba ku mikono yake bulongo ya matope na anaitegeneza kwa mikono yake moja pot ya fleurs. Vile na Mungu alibeba kwa mikono yake bulongo ya matope. Alifanya mutu moja na alimusimamisha. Tena hasiseme, hasitengwa, hasisikie na hasione. Na moja pumuzi alimupatia uzima. Kisha huyu mutu alifungula ma macho yake, alitenga mikono na mikulu yake na ilianza kutumika roho yake. Vile mwili yake inatumika muzuri kabisa. Kisha saa ilikuja kumupatia na moja ingine zawandi munene. Ni nani?

Mungu alimupatia moja kintu yake. Nafsi ya kila mutu inafuchama ndani yake hii «Sura» ya Mungu. Nikusema aliuumbwa kila mutu katika Sura ya Mungu, kwa sababu ekona ndani yake nafsi. Na hii nafsi inapatia kwa kila mutu akili na uhuru na mapenzi na nguvu ya akili na mawazo.

Ma nyama wekona uzima, lakini hakuna nafsi. Wanapumuzi, lakini habawaze. Wanatembea, lakini habasikie. Wanakimbia mbio, lakini habaweze kufanya matendo wazuri na culture, sawa anafanya mutu. Wanafokea, lakini habaweze kusuburia. Mutu ekona akili, ekona sauti, ekona

mahasa, ekona uhuru. Na hii yote kwa sababu hana nyama. Ni moja kiumbe ya Mungu ya kuachana. Ekona nafsi usiyekufa.

Mungu alisimama na aliona hii kiumbe ya mikono yake. Na alisema: « Anafanana ngapi hii kiumbe pamoja na Mimi! Weye, mtoto wangu, sura yangu, weye unayekuwa mutu uko mukubwa ya hii ulimwenfu. Weye utakuwa mukubwa ndani ya hii fasi kwa kila nyama, mayani, ma michi na kila kintu ya hii dunia. Utaongezekwa, utazambalishwa na utajaza hii yote dunia.

Yule mutu ya kwanza aliyetosha toka mikono ya Mungu eko moja kiumbe muzuri kabisa. Lakini ndani ya hii dunia kuliko muzuri ilikuwa Paradizo. Pale ndani ya hii fasi takatifu Mungu aliweka yule mutu ya kwanza.

Katikati ya ma zawandi wenye Mungu alipatia kwa mutu alikuwa hii ushirika na mapendo katikati ya Mungu na mutu. Nikusema yule mutu aliishi pamoja na Mungu. Na ndani ya hii fasi ya Paradizo mutu ilikuwa namna kufika kwa hii kazi, Mungu aliyemuumba, nikusema juu ya kufika ku utakaso, kufanana na Mungu Baba na Muumba yake.

Mutu, sawa na mweye munajua, alimutosha Mungu toka Paradizo. Juu ya ninyi yote mweye munajua. Hapa tutasimama historia yetu. Sasa inapaswa kusuburia yulu ya mambo wazuri na ya kadiri kabisa.

MAELEZEO. Ulizo: Ni nani huyu Mufundi, milimiambia leo?

Jibu: Yeye ni Muumba na Mwenyezi Mungu wetu.

Ulizo: Ni nani hii nyumba Mungu aliiumba?

Jibu: Hii ni dunia sisi tunaiona.

Ulizo: Ni kweli ya kama aliumba na dunia ile hasionekane, nikusema Majeshi ya wa Malaika. Tunasema ninyi kwa Simvolo ya Imani wetu:

Jibu: « Nasandiki Mungu mmoja, Baba Mwenyezi, Mwumba wa mbingu na wa dunia hata vyote vilivyoonekana na visivyoonekana» Ulizo: Na ni nani eko huyu mwenye iconographe ya hii fundisho yetu ya leo? Jibu: Mara ingine Mungu. Yeye aliumba dunia. Aliumba na mutu. Ulizo: Ni ninyi mutu na tunamuita Mungu Iconograpfe?

Jibu: Ni picha-Ikona ya Mungu.

Ulizo: Ndivyo, ni mufundi na iconographe. Mutume Paulo anasema: Bintu vyote walijengwa ya huyu. Na huyu mumoja, wakati alitaka kujenga mutu alisema: « Tufanye mutu kwa mufano wetu». Hii sauti ya Mungu, munaweza kuisikia? Inatuonekana ninyi?

Jibu: Inatuonekana ya kama mutu ekona kadiri munene.

FUNDISHO. Kila mutu ni kiumbe katika mufano ya Mungu. SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Tufanye mutu katika mufano wetu, mwenye sura yetu» (Mwanzo 1, 26).

MATENDO KU UZIMA YETU. Hii sauti ya Madiko zamani ilikuwa namna kuisikia mutu moja, lakini eko ni lazima kuisema nguvu na kuubiri na kwa watu weingine. . Munajua juu ya ninyi?

Juu ya kuonyesha shukrani yetu kwa Mungu, aliyetufanya watoto wake.

Kila mutu iko namna kufanana na mwili na ma nyama beingine, kwa mufano na makaka, lakini kadiri ya mutu ni ya kama yeye ekona nafsi ya milele. Mutu ni moja kipande ya mbingu.

Sisi tuko watoto ya Mungu. Hii ni sifa munene! Tuko mifano ya Mungu.

Hii ni kadiri munene. Hii ikona na moja ingine maana. Kama ukona moja Ikona, unaipika, unaipatia uchafu, unaitupa ndani ya buchafu? Hapana, hata saa moja. Kwa sababu unaeshima.

Vile, watoto wangu, inapaswa kueshimiwa watu weingine, kwa sababu wote weko katika mufano ya Mungu. Kama tunatema mutu moja, iko sawa kutema yulu ya moja Ikona ya Mungu wetu. Kama tunapika mutu mwingine, iko sawa kupika Ikona ya Mungu wetu. Na wakati sisi tunaanguka ku zambi moja, iko sawa kutupa ikona moja ndani ya buchafu.

Sisi wote tuko ma Ikona-mifano ya Mungu. Wakati moja tutarudia mara ingine ndani ya Paradizo, iliyetufungula Mungu Yesu Kristu kwa mapendo yake kwa sisi. Basi, sasa inapaswa kukombana juu ya kufanana na Mungu Baba wetu. Vile na ma nafsi wetu wazuri tutaenda mu Paradizo ya Mungu. Sasa, basi, tuende kusema wote pamoja hii fundisho yetu ya leo: « Kila mutu ni kiumbe na mufano ya Mungu».

## FUNDISHO YA TATU
## KAINA NA ABELI
(Mwanzo, 4)

Mukona one mulimanji? Mukona ona muchungaji?

Iko namna kuniambia, juu ya ninyi mutuulizeni?

Wale watoto walizaliwa na walikomea ku moja mukini wanajua na wekona ufamio toka hii uzima ya mulimanji na muchungaji. Ma shamba na ma nyumba ya ma nyama yao ni ma fasi, ile wanapenda sana.

Watoto wa nani katikati yenu wanaikala ku moja mukini ao wanaenda hii wakati ya kipwa. Munyanyule mikono yenu yulu.

Minaona ya kama muko wa mingi. Basi, mukona ona mulimanji? Wanatumika nguvu na mikono yao kila kazi ma shamba wao juu ya kutafuta ma chakula yao. Wanachoka, wakati wanataka kupanda moja mbeko mpaka hii wakati watafanya mavuno yao.

Mukona ona na wachungaji? Mifano wao ni muzuri. Hawa wekona ma kondoo ao ma mbuzi wa mingi na wanaenda mu pori. Wanaimba na moja baragumu na hawa tena wanasikia ma sauti ya ma nyama yao na wanafurahi.

Lakini misijue, mweye munapenda kupita kuishi sawa walimanji, ao sawa wachungaji?

Leo, kama mutasikia hii fundisho yetu, mutaniambia nani alikuwa kuliko muzuri huyu muchungaji Abeli ao mwingine mulimanji Kaina?

HISTORIA.

Waliishi wakati moja wa nduku wa mbili, wanaume. Wazazi wao waliwapenda yote mbili. Walizaliwa mu nature na hii nature waliipenda yote mbili tangu kipimo wao udogo. Wakati walikomea kila mtoto alichakula njia ya kazi yake.

Mtoto ya kwanza na mukumbwa tangu kipimo udogo alipenda inchi.

Alifurahi kuishi na kutumika ma shamba. Kila asubui alienda ma shamba. Alitegeneza shamba yake, alipanda mbeko, aliweka michi ya matunda, alimwanga mayani yake. Alifurahi kuangalia ya kama ma shamba yote yake wekona moja ragi maesombe, kutosha mayani na matunda wazuri. Furaha yake ilikuwa kuliko mingi, wakati ilikuja wakati ya mavuno. Uzima yake ilikuwa muzuri. Lakini muzuri ilikuwa na uzima ya mwingine muloko yake, mwenye alichakula uzima ya muchungaji. Yeye alipenda kutembea na kundi ya ma nyama yake mu pori. Aliwaongoza ma nyama yake karibu ya kizipa na ma mutoni juu ya kupata ma nyama yake mayani. Na wakati ilikuwa kivukutu mingi ilipaswa kurudia ku moja fasi ya kimvuli juu ya kupumuzika ma nyama yake. Furaha yake ilikuwa mingi, wakati aliweka ma nyama yake ndani ya nyumba yao na yeye alikamuna na alitosha mazima yao. Vile na yeye aliishi moja uzima safi na furaha. Kwani alitembea yeye mweyewe mu pori alikumbuka Mungu na daima alisuburia na Yeye.

Basi wale wa nduku ya hii fundisho yetu ya leo walikuwa moja mulimanji na mwingine muchungaji. Moja alipeleka kwa nduku yake matunnda ya kazi yake. Na invers. Nikusema mukubwa nduku alimupatia kwa muloko yake mbeko ya ngano na matunda ingine, lakini na muloko yake alimupatia kwa mukubwa yake mazimba, nyama na ingine ya ma nyama yake.

Lakini ilikuja siku moja na hii mapendo yao ilipotea. Huyu muloko hasikukuwe na moja mambo mbele ya mukubwa yake. Lakini mukubwa yake alikuwa na moja mufano mubaya mbele ya muloko yake. Richo yake ilionekana ya kama alimuchukia juu ya tamaa. Ku mwanzo alimuangalia na richo makari, kisha alimusema na namna makari na kisha hasikupende hata kumuona kwani alimuchukia.

Lakini, juu ya ninyi? Mambo gani ilizaliwa katikati yao? Kintu kibaya ninyi alimufanyisia muloko yake?

Musikieni, watoto wangu. Muloko yake, mwenye alikuwa muchungaji, alipenda sana Mungu. Na juu ya kuonyesha hii mapendo yake kwa Mungu alibeba kila wakati moja nyama yake, muzuri na ya kunenepa na aliitoa kama sandaka kwa Mungu. Ile wakati hii ma sandaka walitoa, watoto wangu, watu mbele ya Mungu. Na Mungu, mwenye aliangalia roho safi yake, alipokelea hii sandaka yake na furaha mingi. Simoko ya hii moto ya sandaka yake ilinyanyula safi kwa mbingu.

Na mukubwa yake? Na yeye alitoa sandaka kwa Mungu. Ilipaswa na yeye kumutoa kintu moja. Lakini, kwani alipenda kuliko matunda juu ya uzima na maugu yake, alitoa kwa Mungu hapana ile matunda wazuri, lakini hii iliisha kuoza na ilikuwa kadiri ya kuitupa. Lakini hii sandaka Mungu hasipokelee. Anapenda kupokelea ma sandaka, ile inatoka toka moja roho safi na kujaza na heshima na mapendo mbele Kwake. Joo vile hasikupokelee sandaka yake, kwa sababu huyu nduku mukubwa yake hasikukuwe na mapendo mbele ya Mungu.

Hii mambo ilikuwa, watoto wangu. Tangu hi saa mukubwa yake alisikia, ya kama paka sandaka ya muloko yake aliipokelea Mungu. Tangu hii saa ilizaliwa na ilibakia ndani ya roho yake tamaa na chuki kontre ya muloko yake.

Mtoto wangu, alimwambia siku moja Mungu. Juu ya ninyi unasikitika na unataambu? Haukujue ya kama inapaswa kutoa sandaka kwa Mimi ya kila kintu muzuri ukona yo? Weye ulifanya hivi, lakini na bintu vibaya yako. Haujue ya kama ni zambi kutoa kwa Mimi bintu vibaya yako, lakini mimi minakupatia yote bintu yangu na wema na mapendo mingi? Lakini hata ma sauti ya Mungu hababakuweze kuleta butamu kwa roho ya mukubwa nduku yake. Ndani yake tamaa ilikomea kabisa. Na hii saa, aliikala na giza ya akili yake, alisimama. Aliisha kutegeneza picha uovu yake.

Anakimbia. Anaenda kumutafuta muloko nduku yake. Anageuza na udanganyifu mufano yake na anamwambia na namna butamu ya wongo:

E, nduku wangu, unakuja kutembea kiloko pamoja mpaka ma shamba yangu?

Tuende, alimujibu muloko yake, mwenye alimuheshimiwa na alimutii.

Juu ya mapendo yako minakuja na haina mambo kwani niko na na muchoko mingi.

Walitembea pamoja wa nduku wa mbili. Waliepuka sana ya nyumba yao.

Mbali ya ma macho ya wazazi wao. Wakati walifika ku moja fasi mbali kabisa muloko yake alianza kusikia moja kintu kibaya. Mukubwa yake hasikusuburie na yeye. Paka alitembea na kichwa yake chini. Aliwaza kintu moja kwa akili yake. Alitegeneza kintu moja. Na, kwa sababu hakuna mutu mwingine ya kumuona, alikuja kupika muloko yake. Muloko yake alivumilia, kwa sababu alikuwa mudogo kwa kipimo yake na hasikuweze kutoka, kwani mukubwa yake alimukamata.

Kazi ninyi kibaya, ee nduku wangu, milikufanyisia? Juu ya ninyi unanipika? Mimi minakupenda. . . Lakini hasikutagurie kusema na sauti ingine. Ndani ya ma dakika kiloko kazi kibaya iliisha. Mukubwa nduku alimwua muloko yake na moja upanga. Kwa hii kazi ilimusukuma tamaa yake. Vile, aliwaza ya kama ataokolewa toka nduku yake. Hasikuweze kuangalia ya kama Mungu alipokelea paka sandaka ya nduku muloko yake na hapana yake.

Hii kazi ya giza ilionekana ya kama iliisha. Damu ya muloko yake ilimwanga inchi. Ilikuwa tena moja ingine sandaka. Sandaka ya mwili ya Abeli.

Huyu Abeli alikuwa mutoto muzuri na muchungaji, mwenye alitoa sandaka kwa Mungu na Yeye alipokelea sandaka yake. Na Kaina alikuwa mukubwa yake, lakini sandaka yake Mungu asikupokelee, kwa sababu alimutoa bintu yake ya kuoza na mabaya.

Kwa sababu Kaina aliwua nduku yake inaonekana ya kama historia yetu inaisha. Historia juu ya Kaina inaanza tanga sasa. Na ni historia ya mateso. Historia gani? Sasa munaisikia.

Kaina kisha kazi kibaya yake alibeba njia ya kurudia. Hata richo ya mutu moja hasikumuone. Kweli, hata richo moja hasikumuone? Ilikua kosa yake. Moja Richo alimuona. Hii saa aliwua nduku yake, moja Richo alimuangalia kazi yake. Na tazama, anamuita:

Kaina! Kaina! Kaina! . . .

Anasikia jina yake na anasimama. Anauliza maugu yake nani sasa

anamuita? Alirudia mukongo, alitafuta mutu moja, lakini hasikumuone hata mutu moja.

Kaina! . . . Kaina! . . . Kaina! . . .

Alisikia mara ya mbili jina yake. Hii mara alifamia hii sauti ilikuwa ya wapi. Ilikuwa sauti ya Mungu.

Kaina! . . . Muloko yako eko wapi? Kaina! . . . Muloko yako eko wapi?

Muloko yangu? . . .

Anaonyesha ya kama hasijue. Anataka kufuchamwa toka Mungu, kusema ma sauti ya wongo. Lakini, nani anaweka kufuchamwa toka Mungu?

Muloko yangu? Eko wapi muloko yangu? E Bwana, miye mitakuwa zamu ya nduku muloko yangu?

Ee Kaina, juu ya ninyi ulifanya hii kazi kibaya? Tazama, damu ya nduku yako inamwanga inchi na ni chini na inakuita. Malalamiko ya hii damu inaniita na ilifika kwa masikio yangu. Juu ya ninyi ulifanya hii kazi kibaya?

Kaina alitetemeka na yote mwili yake. Sasa alisikia ya kama alimuona Richo moja. Na hii ilikuwa Richo ya Mungu. Na sasa? Atafanya ninyi? Jashu mingi ilimulobana. Ilikuwa kuliko kizuri kufungula inchi na kumukunywa na hapana kusikia hii sauti ya Mungu! Mambo gani itafanyika sasa? . . .

Ee Kaina! Ilisikiwa mara ingine sauti ya Mungu. Hii kazi kibaya yako italipizwa. Hautakuwe mara ingine mulimanji mubarikiwa. Utapanda mbeko kwa inchi, utaimwanga, utaitegeneza, lakini hautaone matunda. Utatumika, lakini utachoka ya bule. Na tena. . .

Kaina anasikia na sikitiko. Sasa anaongolea maendeleo ya ingine malipizo nguvu toka Mungu.

Kaina, hautapate kimya ku uzima yako. Utapita uzima yako na tetemeko.

Ku kila fasi utaenda, utaishi na tetemeko. Damu ya nduku yako, itakufukuza. Ee Kaina, inapaswa kulipizwa. . .

Ilisimama sauti ya Mungu. Alibakia yeye mwenyewe Kaina. Na tangu ile siku ilianza mateso yake. Aliwua nduku yake, Abeli, kwa sababu hasikupende kumuona. Lakini sasa anamuona daima na kila saa. Abeli! Tazama Abeli! . . . Ku kila mwendo yake anaona uso ya nduku yake Abeli. Abeli anamuangalia na richo ya mapendo na anamuuliza:

Ee nduku wangu, kintu kibaya ninyi milikufanyisia? Juu ya ninyi uliniwua? . . .

Kaina anakimbia kuokoa toka mvuli ya Abeli, lakini hakuna namna. Haina mvuli. Ni ndani yake moyo, iliyemupatia Mungu. Hii moyo yake ilimuuzi sana. Ilimupingilia. Ilimupika. Hasikuweze kupata kiloko kimya. Alienda kularia juu ya kupumuzika, lakini alilamuka na tetemeko na boka. Ku musigishi yake alikuja Abeli. Alilamuka. Anatembea fasi yote, lakini inamufukuza daima haya juu ya hii kazi kibaya yake. Ma fasi yote inakokota karibu yake na moyo yake, inayemupika sana. Ku

kila fasi anatembea, anaomboleza na anatetemeka. Ninyi wale watu walimuona, habakusikie, juu ya ninyi ule mutu kila saa anatetemeka. Lakini yeye anajua. Tazama mara ingine ndani yake hii sauti ya Mungu:

Ee Kaina! . . . Kaina! . . . nduku yako eko wapi? . . .

MAELEZEO: Sasa, watoto wangu, munasikia moja Historia. Ni moja historia ya ile ya kwanza ku uzima ya watu ya kwanza. Ndani ya historia ya watu hii ni crime ya kwanza. Tulisikia namna gani ilimwangisha hii damu ya kwanza ku inchi yetu. Tangu ile wakati mpaka leo, damu ngapi ya watu ilimwangishwa! Ku kila nvita, ku crime, ku kila accident! Lakini mutoni ya damu ilimwangushwa toka mufano mubaya ya watu kontre ya wa nduku wao. Hii Historia mulisikia mutaweza kuipata mu Kitabu ya Mwanzo ya Agano la Kale. Ulizo: Mweye, watoto wangu, munawaza nani alikuwa mukubwa mutu ya hii historia: Yule mulimanji ao mwingine muchungaji?

Jibu: Bila shaka mukubwa alikuwa yule muchungaji Abeli.

Ulizo: Ndivyo, Abeli alikuwa yule Uso ya mwangaza ya hii historia. Abeli anatupatia maana ya Yesu Kristu, kwa sababu na Yeye alikuwa Sura ya mwangaza kuliko mingi ya kila ingine Uso ya hii dunia, mwenye kwa ajili ya chuki aliwuwa. Walimwua wa nduku wake, wale waebrania. Mutaweze kunisema matendo gani mabaya alifanya Kaina?

Jibu: Ya kwanza alimuchokoza Mungu. Alimutoa bile bintu ya kazi yake, wenye waliisiha kuoza na kuharabika. Kisha alichunga tamaa ndani ya roho yake kontre ya nduku yake Abeli. Na ku mwisho alifanya hii crime. Aliwua Abeli, mwenye hasikukuwe mukosefu.

Ulizo: Wakati alifanya hii crime, nani alimuangalia?

Jibu: Hata mutu moja, hasikumuone, kwa sababu alikokota nduku yake mbali ya ma nyumba ya watu weingine, ma shamba.

Ulizo: Nikusema, hata richo moja hasikumuone?

Jibu: Alimuona richo moja. Na yeye alikuwa Mungu. Richo ya Mungu alimuangalia alifanya ninyi na alitembea wapi.

Ulizo: Sisi tunaweza kufuchamwa toka richo ya Mungu?

Jibu: Hapana! Yeye anaangalia bintu yote. Mungu anajua yoyote bintu ya dunia na ile tukona yo ndani ya ma roho yetu na ma akili yetu. FUNDISHO: Mungu anaona bintu wote, anajua matendo na mawazo wetu yote. SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: «Niende wapi mbali na roho yako? Ao nikimbie wapi toka uso wako? « (Zaburi 138(139), 7).

MATENDO KU UZIMA YETU. Inje ya moja masomo, watoto wangu, ilikuwa moja daftari, pahali iliandikwa hii:

Ni moja richo, inayeona yoyote.

Ni moja risikio, inayesikia yoyote.

Ni moja mkono, inayeandika yoyote.

Hii ni mukono, richo na risikio ya Mungu. Huyu, mwenye aliumba masikio ya watu na wa nyama, hasisikie? Huyu aliyeumba ma macho ya watu, hasione?

Mungu ni mwenye kufamia yote bintu ya dunia. Yeye anaangalia yoyote.

Tena anajua na ma roho yetu, kwa sababu anajua yote mawazo na kila kintu tunaifuchama sisi toka ma macho ya weingine watu. Mungu ni ma fasi yote. Anatuangalia ku kila fasi sisi tunaenda.

Mara ingine, wakati tunataka kufanya moja kazi kibaya, tunafanya nguvu kuifuchama hii kazi yetu, juu hatutake kutuona watu weingine. Lakini wambafu ngapi tuko mbele ya Mungu! Toka ma

macho ya watu iko namna kufuchamwa, lakini toka richo ya Mungu hatuweze kufuchama ma kazi mabaya yetu.

Hii saa moja mtoto anafungula mkono yake kuiba kintu moja ugeni na anasema: « Muzuri, hasikunione hata mutu moja», hii saa alimuona Mungu. Wakati mtoto mwingine anafungula kinywa yake na anachabula na anawaza: « Muzuri, kwani hasikunisikie mwalimu ao mama wangu», lakini hii saa Mungu alimusikia.

Wakati moja walimwambia kwa moja mutawa ya jangwa kufanya moja zambi.

Na yule alijibu:

Mitaifanya hii zambi, lakini minataka kuenda katikati ya muji yetu mbele ya ma macho ya watu wote.

Usisikie haya? Walimuuliza. Na yule mtakatifu aliwajibu: Mbele ya watu mukona haya na munawaza watasema ninyi, lakini hamuwaze Mungu, mwenye anaona yoyote ma kazi na mawazo wetu?

Munataka, watoto wangu, kuchunga ma lunrimi yenu safi toka kila neno mubaya na kila chabulana? Muchunge ma macho yenu mbali ya kila kintu, itayemiletea buchafu ku rohu yenu. Tena, muchunge masikio wasafi ya kila wimbo na sauti ya hii dunia. Tena tazama moja sindano ya roho tangu leo:

Misitaseme hata moja sauti, ile hasipende kuisikia Mungu. Misitaende ku fasi moja, pahali misitake kuniona pale Mungu. Misitafanye kintu moja, ile misitake kuiangalia Mungu.

Watoto wapenzi wangu, musisahabu, ya kama kila saa Mungu anatuona!

## FUNDISHO YA INE
## MUFANO YA MUPANDAJI MBEGU

NAMNA YAKUKARIBIA

Leo fundisho yenu atafanya mwalimu mwingine. Munataka, watoto wangu?

Sisi tunafurahi kusikia fundisho na ya mweye. Lakini ni nani huyu mwalimu mwingine?

Ni mwalimu kuliko mukubwa ya walimu weingine ya hii dunia muzima. Ni Bwana Yesu Kristu. Ni ninyi? Munashangaa, kwa sababu milimiambia ya kama fundisho leo atafanya Bwana Yesu Kristu?

Jibu ya watoto: Ndivyo, tunashangaa, kwa sababu tunazania ya kama hii yote mafundisho tunaifanya hapa ni mafundisho ya Kristu. Mweye, paka munaitupeleka kwa sisi.

Hii jibu yenu, watoto, ni kweli sana. Na minafurahi kwa sababu mukona hii akili kizuri. Na leo mutasikia hii fundisho toka kinywa yangu. Lakini itakuwa sawa aliituwaambia Bwana Yesu Kristu. Juu ya ninyi milimisema ku mwanzo ya kama hii fundisho ya leo atafanya Yesu Kristu? Kwa sababu, watoto wangu, hii fundisho ya leo, alikuwa mufano ya kwanza, iliyesema Yesu. Lakini ni ninyi mufano, ao parabole?

Ni moja historia, mukongo yake inafuchamwa moja fundisho ukweli. Ni vile. Watu wenye wekona akili kiloko yuu ya kusikia mafundisho ya nguvu, habaweze. Joo vile Kristu aliwasema parabole juu ya kusikia hapana paka watu ya akili kiloko, lakini na wale wenye ilipaswa kusikia. Na hii parabole Kristu alionyesha mwalimu muzuri ngapi alikuwa. Ma Parabole walikuwa na ma historia ya kweli ao beingine symbolique. Ma Parabole ni ma historia ya kweli, ile alibeba Kristu toka uzima ya watu, wenye wanatupatia moja fundisho kizuri na tangazo kwa uzima yetu. Sasa minaanza kumiambia hii mufano ya kwanza aliisema Yesu Kristu kwa wanafunji na watu weingine. HISTORIA. Wakati moja ilikuwa moja mupandaji mubarikiwa. Alipenda sana kazi yake. Alikuwa na mbego kizuri. Aliweka moja asubui, pa mabeka yake mufuko na mbego na alienda ma shamba

yake juu ya kuipanda. Kila mbego aliitupa chini ilikuwa na moja sala: Mungu kubariki kila mbego juu ya kuotesha na kukomea kuivya na kumupatia matunda yake.

Hii ma mbego ya kwanza aliitupa habakuangukie ku moja fasi ya bulongo kizuri. Waliisha kuikanyanga watu, wenye walipita pale. Ilionekana kama njia udogo. Toka hii fasi walipitisha na watu na wa nyama. Ku mwanzo aliwaza juu hapana kupanda hii fasi. Kisha alikuwa na moja kitumaini ndani yake na iko namna mbego yake kuiota. Vile na hii kitumaini alipanda mbego yake.

Alichofa ku fasi ingine. Mbele ya ma macho yake sasa anaona moja injine bulongo. Ilionekana ya kama ilikuwa shamba, lakini ndani yake walikuwa wa mingi maimbwe.

Hapa mitapanda mbego ao hapana? Milipanda kwa ile fasi ku mbele, juu ya ninyi misitapende hapa? Na hivi alifungula mukono yake na alitupa ma mbego. Ingine mbego ilianguka yulu ya maimbwe na ingine pa bulongo kizuri kiloko.

Alichofa kiloko ku fasi ingine. Roho yake ilifurahi, kwani pale shamba ilikuwa na bulongo kizuri. Vile inaonekana. Na mapendo mingi alitupa ma mbego mingi. Wakati alichofa toka hii fasi, aliwaza, kama itaota ao hapana, kwa sababu aliona kuotesha na mayani ya miimba.

Alisema! Haina mambo tutaangalia. Minatumainia, ya kama tutabeba matunda.

Alichoka sana huyu mupandaji, lakini aliendelesha kazi yake.

Ku mwisho alipaza sauti na furaha mukusema: Tazama! Hii bulongo militafuta. Hapa mbego yangu itaota, itaivya na itanipatia matunda yake.

Na kweli. Hii fasi ya ine ilikuwa moja shamba kizuri na safi.

Hasikukuwe hata maimbwe, hata miimba, hata bulongo nguvu. Hii bulongo ilikuwa teketeke, sawa iliongolea hii mbego ndani yake. Na furaha mingi alipanda kwa hii bulongo huyu mupandaji. Yote ma mbego iliisha hapa.

Kazi yake ilionekana ya kama iliisha. Lakini hasikuishe. Wakati alirudia kuangalia ma fasi ingine, alitaambu. Aliona kwa hii fasi ya kwanza alipanda mbego, ma ndeke walipita na walikula hii mbego. Tena roho yake ilisikitika, kwa sababu walitambuka toka hii fasi na watu wasafiri na walikanyanga hii mbulongo na walikusugulika hii mbego.

Wakati ilipita ya mingi. Kisha ma mwezi wadogo huyu mupandaji alitembelea ile ma fasi ya kazi yake. Kwa hii fasi ya kwanza aliona, ya kama walikanyanga watu bulongo na hii mbego ilipotea.

Vile ilikuwa mwisho na kwa hii fasi ya mbili. Fasi ilikuwa na maimbwe wa mingi na bulongo kizuri kiloko sana. Waliota ma mbego wadogo ma fasi ya kuachana. Lakini habakukuwe mizizi ya nguvu. Maji hakuna na baridi. Na vile walikauka.

Alichofa kwa fasi ingine ya tatu. Bulongo ilionekana kizuri. Waliota ma mbego wazuri, lakini pamoja waliotesha na mayani ya miimba. Na hii miimba ilikomea kupita mbio na waliharabisha hii mayani ya mbego kizuri. Na yeye hasikuweze kutembea ndani yake kwa ajili ya miimba wa mingi. Toka mikono na mikulu yake ilitoka damu ya ma bilonda wa mingi juu ya miimba.

Taambu yake ilikuwa mingi, lakini alikuwa kitumaini ku fasi ya ine. Na pale kweli, hasikupoteshe kitumaini yake.

Na furaha mingi alipaza sauti na alisema: Mingi, mingi mayani ya mbego kizuri. Utukufu kwa Mungu. Baraka ya Mungu.

Yesu Kristu ku hii fasi ya Parabole yake alisimama. Wale walimusikia, walipumuzi kiloko. Sasa waliongolea kuwafafanusha Kristu maana ya hii parabole:

_ Ni ninyi maana ya hii Mufano, ulituwambia, Mwalimu wetu? Walimuuliza.

Mitamielezea! Kristu aliwajibu. Ninyi watu wekona masikio watasikia.

Na ya kwanza mitamielezea ni ninyi maana ya hii mbego. Mbego ni neno ya Mungu. Mupandaji Mukubwa ni Bwana Yesu, mwenye alikuja toka mbingu. Alifika kwa inchi yetu juu ya kupanda mbego ya fundisho yake kwa ma roho ya watu. Sasa munataka kusikia ma mbego yake walienda wapi?

I. Basi, yule mbego ilianguka kwa hii fasi walimukula ma ndeke na watu wasafiri waliikanyanga, munajua watu wa nani weko? Weko wale watu, wenye wanasikia neno ya Mungu. Lakini kwa roho yao hakuna faida, kwa sababu anakuja moja ndeke munene na anaiba hii mbego toka ma roho yao. Munajua ni nani huyu ndeke? Ni Shetani. Kwa hawa watu ilianguka mbego-neno ya Mungu, na mara moja hii neno ilitoka.

2. Sasa mutasikia maana ya hii fasi ya mbili, pahali walikuwa na maimbwe wa mingi. Weko wale watu, wenye habaonekane wazaifu. Nikusema wanasikia na furaha mingi neno ya Mungu. Inawapendeza sana na wanafurahi. Wanaona ya kama hakuna kintu kizuri kuliko, mbele ya neno ya Mungu. Lakini, wakati wanatoka, habaendelee kusaidia ma roho yao na chakula ya neno ya Mungu. Wanakatala kumwanga ma roho yao na maji ya neno ya Mungu. Vile, inatoka hii matakio yao ya kwanza. Na, wakati wataonekana ma majaribu na mateso ya kwanza, wanasahabu yoyote maneno ya Mungu na wanarudia ku uzima yao ya zamani. Hakuna mizizi mbego yao. Walikuwana heshima na mapendo ya neno ya Mungu ya bure na ya wakati kiloko.

3. Ni ninyi maana ya wale watu wanafanana na hii shamba pahali mbego iliota, lakini pamoja iliota na miimba. Hawa watu wanapokelea neno ya Mungu, bila shaka na bila mabishano. Waliikamata hii faida ya neno ya Mungu ndani yao ya wakati mingi, lakini ndani yao ni na miimba. Habakutumike mbele kutosha ma miimba. Ni ninyi hii miimba? Ni ma zambi na ma zwezo mabaya wetu. Ni ma mambo wa mingi na mateso na sikitiko mingi ya hii uzima. Watu leo wanapenda kuishi na furaha ya hii dunia, na muchezo, kukunywa vinyo na hivi furaha ya neno ya Mungu inakimbia na mapendo ya wokovu yao inazimisha. Vile ma nafsi wao inapotea.

4. Na sasa mitamielezea na hii maana ya hii fasi ya ine. Hii fasi ilikuwa na bulongo kizuri. Nikusema weko watu, wenye wanapokelea hii neno-mbego ya Mungu na mapendo mingi na wanaichunga ku uzima yao. Wale watu wanaokolewa. Wanatumika kila siku matendo wazuri juu ya wokovu wao. Vile wekona baraka ya Mungu ku uzima yao. Vile itakuja na hii wakati ya matunda yao. Ni ninyi matunda? Uzima ya milele mu Paradizo ya mbingu. MAELEZEO. Hapa, watoto wangu, inaisha hii parabole na ufafanusho yake, sawa alituifundisha Bwana Yesu Kristu, toka Evangelion ya Mwavangelizaji Luka. Ulizo: Namna gani inaitwa hii historia ya leo?

Jibu: Mufano ao Parabole. Hii ni parabole ya kwanza, iliyeyoka toka kinywa ya Bwana Yesu.

Ulizo: Namna gani inaitwa hii Parabole?

Jibu: Parabole ya Mupandaji.

Ulizo: Munakumbukeni hii ma fasi ya ine alipanda mbego yake huyu mupandaji? Jibu: HIi fasi ya kwanza ilikuwa kama njia, pahali walipita watu na walikanyanga bulongo. Fasi ya mbili ilikuwa na ndani maimbwe kiloko-kiloko, Fasi ya tatu iliisha kujaza na miimba na fasi ya ine ilikuwa bulongo kizuri.

Ulizo: Ni ninyi maana ya hii shamba na maana ya hii mbego?

Jibu: Mbego ni neno ya Mungu, Evangelion yake, Ubiri, fundisho ya Kristu na ya Kanisa yetu. Shamba ni ninyi? Ni ma nafsi ya watu wote ya dunia. Ulizo: Na ndani ya ma roho yetu inaanguka mbego ya Mungu. Lakini sisi kama tunapenda kutosha matunda hii mbego, inapaswa kufata categorie nani? Jibu: Kategorie ya ine. Nikusema ma roho yetu inapaswa kufanyika bulongo kizuri juu ya kuota mbego-neno ya Mungu na kutusaidia kuokolewa. FUNDISHO: Inapaswa kusikia ma sauti na mafundisho ya Mungu na ya Kanisa yetu. Sauti ya Madiko tutabeba hii ma sauti alisema Bwana Yesu ku mwisho ya hii Mufano yake:

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Wanasikia neno, na kulishika, kisha wanazaa matunda kwa uvumilivu» (Luka 8, 15).

MATENDO KU UZIMA YETU. Hii Parabole inatujibu kwa moja ulizo tunasikia sisi ao tunasema. Ni hii:

Juu ya ninyi watu wote habakuwe wa Kristiani?   Na wale, wenye weko wa Kristiani, juu ya ninyi kuliko ya wamingi habatumike matendo wazuri, habajue uzima ya Kristu, wanaishi mbali ya Kanisa ya Kristu?   Ni nani mukosefu ya hii mambo?

Iko namna kukosana wa mingi na hapana mpaka moja. Huyu moja ni mbego.

Hii mbego ni neno ya Mungu, iliyekuja toka Mungu mu dunia.

Wale walisafiri mara ya kwanza ku Amerika walibeba na ma mbego ya mbego ngano na leo Amerika ni chem-chem ya kutosha ngano ya milioane kilograme. Vile ilifanyikwa na Yesu Kristu. Mungu alikuja mu dunia na pamoja yake alileta na mbego, neno ya fundisho ukweli yake. Evangelion ya Kristu ni chem-chem ya hii mbego ya Kristu.

Haina, basi kosa toka mbego; moja mwingine anakosana. Kuliko inakosana shamba, nikusema watu. Watu wa mingi weko kwa ile vipande ya shamba, tulisema yulu. Mungu anapanda na mbego yake ma roho ya watu wote. Lakini hasipende na force kufata watu fundisho na imani Yake. Wakosefu ma shamba, ma roho ya watu. Beingine ma roho ya watu wanafanana sawa ile njia, iliyeikanyanga watu. Ma roho yao iko ya nguvu sawa ciment. Hakuna wema kwa roho yao. Wanachabula wa nduku wao, wanawapika, wanawawua. Neno ya Mungu hasikupande hata kiloko ndani ya ma roho yao.

Watu weingine wanafanana kama moja shamba, pahali ndani yake ni na maimbwe ya kiloko ya mingi. Nikusema matendo yao ni beingine. Kwa mufano watoto wa ngapi wanapenda kupita muchezo ya football na hapana mafundisho ya masomo yao na neno ya Mungu?

Watu weingine wanafanana kama ma shamba ya miimba. Kama utawakaribia, watakupingilia na miimba yao, nikusema na ma kosa na zwezo mabaya yao. Wanakombana paka watakula ninyi kila siku, watakunywa ninyi, watacheza namna gani. Vile wanawaza na vile wanaishi.

Mweye, watoto wangu, minazania ya kama munataka kufata hii kipande ya wale watu wanafanana na hii shamba kizuri. Mulikuja ku hii Masomo yetu juu ya kufamia huyu Mupandaji mukubwa, Yesu Kristu. Nafsi yenu inapokelea fundisho Yake. Basi, muichunge hii neno ya Kristu, kwa sababu iko hatari kuiba wamwivi, nikusema shetani. Hii ni zahabu ya ma roho yenu.

Dunia muzima ilijaza na matunda ya mbego ya shetani. Beingine watoto kuliko wakumbwa ya mweye walifanyikwa watu mabaya. Lakini muji yetu na wazazi wetu na sisi tunataka kuona mweye kutondola ma mbengo wazuri. Matunda ya wema na mapendo ya Mungu na watu wote. Kila mtoto inapaswa kisha kufanyika moja mupandaji mudogo. Mbego yenu itapata shamba muzuri kwa ma roho ya watu na italeta matunda wazuri.

## FUNDISHO YA TANO
## EFTIHOS
## (Matendo ya Mitume 16, 9-10 na 20, 7-12)

Ile wakati aliishi Mutume Paulo mu inchi Asia Udogo ilikuwa muji moja iliyeitwa Troa. Leo ndani ya hii muji, watoto wangu, mutasikia moja ukusanyo ya wa Kristiani ya ile wakati. Hii historia na ukusanyo iliandikwa mu Kitabu Matendo ya Mitume, pahali tunasoma mashindano iliwafanya wa Mitume Paulo na Petro.

Basi, wakati moya, alienda ku hii muji Mutume Paulo. Kazi ya Paulo ilikuwa kukokota watu kwa imani ya Kristu. Wale, walimuamini Kristu ya hii muji walikuwa kundi ya kwanza ya wakristiani ya

Kristu. Mutume aliwafundisha namna gani watamwabudu Mungu na namna kweli. Yeye inapaswa kuendelesha safari ya utume yake. Mawazo wa mbili walimuuzi ndani ya akili yake. Uwazo moja ilimwambia kurudia ku muji Antiohia, na uwazo ingine kuendelesha hii kazi takatifu yake. Ile wakati Mbulaya muzima na Grekia na Makedonia walikuwa ndani ya giza ya kila zambi. Waliongolea tangazo ya wokovu.

Busiku moja, kwani aliisha kuchoka, alilaria kupumuzika. Kisha saa kiloko alilamuka mara moja na aliwaambia kwa wasaidizi wake:

Wanatuita. Inapaswa kwenda. Inchi Grekia inatuita! . . .

Mambo ninyi ilifanyikwa? Aliona ku musigishi yake ndoto moja. Aliona mutu moja toka fasi Makedonia, kwa sababu alivaa manguo ya hii fasi. Alisimama mbele ya uso ya Paulo na alimwambia: «Vuka, uje Makedonia kutusaidia». Nikusema, pita kwa ngambo ingine ku inchi Makedonia na utusaidie. Utupe na kwa sisi hii nuru uliipatie na kwa ma fasi ingine. . . .

Hii ndoto, watoto wangu, ilituwambia ya kama sasa ilianza kuingia Ndini ya Kristianisme mu Mbulaya. Paulo, bila kuchelewa alisafiri ku fasi Makedonia ya Grekia, ku muji Filipi, Thesaloniki, Beria, Athina, Korintho. Tena Paulo alipita ma hii fasi na wakati alifanya na safari ya utume yake ya mbili na tatu.

Alipita na toka muji Troa. Hasikusahabu wa Kristiani ya hii muji. Sasa Paulo alitembea hii muji safari ya tatu yake kwa hii kazi ya Mungu.

Alikuja Paulo! . . . Vile toka kinywa moja mu injine kinywa ilizambalishwa hii tangazo kwa hii muji yao muzima. Busiku ilifanyikwa ukusanyo. Wa Kristiani walikuwa wote juu ya kuona Mwalimu na Baba wao mukubwa, kusikia fundisho yake, kusikia ma tangazo yake ma mukini na ma Kanisa weingine, na ku mwisho juu ya kuomba kwa Mungu kuibariki kazi yake.

Mutume Paulo alibakia ku muji Troa ma siku saba. Ilipaswa kutoka na kutembea na haraka mu Yerusalema. Uwazo moja ilimwambia ya kama hii mara ataona wa Kristiani wake mara ya mwisho. Taji ya Ushahindi ilimuongolea. Mushindano Mutume Paulo iko ku mwisho ya sindano ya roho yake. Busiku ya mwisho alifika ku muji Troa. Siku ingine asubui atabeba chombo na ataendelesha safari yake ku muji Yerusalema. Munasikia, watoto, sikitiko ngapi ilikuwa kwa kundi ya wa Kristiani wake, kwa sababu habataone mara ingine mwalimu yao.

Wakati ilifika giza hii busiku na watu ya sanamu walilaria kulala, kundi moya ya wa Kristiani waliondoka kwenda ku fasi umoja. Inje ya muji Troa ni nyumba moja ya mukristu moja na pale wanaenda wote wa Kristiani. Walipita mulango ya lupango, walipanda magasin ya hii nyumba, kwa sababu hii nyumba ilikuwa na bipande ya tatu. Yulu ya hii kipande ya nyumba ilikuwa kanisa. Habakukuwe ma Kanisa sawa ma kanisa ya sasa. Kisha saa kiloko hii kanisa yulu ya hii nyumba ilijaza ya watu. Ilikuwa inje kivukutu kwa ajili ya hazina ya watu mingi. Kwa hivi walifungula ma dirisha juu ya kuingia ndani pepo baridi.

Ilikuwa Mposho busiku. Ilikujaka mu Juma, siku ya Bwana, ile ni siku mukubwa ya wa Kristiani. Lakini hii busiku wa Kristiani wote walikuwa na moja furaha ya kuachana. Ku saa moja alikuja katikati yao Mutume Paulo. Walinyamaza wote na kimya ilikuwa kwa hii fasi. Watu wote walisimama kuangalia mutume mukubwa.

Sala ya wa Kristiani hawa ilikuwa hii: Ee Bwana, juu ya ninyi atatoka kesho Mwalimu yetu Paulo? Namna gani sisi tutabakia wenye wenyewe? Hii ilikuwa sala yao kwa siri.

Paulo alianza fundisho yake. Kiloko saa ku mbele waliisha kukula na kisha ilifata fundisho ya Paulo. Neno yake ilikuwa butamu na muzima. Sawa hii maji inatoka ya moja chem-chem. Ilipita hii saa na ilikuja katikati ya hii busiku, lakini mwalimu Paulo anaendelea kuhubiri yake. Na wa Kristiani wekona matakio munene ya kusikia neno yake. Hata mutu moja hasikutenge ya fasi yake. Ma macho yao wanaangalia uso ya Mutume na wanatosha machozi kwa furaha. Ma Masikio yake wanasikia bila kuzimba fundisho yake.

Lakini mara moja ilisikiwa kelele moja ndani ya hii utulivu ya busiku.

Inasikiwa sauti moja na malalamiko.

Eftihos! . . . Eftihos! . . . Alianguka chini! .

Watu wote walipindula ma macho yao kuangalia mambo gani ilikuwa, na moja mama katikati ya hazina ya watu anakangamana kutambuka na alilalamika:

Mtoto wangu! . . . Mtoto wangu alifariki! . . .

Alikuwa mama ya huyu mtoto kijana. Watu wote walikelele bila kujua safi mambo gani ilifanyikwa. Huyu mukristu, mtoto Eftihos aliisha kupanda yulu ya dirisha moja, juu ya kuikala na kupumuzika kiloko na kupumuzi pepo baridi. Lakini ma saa ilipita wa mingi na ilianza kumukamata musigishi. Alipotea nguvu yake na alianguka inje chini ndani ya shamba ya hii nyumba. Watu wote walisikia moja kelele nguvu, wakati alianguka chini.

Paulo alisimama fundisho yake. Wazazi, wajirani na watu weingine walikimbia kushuka mbio chini ku lupango. Walikaribia, walilamusha mtoto na waliona ya kama aliisha kufa. Wazazi wake baba na mama walianza kuria na maombolezo mingi:

Mtoto wetu, juu ya ninyi ulifanya hii kazi? Sasa sisi tutafanya ninyi? . . .

Mutume Paulo alisikitika sana na roho yake ilipasuka kwa ajili ya umivu yake. Na yeye alikaribia huyu mtoto na aliwaambia kwa waKristiani wote:

Musiogope! Musisikitike! Mtoto anaishi. Nafsi yake atarudia.

Hii maneno ya Mutume walikuwa wa ajaabu, lakini kwani walikuwa wa Kristiani, walijua ya kama iko namna Mutume kufanya na muujiza moja. Walinyamaza na waliongolea Mutume atafanya ninyi. Paulo alikamata mtoto kwa mikono yake, alifanya sala kwa Mungu na kisha ma dakika kiloko alipatia mtoto kwa mikono ya wazazi wake mukusema:

Mumubebe mtoto yenu na twende yulu kuendelesha kuhubiri yetu.

Mwili ya Eftihos ilianza kutengwa, alifungula ma macho yake na mucheko moja ilionekana butamu kwa uso yake.

Busiku ilianza kutoka na asubui mapema ilikuja, Mutume Paulo alikamata mukate na vinyo kwa mikono yake, aliibariki na aliwapatia kwa wa Kristiani wake Mwili na Damu ya Kristu. Roho Mutakatifu na sala ya Paulo alishuka na aligeuza hii bintu ya mukate na vinyo ku Mwili na Damu ya Kristu. Paulo alipumunika ya kwanza na kisha wa padri na shemasi na Waaminifu wote. Walipewa Mwili na Damu ya Kristu toka mikono ya Mutume Paulo. Vile waliunganishwa katika Kristu na katikati yao.

Kisha Komonyo Takatifu Paulo aliendelea kiloko fundisho yake. Ilikuja asubui. Kila mwaminifu anapita kubushu mkono ya mwalimu yake. Machozi walitelemusha ya ma macho yao, kwa sababu habatamuone mara ingine. Ku mwisho alikuja na Eftihos. Waliisha kumuchunga chini ya hii nyumba, lakini, wakati Liturgia iliisha, walimupeleka yulu. Wa Kristiani wote walifurahi kwa sababu walimuona muzima. Mtoto mudogo Eftihos na heshima mingi alikaribia Mutume. Aliongolea kumufokea, kwa sababu hii saa ya Liturgia Takatifu, alilala, lakini Paulo alimubebelesha na alimwambia: «Ee Eftihos, mara ingine usilale mu Kanisa. Uende na Mungu akubariki».

Chombo saa inakuja juu ya kusafiri. Paulo alisalimia wa Kristiani wote na aliondoka na hii chombo ku muji Yerusalema. Wa Kristiani ya Troa, weko karibu ya kikavu na walipanguza machozi wao. Paulo aliondoka. . . MAELEZEO: Ulizo: Ya nani Mutume mukubwa tulisikia leo kwa hii fundisho yetu, watoto wangu?

Jibu: Mutume Paulo.

Ulizo: Mutume Paulo tulimuona wapi?

Jibu: Ku muji Troa. Paulo alifanya matembeleo yake ya mwisho kwa hii muji.

Ulizo: Ku hii nyumba walisanyikwa watu wa mingi na walifanya ninyi?

Jibu: Walisikia kuhubiri na Liturgia Takatifu.

Ulizo: Mambo gani ilifanyikwa na ilitetemeka kiloko kimya ya hii mapatano ya wa Kristiani?

Jibu: Ilifanyikwa moja accident. Mtoto Eftihos alilala ku hii saa ya Liturgia. Alianguka chini inje ya nyumba na alifariki.

Ulizo: Lakini namna gani ilipaswa kuangalia na kusikia Eftihos Liturgia Takatifu?

Jibu: Na pasopo mingi na boka ya Mungu.

FUNDISHO: Inapaswa kusopoka na kusikia muzuri Liturgia Takatifu. SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Walikuwa wakidumu katika mafundisho ya mitume, na katika ushirika, na katika kuvunja mukate na kuomba. (Matendo ya Mitume 2, 42).

Hii sauti tunaandika leo, watoto wangu, inatuonyesha hii mapendo waliikuwa wa Kristiani ya kwanza. Sawa sasa watu wa mingi wanapenda sana kusikia television, football ao cinema, vile hii wakati ya kwanza ya Kanisa yetu waaminifu walipenda hii mapatano na uzima ya kumwabudu Mungu. Vile walionyesha matakio yao na hii ma sauti: « Ah, wakati ngani saa itafika juu ya kusikia kuhubiri toka kinywa ya wa Mitume, kuishi umoja sawa wa nduku katika Kristu, kupewa Mwili na Damu ya Kristu na matakio yao ya ine: Kumuomba kwa Mungu wote pamoja!

MATENDO KU UZIMA YETU. Sisi watoto wangu, tukona hii matakio? Tukona mapendo kuingia mu Misa, kusikia Liturgia Takatifu, kupewa Mwili na Damu ya Kristu, kuishi pamoja kama wa Nduku katika Kristu? Sasa tutafanya moja kipimo. Watoto ngapi ya mweye mulikuja hii mu Juma ilipita mu Kanisa? Munaona mweye mwenyewe ya kama hamukuje kila mu Juma? Kengele inapika mwalimu yetu ao padri yetu, juu ya kusikia sisi sauti ya Mungu toka mbingu. Ile wakati ya kwanza hasikupike kengele, kwa sababu hasikukuwe. Lakini hii wakati ilipika roho yao. Ile wakati hakuna ma Kanisa sawa sasa na wa Kristiani walifuchamwa ndani ya ma nyumba ao ndani ya bulongo mu Katakombe. Sisi sasa, utukufu kwa Mungu tukona ma Kanisa na kengele, wenye wanapika, lakini watu na watoto wetu habasikie sauti ya kengele?

Mweye munawaza ninyi. Juu ya ninyi watoto wa mingi leo habaende mu Misa?

Kwa sababu habakuwa na zwezo tangu kipimo yao udogo. Habajue ya kama ni lazima kuenda mu Misa.

Ni kweli ya kama hii zwezo juu ya kwenda mu Misa ni paka ma jamaa wadogo.

Muniseme na ingine maneno. Kila mu Juma, ao Muposho ao mu Kazi Tano watu na ma motoka yao wanaenda safari. Moja mtoto, mwenye ni mtoto ya Kristu atakombana kuingia mu Misa na kwa hii fasi ataenda ile ma siku, kama ni Kanisa pale.

Maneno ingine ni hii: Ya kama hii saa ya Liturgia weingine watoto wanaikala kusoma mafundisho ya masomo yao, ao wataenda mu kiwanja ya football, ya muchezo na kazi ingine. Hii saa wanamiita wakubwa wa mbili:

Kristu, Mwokozi wetu na mutu moja fulani ya kazi moja hii saa ya Liturgia. Mweye mutachakula nani? Ni kuliko muzuri kufata Kanisa hii saa juu ya kubakia wakristiani wa kweli. Munaweza kucheza saa ingine, lakini saa ingine hakuna juu ya Liturgia Takatifu.

Miye mitamiambia tena na ingine mambo ya tatu. Misipende kusikitika hata moja mtoto katikati yenu:

1. Minaona inje ya Kanisa, hii saa ya Liturgia Takatifu watoto beingine kucheza. Lakini hii kazi musifanye hata mara moja. Saa takatifu kabisa yetu ni hii saa ya Liturgia. Wa Malaika na wakubwa ya wa Malaika wanashuka na wanasaidia kila padri pa Meza Takatifu ndani ya Altari ya Mungu. Na inapaswa watoto wote kuwa ndani ya Kanisa hii saa.

2. Minaona tena ndani ya Kanisa, hii saa ya Liturgia Takatifu, ya kama beingine watoto habasopoke muzuri, na beingine wanafanya makelele na wanauzi watoto weingine. Lakini mweye munasema ninyi. Hii ni moja mufano muzuri, kucheza watoto filani ndani ya Liturgia na ku Fumbo ya Takatifu Komonyo? Inapaswa, basi, kusimama na boka ukubwa na kusikia na pasopo mingi hii yote wimbo na ma somo wanaisoma mu Misa. Moja neno, ile anasema Padri ao shemasi ni hii: Tusikilize! Mweye munajua juu ya ninyi padri anatuwaambia? Juu ya kuanza sisi kumuomba kwa Mungu. Kama tunasikia hii neno, pasopo mingi, aipaswe kutoka akili yetu inje ya Kanisa.

3. Minaona tena ya kama Meza Takatifu inatayarishwa na inatowa Chakula ile ya mbingu, nikusema Mwili na Damu ya Kristu na padri anaita Waaminifu wote kukaribia, lakini Waaminifu wadogo wanakuja kupumunika. Hii mufano, watoto wangu, ni kazi ya kuzarau Bwana Yesu Kristu, Mwokozi wetu. Mu Kanisa tunaenda juu ya kupumunika. Ni kweli ya kama tutatayarisha ma roho yetu juu ya kubeba Takatifu Komonyo. Ku fundisho ingine tutasema namna gani inapaswa kutayarisha roho yetu. Sasa hapa inapaswa kubakia kwa akili yetu hii kintu moja: Ya kama tunaenda mu Misa kupewa Takatifu Komonyo. Itakuwa furaha mingi kama tunaweza kila mu Juma kubeba Takatifu Komonyo.

Mukona kuniuliza ulizo fulani yulu ya hii fundisho tunafanya sisi sasa?

(Hapa mwalimu atajibu ku maulizo ya watoto wake. Paka atasopoka kujibu muzuri na kweli, Nikusema hii ma sauti ataisema inapaswa kuwa mafundisho ya Kanisa yetu na hapana fundisho ya akili yake. Tena ataelezea kwa watoto wake namna gani watasimama mu Kanisa, namna gani watafanya alama ya musalaba, wakati gani watafanya hii alama ya musalaba, wakati gani tuinamisha ma kichwa yetu. Itakuwa muzuri hii fundisho mwalimu kuifanya kisha moja Liturgia Takatifu juu ya kukumbuka watoto hii yote Ibada na kisha atawaelezea muzuri).

## FUNDISHO YA SITA
## SAMWELI NABII NA MWAMUZI.

NAMNA YA KUKARIBIA

Mukona ona, watoto wangu, watu, wenye wanapika magochi yao mbele ya picha (Ikona) na wanaomba kwa Mungu na machozi? Mara wa mingi watu wekona mambo ya sikitiko wa mingi na wanakimbilia kwa Mungu. Ni muzuri kukumbuka na sisi Mungu. Wakati watu wanaomba kwa Mungu juu ya mambo yao ya nguvu, wanalaka kwa Mungu. Lakini sisi ni muzuri hapana kumulaka kwa Mungu, kwani iko namna hii malako yetu kwa Mungu itakuwa yulu ya ma nguvu yetu ao itakuwa malako umbafu ya bule.

Lakini iko na malako ya Waaminifu, ile ni ya kweli na wabarikiwa. Ni malako ubarikiwa tutasikia ku hii fundisho yetu leo.

HISTORIA. Tuko ile wakati ya Waamuzi ya Agano la Kale. Walikuwa wanaume, wenye Mungu aliwaita kuongoza Taifa yake, Israeli mu njia ukweli. Ile wakati taifa ya Israeli hasikukuwe na kanisa yake. Lakini walimwabudu wapi Mungu? Mu Hema ya Ushuhuda!

Ndivyo, ndani ya hii Hema ya Ushuhuda watu ya Ebrania walichunga kila kintu takatifu walikuwana yo toka hii mwendo yao kutoka ya Misiri na kufika ku inchi ya Palestina. Pale ndani ya hii Hema ilikuwa Sanduku ya Jipya (Masikilizano). Hii Hema ya Ushuhuda ilikuwa ma vipande ya mbili. Kipande ya kwanza iliitwa Matakatifu, pahali waliingia wa padri yao na fasi ya mbili iliyeitwa Vitu Vitakatifu, pahali waliingia paka wa askofu wao. Ile wakati sasa tunasema askofu alikuwa mutu moja aliyeitwa Ili.

Siku moja Ili alienda mu Misa yao juu ya kumwabudu Mungu na ndani ya hii Hema Takatifu aliona mwanamuke moja ya kupika chini magochi na kuomba kwa Mungu kwa siri.

E, alimuita, hapa unafanya ninyi? Ulilewa?

Hapana, yeye alimujibu, misikulewa. Minafanya sala. Minaacha nafsi yangu kufugula mbele ya Mungu na kumusema umivu yake.

Iwe mubarikiwa. Uende kwa amani. Hii matakio ukona yo Mungu atakuipatia.

Nani alikuwa huyu mwanamuke na nani ilikuwa umivu yake? Aliomba ninyi toka Mungu? Alikuwa bibi ya Elkana, mutu moja aliyekuwa padri ku muji Silo, nikusema ku hii fasi ilikuwa hii Hema ya Ushuhuda. Alikuwa mwaaminifu na mweshimiwa Anna. Ma saa wa mingi alikuwa chini na aliomba kwa Mungu. Na umivu yake ni nani? Hasikukuwe na watoto na alisikitika sana. Alionaka wanawake beingine na watoto kwa mikono yao na alipata huzuni ya roho yake. Tazama, basi, kintu ninyi aliomba toka Mungu.

Aliomba kwa Mungu kumupatia mtoto moja na yeye atakuwa mwanaume. Tena alimulaka ya kama, kama atamupatia moja mtoto mwanaume, atamupatia mu Kanisa yake. Vile alimwambia:

Ee Mungu wangu, huyu mtoto atakuwa yako, kama utanipatia.

Mitakurudisha Kwako.

Imani yake ilikuwa ngapi munene? Sala yake ilikuwa nguvu na ilifika kwa masikio ya Mungu. Na Mungu alimujibu, ndivyo! Hii matakio aliomba Anna na bwana wake Elkana ilitimizwa. Hasikuchelewe kukuja mtoto moja mwanaume. Ilikuwa moja muujiza ya ajaabu mbele ya ma macho yao. Na hawa wanajua ya kama hana wenye stahili ya hii muujiza. Na, wakati ilikuja saa kumupatia jina, walimuita Samweli. Maana yake ni hii: Niliomba toka Mungu na alinipatia.

Wakati tena huyu Samweli alikuwa mtoto mudogo, baba yake Elkanas na bibi yake Anna walienda pamoja ku muji Silo juu ya kutoa kwa Mungu sandaka.

Lakini Anna, bibi yake alikatala, na alimwambia:

Uende weye. Mimi mitabakia hapa. Wakati mtoto yetu atakomea na atasimama kukunywa mazimba hii wakati tutaenda pamoja. Elkanas aliichika kwa sababu alijua ya kama bibi yake ni mwaaminifu kwa Mungu na hii saa alitaka kuonyesha moja mapenzi ya Mungu.

Wakati Samweli alikuwa miaka ya tatu, Anna alikamata mupango kutimiza malako yake. Huyu mtoto ya muujiza eko mtoto mwenye inapaswa mutatoa kwa Mungu. Alitayarisha na bwana yake, alibeba bile bintu ataitoa kwa Mungu ku hii sandaka ya muji Silo, pahali ilikuwa Hema ya Ushuhuda na fasi, pahali walimwabudu Mungu ukweli. Lakini na Anna alibeba na yeye ma zawandi yake kama bintu ya hii sandaka kwa Mungu. Lakini ile bintu walikuwa ninyi? Walikuwa ma mwana ya ngombe. Kweli moja alikuwa moja mwana ya ngombe na mwingine alikuwa mtoto yake Samweli. Aliisha kumusaidia ya kukomea muzuri na sasa eko tayari kumutoa kwa Mungu kutimiza malako yake. Vile wote pamoja: Elkanas, Anna, Samweli, mtoto wao waliondoka ku hii safari.

Wakati walifika kwa Hema Takatifu ya Ushuhuda, walipatia ma zawandi wao. Na kisha ilikuja hii saa ya kutoa na mukubwa zawandi wao, nikusema mtoto wao. Anna alikaribia askofu ya hii mwaka, aliyeitwa Ilia na alimwambia:

Mimi ni huyu mwanamuke uliniona kukuja hapa ya zamani na miliomba kwa Mungu na machozi. Mungu alinipatia hii kintu milimuomba. Tazama, ni hii matunda ya maombi yangu. Hana tangu sasa mtoto yetu. Ni mtoto ya Mungu. Minamutoa kwa Mungu juu ya kumutumia Mungu ma siku yake yote. . .

Askofu Ilia alikamata kwa mikono yake huyu mtoto Samweli. Tangu hii saa atakomea kama mtoto ya Mungu karibu ya Hema ya Ushuhuda juu ya kutumika kwa Mungu siku ingine, wakati atakomea. Saa ya kutoka ilikuja. Huyu mama na bwana yake habaonekane na taambu kwa uso yao, ile saa walitoka. Invers. Anna aliisha kujaza na furaha mingi na mwangaza ilizambalishwa kwa uso yake na aliimba moja muzuri wimbo. Na hii wimbo alimutukuza Mungu vile: «Ee Bwana, hana mwingine Mtakatifu, sawa Weye, uliye wa pekee na musiyezambi. . . «

Munataka kusikia namna gani alipita huyu mtoto Samweli karibu ya hii Fasi Takatifu ya Taifa ya Israeli? Yeye alikuwa moja mtoto mutumishi ya Mungu. Alikomea na boka mingi mbele ya

Mungu na alifanya kila kazi alimwambia askofu Ilia. Nikusema, sawa sisi tunasema leo, alikuwa mtoto ya Altari Takatifu. Aliachana ya watoto weingine. Tena aliachana mbele ya watoto ya askofu Ilia, wenye habasimame muzuri ndani ya Kanisa yao na habakuwa na heshima na boka ya Mungu ndani ya hii Fasi yao Takatifu. Watoto ya Ilia, hii saa yeye alitoa sandaka kwa Mungu, wale walienda karibu, walibeba nyama, waliipika na waliikula na mucheko na kelele. Samweli aliona wale watoto, wenye walikuwa na moja mufano mubaya, na wakati alikomea tena, alifokea hawa watoto na baba yao, mwenye alionanaka hii kibego ya watoto yake na alivumilia bila kuwafokea na kuwasauria.

Busiku moja, huyu kijana Samweli alipumuzika karibu ya hii Hema ya Ushuhuda, kiloko mbali ya chumba ya askofu Ilia. Kisha saa kiloko alilamuka mbio na tetemeko. Alisikia sauti moja, ilimwambia hivi:

Ee Samweli, Samweli! . . .

Nani anamuita? Bila shaka alikuwa Ilia. Alilamuka na alikimbia kwa askofu Ilia.

Oti, mimi ni huku. Unanitaka ninyi?

Ilia alisikia ya kama mambo ingine ya ajaabu ilifanyikwa na alimwambia Samweli kurudia mu chumba yake kupumuzika. Haina mambo.

Kisha saa kiloko mara ya mbili, ya tatu alimuita moja sauti. Ilikuwa hii sauti umoja na alimuita hivi:

Ee Samweli! Samweli!

Hii sauti ya fasi ngani ilikujaka? Alilamuka huyu kijana na alikimbia mara ingine kwa mukubwa Ilia. Na yule Ilia alimutuma kupumuzika mara ingine. Lakini mara ya tatu alisikia hii sauti ya ajaabu.

Samweli alisikia hii mara ya kama ilikuwa sauti ya Mungu, mwenye alimuita kuanza afanye tendo Yake. Hivi Samweli alimujibu:

Sema, ee Bwana, na mutumishi wako anasikia kila sauti utamwambia.

Alilamuka na mukubwa Ilia. Vile na yeye alielezea hii jabo. Kweli,

ilikuwa muito ya Mungu. Mungu aliita mutumishi mwaminifu yake Samweli mu kazi ya Nabii. Moja tendo munene tangu hii saa ataanza kumaliza Samweli juu ya wokovu ya Taifa yake.

Tangu hii jabo, ilipita wakati ya miaka 20. Askofu Ilia aliisha kufa.

Mungu alimulipiza juu ya kibego ya watoto wake. Pole-pole taifa ya Israeli aliepuka toka imani ya Mungu ukweli. Bila moja mutu mukubwa alianguka taifa muzima kwa mikono ya wa adui yake. Wa Adui yao, walikuwa wa Filistei, wenye waliwauzi daima Taifa ya Israeli. Wa askari ya Israeli habaweze kuwafukuza wa adui wao na walipata ma hatari na mambo wa mingi. Hema ya Ushuhuda iliisha kuharabika na wa Adui wao walikamata Sanduku ya Masikilizano. . . Tena watu ya Israeli habasikitike kwa sababu walipotesha bintu Takatifu yao na habaweze sasa kumwabudu Mungu wao. Waliisha kuacha imani na kuwabudu Mungu wao ukweli na walianza kuwabudu ma sanamu.

Kisha mateso wa mingi toka taifa ya WaFilistei, watu wa mingi toka Taifa ya Israeli walianza kukumbuka Ndini na uzima yao ya zamani karibu kwa Mungu wao. Ilikuwa hatari kuishi miaka wa mingi kama watumwa ya wa Filistei. Walitafuta mutu moja kama mukubwa yao, mwenye atawaokoa, sawa vile waliokolewa zamani na ma hatari ingine.

Na mukubwa alikuwa Samweli. Huyu mutu alichunga Mungu juu ya hii saa ya hatari ya Taifa yake. Samweli na baraka ya Mungu alikamata hii tendo kulinzi taifa ya Israeli. Tendo yake ya kwanza ilikuwa hii: Aliita watu wote ya taifa yake na kama Nabi ya Mungu aliwaambia:

Kama mweye wote mutaacha wa mungu wa wongo na mutarudia kwa Mungu wetu ukweli, Yeye atatuokoa.

Kisha aliita wakubwa wote ya kila kabila yao na wakubwa ya kila jamaa munene yao. Ndani ya kiwanja Masifari ilifanyikwa hii makusanyo yao. Pale walisikia wote ma hamuri ya mukubwa mupya yao, aliyemutuma Mungu. Walikuja bila ma bunduki. Mukubwa yao, Samweli aliwaambia kutubu na aliwalaka ya kama yeye alimuomba kwa Mungu juu ya uzima na wokovu wao.

Na kitubio ya watu ilikuja. Hii kiwanja ya Masifari ilitetemeka toka kitubio nguvu yao, wenye walisemaka: «Tulikosana, tulikosana mingi» Tuliepuka toka  Mungu ya wokovu wetu na tulienda kwa wa mungu ya wongo.

Kitubio yao ilikuwa ukweli. Hii kiwanja ilimwanga na machozi ya hii taifa. Walianza na kifungo ya chakula na walimuomba kwa Mungo sana.  Samweli alikamata tendo ya Mwamuzi. Yeye alihukumu kila mambo ya taifa ya Israeli.

Saa moja, wakati watu wote walikuwa kwa hii fasi Masifari, walisikia moja kelele. Mambo gani ilikuwa?   Mutu moja aliita nguvu: Wa Filistei!  Wanakuja wa Filistei! . . .

Watu ya Israeli walitetemeka. Walikuwa bila ma bunduki. Namna gani sasa watakombana wa adui wao?   Walikujaka wa Filistei ya mukongo kuwakombana.

Mutu mukubwa yao, Samweli, aliwaambia kufanya kimya na aliwaambia: Kweli ni ya kama sisi tuko huku bila ma bunduki, lakini tukona musaidizi yetu Mungu Mwenyezi. Basi, tuende sisi wote mbio kwa Mungu.

Watu ya hii taifa muzima waliomba kwa Mungu. Walianza kupaza sauti na kusema kwa Mungu juu ya kuwaokoa. Kabisa mingi aliomba Samweli. Na muujiza asikuchelewe kufanyika. Kisha saa kiloko wa Filistei walianza kukimbia mukongo juu ya kuokolewa. Hata ma uso yao habapindule mukongo.

Lakini, ju ya ninyi?   Mungu alisikia ma sala ya Taifa Yake. Ku mbingu ilianza kupika umeme na kogoloma. Ilinyesha nvula mingi. Ilianza kunyanyula pepo mingi na wa Filistei waliogopa sana na walianza kukimbia.  Mukongo yao walianza kuwafukuza watu ya Israeli. Hawa sasa walikuwa washindi na saidio ya Mungu. . .

MAELEZEO. Ulizo: Mutu nani mukubwa tuliona ku hii fundisho yetu leo?

Jibu: Tulisikia juu ya Samweli, mwana ya Anna na baba yake Elkanas.

Ulizo: Namna gani Mungu alimuita?

Jibu: Busiku moja alisikia mara ya ine sauti ya jina yake. Mungu alimuita.  Ulizo: Ndivyo. Mungu anasaidia watu wake, lakini namna gani alilinzi taifa yake?

Jibu: Alituma Samweli na aliita watu ku Kitubio.

Ulizo: Na wakati walipata mambo ya hatari toka wa Filistei, namna gani Mungu aliwaokoa?

Jibu: Alisikia sala yao.

Ulizo: Nikusema, namna gani walikimbia wa Filistei?

Jibu: Mungu alileta tetemeko ya inchi na kogolomo na umeme na wa adui wao walikimbia, bila kuuzi taifa ya Mungu.

FUNDISHO: Mungu analindi watu wake.

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Basi, Bwana anajua namna gani kuokoa watawa katika majaribu. . .  « (Barua ya Mbili ya Mut. Petro 2, 9)

MATENDO KU UZIMA YETU. Tukona lazima ya ulinzi. Munaweza kuniambia wakati gani mutu anaomba saidio ya Mungu:

Kwa mufano, kama inanyesha nvula mutu moja ekona lazima kuikala chini ya moja nyumba, moja mufuniko juu ya kujilinda ya nvula.

Kama Jua inaleta kivukutu mingi na grade inafika yulu ya hesabu 40, mutu anatafuta fasi ya baridi ao mutoni ao bahari kunawa juu ya baridi.

Kama anafukuza mutu moja mwingine, yeye anatafuta fasi ya kuokolewa.

Ku wakati ya nvita mashasi wa mingi inaanguka chini mutu moja ataenda ku fasi moja juu ya kuokoa mwili yake.

Munaisha kusema mambo ya mingi, watoto wangu. Iko na ingine. Mbele ya kila hatari tukona lazima kulinda uzima na mwili yetu.

Watoto wadogo wekona hatari. Walinzi wao weko wazazi wao. Kila mama anakamata ku mikono yake mtoto yake juu ya kumulinzi. Na baba ni musaidizi juu ya kila mambo ya mtoto yake. Lakini yulu yao mulinzi mukubwa ni Mungu. Yeye anatupenda kweli kuliko ya watu weingine kwa sababu Yeye ekona nguvu kupita mingi.

Namna gani anatulinzi? Wakati ingine anatuma Malaika yake, wakati ingine huyu Malaika anayetulinzi daima, sawa wanalinzi watu wakubwa kundi moja ya wa askari. Wakati ingine anakuja huyu Mungu mumoja kutusaidia.

Tukona Mungu Baba wetu. Lakini tunamusikia hivi? Kama tunamusikia paka kazi moja inapaswa kufanya: Kuacha uzima yetu, nyumba yetu, na wazazi na jerani yetu na inchi yetu chini ya ulinzi wake.

Watoto wangu, ma michi wadogo juu ya kukomea muzuri na kunioloka yulu watu wanaweka karibu yao muti moja kama nguzo juu ya kuisaidia hii muchi kiloko, wakati pepo ni nguvu. Na mweye muko ma michi wadogo. Wanapumuzi ma pepo nguvu, pepo ya zambi. Wanakuja pembeni yenu watu mabaya kama nyama ya pori na wanataka kuharabisdha hii muzuri uzima yenu. Basi, mweye muache uzima yenu kwa mikono ya Mungu. Yeye atamilinzi na nguvu ya musalaba yake. Atamilinzi ndani ya lupango ya Kanisa yake.

Musiogope! Karibu yenu ni Mungu kama Mulinzi, Baba na Musaidizi yenu.

Nani anataka sasa kutukumbuka hii fundisho yetu ya leo? (. . . ) Mungu analinzi watu wake.

## FUNDISHO YA SABA
## MTAKATIFU YOANE MURAHIMU

NAMNA YA KUKARIBIA.

Sisi wote tukona, watoto wangu, jina moja na jina ingine ya mbili. Ndani ya Kanisa yetu tukona Watakatifu, wenye walichunga

ma jina yao kwa ajili ya ma fazila yao. Moja Mtakatifu na uzima yake leo tutasema ekona jina Yoane, na jina ya mbili Murahimu. Sasa mutasikia juu ya ninyi alibeba hii jina ya mbili.

HISTORIA. Ku mwaka 550, kisha ya kuzaliwa Bwana Yesu mu Kisanga Kipros aliishi mukubwa moja aliyeitwa Epifanios na bibi yake Kosmia, mwenye kweli alipabwa na mafazila ya mingi.

Ndani ya hii nyumba alizaliwa mtoto yao Yoane. Mu nyumba yake alikuwa na bintu wote. Tena alikuwa na mafundisho ya Mungu kizuri juu ya kutumika muzuri mu dunia, wakati atakomea huyu mtoto.

Wakati alikomea Yoane, wazazi wake walipata binti moja na walimundoa na huyu binti. Wote walizania ya kama pamoja na yeye ataishi moja uzima wa heri na kizuri, lakini ingine ilikuwa

mapenzi ya Mungu. Alimuongolea moja taambu munene juu ya kupima imani yake. Ndani ya wakati kiloko, ilikuja lufu na alibeba bibi yake na wote watoto wake. Yoane hasikushake mbele ya Mungu ju ya hii mateso yake. Roho yake ilibakia muzuri na kisha lufu ya watu ya jamaa yake.

Yoane alipotea watoto yake, lakini Mungu alimupatia nguvu kusaidia binti moja, aliyemupenda sana. Huyu binti alimufamia, wakati Yoane alikuwa miaka 15. Hii mwaka busiku moja aliona ku ndoto yake moja vision. Aliona moja bintu na uso yake muzuri na mwanagaza mingi, na pa kichwa yake alikuwa na moja taji ya mayani. Huyu binti alitembea na mwendo muzuri na alikuja na alisimamaa mbele ya Yoane. Yoane alilamuka na alitetemeka. Lakini, na wakati alilamuka aliendelea kuona huyu binti muzuri. Yoane alifanya alama ya musalaba na alimuuliza na boka kiloko:

Nani uko? Ni nani jina yako? Toka fasi gani unakuja na unataka ninyi hii busiku hapa?

Na huyu binti na uso ya utulivu na upole na sauti nguvu alimujibu:

Mimi milizaliwa pa hii inchi. Niko mtoto ya kwanza ya Mufalme mukubwa ya Mbingu. Mimi milishuka Mwana wa Mungu hapa chini ya Inchi. Kama utanipenda, mitakubeba na mabawa yangu na mitakupeleka mbele ya Kiti ya Mungu. . .

Na ni ninyi jina yako? Alimuuliza mara ingine Yoane.

Wananiita Huruma.

Yoane alianguka shini na alimusujudu. Lakini, wakati alilamuka, huyu binti, mwenye mbingu aliisha kutoka.

Huyu Huruma alitumika nguvu Yoane. Lakini namna gani? Ile miaka, watoto wangu, Kiti ya Askofu mukubwa ya muji Aleksandria ya Misiri, ilikuwa wazi. Taifa ya Mungu alitakia kuchakula moja askofu mtakatifu. Huyu Yoane alikuwa kweli mtakatifu na tangazo ya ma fazila yake walifika toka Kipros mu muji Aleksandria. Watu wote waliisha kujua ya kama huyu Yoane alikuwa mutu ya akili na mufazili. Wote walimupenda na walimuomba kukuja kama askofu yao ku muji Aleksandria ya Misiri.

Siku moja watu wote waliongolea hii chombo italeta Yoane ku muji yao. Wote walimupenda kufanyika Baba na askofu yao. Paka moja hasikupende kufanyika askofu. Na huyu nani alikuwa? Alikuwa huyu mmoja Yoane. Kwani alikuwa munyenyekevu, hasikutake kusikia hii mambo. Alijua kintu gani ukubwa na nguvu sana ni hii cheo ya askofu na hii mambo alifuchamwa. Yeye hasikupende ma cheo na masifu, lakini watu ya taifa alimutafuta na alimupata.

Bila kupenda yeye, walimuongoza kwa muji Aliksandria na walimufanyisia askofu yao.

Tangu hii siku alifanyika askofu, hasikusimame hata kiloko. Aliangalia kusaidia watoto wa roho yake juu ya kila mambo yao. Ya kwanza alisubuka juu ya imani ya Waaminifu yake. Ku muji Aleksandria daima walionekana mafundisho ya wongo na waliharabisha fundisho ukweli ya Kanisa ya Kristu. Ku miaka ya Mt. Athanasios alikuwa moja padri, aliyeitwa Arios, mwenye alisandiki ya wongo. Na ku miaka ya Yoane mwenye Murahimu ilikuwa fundisho ya wongo toka askofu moja aliyeitwa Petros Knafeas. Huyu Petros alisandiki ninyi? Yeye aliisha kugeuza Wimbo Trisagion, hii: Mungu Mutakatifu, mweza Mutakatifu, musiyekufa mutakatifu, utuhurumie». Yeye aliisha kuongeza mafundisho ingine ya wongo. Patriarhi Yoane alikombana kutosha na kuzimisha hii fundisho ya wongo kwa hii fasi yake. Wakati alifanyika askofu ma kanisa wa mingi walikuwa na watu ya wongo, na wakati alikufa, karibu wote ma Kanisa walikuwa kwa mikono ya wa Orthodoksi.

Patriarhi Yoane alionyesha mapendo yake hapana paka juu ya uzima ya roho ya Waaminifu yake, lakini kabisa juu ya wa masikizi na wale ya mateso. Aliisha kusikia ya kama ma jamaa wa mingi waliteswa ku muji yake. Na alitumika nguvu juu ya kuwasaidia.

Siku moja, wakati alifanyika baba wao, aliita wa padri wote ya njimbo yake na aliwaambia hivi:

Mutaenda kutafuta ku muji yetu na mutaniletea hapa ma jina ya wote watoto ya mfalme.

Wapadri walishangaa na walimuuliza: Na wa nani weko hawa watoto ya mfalme ya muji yetu? Sisi tunajua ku muji yetu wakubwa weko wa ngapi na wanaikala wapi, lakini watoto ya mfalme weko paka ku muji kapitala Konstantinopoli na hapana hapa.

Mtakatifu Yoane aliwalezea hivi:

Kila mutu masikini na bunji na mwenye njaala na mugonjwa mimi minamuona kama mtoto ya Malme ya mbingu.

Na walienda wa padri wake ku muji yao na walitafuta na walipata watu wa mateso na masikini na wote walikuwa 7500. Hawa wote watu Mt. Yoane aliwasaidia sana. Alifanya ninyi? Alijenga ma nyumba ya watoto wenye yatima, obitalo ya wagonjwa, ma nyumba ya wageni na ingine ma nyumba ya kuachana. Alijenga muji muzima juu ya kuikala wamasikini wake. Juu ya kupata makuta kuwapatia chakula yao alifanya ninyi? Aliuza ma chombo 13 na ile walipeleka daima machakula kwa watu wa masikini na wa mateso. Kila mutu masikini alipata mapendo na wema toka Murahimu Patriarhi mukubwa. Kila mutu aliyekuwa na ndeni, alipata makuta paka kwa huyu Mt. Yoane. Watu wote aliwasaidia. Tena na wale watu, wenye habakukuwe wa Kristiani. Alifungula ma bawa ya mapendo yake na alipokelea watumwa na wenye ya bilonda, wenye walikimbilia ku muji Aleksandria toka nvita. Tena alisaidia na watumwa wote na alikombana kuwauhuru. Aliishi paka ya kusaidia watu weingine. Yeye lakini aliishi kama masikini kabisa. Wakati alikuwa mu Kisanga Kipros alikuwa mtoto ya wazazi watajiri sana, lakini sasa kama Patriarhi aliishi kama masikini sana. Yeye mwenyewe alichakula hii njia ya mateso na masikini.

Siku moja alimutembelea mutu moja mutajiri. Alishagaa, wakati aliona pa kitanda ya Patriarhi moja nguo karibu ya kuharabika. Alitoka mbio na alienda mu soko. Aliuza moja nguo upya ingine ya kitanda yake na aliitoa kwa Patriarhi juu ya kufunikwa busiku. Patriarhi aliipokelea zawandi ya yule mutu, lakini hasikuweze kuitumia. Watu wamasikini wa mingi walisikia baridi na yeye atafunikwa na hii nguo nguvu? Siku ingine asubui aliituma na mutu moja mu soko na aliiuzisha. Alibeba makuta na aliuza manguo ya kitanda juu ya waaminifu wa masikini yake. Aliona huyu mutu mutajiri, aliyeiuza na aliimupatia hii nguo mu soko. Aliiuza mara ya mbili na alimuletea kwa Patriarhi. Na patriarhi mara ingine aliipeleka mu soko na aliiuzisha. Mutajiri aliiuza mara ya tatu na alimupatia kwa Patriarhi. Na mucheko alimwambia kwa huyu mutu mutajiri:

Tutaangalia nani ya sisi wa mbili atachoka mimi, mwenye minaiuzisha hii nguo, ao weye, unayeiuza mara ingine?

Vile, watoto wangu, aliishi patriarhi Yoane. Aliishi paka ju ya kupenda na kusaidia wamasikini wanduku wake. Tangazo ya matendo yake iliisha kuzambalala ma fasi yote mpaka na mu kapitala Konstantinupoli.

Ile wakati mfalme pale alikuwa Iraklios, mwenye alipenda kufamia huyu patriarhi Yoane. Alimuita kukuja ku muji Konstantinopoli.

Mt. Yoane na chombo moja aliondoka kumukutana mfalme. Wakati alienda kumukutana, moja mwingine mfalme alimuita. Alikuwa mfalme ya mbingu. Wakati chombo ilitembea mu bahari karibu ya kisanga Rodos, Yoane aliona moja ndoto kwa musigishi yake. Aliona moja kijana na mavazi mweupe na uso ya mwangaza mingi, aliyemwambia:

Ee Yoane, kuja, usichelewe. Mfalme ya wafalme anakuita. Kuja, usichelewe!

Alilamuka Yoane mwenye Murahimu. Alisikia ya kama inakaribia mwisho ya uzima yake. Alisimama safari yake. Alirudia kwa Kisanga Kipros, kwa hii fasi alizaliwa na pale aliacha nafsi yake. Ilikuwa tarehe ya 12 Mwezi ya kumi na moja. Kanisa yetu alimupatia hii jina ya mbili: « Murehemu». MAELEZEO. Ulizo: Ni nani, watoto wangu, hii jina ya mbili ya huyu Patriarhi?

Jibu: Murehemu. Ni Mtakatifu Yoane murehemu.

Ulizo: Juu ya ninyi Kanisa yetu alimupatia hii jina?

Jibu: Kwa sababu, wakati alikuwa askofu ku muji Aleksandria ya Misiri, alisaidia wa masikini na wote watu ya mateso.

Ulizo: Mukumbukeni aliona ninyi, wakati alikuwa na kipimo miaka 15?

Jibu: Aliona binti moja aliyeitwa Huruma. Yeye alikuwa binti ya kwanza ya Mfalme ya mbingu.

Ulizo: Sisi tunaweza kupenda hii binti, aliyeitwa Huruma?

JIbu: Ndivyo, kama ni namna ya kuachana tunasaidia wa nduku weingine wetu.

FUNDISHO: Kusaidia weingine watu.

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Heri wenye rehema: maana wao watapata rehema» (Matayo 5, 7).

MATENDO YA UZIMA YETU. Iko kintu moja na ye mutu moja anaweza kupanda yulu na kushuka?

Avion! Ni kweli. Na hii kintu tunapanda yulu na tunashuka.

Na Huruma ni sawa moja avion ya roho, inayepanda na inashuka. Nani alibeba Mungu toka yulu ya mbingu na alimuletea ku inchi yetu, katikati yetu?

Huruma. Mungu na mapendo na wema mingi alipokelea kushuka katikati yetu na kupanda pa musalaba.

Na nani alipanda Kristu pa musalaba?

Huruma. Juu ya kusaidia watu Yeye alipanda pa Musalaba yake.

Kama Kristu anatupatia moja huruma ukubwa kabisa ya kila ingine huruma, nikusema anatupatia Mwili na Damu yake, sisi inapaswa kufanya ninyi mbele ya wa nduku wetu?

Bintu ya mbili wanafika mara moja, watoto wangu, ku Kiti ya Mungu mu mbingu: Sala na huruma. Kama tunaifanya katika sheria ya Mungu.

Leo iko watu, wenye wanateswa na wekona lazima ya saidio wetu?

Ma siku yote ya hii dunia watakuwa watu, wenye watakuwa masikini na ya mateso ya kuachana.

Munaweza kuniambia ma jeshi ya kuachana ya wale watu?

Weko watu, wenye habakuwa na chakula kukula. Tunasikia ya kama watoto ma elfu ya mingi wanafariki hapa mu Afrika na Azia na ma fasi ingine.

Weko wagonjwa, wenye wekona lazima ya matunzo na lazima ya ndawa, damu na kila utulivu na saidio.

Weko watoto, wenye wekona moja fulani umivu mu nyumba yao na wekona lazima ya saidio yetu.

Weko watu, wenye habakuwa na makuta kuripa hii nyumba wanaikala.

Weko watu, wenye wanaisha bila nyumba ndani ya moja hema.

Ndivyo, watoto wangu, weko wa jeshi wa mingi ya watu, wenye wanateshwa.

Paka huyu mutu anafunga ma macho yake hasiweze kuona maumivu pembeni yake. Yule mutu, aliyeekona ma macho, na roho na masikio yake wazi, ataweza kusikia na kuona kila siku mateso ngani na ngapi wekona wanduku wetu. Inapaswa basi kuonyesha mapendo yake na matendo na hapana paka na ma sauti yake. Munaichika ao hapana?

Ndivyo. Tunataka kusaidia, lakini sisi hatunana kintu. Hatunana makuta wetu.

Ni kweli. Hamunana mweye, lakini wekona wazazi wenu. Mweye mutawaambia kusaidia. Nyumba moja inayefanya matendo ya huruma shetani hasiweze kuiuzi. Vile anatufundisha Mtak. Yoane Krisostomo.

Na tena moja ingine sauti: Leo muko wadogo watoto, lakini kesho mutakomea. Pasopo. Musitumike paka ya makuta na furaha yenu. Mupendeni huruma na wa nduku wa masikini na wagonjwa. Watu wafarisayuo walitosha 1/10 na aliipatia kwa masikini. Lakini sisi aipaswe kupatia na kuliko mingi saidio kwa wanduku wetu ya mateso?

Tendo ninyi ingine munaweza kuifanya?

Huruma haina paka makuta. Huruma ni mapendo kwa kila mambo ya kila mutu na nduku wetu. Nikusema inapaswa kufanya kila siku matendo ya mapendo kwa wa nduku wetu.

## FUNDISHO YA MNANE
## MUTAKATIFU EKATERINI

***NAMNA YA KUKARIBIA***

Inamipendeza, watoto wangu, kusikia juu ya nvita? Leo tutasuburia juu ya nvita, iliyefanyikwa hapana na kisu na bunduki ao mukuki, lakini na lunrimi. Ni nvita ya neno ya filosofie.

Munashangaa kwa hii nvita. Lakini kama mutasikia wa nani weko wa adui, kweli mutaajabu na itazaliwa mafa ndani ya akili yenu ya kufundisha hii nvita. Basi, moja jeshi walikuwa wanaume mia moja na makumi Tani (150), wenye walikuwa wahubiri wakubwa mu filosofie, akili yao ilikuwa nguvu sana.

Jeshi ingine ilikuwa moja mwanamuke, mwenye alikombana wanaume 150, lakini namna gani? Anaweza mwanamuke moja kukombana kontre ya 150 wanaume? Lakini, ni kweli, watoto wangu, ya kama huyu mwanamuke alikombana na alishinda wanaume wa filosofe ku mazungumuzo. Na kisha alifanya ninyi? Mitamielezea ku mwisho ya hii fundisho. Mbele sasa mitamiambia nani ilikuwa huyu mwanamuke.

HISTORIA. Jina yake mukona kusikia yote mweye. Aliitwa Ekaterini, mwenye Kanisa yetu inamukumbuka kama Mutakatifu, mu tarehe ku 25 Mwezi ya Kumi na moja. Tunamufamia kama mtakatifu, lakini hasikukuwe tangu mwanzo mtakatifu. Alizaliwa ya wazazi wapagano ile wakati zamani walitawala wafalme wa pangano ya Roma karibu ku mwaka 300, kisha kuzaliwa ya Yesu Kristu. Baba yake alikuwa mukubwa ku muji Aleksandria ya Misiri na alizala paka huyu binti na alikangamana kumupatia kila fundisho muzuri juu ya kufanyika ku uzima yake na huyu mukubwa.

Ekaterini alikuwa na uso muzuri na akili nguvu. Hasikukuwe mwingine binti hata na uso muzuri kabisa, sawa huyu binti Ekaterini ku muji Aleksandria ile wakati, tena na mwenye akili kabisa na kuliko na mwingine mwanamuke. Alifunda ile wakati filosofie, medecine, rhetorique, poesie.

Muwaze, watoto wangu, watu wa ngapi walistaajabu huyu binti ku muji yake! Alikuwana ma bintu ya ine: Mwili na uso kizuri, fundisho na akili mingi, mali mingi na utukufu. Watu wote walimustaajabu na walimutamaa. Na mama yake alitaka na haraka kumuondoa.

Mama wangu, yeye alimwambia, miye misitake kuowa. Inanipendeza kabisa mafundisho na seans. Kama unasema na weye na watu wote ya kama niko na ma zawandi ya mingi, basi, mitaowa paka kama mitapata moja mwanaume, mwenye atakuwa na na yeye hii ma zawandi nikona na miye. Nikusema, huyu, mwenye mitamuowa inapaswa kuwa mwanaume mwenye akili, mutajiri kuliko mimi, kwa uso yake kupita muzuri ya miye na mutukufu kupita miye.

Lakini namna gani atajipata mutu moja sawa alisema Ekaterini?

Siku moja Ekaterini alienda kwa mutawa moja, aliyeishi mu jangwa.

Hasikukuwe tena mukristu, alikuwa mupagano, lakini aliisha kusikia juu ya huyu mutawa ya jangwa. Ku mwanzo aliende kumuona na kumufamia, juu ya kusikia ma sauti yake.

Mutawa ya jangwa, wakati alimuona, alisikia hii zawandi alikuwa na ya Mungu na ya kama huyu binti atafanyikwa mukristu. Kwa hivi alimwambia:

Sikia mtoto wangu. Mimi mitakuambia moja Bwana-Arusi, mwenye ni kupita muzuri ya weye, kupita mwenye akili, kupita mutukufu ya weye na kupita mutagiri ya weye. . .

Kweli, eko moja Bwana-Arusi hivi? Alimuuliza Ekaterini. Basi, nani eko huyu? Ni nani iko jina yake? Namna gani miye mitaweza kumufamia?

Kweli, unaweza kumuona. Miye mitakumuonyesha. . .

Eko hapa karibu? Minataka sana kumuona!

Ongolea kiloko. . .

Alichofa kiloko huyu mutawa. Aliingia mu nyumba yake. Kisha alikuja mara ingine inje na alikamata na moja picha (Ikona) kwa mikono yake.

Tazama! Huyu ni Bwana-Arusi, Mwenye mimi milikuambia. Kama utasandiki Kwake na utamupenda sana, Yeye atafanyika Bwana-Arusi yako.

Uniseme, juu ya huyu Mwanaume! Alimwambia Ekaterini na mafa mingi.

Mutawa ya Kristu alianza kumufundisha juu ya Bwana Yesu Kristu.

Alimufundisha mafundisho yake, alimufundisha juu ya miujiza Yake na sandaka yake pa musalaba kwa wokovu ya watu wote ya dunia.

Ekaterini alisikia hii sauti yake yote na pasopo mingi. Ndani yake iliwaakisha nuru moja na ilimwangaza. Alisikia juu ya Huyu Bwana-Arusi na roho yake ilifurahi sana. Iliwaakisha ndani ya matakio juu ya kufanyika yeye Bibi-arusi yake.

Sikia, mtoto wangu, alimwambia huyu mutawa. Kama unataka kufanyika

Bibi-arusi ya Kristu, utakangamana kupendeza paka kwa huyu Bwana-Arusi yako. Utafanya kila mapenzi Yeye anapenda, kwani Yeye ni kuliko muzuri kabisa Bwana-Arusi ya dunia muzima.

Hii mapatano ya Ekaterini pamoja na huyu Mutawa ilikuwa ubarikiwa. Tangu hii siku ilizaliwa na ilikomea ndani yake matakio na mapendo mingi juu ya Huyu Bwana-Arusi. Alisikia ya kama imani ya wa sanamu ilikuwa ya wongo na ya kama Yesu Kristu alikuwa kuliko yulu ya kila kintu ya hii dunia. Alisandiki, basi na yote roho yake.

Hii busiku ya kwanza alisandiki na alikamata mupango kuishi sawa vile anataka Yesu Kristu na aliona ndoto moja. Aliona Mzazi-Mungu Maria, mwenye alionyesha na kilole yake Mwana wake Yesu Kristu kwa Ekaterini na alimwambia:

Mwana wangu, pokea huyu binti.

Kisha ilionekana ya kama Yesu Kristu alimubariki Ekaterini. Hii tangazo ya kama Ekaterini alifanyikwa mukristu ilizambalishwa kama kogoloma ndani ya muji Aleksandria.

Ya kwanza alisikia hii tangazo baba yake, aliyekuwa mupagano.

Alisikitika sana. Aliongolea kutegeneza mambo ya uzima ya mtoto yake na namna ingine na kumupatia moja mwanaume, mtoto ya mfalme ya Roma. Lakini Ekaterini hasikupende kusikia hata kiloko juu ya bile bintu ya hii dunia:

mali, utukufu na ingine. Ndani yake sasa paka moja ilikuwa utukufu: Kuishi pamoja na Bwana Yesu Kristu. Anataka kumupatia kwa mikono yake uzima yote yake.

Hii tangazo yakama alifanyikwa mukristu alisikia na mfalme Maksentios.

Alitaambu sana. Alikuwa na majivuno, kama mfalme, ya kama ataweza kugeuza mufano ya Ekaterini na kurudisha akili yake kwa imani ya sanamu.

Ile wakati mfalme alienda ku muji Aleksandria pamoja na bibi yake Fafsta. Kazi yake ya kwanza ilikuwa kufukuza wa Kristiani na moja ufukuzo makari.

Juu ya kupima mufano ya Ekaterini alitegeneza shangilio mbele ya wa sanamu ya muji Aleksandria. Inje ya kanisa ya pagano walisanyikwa wapagano wote wapadri na waaminifu wao. Walitoa ma sandaka mbele ya ma sanamu wamungu wao ya wongo. Wakati wapadri wa magano walikuwa tayari kutoa sandaka mbele ya ma sanamu wao, aliingia Ekaterini ndani ya kanisa yao. Wakati walimuona, walizania ya kama alikuwa kama mtoto ya mukubwa ya hii muji juu ya kuomba mbele ya wamungu wao. Lakini yeye, wakati aliingia, alinioloka kwa askofu pagano yao. Alianza na nguvu mingi kumuhukumu na alimufundisha ya kama Mungu ukweli ni moja, Bwana Yesu Kristu.

Hii mafundisho yenu juu ya wa mungu wa mingi, ni ma sanamu. Wamungu wenu weko ya wongo! , Alimwambia na sauti nguvu Ekaterini.

Munaweza kusikia, watoto wangu, haya ngapi walisikia hii saa wale wapadri na askofu wao, wakati moja binti na miaka 17 aliwaambia hii ma sauti yake. Katikati yao alikuwa na mfalme Maksentios, mwenye alisikitika na alishirika sana. Aliwaza mingi juu ya kupata namna moja kugeuza Ekaterini ku imani yake ya zamani.

Ya kwanza alituma wa askari yake na walileta mbele yake watu ya akili na wa filosofe toka muji Aleksandria. Walifika 150 wanaume watu wa akili. Aliwaambia kusuburia na mtoto Ekaterini juu ya kugeuza mufano na imani yake.

Nvita ilianza. Iko hii nvita milimiambia ku mwanzo ya fundisho yetu.

Mfalme alisikia hii mazungumuzo yao. Alianza kusuburia naye moja filosofe, aliyekuwa kuliko mukubwa ya weingine. Alisema ma sauti wa mingi. Wakati aliisha, alianza kusema sasa Ekaterini. Na mafundisho muzuri aliwaambia ya kama ndini yao ni ya wongo na ya kama Mungu na Mwokozi ya dunia muzima na Bwana Yesu Kristu. Lunrimi yake ilikuwa sawa kisu, kwa sababu alimwangaza Roho Mutakatifu. Watu wa akili habakuweze kupata hata moja kosa kwa mafundisho na ma sauti yake.

Wakati alipotesha hii nvita yule mufilosofe ya kwanza, nani sasa atapata nguvu kusuburia na huyu mtoto Ekaterini? Kama yule ya kwanza alishindwa, watafanya ninyi weingine wanafunji wake? Waliikala na kinywa yao wazi na walisikia mafundisho ya Ekaterini. Ku mwisho wote waliichika kosa yao kwa imani yao na walimuamini ku imani ya Yesu Kristu. Hii ilikuwa moja ukubwa ushindi ya Ekaterini, ao kuliko kusema ilikuwa moja ushindi ya Bwana Yesu Kristu. Walisandiki kwa Kristu 150 watu wa akili. Mfalme alishirika sana na kama nyama ya pori alifanya. Alikamata mupango kuwaakisha moto munene na ndani yake watatupa wale wafilosofe, wenye walimuamini Kristu. Kisha saa kiloko wote wakubwa watu ya akili ya hii muji walikuwa Washahindi ya Kristu. Vile wale walienda kuliko mbio ya Ekaterini mu Paradizo, karibu ya Kristu, mwenye walimukikisha mbele ya watu wa mingi.

Kisha hii sikitiko alibeba mfalme Maksentios, aliwaza kukokota na namna ingine Ekaterini. Alianza na ma sauti yake ya butamu.

Mtoto wangu, Ekaterini, hauone ngapi uko mwenye akili na muzuri! Minataambu uso yako muzuri, ma zawandi yako, ma miaka ya kijana yako. Kuja! Toa sandaka kwa wa mungu wetu na mimi mitakusifu na masifu wanene.

Hapana, ee mfalme, alimujibu Ekaterini. Mabintu na malako yako yote misiipende. Kama unaniambia juu ya mwili na uso yangu muzuri, minajua ya kama siku moja itafumbala na itaharabika. Mimi ni mukristu. Bwana-Arusi wangu ni Yesu Kristu. Minataka kupendeza kwa Kristu. Kwa Kristu minataka kutoa yote bintu na zawandi na uzima yangu. Fanya basi, weye, kila kazi unawaza.

Hii saa mfalme alikamata hamuri ingine. Walimupika na kisha walimutupa ndani ya buloko. Walipasuka mwili yake na damu ilitoshwa mingi ya ma bilonda yake. Vile na ma bilonda mingi walimutupa mara ingine ndani ya buloko.

Ekaterini ndani ya buloko alimutukuza Mungu, kwa sababu alimustahili kuteswa kwa Jina yake. Lakini na ndani ya hii buloko hasisimame kufundisha mafundisho ya Kristu kwa wale walikuwa mu buloko.

Siku moja walifungula mulango ya buloko. Aliona ninyi! Mbele yake alikuja bibi ya mfalme. Alistaajabu Ekaterini. Anataka ninyi hapa ndani bibi ya mfalme? Lakini, mbele ya kumuuliza, aliona huyu mwanamuke na machozi ku macho yake kuomba baraka ya Mtakatifu Ekaterini. Bibi ya mfalme Fafsta aliisha kusandiki kwa Kristu. Iliisha kumufundisha mufano ya Mt. Ekaterini. Na sasa alikuja kubeba baraka yake, kwa sababu aliisha kukamata mupango kuishi ao kukufa, sawa vile anapenda Mungu.

Wakati alisikia bwana yake, mfalme, hasikuwaze ya kama alikuwa bibi yake, alihamuru mara moja kukata kichwa yake.

Basi, kisha lufu ya wale 150 watu wa akili alitoa uzima yake kwa Kristu na bibi ya mfalme, Fafsta. Kisha Fafsta alikufa na mateso ya kuachana na mukubwa ya wa askari Porfirios pamoja na wa askari wake 200. Hawa wote walisandiki kwa kuhubiri ya Ekaterini na walitukuzwa kwa milele. Kanisa yetu inashangilia makumbusho wao hii siku pamoja na Mt. Ekaterini, mu tarehe 25 Mwezi ya kumi na moja.

Ku mwisho ya wote washahindi alikufa na mateso mingi Ekaterini. Na hamuri ya mfalme walikuja wa askari wake na walikata kichwa yake. MAELEZEO:

Ulizo: Juu ya mwanamuke nani tulifundisha leo, watoto wangu?

Jibu: Juu ya Mt. Ekaterini. Ulizo: Mukumbukeni ma zawandi wa ngapi alikuwa huyu binti?

Jibu: Alikuwa mwenye muzuri sana, mutajiri kabisa, mwenye akili na mutukufu kabisa.

Ulizo: Nikusema alikuwa na ma zawandi wakubwa ya hii dunia. Lakini alimuchakula nani kama Bwana-Arusi yake?

Jibu: Bwana Yesu Kristu.

Ulizo: Tangu hii siku alimufamia, alikamata mupango kufanya ninyi ku uzima yake mbele ya Kristu?

Jibu: Kukangamana kupendezwa kwa Kristu. Alimupenda hata mingi, na hasikufanye hata kazi moja, iliyehasikupende Kristu. Ulizo: Na hii mapendo yake alimuongoza wapi?

Jibu: Ku mateso na lufu. Alikufa na yeye na pamoja na yeye na weingine walikufa.

Ulizo: Kanisa yetu inamuita Mushahindi mukubwa. Tena inapaswa kujua ya kama Mwili yake iko yulu ya mulima Sinaya, pahali ni Monasteri yake. Muweze kuniambia fundisho gani tutabeba leo?

FUNDISHO: Hii kazi inapendeza kwa Kristu, hii mitafanya na mimi. SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Kama ningependeza watu, singekuwa mutumwa wa Kristo» (WaGalatia 1, 10).

MATENDO KU UZIMA YETU. Beingine watoto wanauliza:

Mitafanya ninyi juu ya kuwa mukristiani muzuri?
Jibu ni hii: Utafanya hii kintu anapenda Kristu, hii kintu inapendeza kwa Kristu.

Yeye mumoja alisema: Kama munipende, mutatimiza mahamuri yangu.

Kama unapanda mutu moja, haupende hata mara moja kumusikitika. Na sisi,

kama tunapenda Kristu, hatupende hata siku moja kukanyanga mafundisho na hamuri yake, kwa sababu Yeye atatuzarau. Vile alifanya na Bwana Yesu. Alikuja katikati yetu hapana kupendeza ku maugu yake (WaRoma 15, 3), lakini kupendeza mbele ya Baba Mungu wake. Na hasikufanye kintu moja juu ya maugu yake, lakini alifanya yoyote paka kwa sisi. Alisulubiwa kwa sisi. Alifufuka kwa sisi, juu ya kututukuza. Namna gani sasa sisi tutaweza hii Uso Takatifu ya Kristu tutaisikitika?

Ekaterini ku wimbo-Apolitikion yake anaitwa: « Bibi-Arusi ya Kristu».

Hii inatuwambia ya kama aliisha kupenda mingi Yesu Kristu. Na nafsi yetu ni bibi-arusi ya Kristu. Iko kwake. Yeye aliiuza na damu yake. Sasa nafsi yetu hasiweze kufanya kila kintu na mapenzi yake na kukatala mapenzi ya Kristu, mukubwa na Muumba na Mwokozi yake.

Lakini, munaweza, kunisema, watu wa mingi wanafanya ninyi leo?

Wanapendeza kwa Kristu ao ku moja fasi na uso ingine? Wanafata mahamuri ya Kristu ao wanafata mapenzi ya watu weingine?

Watu weingine wanategeneza mwili na uso yao na namna kizuri.

Inawapendeza kuvaa na kutembea muzuri.

Hii zwezo tunaiona kuliko kwa watoto wanawake. Wekona mapendo ya maugu na mwili yao.

Ndivyo, wanasimama mbele ya rikalasi na wanaona ma uso na ma nywele na mwili yao. Ni kweli na lazima ya kama haipaswe sisi kuacha mwili yetu na buchafu. Hapana. Lakini haina muzuri kuishi paka ya kutegeneza ma nywele na mwili yetu kila siku. Hii mapendo ya mwili yetu ni kintu moja umbafu, kwa sababu hii vema ya mwili na uso yetu inafubala na inaharabika. Kama hakuna vema kwa nafsi na roho yetu, utaifanya ninyi hii vema ya mwili na uso yako? Agano la Kale anatuwambia ya kama, kama mutu moja, mwenye nikona buchafu mu nafsi yake na inje ku mwili yake anapambwa na bintu ya mingi, yeye anafanana kama moja ngurumbe pahali pa pua yake waliweka moja kintu ya risikio (boucle d oreilles).

Lakini, ni paka mapendo ya mwili yetu?

Hapana, ni na mapendo ya watu. Nikusema watu wa mingi wanakombana kutegeneza maugu yao juu ya kupendezwa kwa watu weingine. Wanawaza, watasema ninyi watu weingine. Atasema ninyi dunia.

Munaweza kuniambia matendo filani sisi tunafanya juu ya kupendezwa hapana kwa Kristu, lakini kwa watu ya hii dunia?

Kwa mufano, mara ingine tunasikia haya kufanya alama ya musalaba, kama tunapita inje ya Kanisa moja, kwa sababu tunawaza ya kama watacheka watu weingine ao watatuchokoza.

Tunavala manguo ao tunaimba wimbo hapana hii mavazi na wimbo Mungu anapenda.

Ndivyo, inafanyikwa na hii mambo. Watoto wa mingi wanakatala kufata ma zwezo ya Mungu na wanakombana kufata ma zwezo ya warafiki wao.

Lakini inapaswa kusopoka sasa mingi. Ya kwanza tutaangalia bintu wa mbili: Ya kwanza ni hii: Ni ninyi ikona kadiri kuliko mingi: Mwili ao nafsi yetu?

Nafsi yetu.

Basi, inapaswa kupamba nafsi yetu na mawa ya kila fazila, kwa sababu hii mawa habafumbale. Na haipaswe kuwaza juu ya mapambo ya mwili yetu, kwani hakuna kadiri kwa ile. Uwa nani ikona kadiri ukubwa hii iko ya inchi yetu ao hii inafanyikwa ku moja fabrica? Ni kweli, ya kama hii inaota toka inchi. Basi, wakati mtoto moja ni mupole na mubikira, ni moja uwa nature na inatosha harufu ya fazila yake. Lakini, wakati weingine watoto wanakomea na wanaangalia namna gani watapambwa na bintu ya bule, hii zwezo yao inatuonyesha ya kama wale watoto walipotesha vema nature ya mwili na uso yao na walifanyikwa mawa artificiel.

Na hii ni ulizo yangu ya mbili: Nani anatupenda kupita Kristu ao dunia?

Kweli, anatupenda Kristu, kwa sababu Yeye alisulubiwa kwa wokovu wetu.
E, basi, sisi kwa Kristu inapaswa kupendeza. Kristu anasema ninyi sisi kuangalia kuliko? Hii tutafanyia. Tutafunga ma macho yetu mbele ya kila sauti ya watu ya hii dunia, kabisa wakati wale watu weko wanaishi bila imani na boka ya Mungu.

Moja mwanafunji anamuogopa na anamusifu mwalimu yake kwa sababu yeye atamupatia cheo (note) ku masomo yake. Na sisi tutaangalia Kristu na mafundisho na mapenzi yake. Yeye anatupatia note kila siku. Basi, nani anataka kutukumbuka hii fundisho tutabeba leo ku yote uzima yetu? (. . . )

## FUNDISHO YA TISA
## MUTAKATIFU SPIRIDON

NAMNA YA KUKARIBIA.

Inchi Grekia ikona ma kisanga wa mingi. Ku fasi ya mashariki, karibu ya bahari ya Palestina ni moja kisanga inayeitwa Kipros, pahali wanaikala wagreki. Hii kisanga ni takatifu, kwa sababu waliishi katikati ya miaka tangu mwanzo ya uzima ya Kristu mpaka sasa yulu ya 500 Watakatifu. Katikati yao eko na Mutakatifu Spiridon.

HISTORIA. Mtakatifu Spiridon aliishi mu Kisanga Kipros karibu ku mwaka 350. Wazazi wake walikuwa wachungaji ya ma kondoo. Na mtoto wao Spiridon alikomea katikati ya ma nyama na ma nyumba yao. Wakati alikuwa mtoto aliendа na ma kondoo ma shamba na alicheza na baragumu yake. Alisikia furaha mingi kwa agili ya hii kazi yake. Watu wote walimupenda, kwa sababu aliachana ya wachungaji weingine. Alikuwa mupole na munyenyekevu kwa roho yake. Ku uso yake ilijifatula heshima na boka yake mbele ya Mungu. Alikuwa nafsi mwema. Alikuwa picha ya kila fazila. Alikuwa mufano muzuri ya watu wote ya hii njimbo yake. Wakati alikomea, aliowa na alifanya moja jamaa muzuri na ma fazila ya Kristu.

Lakini hasikuikale daima ku hii kazi kama muchungaji huyu kijana Spiridon. Siku moja aliacha kundi ya ma nyama yake na sikitiko mingi. Aliacha hii kundi juu ya kwenda ku moja ingine kundi. Namna gani? Musikieni.

Tangazo ya uzima takatifu yake ilizambalisha fasi yote ya inchi yake.

Hasikukuwe mutu ya akili, kwa sababu hasikuwende ku masomo ya kufunda fundisho ya kuachana, lakini watu wote walimufamia sawa mutu mtakatifu na mufano ya utakaso. Wakati alifariki askofu ya Mitropolia Trimithunta ya Kipros, Waaminifu wote na wa padri wote waliomba kufanyika askofu wao, huyu Spiridon. Tena alikuja ku ii fasi yeye alichunga ma kondoo yake na walimwambia hii mupango ya Waaminifu wote.

Hii mupango ya watu ilikuwa ya ajaabu kwa Spiridon. Namna gani ilikuwa namna huyu muchungaji, kufanyika padri na askofu? Ya kwanza alibishana, lakini ku mwisho hasikuweze kukatala. Mungu mumoja alimuita kuchunga taifa Yake. Basi, Spiridon alimutii kwa Mungu na alipokelea kufanyika Baba mukubwa ya njimbo Trimithunta.

Mtakatifu Spiridon kama askofu alitumika na mapendo mingi juu ya Kundi ya Waaminifu wake. Kwa uso yake Wakristiani kila siku waliona Baba wao mupendwa, mwenye kila siku na busiku alitumika kuwasaidia. Tena aliona moja mutakatifu muzima, moja mutakatifu mwenye muujiza. Mt. Spiridon na unyenyekevu na imani yake ukubwa na utakaso yake ukweli alistahiliwa toka Mungu kufanya miujiza. Uzima yake ilijaza na miujiza ya kuachana.

Musikieni beingine miujiza yake:

Siku moja alifanyia Liturgia takatifu mu Kanisa ya muji yake. Waaminifu wa mingi walisikia hii Ibada. Ku saa moja ilikamata watu wote moja boka. Walipika magochi chini na waliria. Waliisha

kuona ninyi? Ndani ya Altari Takatifu, mbele ya Meza takatifu alikuwa Mt. Spiridon. Hii saa alikuja inje ya Mulangu Mukubwa na alisema: « Amani kwa wote», hii saa watu walisikia ma sauti ya wa malaika, wenye waliimba na walisema: «Na kwa roho yako». Na mara moja waliona na ma macho yao moja jeshi muzima ya wa Malaika, wenye waliluka pembeni ya Meza Takatifu na waliimba pamoja na Mt. Spiridon. Lakini ilikuwa paka hii mambo ya ajaabu? Tena waliona ya kama Mt. Spiridon hasikutembee ku inchi. Aliisha kupanda yulu ya inchi, sawa aliluka. Alikuwa kama ndeke.

Hii muujiza ya ajaabu inatukumbuka na wimbo- Apolikion. Tazama, inasema ninyi: « Na wakati uliimba maombi yako, ulikuwa wa Malaika wasaidizi wako, ee Mtakatifu. . . «

Munataka kusikia na ingine muujiza ya Mt. Spiridon? Wakati moja alilofa ya mujii yake. Ile wakati alifariki binti yake wa pekee. Alikuwa moja binti ubikira na mufazili. Wakati alirudia Mtakatifu na alisikia hii mambo alisikitika sana na aliomba juu ya wokovu ya nafsi yake. Mtoto yake Irini, aliyekufa aliisha kufuchika feza moja ya moja mwanamuke mwingine, mwenye aliisha kumupatia juu ya kuichunga. Hasikujue hata mutu moja fasi gani aliiweka hii makuta mtoto yake Irini. Yule mwanamuke aliria juu ya sikitiko yake. Alisikia hii mambo baba yake. Alienda mu kaburi yake na sawa alisuburia na yeye mwenye muzima, alimuuliza:

Mtoto wangu Irini, fasi wapi ulifuchika hii makuta ya yule mwanamuke masikini?
Na hii dakika alisikia toka kaburi sauti yake, aliyemujibu hivi:

Baba wangu, hii makuta yake nikona yo mu fasi fulani. . .
Na kweli walienda pale, aliwaambia mtoto yake na walipata hii makuta ya yule mwanamuke.

Musikieni sasa na moja ingine jabo ya uzima ya Mt. Spiridon, inatuonyesha unyenyekevu yake. Wakati moja alipata malari mfalme ya Konstantinopoli Konstantios, mwana ya Mt. Konstantinos. Hata moja mungaga asikuweze lumutunza. Hii wakati alisikia mfalme hii miujiza alifanya mt. Spiridon, na alimuita kufika kwake. Mt. Spiridon alibeba pamoja na moja mwanaume kijana na alienda mu nyumba ya mfalme. Wakati mt. Spiridon alikarimbia mulango ya nyumba ya mfalme, mutumishi aliyechunga hii mulango, wakati alimuona, alizania ya kama huyu padri alikuwa moja mutawa ya bule na ya hii mambo alimupika na kofi moja ku uso yake. Mt. Spiridon asikushirike. Alifanya hii sauti Yesu Kristu anatuwaambia. Alipindula na ingine fasi ya uso yake juu ya kumupika na ku hii fasi ingine. Unyenyekevu yake alimushangaa huyu mutumishi. Tena, wakati alisikia ya kama huyu mutu alikuwa Mt. Spiridon, alianguka chini ku mbele yake na alimuomba hurumia.

Lakini, watoto wangu, bado kumiambia na moja mukubwa muujiza ya Mt.

Spiridon. Mukujeni yote na pasopo yenu mingi juu ya kuisikia. Tuko ndani ya moja kanisa ukubwa. Katikati ya hii kanisa anaikala mfalme Konstantinos Mukubwa na pembeni yake wa mingi waaskofu na wapadri. Hii maonekano ilikuwa ya furaha mingi. Wa mingi ya wale wa askofu waliishi hii wakati ya ufukuzo ya mwisho na waliisha kuteswa na namna ya mingi. Kwa askofu moja kwa mufano waliisha kumukata pua, kwa mwingine waliisha kumutosha ma macho yake, kwa mwingine mwili yake ilikuwa na ma bilonda ya mingi. Wa nani walikuwa hawa wote? Walikuwa wa Padri wakubwa 318 ya Makutano Ikumenike ya Kwanza ku mwaka 325, kisha ya kuzaliwa Bwana Yesu. Ku saa moja ilianza mazungumuzo nguvu. Ndani ya hii Makutano walikuwa ma kundi wa mbili. Kundi munene kupita ilikuwa ile ya wa Padri wakubwa Watakatifu wetu, na ingine kundi ilikuwa ya moja mukubwa mupadri ya fundisho ya wongo, aliyeitwa Arios. Yeye alionekana inje moja mutu wa akili mingi na muhubiri mukubwa, lakini alikuwa na mafundisho ya shetani. Yeye alihubiri na alisandiki ya kama Kristu ni kiumbe ya Mungu na hana Mungu. Nikusema yeye hasikusandiki kwa Utatu Mutakatifu.

Wa Padri Watakatifu walishangaa, wakati walisikia hii sauti ya mupadri moja. Walifunga masikio yao. Wale walikuwa na akili na fundisho kuliko mingi walianza kukombana kontre yake. Mukubwa mutheologo alionekana Mt. Athanasios, shemasi ile wakati ya Kanisa ya Aleksandria.

Na hekima yake alimushinda padri ya wongo Arios. Lakini huyu Arios alikuwa na ndani yake shetani. Kisha saa kiloko waliona wa padri wote kulamuka ya kiti yake moja mupole askofu, aliyekwenda karibu ya Arios. Yeye alikuwa mt. Spiridon. Lakini alitaka ninyi huyu musiyeakili katikati ya hii mazungumuzo nguvu ya theologie? Lakini na yeye alikuwa na kumupatia kwa Arios jibu moja. Alifanya ninyi? Alibeba moja matafari kwa mkono yake.

Alimwambia kwa Arios: Uliona hii matafari? Ni moja, lakini mara moja na ya bintu ya tatu. Mara moja alifanya alama ya musalaba na alisema:

Kwa Jina ya Baba na ya Mwana na ya Roho Mtakatifu. . . Na wakati aliisha hii sauti ya Utatu Mutakatifu hii matafari ilichanishwa. Wakati, nikusema, alisema: « Kwa jina ya Baba. . «moja lunrimi ya moto ilipanda mbinguni. Wakati alisema: « Na ya Mwana» ilianguka chini maji na wakati alisema: na ya Roho Mutakatifu. . « ilibakia kwa mkono yake bulongo.

Hii muujiza, watoto wangu, ilifanya ajaabu mingi kwa wa Padri wote ya hii Makutano. WaPadri wa Orthodoksi walimutukuza Mungu, mwenye hii saa ya nguvu kwa hii nvita ya imani ya Utatu Mutakatifu alifanya hii muujiza na alionyesha na namna bila shaka ya kama Mungu ni Moja na wa Tatu ma Uso. Arios, kisha hii muujiza, alipata haya mingi.

Makumbusho ya Mtakatifu Spiridon Kanisa yetu inashangilia kila mwaka mu tarehe ya 12 Mwezi ya kumi na mbili.

MAELEZEO:

Ulizo: Miujiza wa nani ya Mt. Spiridon sisi leo tulisema?

Jibu: Alifanya Liturgia takatifu pamoja na wa Malaika na alisuburia kwa binti yake Irini, mwenye kufa na alichana hii matafari kwa bintu yake ya tatu. Ulizo: Muujiza nani ikona maana nguvu na ikona kadiri mingi?

Jibu: Hii muujiza aliifanya ndani ya Makutano Ikumenike ya Kwanza.

Ulizo: Alitaka kuonyesha ninyi na hii muujiza?

Jibu: Ya kama Mungu ni moja, lakini na ma Uso ya Tatu. Ni na ma Uso ya Tatu: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

FUNDISHO: Ninasandiki kwa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, Utatu wa asili moja na usiyotengana.

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Neema ya Bwana Yesu Kristo, na mapendo ya Mungu, na ushirika wa Roho Mutakatifu ukae pamoja nanyi wote» (Barua ya mbili kwa wa Korinto 13, 14).

MATENDO KU UZIMA YETU. Ma neno ya hii Sauti ya Madiko Takatifu sisi tunaisikia kila mu Juma mu Kanisa yetu. Ni baraka ya Utatu Mutakatifu. Ndani ya Kanisa tunaishi Neema ya Kristu, aliyeeko Uso ya mbili ya Utatu Mutakatifu. Tunaishi mapendo ya Mungu, aliyeeko Uso ya kwanza na aliyetupenda sana Huyu Baba Mungu wetu, kwani Mwana wake wa pekee, alimupatia sadaka kwa wokovu wetu. Tena tunaishi Ushirika ya Roho Mutakatifu.

Imani yetu inafanana kama moja «polieleos», nikusema hii kintu munene ni katikati ya kanisa yetu na ikona ma kandilia ya mingi ao moto ilectrique ya mingi. Hii monyororo inaikamata ikona ma pete wadogo ya mingi. Sasa muwaze, kama moja pete itapasuka, yote Polieleos itaanguka na itapasuka. Na Kanisa yetu Takatifu inafanana kama moja Polieleos. Inajikamata ya moja monyororo, inayeikona ma pete wa mingi. Na hii pete ya hi monyororo ya kwanza ni hii fundisho ya Utatu Mutakatifu, ya kama nikusema, Mungu ni Moja na ma Uso ya Tatu: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Hii fundisho ukweli mbele ya kufika Kristu mu dunia, wale watu waliishi habakuijue kabisa muzuri. Kristu wetu, mwenye ni Uso ya mbili ya Utatu Mutakatifu, Yule alitufunua hii fundisho ukweli. Mara wa mingi alitufundisha hii sauti ukweli yake. Lakini weko na watu sawa zamani

Arios, wenye habasandiki kwa Utatu Mutakatifu. Hawa weko Kundi ya Yehova ao wanaitwa na Washuhuda ya Yehova. Hawa wanaharabisha ma sauti ya Madiko Takatifu na vile wanafundisha watu na fundisho ya wongo na gehena.

Mweye, watoto wangu, inapaswa kusoma Madiko Takatifu juu ya kuweza kujibu kwa hawa watu ya shetani. Na tazama sasa! Mufungule Agano Jipya na mara moja mutasoma ma vipande ya mbili, ile munaweza kuikumbuka. Moja kipande ni ku shairi ya mwisho ya Evangelion katika Matayo na ingine ni shairi ya kwanza katika Evangelion ya Yoane. (Hapa mwalimu atafungula Agano Jipya yake na atatafuta hii ma shairi na ataisoma).

Kwani sisi tuko wa Orthodoksi tunasandiki kwa Utatu Mutakatifu. Na mweye, wakati munafanya ma sala yenu ku mwisho mutaweza kusema kwa Mungu na hii sala: « Ee Utatu Mutakatifu, okoa watu ya dunia muzima».

## FUNDISHO YA KUMI
## MUTAKATIFU ELEFTHERIOS

NAMNA YA KUKARIBIA

Munajua, watoto wangu ni nani kuliko nguvu moja nyama ya pori makari sana?

Simba. Ndivyo, huyu nyama ni mfalme ya wa nyamba beingine.

Minazania ya kama mukona ona ma simba ao hapana? Watoto wa mingi ya mweye muliona ma simba ndani ya ma kitabu yenu, na weingine waliona ndani ya Television.

Namna gani anaitwa, watoto wangu, huyu mutu, mwenye anakamata na anashinda ma nyama ya makari?

Mwenye kukamata na kushinda ma nyama. Mu lugha kigreki: Thiriodamastis.

Ku Historia ya Kanisa yetu munajua mweye mutu moja, mwenye walimuheshimiwa ma simba? Minazania ya kama hamujue. Leo, basi mimi mitamionyesha nani alikuwa yule mutu.

HISTORIA. Tuko ile wakati Kristianisme ilifukuzwa toka wafalme ya Roma.

Kuliko walifukuzwa wakubwa wapadri ya Kanisa yetu.

Ile wakati, mu muji Roma mukubwa ya Italia alizaliwa na alipita miaka wadogo wake Mushahindi ya hii fundisho yetu ya leo, mwenye anaitwa Eleftherios. Ku miaka wadogo yake alipotesha baba yake na mama yake aliyeitwa Anthia, alikuwa mwaminifu na alisubuka kusaidia mtoto yake juu ya kukomea na moha fundisho ya Kristu. Matakio yake ilikuwa kutoa mtoto yake mu Kanisa ya Kristu. Ndani ya roho ya mtoto yake alipanda matakio takatifu wa mingi.

Alikuwa na kipimo yake Eleftherios miaka 15 na kwa agili ya ma fazila yake walimufamia watu wote ya hii kundi ya wa Kristiani ya muji Roma. Yeye alikuwa moja kitumaini ndani ya Kanisa ya Kristu, iliyefukuzwa sana. Siku moja aliingia ndani ya moja katakombe, pahali alikuwa askofu Anikitos, mwenye alimuuliza: Mtoto wangu, unataka ninyi?

Minataka kufanyika padri, alimujibu mtoto Eleftherios. Minataka kutumika mu Kanisa ya Kristu.

Unataka kutumika mu Kanisa yetu, lakini uliwaza muzuri? Leo padri ni kama mushahindi. Utateswa juu ya imani yetu. Ulikamata hii mupango kuteswa?

Ndivyo, ee Mtakatifu ya Mungu, alimujibu mtoto, lakini na toka ma macho yake walitelemusha machozi.

Hii ilikuwa matakio na mawazo ya huyu mtoto Eleftherios. Kufanyika padri. Na hii matakio yake Mungu alimustahili kuitimiza. Mtakatifu askofu Anikitos, kwani aliona ma fazila na mapendo ya huyu mukristu kijana alimupandirisha shemasi na padri. Upandirisho yake ilifanyikwa ndani ya moja katakombe ya Roma. Watu wa Kristiani walifuraha sana wakati waliona mkono ya muzee askofu kuiweka pa kichwa ya kijana Eleftherios na kumupatia cheo ya padri ya Kanisa ya Kristu. . .

Hasikupitishe wakati mingi na ilikuwa lazima Eleftherios kufanyika askofu. Na kweli alipandirisha askofu juu ya kutumika mu Kanisa ya Ilirikon, nikusema leo ku muji Avlona ya

Albania. Alitumika na mapendo mingi huyu kijana askofu. Matakio yake ilikuwa ya kukokota watu wote ya njimbo yake ku imani ya Kristu. Kuhubiri yake ilikuwa na moto mingi ya mapendo ya Kristu. Iko muzuri sasa kuangalia namna gani yeye alifanya moja kuhubiri.

Kanisa iliyala ya watu wa mingi. Pa kiti yake anaikala askofu

Eleftherios, mwenye anahubiri. Watu wote wanasopoka kinywa yake. Mara moja ilifanyikwa moja kelele katikati ya waaminifu. Watu wote walipindula ma kichwa yao kuangalia mambo gani ilifanyikwa. Ma askari beingine na mukubwa yao aliyeitwa Filikas walipomona milango ya hii Kanisa na waliingia ndani ile saa alihubiri askofu Eleftherios.

Halafu, walitaka ninyi? Mfalme aliwatuma juu ya kukamata askofu na kumufunga na kumupeleka ku muji Roma. Wa Kristiani walisikia mara moja mambo gani itafanyikwa na walisikitika sana. Beingine waliria, kwa sababu watapotea muchungaji na baba wao. Wa askari walikaribia. Askofu alisimama kiloko kuhubiri yake na alianza mara ingine na nguvu kupita kuhubiri. Wa askari walifika kumukamata na monyororo kumupeleka mu Roma. Lakini huyu askofu na kuhubiri yake aliwakamata na monyororo ya kuhubiri yake na aliwaongoza kwa imani ya Kristu. Mukubwa aliweka upanga mu fasi yake. Alisimama na alisikia ma sauti ya askofu. Wakati aliisha kuhubiri, huyu mukubwa Filikas alimukaribia na alimufunua juu ya ninyi alikuja kwake. Alitubu na aliomba hurumia. Na yeye alifanyikwa mukristu na aliajaabu uzima ya askopfu Eleftherios. Lakini hamuri ya mfalme ya Roma imalizwa. Vile Askofu na Filikas waliondoka kutembea mu Roma.

Sasa tuko mu kapitala Roma. Mbele ya mfalme kijana askofu anasema bila shaka na anakikisha bila boka imani yake kwa Kristu.

Ndivyo. Minamwabudu Kristu na minahukumu mweye, kwa sababu Mungu alimipatia akili lakini mweye munaabudu ma sanamu. Hii zambi ngapi ni munene! Lakini mimi minamwabudu Mungu ukweli, Rabi Kristu.

Mupango ya mfalme hasikuchelewe kufika. Mt. Eleftherios alihukumwa kukufa na mateso mingi. Ile mateso walimufanyisia iko wa mingi. Hatunana wakati ya kusema yote. Paka mitamiambia beingine.

Busiku ya kwanza alilala pa moja kitanda ya ajaabu. Hasikulale.

Walimularisha pa moja kitanda juu ya kumwua. Walileta kitanda moja ya shaba, chini yake waliakisha moto na wakati hii kitanda ya metale shaba ilifanyika nyekunda, walilarisha yulu yake mt. Eleftherios. Mfalme alizania ya kama mwili ya kijana askofu italugua toka hii moto nguvu na mateso yake itakuwa na umivu mingi. Lakini askofu kijana hasikupate hata mambo kiloko. Hii muujiza na beingine walifundisha wa pagano kuamini kwa Kristu na ku fundisho ukweli yake. Moja, katikati yao alikuwa na askari Koremon, mwenye, wakati aliona hii miujiza Mungu aliifanya na aliokoa mutumishi yake Eleftherios, alimusandiki kwa Kristu na alibatiziwa mukristu. Sasa mfalme alishirika kupita mingi. Mbele ya askofu kijana alihamuru kukata kichwa ya mukubwa wa askari Koremon. Na kweli, huyu aliyefukuza watumishi ya Mungu, sasa yeye alitoa uzima yake kama sadaka kwa Mungu ukweli. Hii siku Kanisa yetu inashangilia makumbusho ya Mt. Eleftherios inashangilia na Mushahidi Mt. Koremon.

Sawa tulisema, watoto wangu, wa askari waliteswa sana Mt. Eleftherios, lakini Mungu alimuokoa ya kila mateso yake. Mitamielezea tena na moja ingine mateso yake. Mfalme alihamuru kumukamata na kumutupa ndani ya ma simba, wenye njaala. Kweli! Ndani ya theatre ya Roma siku moja walifika watu wa mingi. Walikuja kuangalia hii muchezo. Moja askofu ya wa Kristiani atakombana na ma simba wenye njaala. . . Ma kiti waliisha kujaza mbele ya wakati. Kisha saa moja waliongoza askofu kijana ndani ya hii kiwanja. Walifungula nyumba moja na walitosha inje ma simba ya mbili. Walikimbia mbio yulu ya huyu Mushahindi. Watu wote walikamata pumuzi wao.

Wanajua ya kama kisha saa kiloko hasitakuwe hata bilato yake.

Lakini mambo ninyi ya ajaabu sasa wanaiona? Ma simba wenye njalaa wanakarimbia askofu na wanasimama karibu yake. Wanasimama na heshima. Waliheshimiwa askofu ya Kanisa yetu.

Ku mwisho, watoto wangu, Eleftherios alikufa. Lakini namna gani? Mfalme alihamuru kukata kichwa yake. Kichwa uheshimiwa yake ilianguka chini na damu ilimwangisha bulongo ya hii inchi, lakini nafsi yake aliluka kwa Muumba ya dunia yote. Hasikupitishe saa mingi na karibu ya kichwa yake ilikuwa na kichwa moja ingine. Ilikuwa kichwa ya mama yake, Mt. Anthia, mwenye anashangilia Kanisa yetu hii tarehe ya 15 Mwezi ya kumi na mbili. Mama yake, wakati iliisha uzima ya mtoto yake, alipika magochi kubushu kichwa takatifu ya mtoto yake, lakini hii dakika moja askari alikata na kichwa yake. Mama na mtoto sasa weko Washahindi ya Kristu.

MAELEZEO- MATENDO YA UZIMA YETU

Leo tulisikia, watoto wangu, uzima ya moja kijana mukristu. Ndani ya roho yake, wakati alikuwa mtoto mudogo, ilikuwa moja matakio. Mukumbukeni matakio gani ilikuwa ndani yake? (. . . ) Matakio juu ya kufanyika padri ya Mungu. Na alifanyika padri na alitoa sadaka uzima yake kwa Mungu. Mukumbukeni wale ma simba wa mbili walifanya ninyi, wakati walimuona Mushahindi Eleftherios? (. . . ) Walimuheshimiwa kama mutumishi ya Mungu na hasikumulumize. Iko muzuri kusimama kwa hii maana ya mbili, watoto wangu. Nikusema tutasimama kuangalia maana ya hii ya mbili bintu yake: Matakio yake ku uzima ya upandri na hii heshima walionyesha ma simba mbele kwake. Ndani ya ma roho ya watoto ni matakio wa mingi. Mtoto moja anataka kufanyika mecanicien, mwingine anataka kufanyika mwalimu, mwingine kapita ya chombo ao ya shamba, mwingine avoka, mwingine mungaga, mwingine jemadari. . . Lakini leo weko watoto, wenye wanatakia kufanyika wapadri, watumishi ya Kanisa ya Mungu? Hakuna ingine matakio ukubwa kuliko mbele ya hii matakio ya kutumika kazi ya Mungu. Sisi tunamitakia na toka hii masomo yetu kuzalia hii matakio kwa roho hata ya moja mtoto juu ya kutumika kazi ya Mungu. Tunatakia Mungu kuwaakisha moto ya mapendo yake na kwa ma roho yenu juu, wakati mutakomea, mutatumika kama walimu, wapadri, Mitume na wa askofu ya Kanisa yetu. Na kama sisi beingine hatuweze kufanyika, inapaswa kusaidia wa nduku wetu weingine, kama wataonyesha hii matakio. Kama hakuna watoto toka ma jamaa ya Kristu juu ya kutumika mu Kanisa ya Kristu, fasi gani wapi tutatafuta watoto juu ya hii kazi?

Tena inapaswa kusopoka na ingine mambo. Ma simba ya mbili walimuheshimiwa askofu kijana. Lakini leo wanaishi katikati yetu na watu, wenye weko kupita mabaya na makari ya hii nyama ya pori, kwa sababu mufano yao mbele ya wa padri wetu ni na kibego na bila heshima na sifa. Wakati ya zamani alipita padri moja mu njia moja na wale watu waliikala pale walisimama juu ya heshima na sifa na walimubushu na mkono yake. Mweye, watoto wangu, muendelee kuheshimiwa wa padri wetu. Munaona padri moja, mutaenda mbio kubushu mkono yake, mutasikia ma sauria yake na mutamupenda. Na, kama munaona beingine watoto, wenye wanachokoza wa padri wetu, mweye mutawasauria ya kama inapaswa kuwaheshimiwa nguo mweusi yao. FUNDISHO: Heshima mu nguo mweusi ya wapadri wetu.

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Wazee wanaotawala vema wahesabiwe kustahili heshima mara mbili» (Barua ya kwanza ya Timotheo 5, 17).

(Kama hii fundisho watasikia na watoto wanawake mwalimu atafundisha kuliko mingi juu ya mama ya Mt. Eleftherios Anthia, mwenye alifurahi, wakati mtoto yake alifanyika padri na alikuwa na matakio ya kutumika kwa Kristu na kutoa sadaka uzima na mwili yake).

## FUNDISHO KUMI NA MOJA
## NDANI YA SADUKU MOJA YA KULISHA NYAMA

NAMNA YA KUKARIMBIA

Mu Mbulaya, watoto, sawa na mweye munajua baridi ni matata kabisa. Watu wote wanafanya kila kazi, kila namna juu ya kuleta kivukutu ma nyumba yao. Na mwili wao wanaifunika na

manguo ya nguvu, kwa sababu pale grade ya baridi inashuka chini ya zero (0). Sasa, muwaze mweye, kama mutalala inje busiku moja na baridi ni vile kuliko chini ya zero. . .  Mutakufa juu ya baridi mingi. Hii mambo ilifanyikwa ku moja jamaa. Sasa musikieni hii Historia.  HISTORIA. Zamani kabisa waliishi katikati ya hii dunia Mama mzazi-Mungu Maria na mulinzi yake Yosefu. Ile wakati ilipaswa kutembea toka Nazareti ku mukini Betelehemu, pahali alizaliwa Yosefu, juu ya kuandika ma jina yao mu kataloge ya inchi ya Roma.

Ile miaka aliongoza dunia muzima Kadiri ya Roma na mfalme alikuwa Oktavianos Avgustos. Huyu mfalme alikamata hamuri wote watu ya ufalme wake kutembea ku fasi ya mukini walizaliwa juu ya kuandika ma jina yao mu liste ya Inchi yake. Nikusema, yeye alitaka kujua watu ya ufalme wake walikuwa ngapi, juu ya kuweka palata kwao. Hamuri yake ilimalizwa. Vile na Yosefu anakuja ku mukini Betelehemu. Lakini hapana paka yeye. Watu wa elfu ya mingi walisanyikwa kwa hii mukini udogo. Yosefu na mtoto mwanauke Maria walichelewa kufika. Ma fasi yote ya hii mukini waliisha kuyala na watu wa mingi. Na sasa Maria fasi wapi atapata nyumba juu ya kuikala? Alikuwa na mimba na mambo yake ilikuwa ya hatari na nguvu kabisa. Ile siku ya Habari Njema alibeba tangazo ya Mungu, katika moja Malaika ya kama atazala mtoto mwanaume. Yeye ni Mungu mwenye anafanyika na mutu muzima bila zambi. Ndani yake nikusema yeye ekona Mungu na mutu Yesu Kristu. Eko karibu ya kuzala, lakini hakuna fasi hata.

Muzee Yosefu mulinzi yake, alisikitika. Alikokola mulango moja.

Alifungula mutu moja na alimwambia:

Ee mutu wangu, hakuna fasi hapa, ulichelewa. Minasikia mambo yako, lakini misiweze kusaidia. Uende ma fasi ingine chini.

Yosefu alitoka na machozi ilitelemusha ya ma macho yake. Haina mambo ya maugu yake. Anasikitika juu ya Bikira Maria na juu ya Huyu alimuchunga ndani ya tumbo yake. Alikokola na mulango ingine. Ni moja nyumba munene.

Hapa ni fasi moja ya sisi?    Munaona hali ya huyu mwanamuke. Na tazama jibu Walikuja wa nduku na wa jerani. Walikamata hii ma fasi wote. Hakuna kintu. Mwende kiloko mbali.

Walitembea hawa wageni ya kutafuta fasi ya kupumuzika. Giza ilifika na baridi ilikuwa nguvu sana. Yosefu alikamata mupango kukokola mara ingine.

Alifungula mulango mutu moja na  aliyemwambia:

Mutabakia wapi?     Hakuna fasi. Lakini musitokeni, haina muzuri. Munataka kubakia hapa karibu?   Niko na moja pango juu ya ma nyama yetu. Pale ya kona mutaweza kupata fasi moja. . .

Maria, tutaikala hii busiku hapa. Itapita na kiloko nguvu, na kisha tutaangalia kesho tutaenda wapi.

Wakati waliingia mu hii pango walisikia ma sauti ya ma nyama. Sawa waliwapokelea. Bikira Maria aliisha kuchoka sana. Yosefu alikuwa karibu yake juu ya kumusaidia kama ekona kintu moja lazima. Na ile busiku, watoto wangu, ilifanyikwa muujiza moja kuliko ukubwa ya ingine ya dunia muzima. Alizaliwa Mwokozi ya dunia, Yesu Kristu.

Watoto ya hii dunia wanazaliwa ndani ya mabawa na manguo masafi na mazuri, lakini Huyu Mtoto ya mbingu alizaliwa ndani ya sanduku ya kulisha nyama. Ma nyama bila kutaka, walipatia sanduku ya chakula yao kwa Huyo Mtoto, Yesu Kristu.

Maria Bikira Mama Mzazi-Mungu alikamata Mtoto yake na aliweka ndani ya hii sanduku ya chakula ya ma nyama. Mayani ya kukauka ilikuwa manguo yake ya chini. Kivukutu kwake ilikuwa ma pumuzi ya ma nyama.

Yosefu na Maria wanaishi moja muujiza mukubwa. Nuru ya mbingu, yulu ya hii nuru iko pembeni ya Uso ya Mtoto Mtakatifu. Hii pango inaangazwa ya moja nuru takatifu. Pale ndani ya hii

pango alipokelewa Muumba ya dunia. Na anandika Mwevangelizaji Luka: «Akamulalisha katika sanduku ya kulisha nyama, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni» (Luka 2, 7).

Mu muji Betelehemu watu wote wanalala. Habajue mambo gani inafanyikwa hii busiku ndani ya moja pango. Lakini beingine habalale. Na wale weko wachungaji ya Betelehemu. Kiloko mbali ya muji ndani ya ma shamba na ma kiwanja wao wanachunga ma kundi ya ma nyama wao. Wanasuburia kiloko. Mara ingine wanasuburia juu ya ma sauti ya wa Nabii ya Israeli. Waliwaakisha moto na wanaikala pembeni yake kwa sababu baridi ilikuwa nguvu.

Kisha saa kiloko iliangazwa pembeni yao moja nuru ya ajaabu. Ilikuwa nguvu sana na wale waliogopa. Waliangalia moja mwingine na walipotesha ma sauti na pumuzi yao. Ile saa walisikia kufika karibu yao mutu moja. Lakini hasikukuwe mutu. Alikuwa moja Malaika ya Mungu toka mbingu. Mungu alimutuma. Na mabawa yake mweupe alisimama karibu yao na aliwaambia:

Musiogope, ee Wachungaji ya Betelehemu. Mimi ni karibu yenu, juu ya kumipatia moja furaha munene kabisa. Hii tangazo itayala ma roho yenu. Na hapana paka mweye, lakini watu wote ya hii dunia watafurahi. Ni moja tangazo ya furaha. Leo alizaliwa Mwongozi ya dunia, Yesu Kristu, Bwana wetu. . .

Ndivyo. Juu ya ninyi munaniangalia na munashangaa? Minamikikisha ya kama hii busiku alizaliwa Yesu Kristu.

Wachungaji wanaangalia huyu Malaika bila kusema hata sauti moja. Hii ma sauti ya Malaika inaonekana kwao ya ajaabu. Wanazania ya kama wanaona ndoto, Malaika anaendelea sauti yake:

Alizaliwa ku muji ya Daudi, ku muji yenu, Betelehemu. Mwende na mweye mumuangalia. Alizaliwa ndani ya moja pango.

Wakati aliisha kusema hii ma sauti Malaika alikimbia ya mbele kwao.

Wale walinyanyula ma macho yao yulu kwa mbingu.

Moja muchungaji aliwaambia kwa weingine: Musikieni! . . . Musikieni! . . . ni moja wimbo ya ajaabu.

Toka mbingu wa Malaika ma elfu wa mingi walishuka na walipanda ku mugazi moja. Waliimba na walicheza na furaha mingi. Tena walisikia na ma neno ya hii wimbo wao: « Utukufu kwa Mungu aliye juu pia, na salama duniani, katika watu wanaopupendeza» (Luka 2, 14). Ya saa ya kuenea wachungaji wanaangalia yulu kwa mbingu na wanafurahii kwa hii wimbo ya wa Malaika.

Kisha saa kiloko ilisimamamisha hii shangilio ya wa Malaika. Watu wachungaji walibakia wenye wenyewe. Hasikuseme hata mutu moja sauti moja.

Lakini mbio walisema:

Tuende mpaka ku muji Betelehemu kuangalia na ma macho yetu hii mambo ya ajaabu.

Waliweka mabawa kwa mikono yao na walifika na haraka mingi. Walikuwa moja mapendo mingi juu ya kuona Mwokozi ya dunia, Yesu Kristu. Walisimama kiloko inje ya hii pango. Ndani waliona moto na ku moja fasi ya kona waliona hii nuru ilionekana na karibu ya ma kondoo yao. Waliona Mtoto Mtakatifu na Mama yake Maria na walipika magochi na walibushu Yesu Kristu. Kisha Mama Maria na Yosefu waliwaambia namna gani ilifanyikwa hii jabo ya ajaabu hii busiku.

Wachungaji walirudia ma kundi wao. Walimutukuza Mungu, kwa sababu aliwastahili kusikia na kuona Mwokozi ya dunia. Sasa ni mustari yetu juu ya kukaribia na sisi, watoto wangu, hii fasi ya pango kuona Yesu Kristu na akili yetu.

MAELEZEO:

Ulizo: Fasi wapi, ilikuwa namna kuzaliwa, watoto wangu, Mungu wetu Yesu Kristu?

Jibu: Ndani ya moja kabisa muzuri nyumba ya dunia.

Ulizo: Lakini alichakula kuzaliwa wapi?

Jibu: Ndani ya moja pango.

Ulizo: Juu ya ninyi alizaliwa mu pango?

Jibu: Kwa sababu hakuna fasi ndani ya hii muji, ile busiku.

Ulizo: Sisi, watoto wangu, tunaweza wapi kumupokelea Yesu Kristu?

Jibu: Ndani ya ma roho yetu.

FUNDISHO: Roho yetu ni nyumba ya Yesu Kristu wetu.

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: «Akamulalisha katika sanduku ya kulisha nyama. . . «(Luka 2, 7).

MATENDO KU UZIMA YETU: Watu ya dunia walifunga milango yake. Hasikupokelee Kristu. Lakini Mungu anapatia bintu bote kwa kila mutu. Na mutu sasa hasikupatie hata kintu moja kwa Kristu. Dunia alipata paka ma fasi ya mbili juu ya kupokelea Kristu: Hii pango ya buchafu na musalaba ya umivu. Alimupokelea ku uchafu ya pango na ku umivu ya musalaba. Minazania ya kama munasikitika, kwani munasikia hii ma sauti yangu. Mara ingine mutasema ndani yenu: Kama mimi milikuwa ile wakati, mitafungula nyumba na roho yangu kuingia ndani Yesu Kristu. . .

Vile alisemaka wakati moja ya zamani na moja mwanamuke:

Ee Kristu wangu, unipe furaha juu ya kupokelea Weye leo mu nyumba yangu. Kuja mu nyumba yangu na utaangalia namna gani mitakupokelea. Na alibeba jibu ya Kristu: Hii mwaka ku busiku ya kuzaliwa wangu, mitakutembelea. Uwe tayari.

Huyu mwanamuke alifurahi sana. Hii busiku hasikukuwe na mwingine mutu mu nyumba yake. Alikuwa yeye mwenyewe. Alisafisha nyumba yake, aliweka chini ma tapis wazuri, alitayarisha ma switi, aliwaakisha ma taa na aliongolea. Busiku ilipitisha na yule aliongoela kusikia inje ya nyumba yake ma mwendo ya Bwana Yesu. Na tazama! Alisikia mwendo yake. Mutu moja alikokola mulango yake. Haina ndoto aliwaza. Ni kweli. Ni Yesu Kristu, alisema. Na alikimbia kufungula mulango yake. Lakini alisikitika sana, kwani hasikukuwe Kristu. Alikuwa mutu moja muzee na masikini. Alivaa manguo ya kuharabika na alitetemeka kwa baridi. Mwili yake ilikuwa ya kukonda sana kwa njaala mingi.

Mama wangu, alimwambia: Unifungule. Nikona lazima kiloko kupata kivukutu ku mwili yangu. Kupumuzika kiloko. Minasikia njaala. Mitakufa. . .

Hii busiku ulikuja? Misitaweze, inapaswa kutoka. Minaongolea hii busiku kukuja Yesu Kristu. Sasa ni karibu mafikisho yake. Usikarimbie kwangu. Toka. Utaniharabisha ma tapis yangu. Toka sasa. . .

Na alimufunga mulango yake huyu mwanamuke.

Aliikala karibu ya moto aliaikisha ndani ya nyumba yake, kwani inje

ilikuwa baridi, na aliongolea Musafiri mukubwa. Aliwaza: Juu ya ninyi alichelewa Kristu? Lakini mara moja alisikia mara ingine kukokola mlango yake mutu moja. Huyu ni, alisema. Ee Kristu wangu, minakuongolea ma saa mingi. Na alikimbia kufungula mulango yake. Lakini mbele yake sasa alikuja mwanamuke moja na mtoto moja kwa mikono yake. Mtoto yake anaria na juu ya baridi na njaala. Mama yake anakangamana kumupatia kivukutu kwa ubatio yake, lakini hakuna namna.

Mama muzuri wangu, iniache kuingia kwako. Niko mu njia hii busiku.

Minaomba kiloko mapendo ya weye. Mpaka asubui kupumuzika kiloko. Angalia mtoto wangu anasikia baridi, Ekona na kivukutu na inapaswa kukula na kupumuzika. . . Na alipima huyu mama masikini kuingia ndani ya mulango yake. Lakini alisikia mkono moja kumusukuma inje.

Hapana! Alimufokea huyu mama mukubwa. Usiingie ndani. Utaniletea poto-poto. Hii busiku misitaweze. Toka. Leo minaongolea kukuja Bwana Yesu Kristu.

Na huyu mama masikini na mwenye mateso, alitoka. Mtoto yake aliria na malalamiko kwa mikono yake. Huyu mama mukubwa alifungwa nyumba yake na aliongolea Musafiri mukubwa yake. Ilipita hii busiku na huyu mama alisikitika kwa sababu hasikufike Bwana Yesu.

Juu ya ninyi, ee Kristu wangu, ilinilanda? Juu ya ninyi hahukukuje?

Na alibeba jibu yake:

Milikuja mara ya mbili, lakini weye usikuniache kuingia ndani ya nyumba yako.

Wakati gani, ee Bwana wangu, ulikuja? Miye milisopoka na milikuongolea ma saa yote. Misikukuone.

Wakati alikokola mulango yako yule mwanaume muzee mimi milikuwa kwa uso yake. Wakati alikokola mulango yule mwanamuke na mtoto yake, aliyeria sana, mimi milikuwa. Usikuniache kuingia. Uliogopa ya kama mitaleta poto-poto mu nyumba yako. Yule mutu, mwenye hana na mapendo kwa wanduku wa masikini na wamateso yake, hana na Kristu.

Watoto wangu, Siku Kuu ya Kuzaliwa Kristu ni Siku Kuu ya mapendo. Mungu kwa ajili ya mapendo mingi kwa sisi watu alifanyikwa mutu. Na sisi mapendo inapaswa kuonyesha. Paka vile tukona Kristu ku uzima yetu. Na kintu ingine tena. Kama mutaenda sasa ku muji Betelehemu, hamutaweze kutafuta hii pango, pahali alizaliwa Kristu, kwa sababu yulu yake ilijengwa Kanisa moja ukubwa. Lakini pango ya buchafu iko tena ma roho yetu. Lakini kama ndani ya ma roho yetu atazaliwa Yesu Kristu, roho yetu inafanyika kanisa usafi kabisa. Basi, inapaswa kusafisha ma roho yetu. Kuinawa na maji ya Ungamo Takatifu. Paka vile na roho safi tutapokelea Yesu Kristu ndani ya ma roho yetu.

## FUNDISHO KUMI NA MBILI
## MUTAKATIFU YOANE MUTANGULIZI
## (Luka 1, 5-25. Luka3, 3-18 Matayo 3, 1-12 na Marko 14, 1-12)

NAMNA YA KUKARIBIA

Munajua kuniambia, watoto wangu, nani alikuwa mutawa ya jangwa ya kwanza? . . . Minamiona na munashangaa. Mara ya kwanza munasikia hii neno mutawa mukubwa ya jangwa? Tukona mu Kanisa yetu na watawa wenye waliishi mu jangwa. Hawa wanaishi mbali ya watu ya hii dunia, ku Monasteri ao mu jangwa. Wanakombana kutakaswa na kufata uzima ya Mungu. Wanaishi pamoja na Kristu. Kazi yao ni sala kwa Mungu.

Basi, munajua kuniambia mutakatifu moja aliyekuwa mutawa mu jangwa?

Mtakatifu Antonio.

Muzuri sana. Lakini munajua na mwingine?

Mwingine? . . .

Minaona ya kama hamujue watawa ya jangwa wa mingi. Basi, mimi leo mitamifundisha yule, aliyekuwa mutawa ya kwanza na aliishi mu jangwa.

Alikuwa kama moja malaika hapa ya hii inchi yetu. Mutu na malaika! Tazama,

inaweza kutufanyisia Neema ya Mungu. Kila zambi inafanya watu ma nyama ya

pori, inawashukisha chini mugazi moja, lakini utakaso inafanyia watu wa malaika; inawapandisha yulu mugazi moja. HISTORIA. Historia ya uzima ya huyu malaika toka hii inchi ilianza na moja kintu ya ajaabu. Mu Kanisa ya Yerusalema siku moja wale watu walikuwa ndani

waliongolea kukuja inje yule padri alikuwa ndani ya Altari Takatifu. Lakini habakumuone ya kutoka inje juu ya kufukiza na kuomba kwa Mungu. Saa ilipita na padri hasikuonekane. Lakini walijua ya kama yeye alikuwa ndani.

Mambo gani ilifanyikwa? Alipata mambo moja? Vile waliuliza mutu moja kwa mwingine.
Huyu padri Zakaria, vile ilikuwa jina yake, alichelewa kutoka inje.

Lakini kisha saa kiloko walimuona kutoka inje. Lakini waliona ya kama hasikuweze kusema maombi yake. Kinywa yake aliisha kuifunga.

Ni kweli ya kama Zakaria aliisha kupata mambo moja. Hii saa alikuwa ndani ay Altari ya Kanisa alisuburia na moja malaika ya Mungu. Yeye alikuwa Malaika Gabrieli. Mungu alimutuma kumwaambia moja tangazo kizuri.

Mimi ni malaika Gabrieli, mwenye minasimama karibu ya Kiti ya Mungu mu mbingu. Mungu alinituma kukuwambia ya kama maombi yako alisikia. Bibi yako Elisabeti atazala mtoto.
Elisabeti atazala mtoto? Namna gani? Zamani milifanya sala juu ya hii mambo. Kisha milisimama. Sasa yeye ni muzee. Namna gani itafanyikwa hii mambo?
Ee Zakaria, juu ya ninyi unashaka ku hii tendo na mapenzi ya Mungu?
Elisabeti atazala na huyu mtoto atazaliwa utamuita Yoane. Na, kama unataka kusandiki bila shaka ya kama ma sauti yangu ni ukweli, tangu hii saa utabakia bubu. Hautaweze kusema mpaka atazaliwa mtoto yako. Na hii malipizo Mungu atakupatia, kwa sababu haukusandiki mara moja.

Alipima kusema sauti moja Zakaria, lakini hakuna namna. Lunrimi yake ilitengwa, lakini sauti hasikutoke. Watu ya Hekalu walisikia ya kama padri Zakaria aliona moja vision.

Hii malipizo ya Mungu iliisha, wakati alizaliwa mtoto. Elizabeti na namna ya ajaabu alizala huyu mtoto alipenda. Wakati ilifika siku ya tohara ya Yesu Kristu, watu wote waliuliza jina ya mtoto.

Yoane! Hii itakuwa jina ya mtoto yetu, alisema Elisabeti.
Yoane! Lakini hakuna mutu ya ma jerani yenu. Juu ya ninyi hii jina?
Walimuuliza watu wa mingi.

Elisabeti aliangalia Zakaria. Yule, bila tena kuweza ya kusema, alibeba matafari moja na yulu yake aliandika jina: Yoane.

Wate walishangaa. Lakini kabisa walishangaa, wakati Zakaria alianza kusuburia. Neno ya kwanza iliisema ilikuwa: Mubarikiwa Mungu. . . Hii saa na mwangaza ya Mungu Zakaria aliimba moja wimbo, iliyesema na maana juu ya huyu mtoto yake Yoane. Lakini na Malaika aliisha kumwaambia juu ya hii kazi atafanya mtoto yake.

Sikia, ee Zakaria, alimwaambia Malaika ya Mungu: Huyu mtoto atakuwa mukubwa mbele ya ma macho ya Mungu. Ndani ya tumbo ya mama yake atakuwa, lakini atayala na nguvu ya Roho Mutakatifu. Huyu atapita mbele ya kufika Mwokozi ya dunia. Yeye (mtoto yako) atatayarisha njia yake( ya Kristu).
Hii sauti alisikia Zakaria na ajaabu mingi. Sasa, wakati alizaliwa huyu mtoto, na yeye mwenyewe anasema hii ma sauti na watu weingine wanashangaa.

Kisha saa kiloko alipindula ma macho yake kwa mtoto yake na alimwaambia:

Na weye, mtoto wangu, utafanyika Nabii ya Mungu Mwenyezi. Utatayarisha njia juu ya kupita Yule, anayekuja toka mbingu juu ya kutuokoa. Weye utaenda ku mbele juu ya kuonyesha Yule anayekuja kisha kwako.
Walipita miaka ya kuenea. Watu wa mingi walipotesha ma mwendo ya Yoane.

Siku moja ilizambalishwa moja kavumu:

Munajua hii kavumu? Pale karibu ya mutoni Yorodani eko mutu moja mwenye ajaabu. Anafanana ya kama alikuja ya ingine dunia.

Anavala ninyi?

Mimi misikumuone. Watu weingine waliniambia ya kama nguo yake ni toka ngozi ya manyonya ya ngamia na katikati yake ekona kama musipi moja ngozi. Ni mutu murefu, ya kukonda na ma nywele warefu na ma ndevu.

Na anaikala wapi?

Hakuna nyumba kwake. Alijibu mutu moja, mwenye alikuja toka fasi ya

Yorodani. Nyumba yake ni jangwa. Kitanda yake ni bulongo na mufuniko yake ni mbingu.

Muzuri, lakini anakula ninyi?

Hasikule sawa sisi. Anakula mayani na sari kiloko ya ile ma nyuki wanaishi mu jangwa. Hii ni chakula yake.

Na juu ya ninyi tunaikala kusuburia juu ya huyu mutu? Alisema mutu moja katika ya wale watu walisuburia. Iko kuliko muzuri kuenda pale kumufamia.

Moja kundi ya watu waliondoka toka Yerusalema na walienda kumutafuta.

Tazama! Ni huyu! Wakati walimuona watu wote, walisikia na sauti yake,

mwenye alisema: « Tubuni, sababu ufalme wa mbinguni umekaribia» (Matayo 3, 2)

Huyu Yoane, watoto wangu, alikuwa Muhubiri ya toba. Na ninyi wote walikuja na walitubu, waliingia ndani ya ma maji ya Yorodani na walibatiziwa.

Yoane alihubiri sauti ya kweli. Alikuwa mungaga ya Mungu, mwenye alionyesha kwa kila mutu kilonda ya roho yake na alimwambia kufanyia ninyi juu ya matunzo ya nafsi yake.

Joo vile watu walimuuliza: Tutafanya ninyi juu ya kuokolewa?

Inapaswa kutubu. Mufanye matunda wazuri ya toba yenu.

Tunataka kutwambia kwa kila kundi ya sisi.

Musikie. Kama mutu moja kwa mufamo ekona ma nguo ya mbili, atapatia moja nguo kwa yule mutu, mwenye hasikuwe na hii nguo. Na yule mutu ekona ma bintu wa mingi atapatia na kwa wale watu weko masikini.

Na sisi tutafanya ninyi, ee mwalimu ya Mungu?

Mweye muko wa mutuzakondi. Watu wote wanajua ya kama mweye munaiba taifa muzima. Basi, tangu leo mutasimama ya kuiba. Musitabebe kupita ya hii sauti inasema Sheria yetu.

Na sisi mwalimu wetu, tutafanya ninyi:

Mweye, kazi gani munafanye?

Tuko wa askari.

Mweye, musisitake wa nduku wenu, musifanye matendo na hanahaki na mutabeba malipo ya hii kazi yenu.

Watu wote walikuja kwa Yoane kubatiziwa. Siku moja alikuja na mutu mwingine, mwenye Yoane alishaka kumubatiza. Munajua alikuwa nani? Yesu Kristu! Alizaliwa ma mwezi sita kisha Yoane, aliishi ku muji Nazareti. Mbele ya kuanza kuhubiri yake mu dunia, alipita toka Yorodani. Minazania ya kama munajua juu ya Ubatizo ya Kristu. Sasa tutaendelesha fundisho yetu ya Yoane paka.

Watu wa mingi waliendelea kufika kwa Yoane kwa sababu walitafuta fundisho ukweli na wokovu. Wa mingi walimukarimbia na walimuuliza:

Utuwaambie, weye uko Kristu, mwenye sisi tunamuongolea?

Yoane, mwenye alijua kazi na kipimo ya kazi na ma fazila yake, aliwajibu:

Hapana! Misina mimi. Huyu, mwenye ni kuliko mukubwa kwangu anakuja sasa. Mimi misina stahili hata kufungua kamba ya viatu vyake.

Atakuwa vile mukubwa? Walimuuliza Nabi Yoane na walimuangalia kwa ma macho yake.

Ndivyo na kuliko mukubwa. Mimi sasa minamibatiza kwa maji. Anakuja
Yeye, mwenye atamibatiza kwa Roho Mutakatifu, kwa moto ya Roho Mtakatifu.

Kisha hii ma sauti ya Yoane, watu waliishi na maongoleo na ulizo:

Wakati gani atakuja?

Siku ingine ya kesho kisha hii zungumuzo Yoane alipokelea watu katika zwezo yake. Alisikia maungamo wao, aliwabatia na aliwasauria. Kisha alisimama kazi yake mara moja. Aliangalia mbali. Alisimama bila kusema hata. Watu wanamuangalia na ajaabu. Yeye alifungula mkono yake na kilole yake alionyesha mutu moja, mwenye alikuja ya mbali. Alipaza sauti kusema:

Tazama, mwana-kondoo ya Mungu, mwenye anasamehe ma zambi ya dunia.
Tazama! tazama! Anakuja. Ni Mwana-kondoo wa Mungu, ni huyu Kondoo, mwenye atatoa sandaka maugu yake juu ya wokovu ya watu ya dunia muzima.

Ni kweli, ya kama alikujaka Bwana Yesu. Uso yake iliangaza. Watu walishangaa. Beingine walitoka ya Yoane, juu ya kufata Yesu. Na Yoane aliendelea kusema hivi:

Huyu ni Yule mimi milimiambia. Miliona Roho Mutakatifu kukuja na kusimama yulu ya kichwa yake. Yeye ni Mwana wa Mungu. . .
Yoane alisema kweli kwa watu wote: Kwa wafarisayo, kwa watu zakondi ya kama anakuja Mwokozi ya dunia. Ilikuja saa kusema kweli na kwa mfalme Herode, mwenye alikuwa mwingine ya yule aliyewua watoto ya Betelehemu. Na yeye alikuwa mutu mubaya kabisa.

Siku moja alikuja mutu moja na alimwambia kwa Yoane ya kama Herode aliishi mubaya. Nikusema aliisha kubeba kama bibi yake, bibi ya nduku yake Filipo. Huyu mwanamuke aliyeitwa Herodiada alifanya ma kazi mabaya kabisa. Yoane alikuwa muhubiri na nguvu sana na bila kuogopa. Hasikuweze kunyamaza. Alipaza sauti yake na alisema ndani ya nyumba yao ya kama hii matendo ya mfalme na huyu mwanamuke ni mabaya matendo na kontre ya Sheria ya Mungu. Vile alimwambia kwa mfalme:

Ee Mfalme, aipaswe kuishi pamoja na bibi ya nduku yako. Ee Mfalme uko mutu musiyesifa na mwenye zambi kabisa. Inapaswa kutubu! . . .
Lakini mfalme hasikutake kusikia juu ya kutubu. Tena alituma wa askari yake na walimukamata Yoane na walimuweka ndani ya buloko. Lakini Yoane hasikufunge kinywa yake:

Ee Mfalme, hii tendo unaifanya ni mubaya, ni uzulumu na zambi ya busharati. . .
Mfalme alitetemeka. Moyo yake alitaka kumuonyesha ma kosa yake, lakini Herodiada hasikumuache na alipata namna juu ya kulipiza Nabi Yoane. Mfalme Herode aliisha kumupatia kwa Herodiada na kwa mtoto mwanamuke yake, aliyeitwa Salomi, yote bintu na nguvu kwa ufalme wake. Ku mwisho mama na binti yake waliomba kichwa ya Nabi Yoane!

Unataka ninyi? Kila kintu utaniomba, mitakupatia! Alimujibu Herode kwa binti Salomi.
Utanipatia kweli? Muzuri, Mbio minataka sasa kunipatia kichwa ya Yoane.
Mfalme alisikitika. Kichwa ya Yoane! . . . Minasikia muzuri? Alimuuliza mara ingine.

Ndivyo. Walimwambia mama na binti yake. Tunataka kichwa yake.
Unatusikia? Ulitulaka kutupatia kila kintu tutakuomba.

Na Herodi aliwapatia. Alituma moja askari yake mu buloko, mwenye alikata kichwa ya Yoane. Vile walizania mama na binti yake ya kama waliisha kuzimisha sauti ya Nabi Yoane. Lakini ku yote uzima yake Herode alisikia ndani ya moyo yake sauti ya Mt. Yoane: Aipaaswe kuishi na bibi ya nduku yako! . . . Aipaswe kuishi. . .

***MAELEZEO***

Hanuna namna, watoto wangu, kuweza mimi kumifundisha ndani ya moja fundisho uzima na matendo ya Mutakatifu Mutangulizi Yoane. Lakini mutaweza kuniambia: Namna gani ilianza historia ya uzima ya Mt. Yoane? Jibu: Ilianza, wakati baba yake Zakaria alibakia bubu ya ma mwezi ya tisa. Ulizo: Sauti ya zakaria ilifungula. Lakini kuliko nguvu ilisikiwa sauti ya Yoane, sauti ya Neno ya Mungu. Muniambie alisema ninyi ku mutoni Yorodani? Jibu: Alisema kwa watu wote: « Tubuni. Ilifika ufalme ya mbinguni. Na kwa kila kundi ya watu alihubiri na namna ingine.

Ulizo: Mukumbukeni alisema ninyi juu ya Bwana Yesu Kristu?

Jibu: Tazama, Mwana wa Mungu, aliyetosha ma zambi ya watu wote ya dunia.

Ulizo: Na alisema ninyi kwa Herode?

Jibu: Alimufokea kwa ajili ya ma zambi yake pamoja na bibi ya nduku yake. Nikusema, watoto wangu, Yoane alikuja juu ya kusema fundisho ukweli. Yeye alileta ushuhuda ya kweli, mbele ya watu wote na ya kila kazi yao. Namna gani, basi, tunaweza kumuita Yoane?

FUNDISHO: Mutangulizi Mt. Yoane alikuwa Mushuhuda ya ukweli. Kama sauti ya Biblia tutaandika hii sauti Yesu Kristu alisema juu ya Yoane. Yesu Kristu na kinywa yake alimutukuza Yoane na alisema hivi:

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Katikati yao wanaozaliwa na wanawake hakuna mukubwa kupita Yoane Mubatizaji» (Matayo 11, 11)

MATENDO KU UZIMA YETU: Munajua, watoto wangu, namna gani anafanana Yoane? Tazama, wanatuwambia ninyi beingine wimbo ya Kanisa yetu. Mbele ya kutoka Jua kila asubui, inaonekana kwa mbingu moja ingine nyota, inayeitwa Avgerinos (etoile du matin (Venus). Wakati ataonekana Venus, inatuonyesha ya kama kisha saa kiloko itakuja na Jua. Na ni kweli, ya kama, wakati inaonekana Jua, Venus hasionekane tena.

Vile ilifanyikwa na kwa Yoane. Ndani ya giza ya dunia ya upagano ile wakati alikuja kama Venus Yoane Mutangulizi na alituhubiri ya kama anakuja kupita mukubwa yangu Yesu Kristu, kama Jua ya dunia muzima. Kwa hii mambo Yoane anaitwa Mutangulizi ao Prodromo mu lugha kigreki, kwa sababu alitayarisha njia juu ya kutembea Kristu na yeye alitoka ya hii uzima. Kazi yake ilikuwa paka moja: Kuonyesha kwa watu mafikisho ya Yesu Kristu. Sasa munaweza kusikia unyenyekevu yake, watoto wangu.

Na sisi paka moja kazi tukona yo: Kuonyesha mbele ya watu wote ya dunia na namna ya uzima na masauti yetu nani eko Yesu Kristu. Lakini hapana juu ya kutukuza sisi, paka juu ya kusandiki na kufata uzima na fundisho ya Kristu.

Tena inapaswa, watoto wangu, kusifu na sisi Makumbusho ya Mut. Yoane.

Na Kanisa yetu inamusifu sana. Munaona ku Ikonostasi ya Kanisa. Pembeni ya Ikona ya Kristu ni Ikona ya Mt. Yoane. Na yeye ni wa pekee Mutakatifu, kisha Mzazi-Mungu Maria, mwenye ekona mama shangilio ya mingi kwa makumbusho yake mu Kanisa yetu.

Aliishi kama malaika ndani ya hii dunia. Na mweye mukombane kuishi kama

wadogo wa malaika ya Kristu. Tena na kwa maombi yenu muzombelee kusema

Ee Mubatizaji ya Kristu, utuombe juu ya wokovu wetu.

# FUNDISHO KUMI NA TATU
# YESU KRISTU ANATEMBELEA ZAKAYO MU NYUMBA YAKE
# (Luka 19, 1-10)

NAMNA YA KUKARIBIA

Hii ma siku yetu wanafanyikwa matendo mabaya ya kuiba na kunyanganya ya mingi. Kila siku tunasikia ya kama watu filani waliiba makuta, waliiba bintu ya wa nduku wao.

Kama mutu moja ataiba kintu moja, kisha anafanya ninyi?
Anakimbia kufuchikwa juu ya hapana kumukamata.
Mukona ona moja mwivi, mwenye anapanda yulu ya muti moja? Mimi leo mitamiambia historia moja na moja mwivi mukubwa, mwenye walimuona watu siku moja kukimbia na kupanda yulu ya muti moja.

HISTORIA. Hii historia yetu ilifanyikwa ku miaka ya mafikisho ya Bwana Yesu mu dunia. Wakati ya miaka ya tatu, Yesu Kristu alitembea fasi yote ya Galilaya, Yudea na Palestina. Alifundisha na alifanya miujiza. Wale watu walikuwa na masikio wazi walisikia mafundisho yake. Na wale walikuwa ma macho wao wazi waliona na miujiza yake.

Siku moja Yesu alipita ya muji Yeriko na watu wa mingi walikwenda na haraka karibu yake. Wote walipenda kumuona. Mutu moja mufupi hasikuweze kumuona. Alikuwa mwenye kipofu na masikini.

Alisikia pembeni yake kelele, alifungula mikono yake juu ya kupapasa bintu na watu pembeni yake, lakini hasikuweze kusikia bintu ya mingi. Alikuwa daima mbele yake moja giza mingi. Watu weingine walimuona Kristu na walifurahi, lakini yule mutu kipofu hasikuweze kumuona. Lakini ilikuja saa na alimuona. Namna gani? Kristu alimurudisha nuru ya ma macho yake. Sasa huyu kipofu anaona muzuri na ma macho yake Yesu Kristu.

Kisha hii muujiza Kristu wetu aliendelesha mwendo yake ndani ya Yeriko.

Watu wa mingi mukongo yake walimufata. Waliisha kusikia wote hii ya hii mafundisho na miujiza yao na waliacha ma kazi wao na walitoka inje ya njia kumuona na kumusikia. Katikati yao alikuja na mutu moja, mwenye watu wa mingi walimuchukia. Juu ya ninyi? Alikuwa moja mwivi mukubwa. Aliiba watu, bila kumuuzi hata mutu mwingine. Na hii makuta ya kuiba aliisha kufanya moja mali mingi. Alikuwa mutozakodi.

Ile wakati, watoto wangu, watozakodi walikuwa cheo na nguvu kubeba ma palata ya watu wote. Na ni kweli ya kama habakubebe paka hii makuta iliwaonyesha sheria ya inchi yao, lakini walibeba na kupita ya mingi. Nikusema waliiba makuta mingi na kabisa toka watu wamasikini. Walikuwa namna kuwauzi na nguvu mingi na kubeba makuta yao. Vile watozakodi walikuwa watu, wenye watu weingine waliwachukia sana. Hata mutu moja hasikuwapende na waliwaona kama watu wenye zambi sana. Mukumbukeni na yule mutozakodi ya Parabole, mwenye alipika ma kilari yake na aliomba hurumia kwa ajili ya ma mingi ma zambi yake? . . .

Vile alikuwa na huyu mutu, aliyekuwa mukubwa ya watozakodi weingine.

Aliikala ndani ya Yeriko na aliitwa Zakayo. Mpaka hii saa alipenda sana makuta. Watu weingine waliisha kutoka inje ya njia kumupokelea na kusikia Kristu na yeye alikuwa mu nyumba yake na alibalula makuta yake. . .

Lakini alisimama ku moja dakika. Ilifika kelele kwa masikio yake ya kama karibu ya nyumba yake atapita Yesu Kristu. Alisimama na alianza kuwaza muzuri. Ndani yake alizaliwa mara moja matakio moja: Anataka kuona Kristu! Ndivyo, Zakayo anataka kuona Kristu. Huyu nikona makuta mingi na mali mingi na anataka kuona Yule, mwenye eko masikini, Bwana Yesu Kristu.

Inapaswa kumuona. Mitaenda. Namna gani watu weingine wanamuona?

Inapaswa na mimi kuona Uso yake.

Na hivi, bila kuchelewa, alifunga magasin yake na kama mtoto mudogo alitembea mbio. Kisha saa kiloko alifika ku hii njia anatembea Kristu. Lakini namna gani atamuona? Watu wa mingi walitembea pembeni Yake na walimufunika. Hasikuweze kupita katikati yao kwa sababu iko namna watu beingine kumuuzi ao kumupika kwa sababu yeye alikuwa mutozakondi na watu wote walimuchukia. Kipimo ya mwili yake ilikuwa kifupi.

Kisha saa kiloko alipindula na alianza kukimbia. Walimuona watu weingine na waliuliza moja mwingine: Anaenda wapi huyu mutu? Juu ya ninyi anatembea hivi?

Wakati alisikia Zakayo ya kama hasikuweze kuona Kristu, aliwaza kintu ingine. Alienda mukongo na alipanda yulu ya moja mukuyu na, wakati Kristu atapita na Kundi ya watu wake ya hii fasi, yeye atamuona muzuri kabisa na atafurahi kwa sababu ataona Uso Yake. Kama mtoto mudogo alifika mbio ku hii fasi. Alipanda yulu ya hii muti na aliongolea. Hii saa hasikuwaze hata mali, hata kazi, hata utukufu yake ao kintu ingine ya dunia. Paka kintu moja ilikuwa ndani ya akili yake: Kuona Kristu.

Hasikupitishe saa mingi na Kundi hii na Bwana Yesu katikati yao ilifika pale karibu. Watu walimuona mutu moja yulu ya muti moja.

Waliuliza maugu yao: Juu ya ninyi yule mutu alipanda yulu ya hii muti?

Na namna gani alipanda. Iko hatari kuikala pale yulu.

Walimuona watu, wenye habakumujue, lakini alimuona na Kristu, mwenye na Yeye hasikumujue. Zakayo aliona Uso ya Kristu na ngapi ilikuwa na mwangaza mingi. Lakini na Kristu alinyanyula ma macho yake yulu ya Zakayo na alimuona. Zakayo aliogopa kiloko. Roho yake ilianza kupika nguvu.

Lakini mbele ya kusikia hii mambo, alisikia Yesu Kristu kumuita:

Ee Zakayo! . . .

Namna gani ananijua mimi na ananiita na jina yangu?

Ee Zakayo, shuka mbio. . . Leo hii busiku mitakuja na mitakula na wewe my nyumba yako.

Sasa muweze kuwaza, watoto wangu, furaha na mapendo ngapi ilizaliwa ndani ya roho ya huyu mutozakondi!

Yeye na aliluka chini na alitembea mbio mu nyumba yake. Ilipaswa kuwambia kwa bibi na watoto yake ya kama hii busiku Yesu Kristu atakuja mu nyumba yao.

Yesu Kristu alisimama hii mwendo yake na aligeuza na alikamata hii njia inatembea mu nyumba ya Zakayo. Watu wote walimuangalia na ajaabu. Mara ingine beingine walipata kisilani kwa roho yao.

Munaona, walisema kwa watu weingine, mu nyumba gani leo ataenda Yesu

Kristu. Hasijue ya kama huyu mutu ni mwenye zambi? Watu wa ngapi aliiba na watu wa ngapi wanamuchukia? Huyu ni mwivi mukubwa na Kristu ataenda kwake? Hakuna ma nyumba ya watu weingine wenye wazuri?

Hii ma sauti hawa walisema katikati yao, kwa sababu habakuweze kuona ndani ya roho yake kintu moja, ile paka Kristu aliiona. Kristu, wakati alimuona yulu pa muti aliona ya kama ndani ya roho yake ilikuwa mapendo ya toba. Basi, Kristu hasikutembee mu nyumba ya mutu moja mwenye zambi, lakini alienda mu nyumba ya mutu, mwenye aliisha kutubu.

Watu weingine habaweze kuona toba yake na iko namna kumusimanga Kristu.

Lakini kisha saa kiloko walishangaa. Zakayo alisimama inje ya nyumba yake na furaha mingi alipokelea Kristu, aliyepita ku mulango ya nyumba yake. Matone ya mbili walianguka toka ma

macho yake. Walikuwa machozi ya furaha. Walikuwa machozi ya toba. Na wakati aliikala Kristu, alimutoa zawandi moja. Zawandi ya uzima mupya tangu hii saa. Zakayo, basi, alisimama na alimwambia kwa Kristu mbele ya ma jamaa yake:

Tazama, Bwana, nusu ya mali zangu ninawapa masikini, na kama nimetwaa kitu cha mutu kwa kumusingizia uwongo, ninamurudishia mara ine. . .

Hii ma sauti yake walisikia watu wote, wenye waliisha kuingia ndani ya nyumba yake. Walisikia ma sauti yake na habakuweze kusandiki kwa masikio yao. Zakayo aliisha kugeuza mufano yake. Ilitoka hii mufano ya uovu na makari. Sasa uso yake iliyala na mwangaza ya Mungu. Alikamata mupangu ukubwa. Tangu hii saa atasaidia paka wa nduku wa masikini wake. Aliacha na hii kazi yake iliyekuwa ya zambi.

Nani alimugeuza? Yule, aliyekuja kugeuza mufano ya watu wote ya hii dunia. Aliingia Kristu mu nyumba ya zakayo na muzima nyumba yake iligeuzwa. Na wakati Kristu aliona hii toba ukweli ya yule mutu, aliyekuwa mbele mwivi mukubwa, alisema mbele ya watu wote:

Minamiambia kweli, ya kama ndani ya hii nyumba leo ilifanyikwa muujiza ya wokovu. Na huyu mutu, Zakayo, ni mtoto ya Abrahamu, lakini ya miaka mingi alikuwa mtoto ya zambi. Musisahabu ya kama Mwana ya mutu, Mwokozi, alikuja juu ya kurudisha kondoo mupotevu karibu yake. MAELEZEO: Ulizo: Wakati Kristu alienda ku muji Yeriko, aliingia mu nyumba ya mutu nani?

Jibu: Mu nyumba ya zakayo.

Ulizo: Zakayo mbele alikuwa mutu muzuri?

Jibu: Hapana. Alikuwa mutozakodi mukubwa, nikusema mwivi mukubwa. Ulizo: Na mafikisho ya Kristu mu nyumba yake, ilifanyikwa ninyi mu nyumba yake?

Jibu: Ugeuzi

Vile, watoto wangu, ma nyumba yetu watageuza, kama ataingi na ndani yao Yesu Kristu.

FUNDISHO: Inapaswa kuingia ndani ya nyumba yetu Kristu. SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Zakayo shuka mbio, sababu imenipasa kukaa nyumbani mwako leo» (Luka 19, 5).

MATENDO KU UZIMA YETU. Yesu Kristu ni ndani ya ma nyumba yetu?

Watoto beingine watatujibu: Ndivyo, Kristu ni ndani ya nyumba yangu, kwa sababu pa kibabashi tukona picha (Ikona) Yake na watakatifu beingine.

Na mu nyumba yangu ni Kristu, atasema mtoto mwingine, kwani ndani ya kabachi tukona Agano Jipya, ao Evangelion yake.

Lakini inenea kama tukona pa kibabashi Ikona ya Kristu ao Evangelion ndani ya kabachi yetu, watoto wangu? (. . . ) Hapana. Lakini sasa, mukujeni kuona pamoja bintu wa gani ikona nyumba muja kama ndani anaikala Kristu.

Anatawala ma fasi yote Kristu. Nikusema watu ya hii jamaa wanafanya pamoja sala busiku. Wanasoma kila siku kipande moja toka Madiko Takatifu. Wanafunga chakula kila mukazi tatu na mukazi tano na ingine ma siku ya kwarezima. Ni mapendo katika ya watu wote ya hii jamaa. Hakuna makelele na funjo katika yao. Watoto wanatii wazazi wao. Habasikie wimbo ya dunia ao wimbo ya zambi toka radio ao televizion. Habafungule kuangalia mu televizion ma picha ya zambi. Wanasopoka juu ya hapana kusema ma chabulana ao ma sauti ya zambi. Kila mu Juma na Siku Kuu ya Kanisa yetu watu wote pamoja wanaenda mu Kanisa.

Mweye, watoto wangu, mwenye sasa muko watoto wadogo na mulifamia Kristu, inapaswa kuletea Kristu ndani ya nyumba yenu. Kama kwa mufano mtoto moja, mwenye alileta baba yake mu Kanisa, ao alisaidia baba yake hapana kusema machabulana, ao alisaidia na alisauria watu wote ya nyumba yake juu ya kufanya kila siku busiku na asubui sala mbele ya Mungu, ao alisema kwa

nduku yake juu hapana kusikia wimbo ya zambi na paka wimbo ya Kanisa, huyu mtoto kweli analeta Kristu mu nyumba yake.

Watoto wangu, mufungule milango ya ma nyumba yenu juu ya kuingia Kristu ndani. Kama Kristu ataingia ndani, nyumba yenu itakuwa na furaha na heri. Itakuwa moja fasi ya paradizo.

## FUNDISHO KUMI NA INE
## WA MITUME YA WILI

NAMNA YA KUKARIBIA.

Mtoto moja anaweza kufanya ninyi?

Anaweza kufanya matedo ya mingi. Anaweza kutumika na kuharabika.
Anafanya ma kazi, anafanya makelele, anasema ma sauti ya kucheza, lakini anasaidia na watu weingine.

Leo na hii historia, itamifundisha minataka kumionyesha ya kama watoto wekona nguvu mingi. Wale watoto ya hii historia wetu walifanya matendo ya ajaabu kabisa.

***HISTORIA.***

Ku moja nyumba ya muji moja ya Grekia aliishi moja bwana na bibi yake.

Huyu alikuwa avokat mukubwa. Alitumika muzuri. Bibi yake alikuwa mwalimu ya fundisho mu lugha kianglais na alibeba makuta ya mingi. Waliikala mu nyumba moja muzuri na pembeni yake walikuwa maua na shamba munene na michi ya kuachana. Ma jina wao ilikuwa bwana Themis na mama Sofia. Pamoja walikuwa na binti moja, aliyeitwa Katika, aliyewasaidia ma kazi ya nyumba.

Siku moja bwana Themis alibeba barua moja, kwa ajili ya hii alifurahi yeye lakini alisikitika na kiloko.

Angalia, ee Sofia, anatuandika ninyi nduku wangu, Ntinos. Anasema ya kama anaondoka pamoja na bibi yake ku Amerika. Ni lazima kutegeneza mambo yake na anatwaambia kubeba na kuchunga sisi watoto wake wa wili ya mwaka moja.
Muzuri sana, alisema bibi yake. Tutapata furaha ndani ya nyumba yetu.
Wale watoto weko wenye furaha.

Ni kweli, tutapata furaha, lakini tutapata na makelele. Na sisi tukona kila moja ma kazi yetu.
Ndivyo, lakini hatuweze kukatala. Yeye ni nduku wetu. Tutabeba watoto wake kama watoto wetu, paka uliza wakati gani watakuja.
Tazama, anandika mu barua yake. Mu tarehe 15 ya hii mwezi inapaswa kwenda mu station ya mashua kuwabeba.
Hawa watoto, waipwa ya Themis walikuwa watoto wazuri. Ma jina yao Nikolaos na Heleni. Wakati walisikia ya kama wataenda mu nyumba ya muyomba yao, walicheza na furaha mingi. Ni kweli ya kama na karibu ya wazazi wao walikuwa furaha, kwa sababu toka wao walifunda kupenda Mungu Yesu Kristu na kusuburia ma sauti ya Kristu bila haya. Wazazi wao walikuwa watu ya heshima na imani ya Kristu. Na vile waliisha kuwapatia kwa watoto wao mapendo kwa Mungu na boka.

Hii siku ya kusafiri Nikolaos na Heleni ilifika. Mama yao aliwasidikiza mpaka station ya mashua. Wakati walifika mu station, waliona muyomba yao, mwenye aliwaongolea.

Tazama! Huyu ni muyomba wetu, mwenye anatuongolea na makalasi manene.
Kisha saa kiloko hawa watoto walifika mu nyumba ya muyomba Themis, mwenye aliwatayarisha kukula. Watoto walianza kuona bile bintu waliona pembeni yao mu nyumba na ma shamba yao. Waliangalia ma kitabu ya muyomba yao, meza ya kazi yake, pisi yao na kisha walikimbia kucheza ma shamba. Pale walifurahi pamoja na mawa, ma michi mazuri na ma ndeke ndani ya mashamba.

Hapa tutaishi muzuri alisema Nikolaos kwa dada yake Heleni.

Wakati ilipita mbio na watoto walianza kuenda ku masomo. Nikolaos ku

daraja ya tatu na Heleni ku daraja ya mbili. Walikuwa watoto wa akili na waliachana ndani ya ma daraja wao. Lakini kuliko waliachana kwa wema wao na mufano muzuri wao. Siku moja, wakati walirudia alisema Heleni kwa nduku wake:

Ee Nikolaos, ulisikia mambo moja? Ndani ya nyumba ya muyomba yetu abaseme hata kiloko ma sauti ya Mungu. Misikuone muyomba yetu kufanya alama ya musalaba ao kusema sala moja kwa Mungu hata mara moja. Juu ya ninyi? Kumbuka mu nyumba yetu baba na mama yetu ma sala ngapi wazuri walisema pamoja na sisi?

Minaisha kuangalia hii mambo, Heleni, alijibu Nikolaos. Muyomba yetu anaonekana mutu muzuri, lakini hasionekane ya kama anapenda Mungu. Inapaswa kumwambia ma sauti kiloko. Mara ingine Mungu alitutuma mu nyumba yao paka ya hii kazi. . . Minasikia ndani yangu, Ee Heleni, furaha moja. Inaniambia kintu moja ndani yangu ya kama muyomba yetu inapaswa kumukokota karibu ya Kristu.

Na mimi minataka, ee Nikolaos. Mitasaidia na mimi. Mitakuwa na mimi furaha. Haina vile? Utanipatia na mimi kiloko furaha kwa hii kazi yetu.

Vile, watoto walianza kutegeneza namna juu ya kusaidia muyomba yao mu uzima ya Kanisa na Kristu. Akili yao ilitumika namna gani watapata namna moja kusuburia na yeye juu ya Kristu. Siku moja, walipanda yulu ya nyumba moja. Pale Nikolaos alipata moja mavazi, aliivala na alifanana kama Napoleon mukubwa.

Hii mavazi ni mazuri, ee Nikolaos, alimwambia Heleni

Sikia, minapata na moja nguo juu ya weye, Heleni. Angalia, kama utavaa hii nguo, utafanana kama Kambo mwanamuke yetu.

Munafanya ninyi, pale yulu? Aliwauliza na namna makari muyomba mwanamuke yao. Mbio, mushukeni chini.

Na watoto wa wili walikimbia kuchuka. Lakini, wakati walishuka, walipata na kitabu moja; ilikuwa Madiko Takatifu. Nani anajua ya miaka ngapi waliitupa pale. Watoto waliisafisha hii kitabu na walianza kupindula ma ukurasa yake. Mu nyumba yao, baba wao aliwasoma kila busiku kipande moja. Lakini hapa mu nyumba ya wayomba wao hakuna hii zwezo.

Busiku, wakati ilifika saa ya kupumuzika, watoto wa wili walikokola mulango ya chumba ya muyomba yao, ile wakati yeye alisoma ma kitabu yake.

Oti. . . ilisikiwa sauti ya muyomba yao toka ndani ya chumba yake.

Ee Muyomba mupendwa wetu, tazama, tulipata hii Kitabu na tunataka kutusoma kiloko ya hii fundisho.

Kujeni karibu kuona Kitabu gani ni hii. A! Ni Madiko Takatifu! Watoto wapenzi wangu, mimi misisome Madiko Takatifu. Nduku yangu, mwenye ni baba wenu, yeye anasoma hii Kitabu kila siku.

Ndivyo, baba wetu anaisoma. Soma na weye, ee Muyomba yetu. Utaona ma sauti ngapi wazuri ni ndani ya hii Kitabu.

Na mtoto Heleni, hii saa nduku yake alisuburia na muyomba Themis, alianguka kwa mikono yake na namna ya malaika alimwaambia:

Kuja, muyomba mupendwa wetu, fanya hii matakio yetu. Unajua ngapi minakupenda. Soma kipande moja kusikia na sisi sauti ya Mungu. Hii Kitabu ni Kitabu ya Mungu, sawa vile baba yetu alituwambia.

Hii busiku munaniuzi mingi, watoto wangu, aliwajibu na mucheko muyomba yao. Lakini, mitamifanyisia matakio yenu. Muikale hapa na mimi mitasoma.

Yeye aliacha cigarette yake na alikamata kwa mikono yake hii Kitabu ya Mungu. Alifungula. Ma macho yake walianguka ku hii fasi Kristu anasema: « Kwani ni faida gani kama mutu akipata dunia nzima, na kupata hasara ya uzima wake? (Matayo 16, 26). Alisimama. . .

Ee Muyomba, juu ya ninyi ulisimama? Utufafanusha maana ya hii ma sauti ya Mungu?

Hii masauti ni juu ya mimi, watoto wangu. Tazama, hapa anasema ninyi

Kristu. Ni nani itakuwa faida kama mutu moja atapata dunia muzima, atatukuzwa na ataishi na mali mingi, lakini atapotesha nafsi yake. Nafsi yetu. . . Nafsi yetu. . . Kweli, ni ya kama tulisahabu wokovu ya nafsi yetu.

Wakati hii ma sauti muyomba yao uso yake iliisha kugeuza. Moja nuru ya Mungu ilikuja ndani ya roho yake. Alinyamaza kiloko. Watoto waliepuka pole-pole. Waliacha paka muyomba yao kuwaza hii sauti ya Mungu. Wakati walikuwa wenye wenyewe walisema katikati yao: Tunatakia hii busiku Mungu kufanya muujiza Yake! Twende kuomba kwa Mungu juu ya kuwangazia muyomba yetu. Na wote wa wili walipika magochi na waliomba kwa Mungu juu ya wokovu ya muyomba yao.

Muujiza hasikuchelewe kufanyika. Muyomba yao Themis alianza kugeuza uzima yake. Alipenda kuishi moja uzima ya Kristu.

Ilipita hii ma siku. Watoto walifurahi juu ya hii kazi yao, lakini habakusimame. Siku moja, wakati walirudia toka masomo yao, waliona kiloko chini ya nyumba ya muyomba yao moja ingine nyumba muzuri sana na shamba pembeni yake. Lakini ilionekana ya kama hakuna mutu ndani. Waliuliza wale watoto na walisikia ya kama ndani ya hii nyumba aliikala mutu moja muzee. Alikuwa mutajiri, lakini alikuwa muchoyo. Kama, kwa mufano, aliona mutu moja kukufa kwa njaala, hasikumusaidie. Alikuwa mugumu. Mu Kanisa hasikuende hata mara moja. Watu wa jerani yake walimuogopa.

Ee Nikolaos, alimwambia siku moja dada yake Heleni. Unajua minawaza ninyi?

Tutaenda kukutana yule Kambo mwanaume, anayeikala ndani ya hii nyumba.

Twende, Heleni. Hatunana kupotesha kintu moja. Kama atatufukuza, tutakimbia, bila mambo. Twende! . . .

Waliondoka kwenda mu nyumba ya yule Kambo, bila kumufamia. Mtoto Nikolaos alipanda kiloko yulu juu ya kufugula mulango ya lupango yake. Lakini, maimbwa ya wili na mufano makari walifika kulumiza wale watoto.

Wale watoto na boka mingi walikimbia.

Habakupoteshe kitumaini yao. Siku moja walipita inje ya hii mulango na waliona ya kama maimbwe waliisha kufungwa. Basi, sasa, waliwaza, ni moja wakati kizuri ya kutembelea yule muzee. Pamoja na dada yake walienda, walipika kengele ya nyumba yake na mara moja ilionekana kichwa ya huyu muzee toka dirisha na hali makali.

Juu ya ninyi watoto mabaya, mulipika kengele ya nyumba yangu? Sasa mitakuja na mitapasuka ma kichwa yenu na hii bakora.

E Kambo, hatukuje ya kufanya kintu moja kibaya, alimwambia Nikolaos.

Tulikuja kwani tunataka kusema sauti moja kizuri.

Munataka kunisema ninyi? Muongolee. Minakuja.

Kisha saa kiloko huyu muzee mupenda-feza alishuka na alifungula mulango kwa wale watoto, wenye walimuongolea.

Basi, museme, munataka ninyi? Nani alimituma? Munataka matunda ya shamba yangu? Misipatie hata kwa mutu moja.

Hapana, Kambo, hatupende matunda, na hatukutume mutu mwingine.

Tulikuja sisi wenyewe, alisema Heleni na kiloko tetemeko kwa roho yake.

Sema, mtoto wangu, minataka kusikia juu ya ninyi mulikuja? . . .

Ee Kambo, unajua ya kama Mungu ni karibu yako. Anakupenda. Sisi, basi tunataka, kukuja na weye karibu ya Mungu. Tunataka siku moja ya Mungu kukuja mu Kanisa pamoja na sisi. Kuja mara moja na kama hasikuipendeze Kanisa, usikuje mara ingine.

O, ya hii mambo mulikuja? Padri nani alimituma?

Hata padri moja, ee Kambo. Mungu alitutuma, alimujibu Nikolaos.

Muonekane kama watoto wazuri. Mitawaza matakio yenu, lakini mimi misizombelee kuenda mu Misa. Sasa mwende. . .

Watoto walibeba njia ya kurudia mu nyumba ya muyomba yao. Lakini, ndani yao iliwaambia sauti moja ya kama watamusaidia Kambo kufika mu Misa. Juma iliyefika, tazama na watoto hawa mara ya mbili inje ya nyumba ya yule muzee. Hii mara walipika kengele na kiloko mingi kitumaini. Sasa Kambo alionekana mu dirisha na kuliko mingi wema ya zamani.

Ee Kambo, tulikuja juu ya umoja kintu. Utumaliza matakio yetu.

Kwa ajili ya mweye, muzuri, mimi mitakamata mupango na mitakuja mara moja mu Kanisa. Kujeni hii mu Juma kunibeba.

Watoto, furaha ninyi walisikia! Sasa walikuwa na mabawa kwa mikulu yao.

Waliongolea na mingi matakio kukuja siku ya Mungu juu ya kuongolea huyu Kambo inje ya nyumba yake. Ilikuja siku ya Mungu. Watoto, tazama, walikuwa inje ya nyumba ya huyu Kambo. Walimuongolea. Na, wakati walimuona, kushuka na mavazi wazuri, walicheza na furaha mingi. . .

Kisha saa kiloko huyu Kambo na wale watoto walitembea mu njia ya Kanisa. Walifika pale. Hii saa Padri alianza kusoma Evangelion. Ilikuwa Parabole ya Mutajiri na mwenye masikini Lazaro. Watoto waliangalia kwa siri huyu Kambo. Kisha kuhubiri alianza kuria Kambo. Maombi ya wale watoto walifanya muujiza. Kambo aligeuza mufano ya uzima yake. Alitubu. Aliomba Padri na aliungama. Alifungula milango ya nyumba yake na alikabula mali yake kwa watu wa masikini. Na alianza kutayarisha nafsi yake juu ya ile safari murefu kwa milele. . .

Hasikupitishe wakati mingi na Kambo na toba ukweli alitoka mu mbingu.

Waliisha kumutuma wale watoto wa wili, Nikolaos na Heleni. . .

***MAELEZEO:***

Ulizo: Minaona ya kama mulisikia na mafa mingi, hii Historia ya wale watoto wa wili, watoto wangu. Ni vile? Munakumbuka ma jina yao? Jibu: Mwanaume alikuwa jina Nikolaos na binti jina Heleni.

Ulizo: Kazi ninyi walimaliza wale watoto?

Jibu: Walimaliza ma kazi wa mbili wanene. Moja ni hii: Walileta Muyomba yao ku Imani ya Kristu. Kazi ya mbili: Yule muzee, mupenda-feza, walimuongoza mu Misa na ku wokovu.

Ulizo: Na namna gani walimaliza hii ma kazi yao?

Jibu: Na kitumaini na imani yao. Walisandiki ya kama na saidio ya Mungu wataweza kuleta na ma nafsi beingine kwa Kristu na wokovu ya milele. Basi, fundisho ninyi tutabeba juu ya uzima yetu?

FUNDISHO: Inapaswa kukombana kuongoza na watu weingine kwa Kristu. Kama sauti ya Biblia tutabeba, watoto wangu, hii ma sauti aliandika Mutume Yakovo ku mwisho ya Barua yake.

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: «Jueni ya kuwa mwenye kumurudisha mwenye zambi hata atoke kwa njia ya upotevu, ataokoa roho na mauti, na kufunika wingi wa zambi». (Yakovo 5, 20).

MATENDO KU UZIMA YETU. Kama kwa mufano watoto wa tano munapanda yulu ya kilima moja. Kivukutu ni mingi. Kihu ya maji munene lakini maji hakuna. Mtoto moja, lakini alitafuta na alipata maji. Alikunywa, alifurahi. Kisha atafanya ninyi? (. . . ) Muzuri. Ataita na wa nduku wake kuwaambia ya kama alipata maji.

Kama kwa mufano muko ndani ya fasi moja ya jangwa na pale mutapata moja chumba ya mukate kizuri. Bila shaka, mutafanya ninyi? (. . . ) Mutakula juu ya kuzimba. Kazi gani ingine mutafanya? (. . . ) Mutaacha na ingine mukate kukula na wa nduku weingine, wenye watatembea ya hii fasi.

Kama, kwa mufano, wa mungaga watapata ndawa ya malaria na walimipatia ma ndawa ya mingi juu ya matunzo wenu. Mweye mutafanya ninyi, kisha matunzo yenu? (. . . ) Muzuri. Mutaita na wagonjwa weingine kuwapatia hii ndawa juu ya matunzo wao.

Munasikia juu ya ninyi sisi tulisema hii bintu ya tatu: maji, mukate na ndawa?

Kristu ni maji, anayefurahi wale watu wenye wekona kihu. Kristu ni mukate, inayewakula, wale wanasikia njaala. Tena Kristu ni ndawa, inayetunza wagonjwa toka malari munene, inayeiko zambi.

Mukumbukeni mutu moja, mwenye, wakati alipata Kristu, alikimbia kutafuta murafiki yake kumwambia ya kama alikutana Kristu?

Ni Filipo. Yeye alipata murafiki yake Natanaeli na alimwambia: « Tulipata Kristu, mwenye tulimuongolea».

Mweye, mufanane kama huyu mutume Filipo. Munapata Kristu, mwenye alimisaidia ku masomo na mu nyumba yenu ya kila mambo. Yeye (Kristu) anamijulisha hivi: « Mimi ni maji muzima, Mimi ni Mukate ya uzima». Sasa mweye mutafanya ninyi tangu sasa?

Tutachunga muzuri ku uzima yetu Kristu na aipaswe kumupotesha.

Munajua wakati gani hasipotee mtoto moja Kristu? Wakati anamupatia na kwa watu weingine. Wale watu wa wili ya historia moja toka Evangelion, wenye walikuwa wakipofu, wakati Kristu aliwapatia nuru ya ma macho yao, walienda mbio kujulisha hii muujiza ya Kristu. Lakini Kristu eko na lazima kujulisha Jina yake mu dunia? Hapana, lakini dunia eko na lazima kusikia sauti ya Mungu, na hapana Kristu. Lakini nani atafanya hii kazi: Nikusema kusikia dunia sauti ya Mungu? Mweye, watoto wangu.

Namna gani sisi, bwana mwalimu wetu, tutaweza kukokota watu kwa

Kristu, kwani tuko watoto wadogo?

Mutafanya sawa vile walifanya na wale wanduku ya hii historia mulisikia leo. Mutasema na namna muzuri sauti ya Mungu na mutakombana kusaidia watu kusikia na hawa hii furaha yenu.

Ndivyo. Iko namna kusuburia na wale watu, wenye habaingia mu Misa.

Lakini namna gani namna ingine?

Iko namna kuwapatia kwa wale watu ma kitabu ya Kanisa yetu. Na hii namna ni kizuri. Hii namna na kitabu waliitumia wa eretiki (watu ya fundisho wongo) Kabisa wa Yehovaite, wenye wanakabula ma kitabu yao ku fasi mingi ya kuachana. Na kweli, wanakokota watu waorthodoksi toka Kanisa yetu kwa Kundi yao ya wongo. Kama wanafanya hivi watu wa wongo, mara ngapi inapaswa kufanya sisi hii kazi kukokota watu mu Kanisa ya Wokovu! Basi, kila siku tutakamata pupango kuleta watu mu Kanisa yetu na sauti yetu kizuri na kukaburia kwao na ma kitabu ya Kanisa yetu.

Uzima yetu inatukuza ao inatosha utukufu ya Bwana Yesu Kristu mbele ya watu ya hii dunia. Kama watu weingine wanaona mtoto moja na imani na mufano kizuri wanatukuza Mungu na wanakaribia na Kanisa yake.

Uzima yetu inapaswa kuwa wa malaika. Mweye muko wa malaika wadogo mu hii dunia. Inapaswa kuzambalisha daima fundisho ya Mungu na kwa wa nduku wenu weingine. Musisikie haya kusema sauti ya Mungu. Kila mukristu anaweza kuongoza ku imani ya Kristu wa nduku wake, ma jerani na warafiki wake. Na neema ya Mungu mutaweza, kama munataka.

Ee Bwana! Saidie na watu weingine kupata wokovu na kuishi na Weye kwa milele.

# FUNDISHO KUMI NA TANO
# MWIVI AHARI

***NAMNA YA KUKARIMBIA***

Sasa minataka kupima nguvu ya akili yenu. Ku fundisho iliyepita fundisho ninyi tulifanya?

Juu ya watoto wa wili, Nikolaos na Heleni, wenye na mapendo ya imani ya Kristu walimaliza matendo ya ajaabu.

Muzuri sana. Sasa tutaangalia kama munakumbuka mbele ya hii fundisho ya wale watoto, fundisho gani tulifanya.

Juu ya mwivi moja mukubwa, aliyeitwa mutozakondi Zakayo.

Ni kweli. Huyu Zakayo, mukubwa mwivi kisha alitubu. Alipanda yulu ya muti moja juu ya kuona Kristu na kisha Kristu alikuja mu nyumba yake.

Nikusema, watoto wangu, kama hata na moja mutu mwivi, kama atatubu, anaweza kufanyika mtakatifu na mutume. Lakini, kama mwivi moja hasitubu, mambo gani kisha inafanyikwa? Minazania ya kama sasa munataka kusikia mateso gani anapata yule mutu, mwenye alikuwa mwivi, lakini alikatala kutubu.

HISTORIA. Tuko ku miaka ya zamani kabisa, mbele ya kyuzaliwa Bwanma Yesu. Taifa ya Israeli anatembea mu inchi ya Palestina. Mukubwa yao ni Musa mukubwa mwanaume ya Taifa ya Israeli.

Walihuhurwa toka utumwa ya wakubwa ya Misiri na wanatembea ku inchi yao. Miujiza wa mingi anawafanyisia Mungu. Mukumbukeni beingine miujiza?

Bahari Nyekunda ilifungula na alitambuka katikati yake taifa muzima ya Israeli.

Toka riimbwe moja ilitoka maji safi na toka mbingu Mungu alituma ma ndeke.

Ni vile, watoto wangu. Wakati ingine hii nyoka ya shaba iliponyesha watu toka ulumizo ya ma nyoka, wenye walilumiza watu ya Israeli na wakati ingine miujiza ingine ya Mungu walichunga na ajaabu watu ya Israeli. Tena na muujiza ingine ilikuja kuongezekwa. Musa mukubwa yao aliisha kufa na mukubwa yao alikuwa Yosua wa Nuni. Kizimbirio yake ya kwanza kwa hii safari yao ilikuwa muji Yeriko. Pembeni yake walikuwa ma kibabashi warefu na ilikuwa nguvu sana juu ya kuikamata. Lakini ilipaswa kuanguka Yeriko. Na ilianguka. Na saidio ya Mungu. Lakini Mungu aliwasaidia na hii sheria yake:

Musikie, ee Wanaume ya Israeli, aliwaambia Yosua wa Nuni kwa wa nduku wake. Yeriko itaanguka kwa mikono yetu. Mungu alitulaka. Ma padri ya saba watakamata baragumu na watacheza na nguvu. Mbele yao watatembea wa askari na ma bunduki wao. Kisha wa padri na baragumu yao, kisha Sanduku ya Agano na kisha taifa muzima. Watu wote watanyamaza na paka wa padri watapika na baragumu wao. Tutafanya maviringo pembeni ya muji Yeriko mara ya saba. Hii mara ya saba ma kibabashi ya muji itaanguka chini na sisi tutaingia ndani. . . Lakini pasopo mingi. Musopoke sana kwa hii fasi yetu. Ndani ya hii muji tutapata ma bintu wazuri ya kuachana toka zahabu, shaba na arginte na ingine. Pasopo! Musitabebe hata kintu moja. Kwani Mungu alisema, ya kama, kama mutu moja ataiba kintu moja, atalipizwa na yeye na taifa yetu muzima. Bile bintu tutaipata ndani ya muji tatamupatia kama sandaka kwa Mungu.

Furaha mingi ilizambalishwa kwa fasi yote ya watu ya Israeli. Kisha saa kiloko ma kibabashi ya Yeriko itaanguka chini. Lakini watu walikuwa na moja mawazo mubaya ya kama, kama mutu moja ataiba kintu fulani Mungu atawalipiza sana. Mutu moja alisauria mwingine juu hapana kuiba hata kintu moja.

Saa ilikuja na Yeriko ilianguka. Hii muji iliyekuwa na zambi ilianguka kwa mikono ya Taifa ya Mungu. Toka wale watu waliikala ndani ya hii muji paka mwanamuke Rahava aliishi pamoja na jamaa yake. Wote weingine waliwawuwa na muji waliilugusha. Paka bile bintu ya zahabu na ingine waliilokota na waliweka ku fasi moja. Watu wote walikumbuka malako ya Mungu: Musibebe hata kintu moja ya wote ile ma bintu, kwa sababu mutalipizwa. . .

Watu wote waliheshimiwa hii hamuri ya Mungu, lakini iko na shetani.

Sawa vile mu shamba ya Paradizo aliendа shetani na alikelele na flimbi mu risikio ya Eva na Adamu, vile na sasa shetani alienda na alikelele kwa masikio ya mutu moja, aliyeitwa Ahari, mwenye alisikia sauti ya shetani:

Nani atakuona? Uende busiku. Beba na weye kipande moja toka ile ma bintu. Wakati gani utapata mara ingine hii saa kizuri?

Ahari aliteshwa kiloko kwa akili yake: Mitaenda ao hapana? Kama mitaiba bintu beingine iko namna kuniona. Lakini nani ataniona? Hata mutu moja, Mitaenda busiku. . .

Vile alikamata pupango kuiba bintu fulani. Aliona ndani ya nyumba moja mavazi ya nguo kizuri, iliyekuwa kadiri munene, tena aliiba na makuta 200 ya argent na kintu moja ingine ya zahabu, iliyefanana na lunrimi. Richo ya mutu moja hasikumuone. Alijua ya kama hata mutu moja hasikumuone na alikimbia mu hema yake. Lakini mikono yake walitetemeka, kwani walikamata ma bintu mageni. Sauti ya moyo yake ilianza kumulumiza. Lakini yeye, aliendelea uzima hivi bila kutubu na kugeuza akili yake. Wakati alifika mu Hema yake, aliifuchika ku fasi muzuri na alirudia ku fasi yake, pahali walikuwa na watu wa askari weingine.

Yosua ya Nuni, kisha hii muujiza ya kukamata Yeriko bila nvita, alifurahi na alitaka kuendelesha mwendo yake mpaka ku inchi ya Palestina.

Aliita watu beingine na aliwauliza:

Mwende kwa muji iliyeiko ku mbele yetu, iliyeitwa Ai na muangalieni yote mambo ya wale watu, waliikala pale. Kisha murudieni kutuseme tutafanya ninyi juu ya kuikamata na hii muji.

Watumishi wale walienda kwa ingine muji na, wakati walirudia, walimwambia kwa mukubwa yao hivi:

Hi muji Ai ni udogo. Haina lazima kokombana watu wa mingi. Mpaka ma elfu 2-3 ya wa askari inenea.

Yosua ya Nuni alituma paka wa askari ma elfu ya tatu juu ya kukamata muji Ai. Yeye aliongolea kuangalia hii jabo ya ushindi. Lakini taifa ya muji Ai walishinda wa askari ya Israeli. Waliwua watu 36 na weingine waliwafukuza.

Maombolezo na taambu mingi ilianguka kwa Kundi ya watu ya Israeli.

Yosua ya Nuni alibeba wa padri, wakubwa nikusema ya kila kabila ya taifa yao, walianguka chini mu mbulongo mbele ya Mungu na machozi mingi waliomba kwa Mungu. Na sauti nguvu Yosua ya Nuni alisema kwa Mungu:

Juu ya ninyi, Bwaba wetu, ilifanyika hii mambo ya sikitiko kwa sisi?

Juu ya ninyi ulituacha? Sasa watasikia hii mambo taifa ya Wahananei na watatukombana nguvu na watatupika sana. Vile Jina yako itasimamisha kutukuzwa. Juu ya ninyi, ee Bwana wetu ilifanyika hii mambo? Utuwambia?

Na Bwana aliwajibu hivi:

Ee Yosua wa Nuni, simama. Juu ya ninyi mulianguka vile chini. Sikia, ya kama Taifa yako alikosa mbele kwangu. Na ya hii mambo alipata hii musimba. Mutu moja toka taifa yako alikanyanga hamuri yangu na aliiba bintu ya muji Yeriko. Mimi misitakuwe pamoja na mweye mpaka mweye mutapata huyu mwivi na mutamulipiza. Basi, simama na acha machozi. Uende kutafuta yule mwivi. Wakati utamupata, utamulungua.

Nani alikuwa huyu mutu katikati ya Taifa yetu? Aliuliza maugu yake na watu weingine Yosua ya Nuni. Na juu ya ninyi alifanya hii kazi. Hasikujue ya kama atamuongolea malipizi? Na sasa namna gani mitamupata?

Siku injine asubui aliita watu wake wote. Walisanyikwa watu wote kwa kila Kabila. Walikuwa ma Kabila ya kumi na mbili. Vile walisanyikwa ma kundi kumi na mbili. Watu wote wanaongolea kusema sauti moja mukubwa yao Yosua ya Nuni. Kisha saa kiloko aliwaelezea hii mambo ilionekana katikati yao na aliwaambia ya kama inapaswa kutafuta huyu mwivi.

Mungu alimwangaza akili ya Yosua na alisema ya kama huyu mwivi eko mu Kabila ya Yuda. Watu ya ma Kabila beingine mwende. Itabakia paka Kabila ya Yuda. Kisha Yosua na mwangaza ya Mungu alisema: Huyu mwivi eko ndani ya Kundi ya Zarahi. Beingine ma Kundi ya hii Kabila ya Yuda mwende. Itabakia paka hii Kundi ya Zarahi. Wanaume ya hii Kundi wanaangalia moja mwingine. Ni nani basi eko mwivi?

Yosua ya Nuni anatembea pembeni ya watu wote. Anawaangalia ku ma macho yao. Ku mwisho alisimama mbele ya mutu moja:

Weye uko mwivi, alimusema na sauti bila shaka.

Kweli, alikuwa Ahari. Tangu hii saa alisikia ya kama iko mapenzi ya Mungu kufunuwa huyu mutu mukosefu na roho yake ilianza kupika nguvu. Amekuwa majano kama makuta ya zahabu. Yeye mweyenwe alitowa. wakati aliona ya kama Yosua alimukaribia, boka yake ilifika ku urefu sana. Ilikuwa kuliko muzuri kufungulwa inchi na kumukunywa.

Kuja, alimwambia na namna makali mukubwa Yosua. Sema safi, ulifanya ninyi, namna gani ulifanya hii kazi na fasi wapi uliweka hii yote bintu uliiba?

Watu wale walikuwa pale waliongolea kusikia jibu ya Ahari, lakini yeye alinamisha kichwa yake na ma macho na machozi mingi alisema kiloko ma sauti:

Kweli, milikosa mbele ya Mungu. Vile na vile milifanya. Misishangaa toka hii mwangaza ya hii manguo na miliibeba. Shetani alinishinda na miliiba na makuta ya zahabu na argent.

Fasi gani uliweka? Alimuuliza na namna makali Yosua.

Ndani ya hema yangu, alimujibu Ahari.

Walienda pamoja mu Hema ya Ahari na walipata ile bintu wote. Waliibeba na waliipeleka kwa Yosua mukubwa yao. Na wale waliweka ku fasi moja.

Sasa ilibakia mambo ya malipizi yake. Ilikuwa hamuri ya Mungu kulipizwa makari huyu mwivi. Siku ingine asubui taifa muzima aliondoka juu ya hii kazi ya malipizo. Ku mbele alitembea Ahari pamoja na ma jerani na jamaa yake, na mukongo yake walifata watu wote ya Taifa muzima. Walifika ku moja mutoni (Precipice), iliyeitwa Ahori. Na pale ilisikiwa mara ingine sauti ya Mukubwa Yosua:

Juu ya ninyi ulitupotea kwa ajili ya hii tendo kibaya uliifanya?

Ulifanyika maneno kupotesha sisi hii nvita tulifanya kontre ya taifa ya muji Ai. Weye ulitopotea? Na Mungu atakupotea na weye.

Na alisema mu Taifa yake:

Muanzeni! . . .

Mara moja watu wote walitupa maimbwe pa kichwa ya Ahari. Alihukumwa kufa ya kupika maimbwe. Yulu yake, kisha saa kiloko, ilifanyika moja kilima ya maimbwe. Watu wote kisha malipizi yake waliwaza ngapi munene zambi ni hii zambi ya kuiba. . .

Ulizo: Ma muji ma nani waliweza kukamata watu ya Taifa Israeli?

Jibu: Yeriko na Ai

Ulizo: Juu ya ninyi walishindwa kukamata muji Ai?

Jibu: Kwa sababu Mungu alikatala kuwasaidia.

Ulizo: Na juu ya ninyi Mungu hasikuwasaidie?

Jibu: Kwa sababu mutu moja mwenye kibego, aliyeitwa Ahari, alikanyanga hamuri ya Mungu. Aliiba bintu, ile walikuwa kama sandaka kwa Mungu. FUNDISHO: Aipaswe kuiba bintu ya wa nduku wetu.

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: «Usiibe» (Kutoka 20, 15).

Minawaza ya kama, watoto wangu, ilimifanyikwa ugumu na matata hii malipizo kwa huyu mwivi Ahari. Juu ya moja tendo ya kuiba ilipaswa kumuwua na maimbwe? Musisahabu, watoto wangu, ya kama tuko mu wakati ya Agano la Kale, pahali kila kosa inalipizwa nguvu sana. Hakuna usamehe na hurumia ya Agano Jipya. Na tusisahabu ya kama Ahari alifanyika sababu kuteswa taifa muzima ya Israeli. Kwa ajili yake walikufa mu hii nvita ya muji Ai wanaume ya Israeli 36. Ilipaswa kilipizwa juu ya kupata na weingine mufano na fundisho kizuri.

Na leo iko ma inchi, pahali wanalipiza nguvu watu wao wakosefu. Kwa kila inchi, pahali ndini ni Muslimanisme na watu wekona kama kitabu ya Mungu Korani, katika hamuri yake, kama mutu moja ataiba, wakubwa watakata moja mukono yake. . .

Kwa sisi wa Orthodoksi hakuna hii malipizo nguvu, kwa sababu ni hurumia. Kama atatubu mutu moja, Mungu na inchi yake wanamuhurumia, lakini aipaswe kuanguka mara ya mbili kwa hii kosa yake.

Ni mambo ya sikitiko kwa sababu watoto weingine wekona zwezo kibaya kufungula mikono yao na kuiba bintu ya wa nduku wao. Ku mwanzo, wakati weko mu kipimo udogo, wanaiba bintu wadogo toka nyumba yao ao toka ma nyumba ingine. Kama watakomea wanaiba na bintu kuliko wa mingi na wanene, kwa mufanmo makuta, na bintu ingine ya kuachana. Vile hii kazi yao inafanyikwa zwezo na habaweze kuisimamisha.

Wakati moja walikamata mutu moja munyanganyi. Aliisha kufanya tendo moja ya kuiba na kisha aliuwa na watu wa wili. Walimuhukumu ku lufu. Wakati ilikuwa saa juu ya kumwuwa na bunduki, yeye mwivi aliita mama yake. Yeye alifika karibu yake. Watu wote waliongolea kuangalia moja hali ya sikitiko na machozi, nikusema waliongolea kuona mtoto kubatia mama yake, lakini walishangaa kwa mufano ya huyu kijana mubaya. Yeye alimuchabula mama yake na alipenda kumupika na mara moja alimwambia:

Mama mubaya, weye uliniongoza kwa hii fasi ya uzima yangu. Weye uko assassin yangu! . . .

Mambo ninyi iliisha kufanyikwa? Wakati huyu kijana alikuwa mtoto aliiba riyayi moja na aliipeleka kwa mama yake. Yeye alibeba riyayi na hasikumufokee, lakini alifurahi juu ya hii tendo kibaya yake. Wakati mtoto alikomea aliiba kuku moja, kisha kondoo moja. Vile alifika na aliiba kila mutu na kuwua wa nduku wake.

Pasopo, mingi, watoto wangu. Mukamate leo moja mupango. Musifungule mikono yenu kwa ile bintu weko kwa wageni na kwa watu weingine. Na musisahabu hii sauti anasema Taifa yetu: « Mwivi na mwenye wongo wanafurahi paka ku mwaka ya kwanza». Na Ahari alifurahi kiloko, lakini, wakati alifunuwa kazi yake, walimulipiza na lufu.

# FUNDISHO KUMI NA SITA
## ANANIAS NA SAFIRA
## (Matendo ya Mitume 5, 1-11)

Kanisa yetu, watoto wangu, ni Jamaa yetu ukubwa. Nikusema, sisi wate, wenye tuko hapa tusiko wa jerani, lakini tuko wa nduku, kwa sababu tuko ndani ya hii jamaa ukubwa, inayeitwa Kanisa.

Ku miaka ya kwanza, kisha Ufufuo ya Kristu na Siku Kuu ya Pentikoste, Kanisa ilikuwa moja muujiza. Miujiza ya mingi walifanya wa Mitume. Na uzima yote ya Kanisa ilikuwa muujiza moja. Mitamielezea beingine miujiza.

Ilikuwa muujiza namna gani walisandiki watu ma elfu wa mingi ndani ya masiku wadogo na waliumba Kanisa ya Yerusalema. Muujiza ilikuwa uzima yao. Walikuwa wa elfu ya mingi, lakini waliishi kama moja roho na moja nafsi. Kristu eko moja na wale waaminifu ya kwanza walikuwa mwili yake moja, kwani waliisha kuunganisha kwa Jina ya Kristu. Walikuwa katikati yao mapendo ukweli. Walikuwa wa nduku katika imani moja na kwa Jina ya Kristu. Iliwaunganisha imani moja, Damu moja takatifu kamili ya Kristu, ile walipewa kila siku.

Walikuwa wote wa nduku ya roho. Na hii namna gani tunaifamia?

Hasikukuwe katikati yao moja sauti ya mafigo ao chabulana. Hasikukuwe machanisho kwa bintu yao. Sawa vile sisi tunasema leo: « Hii kintu ni yangu. . . Hii kintu ni yako! . . . «

Ile miaka wabarikiwa hasikukuwe hii sauti: Hii ni yangu na ile ni yako. . . « Bintu bote walikuwa kwa watu wote. Mu Kanisa ya kwanza hasikukuwe mutajiri na masikini. Leo mutu moja eko mutajiri na anaishi na furaha na utukufu ya dunia na mutu mwingine eko masikini anakufa kwa sababu hana ndawa juu ya afya ya uzima yake. Leo mutu moja ekona makuta ya milione na mwingine anabeba malipo kiloko kila mwezi kuishi na jamaa yake. Mutu mwingine anaishi ma nyumba kama mfalme na mwingine anaikala ku moja nyumba ya mayani na matafari. Juu ya ninyi? Kwa sababu hakuna Kristu ndani ya ma roho ya watu.

Ngapi muzuri na vema ilikuwa uzima ya wale Waaminifu ya kwanza! Moja ushirika muzuri kamili. Namna gani waliisha kutegeneza hii namna ya uzima yao ndani ya wakati kiloko? Tuende sasa kuona matendo ya mbili toka hii uzima yao ya kwanza na tutasikia hii ulizo yetu.

Tendo moja: Wa Mitume wanafundisha ndani ya nyumba moja. Watu wekona mapendo na amani. Roho Mutakatifu, mwenye aliyala ma roho yao ile siku ya Pentikoste ameungana watu wote na aliwapatia hekima na nguvu ya roho. Sauti ya wa Mitume inakokota wa roho yao ya kuendelea. Lakini na tendo ingine inawakokota. Musikie: Mbele ya mikulu ya wa Mitume walikuwa ma mifuko wadogo na wanene. Kila mutu, mwenye anaingia ndani ya hii nyumba ya kusikia Kuhubiri anapita na anaacha na moja mufuko mbele ya mikulu ya wa Mitume. Ni ninyi ndani ya hii mifuko ya waaminifu? Ni makuta, bintu ya chakula. Na wanapata wapi?

Mutume Petro alimuuliza mwaaminfu moja:

Weye ulipata wapi hii makuta? Na yeye alimujibu na heshima:

Milikuwa na moja shamba, ee Mwalimu na Mutume ya Kristu, na minazania ya kama inapaswa kuiuzisha. Wa nduku wetu wa mingi wanateswa, kwani habakuwa na bintu ya maisha yao. Hii makuta toka hii shamba, iliyeuzisha, mlileta mbele yako. Hii makuta ni ya kanisa yetu na juu ya kusaidia wa nduku wetu wote.

Na weye, ulipita wapi, hii makuta ulileta ndani ya mufuko yako?

Aliuliza Mtume Petro muto mwingine.

Huyu alikuwa toka Kisanga Kipros. Alikuwa mu Yerusalema. Alisandiki kwa Kristu. Na, wakati alisikia kuhubiri, alikamata mupango kufanyika na yeye mutume. Lakini mbele ya kufanyika

Mutume, ilipaswa kutegeneza mambo ya shamba yake. Bila kuchelewa, aliiuzisha na hii makuta alibeba alileta mbele ya wa Mitume mukusema:

Hii makuta ni toka ma shamba yangu, ee Mutume ya Kristu. Haina yangu.
Ni makuta ya Kanisa yetu, kwani sisi tuko wote jamaa moja. Minapatia hii makuta kwa mikono yenu juu ya kusaidia kazi ya Kanisa yetu.

Na hii namna, watoto wangu, walilokota makuta wa mingi. Vile Kanisa alipata nguvu kusaidia ma jamaa wote na kabisa, wale walikuwa wamasikini. Wote pamoja waliikala kukula na meza moja. Walikuwa wa nduku ya kweli. Walikuwa na weingine, wenye walikuwa na shamba na walipenda kuiuzisha wakati ingine.

Katikati yao, wenye walikuwa shaba walikuwa na Anania na bibi yake Zafira.

Unasema ninyi, bibi wangu, na sisi aipaswe kuuzisha hii shamba yetu?
Watu weingine kila siku wanapeleka makuta yao kwa Mitume. Sisi hatukufanye tena huruma moja. Watasema ninyi juu ya sisi?

Wa Mitume ni kweli ya kama wanatuacha kwa mapenzi yetu. Habapende na mushurtisho (force) kutuwambia ya kuuzisha ma shamba yetu. Lakini, kama weye unataka kuiuzisha hii shamba yetu na makuta tutapatia kwa Mitume.

Unajua miliwaza ninyi? Alimujibu bibi yake Zafira. Minaichika juu ya kuuzisha hii shamba yetu, lakini toka hii makuta tutabeba, kipande moja tutaichunga sisi juu ya kila mambo na huitaji wetu na beingine tutaipatia mu Kanisa.
Na kama atatuuliza Mutume Petro makuta ngapi tulibeba ya shamba yetu, sisi tutamusema ninyi?
Tutamujibu ya kama ilitupatia hii makuta sisi tulileta mu Kanisa.
Yeye hasiweze kutafuta makuta ngapi sisi tulibeba toka hii shaba yetu. Vile tutakuwa na makuta mu nyumba yetu na tutaonyesha mbele ya wa nduku wetu ya kama na sisi tuko watu ya huruma. Unasema ninyi? Unaichika?

Minaichika Anania. Tutafanya vile, sawa weye sasa ulisema.
Vile, watoto wangu, aliwaweka shetani kuharabisha hii tendo kizuri waliwaza kuifanya. Anania na bibi yake Zafira walianguka ndani ya mateko. Kisha saa kiloko walimaliza mawazo wao. Walipata yule mutu mwenye alitaka kuuza shamba yao na walibeba makuta yao. Anania aliendа ku mulango yake, alifuchika kipande moja ya hii makuta na ingine alibeba na aliondoka kuenda kwa Kundi ya waaminifu wote.

Petros alimuona wakati yeye alipita ndani ya hii nyumba na aliacha mufuko yake mbele ya mikulu ya wa Mitume. Kisha alitembea kuikala ku fasi yake. Lakini Petros alimusimamisha na alimuuliza:

E Anania, unaenda wapi? Kuja hapa.
Ananias alisimama na alikuwa kama maji ya makaza. Petros na mwangaza ya Roho Mutakatifu alijua yote hii matendo yake na bibi yake Zafira. Kwa hivi alimuuliza:

Uniambie Anania, hii makuta shamba yako ilikupatia?
Ndivyo, ee Mutume ya Kristu, hii makuta.
Ee Anania, juu ya ninyi uliacha mulango ya roho yako wazi na aliingia ndani shetani na alimisauria kusema sauti ya wogo? Nani alikusema nguvu kusema wongo? Nani alikusema kuuzisha shamba yako? Hii ilikuwa yako na, kama ulitaka, uliweza kukamata na kuchunga hii makuta yote mu nyumba yako. Juu ya ninyi uliwaza uovu ndani ya roho yako? Anania, hii saa usiseme wongo mbele ya watu, lakini mbele ya Mungu. Unapima kulanda Roho Mutakatifu.
Ndani ya hii Kanisa yao hii saa ilikuwa unyamaza mingi. Watu wote na pasopo mingi waliangalia hii mambo. Na Anania? Yeye alinamisha kichwa yake chini kwa haya, alifanyika majano kama zahabu na kisha ma dakika kiloko watu wote walisikia kelele moja pa muskingi. Anania alianguka chini na alikufa. Waliangalia wote ya kama yeye aliisha kufa. Malipizi ya Mungu

ilikuja mara moja kwa ajili ya hii zambi matata yake. Mu Kanisa hii ya kwanza, pahali ilipaswa kuchunga watu utakaso, Mungu alipatia hii malipizi kwa mutu moja, mwenye sawa vile na zamani Adamu, alitaka kusema bongo kwa Mungu Baba yake.

Boka na tetemeko ilizambalishwa ma fasi yote ya wa Kristiani. Wote waliwaza ngapi munene zambi ni hii kusema mutu ma sauti ya bongo mbele ya Mungu na ngapi ilipaswa kusopoka tangu hii saa kila mutu. Maiti ya yule Anania ilikuwa mbele ya ma macho yao. Wa kijana ya tatu-ine na nguvu ku mwili yao, na hamuri ya wa Mitume, walinyanyula maiti yake na walienda inje ya kumumazika.

Uzima ndani ya Kundi yao iliendeleshwa. Wa Mitume waliendelesha ma fundisho yao. Hasikupitishe tena wakati ya ma saa ya tatu na tazama! Alikuja na bibi ya Anania Zafira. Wakati aliingia ndani ya makutano ya wa Kristiani, wote walimuangalia na moja richo ya ajaabu. Yeye tena hasikujue juu ya lufu ya bwana wake. Mbele ya kuuliza Mutume Petro mambo gani ilifanyika, Petros alimuuliza:

Utuseme, Zafira, hii makuta alituleta bwana wako munabeba ya shamba yenu, ile munaiuzisha?

Ndivyo, Mutume ya Mungu, hii makuta wote tulibeba toka hii shamba yetu, bwana yangu alimiletea.

Zafira, alimwambia na sauti nguvu, Mutume Petro, juu ya ninyi musikilizane na bwana yako kusema bongo mbele ya Mungu na kulanda Roho Mutakatifu? Rudia na angalia mulango. Unaona wale wa kijana ya ine wanarudia ya fasi wapi? Waliisha kuenda kumazika bwana yako, Anania. Hawa wamoja watabeba na weye sasa mufu na watakupeleka kumazika.

Mbele ya kuishi ma sauti yake Mutume Petro na mara moja Zafira alianguka chini mufu. Na yeye sawa zamani Eva, bibi ya Adamu, alitaka kulanda Mungu. Na hii ilikuwa malipizi ya mufano juu ya kusopoka watu weingine. Na yeye, bila haya, alisema bongo kwa Mutume Petro, mwenye na mwangaza ya Mungu, alijua yoyote mawazo na matendo ya siri ya roho yake.

Wa kijana ya ine walikamata na maiti yake na waliipeleka karibu ya bwana yake Anania.

Hii ya wili mauti walitetemeka Kanisa ya kwanza. Kisha hasikuweze mutu mwingine mara ingine kusema moja sauti ya wongo.

Anania na Zafira na mufano yao mubaya walifundisha watu weingine kusopoka kwa uzima na mufano yao.

MAELEZEO:

Ulizo: Hii historia yetu ya Kitabu gani ya Kanisa yetu tuliibeba?

Jibu: Ni toka Agano Jipya, toka Kitabu Matendo ya Mitume.

Ulizo: Ilionekana moja mufano mubaya?

Jibu: Ndivyo. Ilikuwa hii sauti ya wongo waliisema Anania na bibi yake Zafira.

Ulizo: Namna gani walipizwa?

Jibu: Walipizwa toka Mungu na lufu. Mara moja walianguka chini wafu. Ulizo: Hii mufano yao mubaya aipaswe na sisi kuisahabu. Basi, fundisho ninyi tutabeba na sisi ku uzima yetu?

FUNDISHO: Aipaswe kusema ma sauti ya wongo hata mara moja. SAUTI YA MADIKO TAKATIUFU: «Hukusema uwongo na watu, lakini na Mungu» Matendo ya Mitume 5, 4)

MATENDO KU UZIMA YETU. Kila sauti ya wongo ni matunda ya shetani. Shetani alisema sauti ya wongo mara ya kwanza ndani ya Paradizo. Na hapana paka hii kazi mubaya alifanya, lakini alisema na kwa watu ya kwanza Adamu na Eva kusema na hawa wongo mbele ya Mungu. Sauti ya bongo ni moja bunduki ya shetani nguvu sana. Ni moja zambi iliyefanya watu karibu wote na kila siku.

Ni ninyi moja sauti ya wongo? Uiseme na usiogope. Na moja sauti ya wongo utafunika tendo na mufano yako bila kisha mambo! . . . Vile shetani anasema kwa masikio yetu.

Na ni kweli ya kama watu wa mingi wanasema wongo, wadogo na wakubwa.

Kila mutu ni mwenye wongo. Kama mutu moja atasema ya kama hasikuseme wongo, yeye ni mwenye wongo.

Watoto sawa mweye, juu ya ninyi wanasema ma sauti ya wongo? Mara ingine juu ya kucheza. Ao juu ya kuchokoza mtoto mwingine ao kucheza na yeye ao kumupima. Mara ingine kwa sababu watu wakubwa wanawaambia kwa watoto wadogo kusema bongo. Kwa mufano: Mutu moja anasema kwa mutoto fulani:

Uende na sema kwa bwana fulani ya kama mimi misina hapa mu nyumba yetu. Vile anasema baba kwa mtoto wake, lakini ni ndani ya nyumba yake. . . ) Mara ingine wanasema wongo kwa sababu waliisha kuzombelea. Mutu moja, kama anazombelea kusema daima ma sauti ya wongo, kama kwa mufano atasema siku moja na sauti moja ukweli, watu beingine habatamusandiki.

Wakati moja, alikuwa mtoto moja muchungaji na juu ya kucheza alianza kuita watu:

Mukujeni kunisaidia alikuja mbwa mwitu ndani ya ma kondolo yangu!

Watu ya mukini yake walikimbia na ma bunduki na ma piki yao juu ya kufukuza huyu nyama ya pori. Yule mtoto alicheka sana, kwa sababu alilanda wa nduku ya mukini yake. Kisha kiloko wakati ingine alifanya hii tendo mara ingine.

Ilikuja mbwa mwitu mu kundi ya ma kondolo yangu! Alisema mara ingine wongo. Na hii mara alicheka mingi. Ilipasuka roho yake kwa macheko yake. Mara ya tatu aliita mtoto wa nduku yake: Mbwa mwitu mu kundi ya ma nyama yangu! Lakini hasikufike hata mutu moja. Hasikumusandiki hata mutu moja ya kama alisema kweli. Alikuja huyu nyama na alikula ao aliwua ma kondolo yake yote.

Watoto wa mingi wanasema moja sauti ya wongo juu ya kufuchika moja tendo yao. Habaseme kweli, walienda wapi, waliiba ninyi, kazi kibaya ninyi walifanya. Nikusema sauti ya wongo ni daima pamoja na moja tendo kibaya.

Basi, pasopo, tangu leo! Inapaswa kusema daima sauti ya kweli juu ya kutusandiki na watu weingine na kabisa juu ya kuishi kama watoto wakweli ya Mungu na hapana watoto ya shetani, mwenye ni baba ya wongo.

## FUNDISHO KUMI NA SABA
## WASHAHINDI WATAKATIFU MAKUMI INE

***NAMNA YA KUKARIBIA***

Ma cheo ya wakubwa ya Inchi yetu inapendeza sana kwa watoto wote. Na, kama utauliza mtoto moja: Unataka kufanyika ninyi, wakati utakomea:

Atakujibu: Minataka kufanyika jemadari, mukubwa ya wa askari, mukubwa ya Inchi yetu.

Misijue kama mtoto moja katikati yenu anataka kufanyika jemadari na mukubwa ya wa askari. Lakini ni kweli ya kama wanaume na sasa na wanawake wanaenda kutumika kwa hii Kundi ya wa askari. Basi, leo fundisho yetu iko na makubwa ya wa askari.

HISTORIA. Tuko kwa wakati ya Ufalme ya Roma. Wa askari makumi ine walitumika juu ya kuchunga ufalme ya Roma. Walikuwa na ma zawandi ya ajaabu. Walikuwa nguvu kwa kila nvita. Walikombana bila shaka na mfalme Likinios alisikia ya kama ndani ya Kundi ya wa askari wake weko na hawa makumi ine, wenye aliwasifa na aliwaita wa askari ya mfalme. Tena aliwapatia kuvaa katikati ya mwili yao na musipi, iliyewapatia mfalme. Joo vile walikuwa sifa ukubwa kwa sababu walivaa musipi ya mfalme.

Mfalme aliwapatia ruhusa yake juu ya kuchunga ma njimbo ya mashariki ya ufalme wake na hawa walichunga mpaka ya inchi ya mfalme ku fasi Mashariki. Walikuwa wazuri hapana paka ku mwili, lakini kabisa walikuwa wazuri na kwa roho yao. Walikuwa na ma zawandi ya mingi. Watu wote waliwatukuza na waliwatamaa.

Siku moja mu kiwanja ukubwa ya muji Sabastia ilifanyikwa makusanyo moja. Walisanyikwa wote wakubwa na wa askari wao. Mukubwa ya hii muji ilipaswa kuwasoma moja hamuri ya mfalme. Na kweli, ndani ya unyamaza alikuja mukubwa ya muji aliyeitwa Agrikola na alisoma hamuri ya mfalme Likinios:

Inapsawa wote wakubwa na wa askari kutoa sandaka kwa wa mungu wetu, ao, kama munakatala, mutakufa. Na lufu hasitakuje mbio-mbio, lakini na mateso matata.

Hamuri ya mfalme ilikuwa ugumu. Likinios, aliyendoa mtoto mwanamuke ya Mukubwa mfalme na mtakatifu ya Kanisa yetu Konstantinos, kwa ajili alikuwa chuki ku Ndini yake (Orthodokse), aliisha kuhamuru ufukuzo kontre ya wa Kristiani ya ufalme wake. Agrikolas alisoma hamuri ya mfalme na namna makari sana. Alisoma mara ya mbili na aliwaza ya kama, kama ni hata moja askari, mwenye atakatala kutoa sandaka kwa wa mungu wao, ataogopa na atatoa sandaka.

Nani ataweza kukatala? Lakini, watoto wangu, katikati ya Kundi ya wa askari walitoka inje wa askari makumi Ine. Walitoka inje na walitembea ku mbele ya huyu Agrikola na kichwa yao yulu walimwambia na sauti nguvu hivi:

Sisi tuko wa Kristiani, tuko wa Kristiani!

Walitumika ku ufalme ya huyu mfalme ya hii inchi, lakini walikuwa na wa askari ya Mufalme ya mbinguni Yesu Kristu. Kama walikuwa tayari kufa mara moja ku moja nvita kontre ya wa adui ya ufalme ya hii inchi, walikuwa kupita mara mingi tayari kufa juu ya mapendo na imani ya Kristu. Sasa, basi, wanasikia ya kama inapaswa kutoa sandaka kwa ma sanamu wao, walitoka inje na walikikisha mbele ya watu wote ya kama weko wa Kristiani.

Agrikolas hasikuweze kuwaza ya kama hawa wa askari makumi Ine walikuwa wa Kristiani. Wakati alisikia sauti yao, alianza kuwatukuza na ma sauti ya butamu. Vile aliwaza ya kama ataweza kulekea mufano na imani yao.

Mweye, muko wa askari kupita wakubwa na wazuri mbele ya weingine!

Mfalme alimisifu na musipi yake na anamipenda sana. Na, kama sasa mutatoa sandaka kwa wa mungu wetu, yeye atamipatia masifu ingine kuliko wakubwa na wa mingi. .

Sikia, mukubwa, alimwambia askari Kandidos kwa jina yao wote. Sikia!

Tunakushukuru mingi ya hii ma sauti yako wazuri. Lakini, sikia ya kama sisi tuko wa askari ya Mfalme Yesu Kristu. Tuko tayari kuteswa mateso yoyote kwa Jina na mapendo ya Kristu. Wa mungu wenu ya wongo tusisujudu, tusisandiki na tusiwaabudu. Basi, fanya kila kazi unazania.

Agrikolas aligeuza mufano yake na alianza na sauti makari kuwaambia ya kama atawateswa.

Mitamipika, mitamiteswa na mateso wagumu kabisa. Muwaze muzuri na muache mawazo yenu ya umbafu. Kama mitaanza kumipika, kisha tutaona kama mutaweza kusema hii ma sauti yenu.

Ee Mukubwa, alimwambia askari Domnos, usipotee ma sauti yako. Masauti makari yako ni kwa sisi sawa vile mtoto moja anatutupa moja mukuki. Basi, usichoke kutusema hii ma sauti yako.

Alishirika Agrikolas na alihamuru wa askari yake kuanza ya kupika Washahindi ya Kristu. Waliwapika nguvu na waliwafanyisia kwa mwili wao bilonda ya mingi. Walipasula ma wili yao, lakini wale walisimama na mufano nguvu na imani nguvu kwa Kristu. Kisha waliwafunga mu buloko. Washahindi waligeuza buloko kama Paradizo. Busiku muzima wanaomba na wanaimba wimbo ya Mungu. Ndani ya ma roho yao wekona moja furaha munene kabisa. Furaha, kwa sababu wanateswa kwa Jina ya Mungu.

Katikati ya busiku waliona moja nuru ya ajaabu kuyala fasi ya buloko yao. Moja nuru ya ajaabu aliwangazia. Walisimama wimbo. Moja sauti walisikia wote. Ilikuwa sauti ya mbingu, sauti ya Bwana Yesu, mwenye aliwaambia: «Huyu mutu, mwenye atavumilia mpaka mwisho, ataokolewa». Tangu hii saa maombi yao ilikuwa kuliko nguvu na kivukutu. Walisema hivi: « Ee Kristu wangu, utupatie nguvu Yako juu ya kubakia wote pamoja mpaka mwisho yetu».

Kisha ma siku wadogo waliwapeleka wote pamoja mbele ya mukubwa Lisias, mwenye alimutuma mfalme na aliyekuwa kupita mukubwa ya Agrikolas. Katikati ya Lisias na Washahindi Makumi Ine ilifanyikwa hii mazungumuzo:

Kama mutatii na mutatoa sandaka kwa wa mungu wetu, mfalme wetu atamipatia ma zawandi wa mingi.

Lakini, kama tutakatala Mfalme wetu aliye mbinguni na tutatoa sandaka kwa wa mungu wenu, tutapotesha utukufu ya Mbingu.

Mutapotesha uzima yenu. Mitamiwua.

Lufu kwa jina na mapendo ya Kristu ni moja uzima butamu na muzuri kabisa.

Inamiongolea moto. Inamiongolea mupeto na ma nyama na mateso ya kuachana. Hamuogope?

Kwa sisi hii yote mateso unatuwaambia haina matata. Sisi wa Kristiani tunaogopa kama tutaachaniswa toka Yesu Kristu, Mungu wetu.

Lisias na Agrikolas, wakati waliona ya kama habaweze kugeuza imani na mufano yao, waliwaza moja mateso nguvu kabisa juu ya kuuwa Wakijana Makumi Ine. Waliwaza ninyi?

Karibu ya muji Sebastia ilikuwa kizipa (ziwa) moja, iliyekuwa maji yake makaza ile ma siku. Yulu yake waliwaza kutupa Washahindi wote wa bunji juu ya kufa.

Hamuri inamalizwa. Lakini mbele ya kutosha wa askari wapagano manguo yao, wale wenyewe walitosha manguo yao na waliingia ndani ya ziwa ya makaza.

Muwaze, watoto wangu, mateso ninyi ilikuwa hii! Kisha saa kiloko mwili yao ilianza kuwa mweusi, madevu wao walitetemekwa kwa baridi na mikulu yao walianza kutetemeka. Damu ilianza kukamatana na kulumiza ma roho yao na ma vipande ya wa wili wao kuanguka chini.

Lakini Washahindi ua Makumi Ine, habalekee. Pembeni yao maji ni ya makaza, lakini ndani ya ma roho yao iliwaakisha moto ya mapendo ya Mungu. Kisha ma saa wadogo watakuwa ndani ya Paradizo, kwa heri ya milele.

Moja katikati yao, Mushahindi Kandidos alisema:

Ee Wa Nduku wangu, baridi ni mingi sana, lakini Paradizo ni butamu.

Pasopo mingi, wa nduku wangu. Tuliingia ndani ya hii ziwa wa nduku Makumi Ine. Makumi Ine tutaingia mu Paradizo. Hata mutu moja aipaswe kulekea na kukatala utukufu yetu mu Paradizo.

Lakini, watoto wangu, mutu moja alilekea roho yake. Tazama! Alinyanyula ma macho yake na aliona inje ya ziwa moto na fasi ya kunawa na maji kivukutu, iliyewategeneza wapagano juu ya kukokota Washahindi. Aliacha wa nduku wake ndani ya ziwa ya makaza na alikimbia inje juu ya kupata kivukutu. Lakini hasikutagurie. Wakati alikaribia, hii mageuzo ya temperature mara moja alimuanguka chini mufu. Zambi ninyi munene ilikuwa! Alikufa kama mutoaji ya Kristu. Kama alipenda kuvumilia kiloko ilikuwa na kitumaini ya kama ataingia mu Paradizo. Alipotesha Paradizo juu ya kupata kiloko kivukutu ya ma saa wadogo. Ndani ya ma dakika wadogo alienda mu gehena.

Sasa wa Washahindi weko makumi tatu na tisa yulu ya hii ziwa. Lakini watabakia na hii hesabu? Moja muaskari mupagano, mwenye aliwachunga na aliona mateso yao alishangaa kwa ajili ya uvumilia wao. Sauti moja ilizaliwa ndani yake na ilimwambia ya kama hawa weko wenye heri. Kisha saa kiloko aliona moja mambo ya ajaabu. Hii ilikuwa ninyi?

Aliona kutoka ya mbingu moja nuru ya ajaabu. Tena aliona kushuka na ma taji makumi ine ya zahabu. Walishuka, walishuka na walisimama kila moja mu kichwa ya kila Mushahindi. Lakini

Washahinmdi wote weko 39. Ilibakia moja taji yulu. Mara moja huyu muaskari alikamata mupango. Alitupa bunduki na mukuki yake, alitosha manguo na aliingia mbio ndani ya hii ziwa mukusema:

Na mimi niko mukristu!

Furaha ninyi walisikia washahindi wote! Mu fasi ya ule mutu, aliyeogopa na alikatala utukufu ya milele, alifika sasa mwingine askari pagano, aliyeitwa Aglaios.

Washahindi ya Kristu walipita busiku moja muzima ndani ya hii ziwa ya makaza. Wakati ilifika asubui mapema wa wili wao wote waliisha kularisha chini ya makaza. Beingine waliisha kufa, lakini beingine waliishi tena. Asubui ingine mateso iliongolea wale waliishi tena. Kisha hii ziwa ya makaza iliwaongolea moto. Ndani ya hii moto wataweka na ma wili wao wote juu ya kulugua na kufanyika maivi. Basi, waliwaweka yulu ya ma motoka yao ya zamani na waliwapeleka ku hii fasi ya moto. Waliwapeleka wote bila moja, aliyekuwa Meliton na alikuwa kuliko kijana mudogo. Alikuwa na tena nguvu ya mwili yake na waliwaza kumukamata juu ya kuharabisha nguvu na imani yake.

Ma motoka wao walikuwa tayari ya kuondoka. Lakini hii saa ilifanyikwa moja jabo ya ajaabu. Mwanamuke moja alikimbia na alikaribia huyu kijana Meliton. Alikuwa mama yake. Wanaongolea wale watu walimuona ya kama huyu ataomboleza, ataria na atakombana kusema kwa mtoto yake juu ya kukatala imani ya Kristu na kuokolewa. Lakini hasikufanyie hivi. Mama alitaka kuona mtoto wake Mushahindi na Mutakatifu ya Kristu. Kwa hivi alibatia kwa mikono yake mtoto yake, alimubushu na alimupanda paka yeye mwenyewe yulu ya motoka, pahali walikuwa yulu na weingine Washahindi.

Uende mtoto wangu, uende pamoja na wa nduku wako. Haipaswe kuonekana weye kuliko chini kwa cheo yao. Uende pamoja mu mbingu. Uende muzuri mtoto wangu mupendwa.

Ma motoka waliondoka. Ma wili ya Washahindi walipeleka kwa hii fasi na walitupa pa moto. Toka baridi walipitisha sasa ku moto, lakini Mungu aliwatosha kwa furaha, aliwaongoza kwa heri ya mbingu. Ma nafsi wao na mataji ya milele walipanda yulu karibu ya Kiti ya Mungu Mukubwa wetu.

Kanisa anakumbuka makumbusho yao kila mwaka mu tarehe ya 9 Mwezi ya tatu.

MAELEZEO: Hii Historia ya washahindi Makumi Ine ilikuwa ya furaha mingi, watoto wangu, wenye walikufa ku mwaka 320, ndani ya ziwa ya muji Sebastia. Ulizo: Namna gani walikufa?

Jibu: Waliwaweka pa moja ziwa ya makaza.

Ulizo: Kintu gani ilikuwa hii, iliwapatia nguvu na furaha na uvumilia mbele ya hii mateso matata?

Jibu: Matakio na kitumaini ya Paradizo.

Ulizo: Mukumbukeni nani alisema sauti moja juu ya hii matakio na mapendo ya Paradizo?

Jibu: Kandidos. Yeye alisema: Ee wanduku wangu, baridi ni nguvu, lakini Paradizo ni butamu».

Ulizo: Paradizo ni paka ya wale Washahindi?

Jibu: Hapana. Kristu anatuongolea sisi wote mu Paradizo.

FUNDISHO: Kristu anatuongolea kwa ufalme ya mbingu.

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Baridi ni nguvu, lakini Paradizo ni butamu».

MATENDO KU UZIMA YETU: Wakati moja ya zamani Paradizo ilikuwa ya kufungwa. Zambi ya watu ya kwanza iliifunga. Na alikuja Kristu na alifungula njia ya mbingu. Inchi yetu ni pale yulu mu mbingu. Hapa tuko ya wakati kiloko. Watakatifu wetu walitakia Paradizo: « Ah, wakati gani itakuja saa ile, itayenipeleka karibu ya Kristu!

WaKristiani habarie wa nduku wao, wenye wanakufa. Ni kweli ya kama habakufe. Wanaishi uzima ukweli na ya milele. Pamoja na Kristu, na Watakatifu na wa malaika wote.

Wakati moja, mama moja alisema kwa mtoto wake:

Mtoto wangu kama utaikala na kimya, mitakubeba moja zawandi kizuri, ile uliniomba ya zamani. Lakini mtoto, hasikuweze kusimama na kimya saa moja na alipotesha hii zawandi, iliyemulaka mama yake.

Na kwa sisi Mungu, mwenye ni Baba wetu, anatusema:

Watoto wangu, mumalize mapenzi yangu hii wakati udogo ya hii uzima yenu na Mimi mitamipatia Ufalme wangu! Mitamifanyisia watoto ya mfalme! Mutaishi hapana miaka wadogo, lakini kwa milele karibu yangu.

Mweye, munasema ninyi, watoto wangu? Aipaswe kushindana hapa ku inchi yetu hii miaka wadogo juu ya kuriti Paradizo? Paka wale wenye wataenda pale, watasikia kintu ninyi ni Paradizo. Minatakia, watoto wangu, sisi wote tuko huku kuingia mu Paradizo. Pasopo mingi, juu hapana kukimbia ao kulekea mtoto moja kwa imani yake na atarudia mukongo sawa vile yule askari ya ziwa ya muji Sebastia.

## FUNDISHO KUMI NA MNANE
## MUFANO YA MWANA MUPOTEVU
## (Luka 15, 11-32)

***NAMNA YA KUKARIBIA***

Mukona ona baba kuria?

Ni zwezo ya kama mama anaria, kwa sababu analekea kuliko ya baba.

Lakini iko namna na baba kuria. Kama kwa mufano, atakufa mtoto yake, hasitarie? Ni vile. Na baba hana mugumu mu roho yake. Hana vile. Kama atakufa mtoto yake! Atafanya ninyi? Hasitarie? Hii umivu ya baba moja tutaona ku hii fundisho yetu ya leo. Lakini juu ya ninyi aliumivu? Aliisha kufa mtoto yake? Itakuwa kuliko muzuri kusikia mambo yake sasa.

***HISTORIA***

Moja baba mwenye taambu aliikala mu dirisha ya nyumba yake na aliangalia inje moja saa ya mangaribi. Kichwa yake alikamata kwa mikono yake. Na ku uso yake ilionekana taambu mingi. Ma macho yake walikuwa ya kulobana na machozi. Tunakombana kutafuta maneno ya sikitiko yake. Tunamusikia kila saa kulalamika na kusema paka yeye mwenyewe ndani ya roho yake:

Mtoto wangu, mtoto wangu mupotevu!

Lakini mambo gani ilikuwa? Huyu baba alikuwa mutajiri na ma shamba na michi na kila kintu ya furaha, lakini sasa juu ya ninyi alijilobeka mu umivu? Toka ndani yake na moja ingine mupya maombolezo inatoka, iliyetusaidia kusikia:

Juu ya ninyi mtoto wangu? Juu ya ninyi ulifanya hii kazi? Kintu gani uliniomba na mimi misikuipatie? Namna gani Mimi mitaishi bila weye?

Alikuwa taambu mingi kwa sababu, aliisha kupotea mtoto wake, moja katikati wa mbili yake.

Muloko mwana wake aliacha nyumba. Hasikuweze kuikala mu nyumba ya baba yake. Mapendo ya baba yake aliiona kama utumwa. Wa rafiki wake waliharabisha akili yake. Wakati alilala busiku moja, ilikuja kwa akili yake mawazo moja. Mawazo ya giza, lakini ilimupendeza sana na ilimufurahisha.

Mitatoka! Mitatoka ya nyumba yangu.

Ya masiku ya mingi hii mawazo ilimuteswa: Mitatoka, mitatoka, mitatoka. . . Na alitegeneza na akili yake moja uzima mupya. Mitatoka na mitakuwa mutu muhuru, mbali ya macho ya baba wangu. Mitafanya kila kazi minaitaka. . .

Na hii saa juu ya kumaliza hii mawazo yake ilikuja. Moja siku asubui alifungula mulango ya nyumba yake na alisema kwa baba yake:

Ee Baba, saa inakuja kunipatia hii kipande ya mali yako. Unaikala ninyi? Unipe hii kipande ya mali yako, kwa sababu minatoka. Minataka kipande ya mali ya nyumba yetu.

Mtoto wangu! ma sauti gani minasikia sasa? Mtoto wangu, uliwaza muzuri hii kazi unataka kuifanya? Mtoto wangu, angalia sikitiko yangu. Misitaweze hii machanisho.

Ee baba, acha hii ma sauti yako na leta makuta yangu. Machozi yako kamata juu ya weye. Mimi misiweze kuishi hapa ndani. Mitaenda kuishi mbali ku fasi ingine ugeni, mimi wa pekee. Minataka kuwa muhuru.

Beba mtoto wangu. Ni hii kipande ya uriti yetu. Lakini usisahabu ya kama unisikitika na hii tendo yako. Tena usisahabu ya kama mimi baba yako misitaweze kusahabu weye, mtoto wangu.

Misipende kusikia hii ma sauti mambafu, baba. Misipende kujua weye utafanya ninyi. Mimi mitatoka.

Na kweli, watoto wangu, alitoka huyu mwana wake ya mbili. Alikamata makuta ya baba yake, alifungula mulango ya nyumba yake na aliepuka na furaha mingi toka nyumba ya baba yake. Kila saa anapindula na kichwa yake mukongo na anaangalia nyumba yake na anacheka na udanganyifu kwa sababu alistahiliwa kutoka na sasa eko muhuru.

Yambo yako, baba wangu, alisema paka yeye wa pekee, na alicheka na furaha ya shetani. Sasa hautaweze kunikamata.

Kisha saa kiloko aliisha kuepuka ya nyumba yake. Alisafiri na alikuja ku moja inchi ugeni, pahali baba yake hasikuweze kumupata na hasikukuwe pale hata mutu ya kumufamia. Makuta kwa mufuniko yake alikuwa na mingi. Alianza kucheza na kukunywa. Alifanya uzima butamu na kila furaha ya shetani. Hasikupitishe ma siku ya mingi na weingine wakijana walisikia ya kama yeye eko na makuta mingi. Walifika karibu yake kundi moja ya warafiki.

Yambo, murafiki wetu, tunatafuta kijana moja sawa weye. Uko mtoto muzuri. Yambo yako, Twende kukunywa na kucheza.

Na yule mwana aliripa kukunywa wa rafiki wake. Vile alipita ma busiku yake yote na muchezo, wimbo ya dunia na kulewa na kila zambi. Wakati ngapi ilifanyikwa hii muchezo ya uzima yake? Ilifanya hii muchezo, hata ngapi walikuwa makuta yake. Hii wakati ya furaha, hasikuwaze hata siku moja juu ya kazi. Kila siku alikuwa mulevi na hasikuweze kusikia alifanya ninyi. Na ma rafiki yake walimutukuza na ma sauti yao wazuri juu ya kukula makuta yake.

Siku moja alilamuka yeye mwenyewe. Aliangalia ku fasi ya kuhume na kushoto, lakini hasikufike hata moja murafiki yake.

Ile busiku, warafiki wake walisema: Twende sisi sasa, makuta ya yule kijana iliisha. Tuende kutoka. Mpaka sasa yeye alikuwa murafiki yetu muzuri, lakini sasa makuta yake iliisha, hana sasa murafiki yetu.

Na huyu mwana mupotevu alibakia yeye mwenyewe. Mbali ya baba yake, bila makuta, bila warafiki, bila watu aliwafamia.

Sasa? Mitafanya ninyi sasa? alianza kuwaza na njaala ilikuja kumuteswa sana. Minasikia njaala, mukate moja kipande nani atanipatia? Hata mutu moja? Na hivi alizuguluka ma njia na aliomba saidia. Lakini nani atamupatia?

Ee Kijana, unatafuta ninyi ya kuzuguluka ma njia hapa? Unataka kula?

Kuja, nikona ma ngurumbe na misina na muchungaji yao. Kuja kutumika na utakula na weye toka hii chakula yao. Kuja!

Alimuangalia na ajaabu huyu mutu mupotevu. Ma macho yake walikuwa na mweusi juu ya njaala. Paka aliweza kusimama. Atafanya ninyi? Alifata huyu mutu, mwenye alimuongoza inje ya shamba yake, pahali walikula mayani ma ngurumbe yake.

Hii itakuwa kazi yako, alimwambia. Beba na hii matunda wanaikula ma ngurumbe. Kula na weye na chunga ma ngurumbe yangu.

Huyu mtoto ya mfalme alifika kuchunga ngurumbe mbali ya nyumba yake.

Iliisha kuisha machezo yake na kila furaha kila utukufu toka nyumba yake.

Na huyu mtoto mutajiri alikuwa moja mutu ndani ya poto-poto ya buchafu.

Wakati ilipita mingi ku hii kazi yake. Njaala yake ilikuwa munene.

Hasikuzimbe na hii matunda ya ngurumbe. Siku moja asubui alilamuka kiloko na mageuzi ku akili yake. Ma macho yake walianza kutosha machozi. Alianza kuria. Alifunika uso na mikono yake. Alikumbuka uzima yake ya zamani na aliria. Aliwaza na alisema hivi:

Ole wangu, ole wangu milifika wapi! Watumishi wa mingi ya baba wangu mu nymba yangu wanaishi muzuri, wanafurahi, wanakula na mimi hapa minakufa kwa njaala. Milifanya ninyi?

Vile aliria na mara moja alikamata moja mupango: Mitaenda. . . Mitalamuka na mitarudia mukongo mu nyumba yangu. Ni kweli ya kama milikosana mingi. Lakini mitaomba hurumia toka baba yangu, na mitamwambia kweli ya kama milifanya zambi. Atanifukuza? Hapana, hapana, ni baba wangu. Hasitaweze kunifukuza. Ku mwisho mitamwambia kunipokea kama mutumishi wake. Ni kuliko muzuri kuishi kama mutumishi mu nyumba ya baba wangu, na hapana hapa kuishi muchungaji ya ma ngurumbe.

Sasa tuende, watoto wangu, kuangalia, tangu ile wakati mwana mupotevu aliisha kutoka, mambo gani ilifanyikwa mu nyumba yake?

Baba, kisha ondoko na upotevu ya mwana wake alianguka mu taambu mingi. Kila siku aliria kwa sababu alitoka. Aliwaza makosa ngapi aliisha kufanya. Na alisema na akili yake:

Mtoto wangu, juu ya ninyi ulifanya hii kazi? Uliacha nyumba utajiri ya baba yako, iliyekuwa na nyumba yako na ulienda wapi? Wapi? Ku fasi ugeni mbali, kufanya ma zambi mingi. Mtoto wangu! . . . ole wangu.

Na wakati aliwaza hii yote mambo ya mwana wake, alitosha na machozi mingi. Lakini ndani yake ilifuchikwa na moja kitumaini. Siku moja atarudia. Ataenda wapi? Atateswa, atatubu, atarudia. . .

Na hii kitumaini alimupatia kila siku furaha na nguvu na alitoka inje kuangalia kama mtoto wake anakuja. Wakati aliona musafiri moja kukuja ya mbali aliwaza ya kama huyu ni mwana wake. Vile mara ya mingi alijilanda. KIla mangaribi aliangalia na aliongolea kurudia mtoto wake. Siku moja mangaribi alipata furaha mingi. Aliweka mikono yake pa uso yake na aliangalia na pasopo mingi. Kisha moja malalamiko ya furaha ilitoka toka kinywa yake. Kama mazimu anapaza sauti na alisema:

Mtoto wangu, Mtoto wangu anarudia! . . .

Kweli, alikuwa mtoto wake, mtoto mupotevu, mwenye alikamata mupango kurudia. Manguo yake iliisha kuharabika, alikuwa na buchafu mingi, na bilonda na kukonda sana. Lakini haina mambo. Baba yake chini ya manguo na bilonda yake anaona mtoto yake. Anamuona kurudia na mwendo pole pole kwa sababu aliisha kuchoka na anasikia haya. Lakini baba yake wakati alimuona, alikimbia kumukutana. Haina mambo kwa sababu ni muzee. Anakimbia. Anamukaribia. Anafungula mikono yake na anamufunga ndani ya ubatio. Anamubusu na anaria na furaha mingi.

Mtoto wangu! . . . Mtoto wangu! . . .

Hii saa hasiweze kusema ma sauti ingine. Na mwana? Na yeye anaanguka mbele yake, anabusu mikulu yake na anaomboleza na anaria.

Baba wangu, milikosa. Minaijua. Minakosa mbele kwako na mbele ya Mungu. Aipaswe kuniita mtoto yako. Unikamate kama moja mutumishi yako.

Lamuka, mtoto wangu, usirie. Lamuka na simama. Uko mtoto wangu. Na hamuri alileta mara moja kwa watumishi wake:

Mwende, mulete hapa manguo kizuri, pete ya zahabu na muiweke mu kilole yake. Mulete hapa bilato wazuri. Mwende kukamata huyu mwana-ngombe na mutaichinja juu ya kushangilia. Inapaswa sisi wote kufurahi kwa sababu huyu mtoto wangu alikuwa upotevu na alionekana, alikuwa kama mufu na alifufuka.

Kisha saa kiloko ilianza shangilio ukubwa. Wimbo na furaha na muchezo.

Lakini mutu moja alilofa toka hii shangilio. Alilofa mukubwa mtoto wake. Alitumika ma shamba. Wakati alirudia mu nyumba busiku na alisikia wimbo na furaha alishangaa na alisirika kiloko:

Mambo gani ni leo? Aliuliza mutumishi moja. Na yule na furaha alimujibu:

Alikuja muloko yako na baba yako kwa ajili ya hii furaha alichinja moja mwana-ngombe.

Muloko yangu? Kwa ajili yake hii yote furaha na chakula? Misitaingie ndani. . . Moja kimvuli ilianguka pa uso na roho ya yule mukubwa mtoto ya huyu baba. Baba aliacha chakula na watu weingine na alikuja inje:

Mtoto wangu, kuja ndani. Alikuja muloko yako.

Nduku yangu nani? Huyu, mwenye aliharabisha yote makuta yake na warafiki na ya kila muchezo na zambi? Na sasa weye ulichinja moja mwana-ngombe? Mimi minakutumika kwako miaka mingi, lakini usinikupatie hata moja mbuzi kufurahi na mimi pamoja na warafiki wangu. . .

Mtoto wangu, uwaza muzuri. Weye uko karibu yangu miaka mingi. Yote mali na uriti yangu ni yako. Nduku muloko yako alikuwa mupotevu na alirudia, sisi tulimuwaza ya kama alikufa na yeye alifufuka. Ilipaswa kufurahi na weye pamoja na sisi, sawa vile walifurahi watu weingine, wenye walimuona na walifurahi. . .

MAELEZEO. Yote mweye munajua, watoto wangu, ya kama hii Historia inatuifamia kama Mufano (Parabole) ya Mwana Mupotevu. Kanisa anapatia kadiri mingi kwa hii Parabole na aliiweka mu Juma ya Mbili ku wakati ya Kwarezima ya Paska. Ndani ya hii Parabole inafuchama mapendo ya Mungu Baba yetu.

Ulizo: Na mara ingine tulisema ya kama mukongo ya hii ma uso ya moja Parabole inafuchika mafundisho ya kweli wanene. Mutaweza kuniambia mukongo ya huyu baba ya hii Parabole nani eko?

Jibu: Ni Mungu Baba wetu.

Ulizo: Na huyu mwana mupotevu nani eko?

Jibu: Kila mutu mwenye zambi. Ni huyu mutu, mwenye alitoka wakati moja toka nyumba ya baba wake, nikusema toka Paradizo.

Ulizo: Sisi tuko wote wenye zambi. Ni mutu moja, mwenye ataweza kusema ya kama hana mwenye zambi? Na, kama mutu ya kwanza Adamu alitoka ya Paradizo, sisi leo kwa ajili ya ma zambi yetu tunatoka toka ingine Paradizo. Ya wapi tunatoka?

Jibu: Toka Kanisa, iliyeiko Nyumba ya Mungu, na ilitupatia Mungu kuikala sisi, watoto wake.

Ulizo: Watu wa ngapi, wakijana wa ngapi, watoto wa ngapi waliepuka toka hii Nyumba ya Mungu! Walikokotwa toka ma sauti ya hii dunia ya hii uzima ya zambi wanaishi uzima upotevu! Lakini Mungu Baba wetu anasimama kupenda watu wote, wenye wanaepuka na wanatoka toka mapendo yake? Jibu: Hapana! Sawa vile, baba moja anapenda watoto wake na wakati walimuacha na walitoka ya nyumba yake, vile kuliko mingi anapenda Mungu watoto wake, nikusema sisi.

Ulizo: Mungu Baba wetu anaongolea watu wenye zambi wote. Na namna gani mutu moja mwenye zambi ataweza kurudia mu nyumba ya Mungu? Jibu: Na toba na ungamo ukweli.

Ulizo: Wakati huyu mwana mupotevu alikuwa mu jangwa mupango ninyi alikamata? Jibu: Alikamata mupango kurudia. Alisema: «Mitalamuka na mitarudia mukongo kwa baba wangu».

FUNDISHO: Inapaswa kurudia mu nyumba ya baba wetu.

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu. . . «(Luka 25, 18)

MATENDO KU UZIMA YETU. Kila zambi inaepuka toka Mungu. Mungu anatuita juu ya kuishi sisi kama warafiki Yake, na ma jerani, watoto na wariti wake, lakini sisi tunaepuka. Tunaharabisha ma zawandi wazuri, wenye, Yeye alitupatia, ma zambi na matendo mabaya.

Toka Parabole ya Mwana Mupotevu minataka bintu ya mbili kumionyesha juu ya kubakia ndani ya akili yenu daima.

1. Hii fundisho ya kwanza ni Ubatio ya Mungu. Baba ya hii Parabole alikimbia na alibatia mtoto yake ndani ya mikono yake. Ubatio ya Mungu ni wazi daima. Munaona Yesu Kristu, mwenye usulumbio. Mikono yake eko na wazi pa musalaba Yake. Anatuongolea sisi wote. Na yule baba mupotevu, mwenye aliacha bibi na watoto wake. Na huyu mwanamuke mupotevu, aliyeacha watoto wake na bwana wake na anafanya ma zambi mbali ya nyumba yake. Na wakijana wapotevu, wenye walitoka ya ma nyumba yao na wanazuguluka na ma kundi ya warafiki wao ndani ya magasin ya zambi. Tena na watoto wapotevu, wenye walikokotwa toka warafiki wao wenye zambi na walizombelea kufanya ma zambi ya kuachana. Kwa hawa wote watu Mungu ekona mikono yake wazi.

Ubatio ya Mungu hasifunge hata siku moja, ni daima wazi ya kila mutu.

Mulango ya Paradizo hasifunge. Hii wakati tunaishi mulango ni wazi. Na anaongolea Mungu, mwenye anatupenda. Kwa mapendo yake kwa sisi Mungu alichinja huyu mwana-ngombe. Ni nani huyu mwana-ngombe?

Ni Yesu Kristu, mwenye alitoa sandaka uzima yake juu ya wokovu wetu.

Yeye ni Mwana-kondoo, aliyekokota zambi ya dunia.

Basi, inatuongolea daima wazi ubatio ya Mungu juu ya kutupokelea na kutuongoza mu shamba ya Paradizo.

2. Fundisho ya mbili, inayepaswa kubakia daima kwa akili yenu toka hi

Historia ya Mwana Mupotevu ni machozi ya toba. Yoyote ma zambi wenye sisi tulifanya inasafisha Damu ya Kristu na machozi ya toba. Hakuna zambi moja, inayehasisamehe na toba. Muniseme mutu moja mwenye zambi, mwenye Mungu hasikumusamehe na Fumbo ya Maungamo. Hakuna. Kama utabeba moja kifulusi makala ya moto na utaitupa ndani ya bahari, nani itashinda makala ao bahari? Kweli, bahari. Makala ya moto itazimisha mara moja na watatoka.

Bahari bila mupaka ni mapendo ya Mungu. Makala ya moto ni ma zambi wetu. Kama tutabeba hii makala ya moto, nikusema ma zambi yetu, na tutaweka mu kifulusi ya toba na hii saa ya Maungamo tutatupa mu bahari ya mapendo ya Mungu, mu Huruma ya Mungu, yote, kabisa yoyote watazimisha na watasionekane.

Zaawandi ukubwa ngapi ni Fumbo ya Maungamo! Muwaze moja mungaga, mwenye anatupokelea kila wakati sisi tunapenda kumutembelea. Anatuangalia, anatutunza ya kila malari bila makuta. Na huyu munajua ni nani? Huyu ni Bwana Yesu Kristu. Kila wakati tunaweza kwenda kwake. Padri ya roho anatupokelea, anasikia ma zambi na makosa yetu, anatusauria na anatusamehe.

Wakati gani inapaswa kwenda mu Fumbo ya Ungamo?

Kwa Siku Kuu wakubwa, Ufufuo ya Kristu, Kuzaliwa Yesu Kristu na ma

Siku Kuu wakubwa ya Watakatifu wetu. Paka ile ma siku? Hapana, watoto wangu. Kwa mungaga tusiende paka beingine ma siku. Tunaenda kila mara tukona umivu na malari. Na kwa Ungamo ya Kanisa yetu inapaswa kwenda kila mara tunaanguka ku moja zambi. Na, kwa sababu tunakosana kila siku na ma macho yetu, na kinywa, na masikio na mikono na mikulu na akili na roho na yoyote mafahamu yetu na kwa hivi ni lazima kuungama kila wakati tunasikia ya kama tukona lazima kwa roho yetu. Tutapata padri ya roho moja, mwenye anapenda watoto na wakijana na tutamutembelea kila wakati.

Vile, kama tunanawa na machozi ya toba na Damu ya Yesu Kristu tunasikia furaha ya wokovu. Tazama moja sauti kizuri, ile tunaweza kuibeba sisi wote:

Ndawa juu ya kupata sisi wokovu ni paka moja: Machozi yetu na Damu ya

Kristu.

## FUNDISHO KUMI NA TISA
## MUTAKATIFU TIMOTHEO

(Mwalimu ni muzuri kusoma toka Matendo ya Mitume hii sehemu 16, 1-3, pahali atasoma muito ya Timotheo mu kazi ya Mungu toka Paulo. Tena iko muzuri kusoma na ma barua ya mbili ya Paulo kwa Timotheo).

NAMNA YA KUKARIBIA.

Mukona Kambo mwanamuke ku mulango? Ninyi ya mweye mukona Kambo mwaminifu, mutakumbuke ile ma Historia anamiambia hii wakati muko watoto wadogo.

Hii mafundisho anapanda mama na Kambo ndani ya roho ya watoto wao, hii mafundisho itabakia daima ndani ya ma roho yao. Tukona na watoto, wenye mbele ya kukuja ku hii Masomo ya Kanisa yetu, walisikia mafundisho wazuri toka ma mama na ma kambo wao.

Leo tutasema juu ya mtoto moja, mwenye alipata faida mingi toka kambo yake aliyekuwa mwaminifu ukweli.

HISTORIA. Jina ya huyu mtoto ilikuwa Timotheo. Alibakia yatima wakati alikuwa mtoto mudogo, kwa sababu baba yake alikufa. Alizaliwa na alipita miaka yake ku muji Listra ya Asia Udogo (Turkia leo). Hasikuje baba, lakini alijua mapendo ya mama yake, aliyeitwa Evniki na wema ya Kambo yake, aliyeitwa Loida. Mama yake pamoja na mazimba yake alipatia kwa mtoto yake na mafundisho ya Mungu. Mama yake alikuwa toka Kabila ya Yuda na alimuhubiri juu ya Mungu moja ukweli na ya kama atakuja mu dunia na Mwokozi yake, Yesu Kristu. Wakati alifunda kusoma Timotheo Kitabu ya kwanza iliyeisoma ilikuwa Madiko Takatifu. Kambo Loida, Mama Evniki na mtoto yake Timotheo ilikuwa jamaa moja takatifu ndani ya muji Listra. Watu wote walipenda na walitukuza hii jamaa. Kabisa walitukuza Timotheo, kwa sababu ilikuwa mtoto mwenye akili na mufazili. Alikuwa moja mtoto ukweli ya Mungu. Pamoja na mazimba ya mama yake alikunywa na mazimba ya imani kwa Mungu. Alisoma Sheria ya Mungu. Kabisa ilimupendeze ma sauti ya wa Nabii juu ya mafikisho ya Mwokozi ya dunia.

Ee Mama wangu, alimuliza, wakati gani atakuja huyu Mwokozi? Alitaka kufamia Mwokozi na saa ilikuja kumufamia. Namna gani? Siku moja mu muji Listra ilitangazwa kavumu moja ya kama alikuja moja mutu muebrania, mwenye alihubiri juu ya Bwana Yesu Kristu. Huyu mutu toka kabila ya Ebrania alikuwa Mutume Paulo, Mutume ya dunia. Na moja bakora ku mkono yake alizuguluka na alihubiri juu ya Yesu Kristu aliyesulubiwa juu ya wokovu ya watu wote ya dunia. Alikuja na ku Muji Listra. Mu Sinagogi ya wa Ebrania walisanyikwa watu mingi kumusikia. Katikati yao ilikuwa na hii jamaa takatifu: Loida, Evniki na mtoto Timotheo. Hawa walikuwa toka wale waliamini na walibatiziwa ya kwanza kwa hii muji yao. Kabisa Timotheo alifurahi sana kwa ajili ya hii kuhubiri ya Paulo. Ndani ya roho yake ilizaliwa moja matakio nguvu.

Hii wakati tuko ku mwaka 49 kisha ya kuzaliwa Yesu Kristu. Wa Kristiani wadogo toka muji Listra wekona furaha moja. Wanaongolea mwalimu wao. Ndivyo, Paulo alifanya safari yake ya mbili kwa hii muji yao. Anatembelea ma muji pahali hii mara ya kwanza alipita na alifungula ma Kanisa. Sasa anataka kuona wa Kristiani yake, kuwapatia fundisho mupya na kuangalia mandeleo yao kwa hii uzima mupya ya Kristu. Wote wanamuongolea na matakio mingi na kuliko mtoto Timotheo. Mawazo ya kama ataangalia mara ya mbili Mwalimu yake inayala roho yake na furaha mingi. Lakini na moja ingine mawazo inazuguluka ndani ya akili yake. Kama atakuja Paulo atamwambia hii mawazo yake. Lakini itatimizwa hii matakio alikuwa na ndani yake?

Sasa Paulo eko katikati ya wa Kristiani ya muji Listra. Kisha makutano na mazungumuzo yao, Timotheo alibakia ku mwisho juu ya kuona na kusuburia na Mwalimu yake. Mutume Paulo mukubwa anasuburia na huyu kijana mwaminifu. Paulo anaonekana mwenye furaha. Wakati mingi sasa anatafuta wasaidizi wake. Kazi ya Kanisa ilizambalisha fasi ya mingi. Paka yeye mwenyewe hanenee. Inapaswa kusaidia na weingine. Na, tazama, sasa anasikia matakio ya Kijana Timotheo:

Minataka kufanyika mutume ya Mungu (misionaire). Kama munazania ya kama ni mustahili kumifata fasi yote mutaenda. Matakio yangu ni kutumika Mwokozi wetu Yesu Kristu.

Mtoto wangu alimujibu Paulo, matakio yako ni kizuri na takatifu.

Bwana Yesu aliipanda ndani yako. Lakini inapaswa kuuliza na nyumba yako, mama na kambo yako.

Yote wa wili pamoja sasa walibeba njia juu ya kufika mu nyumba yake.

Wanawake wa mbili walisikia na furaha hii matakio ya mtoto wao. Walikuwa na paka huyu mtoto. Alikuwa Timotheo yeye wa pekee mulinzi ya nyumba yao na walimupenda mingi. Lakini waliichika na walitoa mtoto yao mu kazi ya Mungu.

Mtoto wetu, uende muzuri na maombi na baraka yetu, walimwambia Mama na Kambo yake. Uende kwa hii kazi anakuita Evangelion ya Kristu. Usiwaze tutafanya ninyi sisi. Mungu atatulinzi. Furaha yetu munene itakuwa kama tunasikia namna gani unatembea mukongo ku mwendo ya Mwalimu mukubwa yako.

Na wakati walimwanbia hivi, walinamisha na walibushu mtoto wao mupendwa mara ya mwisho. Na yeye alibusu mkono ya mama yake na kambo yake. Aliwasalimia alitoka daima ya nyumba na mama yake na alifata Mutume Paulo, mwenye alikuwa na lazima munene toka wasaidizi wakijana na wafwasi wake.

Paulo na Timotheo walitoka ya muji Listra. Mbele ya kutoka Paulo alipenda kusikia matangazo ya weingine watu ya muji Listra juu ya huyu mtoto Timotheo. Lakini watu wote walimwambia ya kama Timotheo alikuwa na mufano ya uzima muzuri ndani ya muji yao. Watu wote walijua mtoto ya mama Evniki, mwenye alisoma Madiko Takatifu na alikuwa uzima safi na uso ya mwangaza.

Sasa Timotheo alimufata Paulo kwa kila safari yake. Pamoja walienda ku muji Filipo ya Makedonia, ku muji Korintho, Yerusalema. Tena pamoja walienda ku muji Roma ya Italia. Pamoja kila siku na pamoja kwa kila mateso na sikitiko yao. Timotheo alikuwa mushuhuda ya ile mateso alivumilia mwalimu yake Paulo. Alimusaidia mu kazi yake kila siku. Bila kuchoka.

Lakini ilifika na hii siku, pahali ilipaswa kuachana mwanafunji toka mwalimu yake. Bila kuomba sifa na cheo, Paulo alimupandirisha Timotheo padri na kisha wakati kiloko alimupatia na cheo ya Askofu na kipimo yake udogo. Alimuweka askofu ku muji Efeso ya Asia Udogo (Turkia leo). Mapendo yake mu kazi ya Mungu ilikuwa munene kabisa. Na neema ya Mungu ilikuwa mingi. Na ma huitaji ya mingi. Timotheo ekona lazima ya saidio na ya hii mambo Paulo aliikala na aliandika ma barua ya mbili kwa Timotheo. Ndani ya hii ma barua Paulo alimuita Timotheo mwanafunji wake mupendwa na ukweli.

Sasa tuko ku mwaka 67 kisha ya kuzaliwa Bwana Yesu. Ilipita wakati ya miaka 20 tangu hii mwaka Paulo alipita ku muji Listra na alibeba karibu yake Timotheo. Sasa Paulo iko ndani mu buloko ku muji Roma juu ya mapendo ya Kristu. Ni muzee sasa. Ma nywele yake ni mweupe na

anasikia ya kama mwisho yake inakuja. Anajua ya kama hasitatoke inje ya buloko muzima. Toka chumba yake ya buloko watamuongoza ku lufu na mateso. Ndani ya buloko, basi, aliikala na aliandika barua ya mbili kwa Timotheo. Anaandika kwa Timotheo mupendwa wake ma sauria ya mwisho. Katikati ya hii masauria yake anamuandika hivi:

Mtoto wangu Timotheo, uko muaskari ya Kristu. Inapaswa kujua ya kama na weye utateswa kwa Jina ya Kristu, sawa vile na mimi minateswa na niko ya kufungwa ndani ya buloko kama munyanganyi.

Ndani ya hii barua, tena anamuandika kuhukumu kila zambi inayefanyikwa mbele ya watu wa mingi.

Na kweli, ile wakati ku muji Efeso waliwabudu sana mungu moja mwanamuke, aliyeitwa Afroditi. Mutume Paulo aliisha kuhukumu na kuhubiri kontre ya kuwaabudu Afroditi. Wapagano juu ya kumusifu mungu mwanamuke Afroditi walifanya ma zambi wanene, walivaa manguo ingine, walicheza kama mazimu, walikunywa, walilewa na walitembea mu njia kama mazimu na wenye shetani.

Timotheo askofu hasikuweze kuvumilia hii hali ya muji yake. Mwaka moja, ile siku watu ya pagano walisha kusanyikwa juu ya kufanya shangilio yao.  Timotheo alisanyika wa Kristiani wote, aliwahubiri nguvu na kisha aliwaita kumufata.

Mukujeni karibu yangu, aliwaambia. Saa ilikuja kupatia ushuhuda wetu mbele ya wapagano. Askofu pamoja na wa Kristiani walitembea kufika karibu ya ile kundi ya wapagano. Mbele ya ma macho yao inaonekana kundi ya wapagano. Timotheo anasimama. Pamoja na wa Kristiani ya muji yake wanafunga njia na wanasimama pale bila kutengwa. Watu ya sanamu wanashangaa. Kisha walishirika. Wanapima kutembea katikati yao, lakini hakuna namna. Askofu Timotheo anawahukumu na anawafundisha bila boka.

Hii ma shangilo yenu ni haya. Ma mungu wenu ni ya wongo. Mutubuni!
Murudia kwa Mungu ukweli. Yeye ni Bwana Yesu Kristu.

Sasa muwaze, watoto wangu, mambo ninyi ilifanyikwa hii saa! Wapagano, kwani waliisha kulewa, walifika kwa askofu Timotheo na walianza kumupika kama wenye shetani. Weingine walianza kupika wa Kristiani. Kisha saa kiloko Timotheo alianguka chini ya bulongo. Walimufanyisia ma bilonda ya mingi. Uso yake ilikuwa ya kuyala na damu juu ya ma kofi na maimbwe walimupika sana.
Lufu! Lufu! kwa adui ya ndini yetu! Walifokea watu ya pagano.
Timotheos aliwaangalia na macho wasafi na kuyala na mwangaza ya Mungu.

Damu yake ilimwanga hii njia. Pamoja na ye na weingine wa Kristiani walianguka chini na ma bilonda mingi na damu ku mwili yao ilitelemuka.  Askofu Timotheos na beingine wa Kristiani ndani ya hii njia waliacha pumuzi ya roho yao ya mwisho, bila kuichika kwa hii shangilio ya wapagano. Walichakula lufu na hapana kupitisha hii kundi yao ya wapagano.

Hii ilikuwa mwisho ya yule mtoto, toka muji Listra, mwenye alifata Mutume Paulo. Kanisa yetu anafanya makumbusho yake mu tarehe ya 22 Mwezi ya kwanza kila mwaka.

***MAELEZEO:***

Ulizo: Fasi wapi tulikutana mara ya kwanza Timotheo?

Jibu: Ku miji Listra ya Asia Udogo. Alimupata Mutume Paulo mu safari yake ya mbili.

Ulizo: Mukumbukeni nani alipanda imani ya Mungu ndani ya roho ya huyu mtoto?

Jibu: Mama yake Evniki na Kambo yake Loida.

Ulizo: Ma barua ya ngapi alimutuma Mutume Paulo?

Jibu: Wa mbili. Na tena mu barua yake ya mbili alimwambia ya kama atakufa na mateso mingi.

Ulizo: Ndani ya muji gani alikufa na mateso?

Jibu: Ku muji Efeso ya Asia Udogo. Yeye ni askofu ya kwanza ya hii muj.

Ulizo: Ilikuwa ninyi maneno ya lufu yake katika mateso?

Jibu: Pamoja na wa Kristiani wake alienda kuhukumu na kuzimbiria watu wa pagano na kundi yao.

Ulizo: Tunaweza sisi wa Orthodoksi leo kufata moja kundi ya wapagano na wa Kristiani na ma Kanisa ingine, wakati wanafanya mashangilio yao?

FUNDISHO: Inapaswa kuishi mbali ya kila shangilio ya mapagano na ya waKristiani ya ma Kanisa ingine ya wongo.

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Watoto wadogo, mujilinde nafsi zenu kwa sanamu» (Barua ya kwanza ya Yoanne 5, 21)

***MATENDO KU UZIMA YETU.***

Leo iko mashangilio ya wapagano na ma kanisa ingine? Ndivyo iko. Watu wote wanaongolea hii wakati ya ile mashangilio juu ya kufurahi na kucheza. Lakini, musisahabu, watoto wangu, ya kama kintu ingine ni watu ya dunia na kintu ingine ni Kanisa ya Kristu.

Kanisa ya Kristu haina fasi moja ya kucheza. Iko fasi takatifu, pahali tunaweza kutubu, kubeba ma Fumbo Takatifu na kutuokolewa. Lakini ma kanisa ingine hakuna boka ya Mungu ndani, hakuna heshima, hakuna imani ukweli, hakuna upole. Watu wanaingia pale, kisha sala kiloko, wanaanza kucheza.

Sisi, watoto wangu, tusiweze kuingia ile ma kanisa, kwa sababu ndani ya kanisa tunaingia kubeba furaha ya roho na hapana furaha ya mwili yetu. Furaha ya mwili tutabeba inje, kisha Ibada yetu ndani ya Kanisa yetu. Kanisa ni nyumba ya Mungu na hapana centre ya kucheza.

Pasopo mingi, watoto wangu, sisi tutaishi na Mapokeo takatifu ya Kanisa yetu Orthodokse. Hatunana lazima kufurahi na furaha ya dunia inje ma fasi pahali anacheza shetani na watu pamoja. Furaha yetu ndani ya Kanisa yetu ni furaha ya akili na roho, furaha ya mbingu, furaha ya kama tukona kitumaini, kama hapa tutaishi muzuri, ya kama tutaingia kwa ufalme ya Mbingu. Hii furaha ya roho itatupatia Kanisa yetu na Ma Fumbo yake.

## FUNDISHO MAKUMI MBILI
## MUSHAHINDI YA KWANZA STEFANO

***NAMNA YA KUKARIBIA***

Munaweza kuwaza moja meza, pahali wanaikala wa kristiani ya kanisa moja? Ndivyo, Iko namna hapa. Kama tukona shangilio na makumbusho ya Mutakatifu moja ku mukini moja padri ya hii kanisa na walimu na wa Kristiani wote, kisha Ibada ya Liturgia takatifu, wataikala na watakula pamoja. Watakula kama moja jamaa, sawa vile walifanya na wa Kristiani ile wakati ya kwanza mu Yerusalema. Lakini hii kazi ya kukula pamoja wa Kristiasni wote ilileta mambo ya mbili: Namna gani watapata makuta ya hii meza ya chakula kila siku. Lakini hii mambo tulifundisha ku fundisho mu Juma ilipita. Wa Kristiani nikusema, waliuzisha ma shamba yao na walileta makuta kipande moja ao yote kwa mikulu ya wa Mitume. Mambo ya mbili ilikuwa hii: Nani atasubuka hii ma meza? Nani atakabula ma chakula yao? Ku fundisho yetu ya leo tutaangalia wale waKristiani na wa

Mitume ya kwanza walifanya ninyi HISTORIA. Wa Mitume ku mwanzo ya Imani ya Kristu walitumika kuhubiri na mategenezo ya chakula ya waKristiani wote. Lakini pole-pole waliogezekwa waKristiani na wa Mitume habakuenee. Tena beingine waKristiani walisikitika kwa sababu walisema ya kama habakukule muzuri. Kwa hivi wa Mitume waliitawa Kristiani wote ku moja makutano na waliwaambia:

Ee Wanduku wetu, haina kazi kizuri kuacha sisi Kuhubiri ya Mungu juu ya kutumika na ma meza ya chaskula yenu. Mweye katikati yenu mutachakula wanaume wa saba, wenye wanawafamia watu wote, weko watu ya mwangaza ya Mungu na waliyala na nuru ya Roho Mtakatifu. Mweye mutawachakula na sisi tutawaweka wakubwa ku hii kazi ya chakula yenu.

Wa Kristiani walisikia sauria ya wa Mitume na walichakula wanaume wa saba. Hawa walikuwa wa shemasi saba ya kwanza. Hii ni cheo ya kwanza ya Upandirisho mu Kanisa yetu. Wa shemasi ya saba walikamata kazi yao ndani ya Kanisa. Walitumika ku matayarisho ya chakula ya wa Kristiani wote na wakati walikuwa uhuru saa walihubiri neno ya Mungu. Katikati yao kuliko mwenye mwangaza na mtakatifu alikuwa moja aliyeitwa Stefano. Ni stahili sasa, watoto wangu, kusikia kiloko Uzima yake.

Stefano mutu nani alikuwa? Alikuwa kijana moja aliyeyala na neema ya Roho Mtakatifu. Roho yake iliisha kuyala na imani mingi. Alitumika na mapendo mingi ku kila kazi. Alikimbia kusaidia wamasikini, wagonjwa na waKristiani wote. Wakati aliisha kazi ya kutayarisha na kukabula chakula ya wa Kristiani wote, kisha aliendа mbio kufanya kazi ingine, kuhubiri neno ya Mungu. Alikwenda ndani ya ma Sinagogi ya wa Ebrania na alihubiri fundisho na uzima ya Kristu.

Siku moja watu wa Ebrania wakati aliisha kuhubiri yake Stefano, walilamuka na walibisha mbele ya Stefano. Walizania ya kama watamushinda kwa kuhubiri yake. Stefano alifungula ma macho yake. Alihubiri na hekima mingi katika nuru ya Mungu na watu wa Ebrania wote walifunga ma kinywa yao. Stefano aliwashindi na kuhubiri yake na beingine watu wa Ebrania waliamini kwa Kristu.

Lakini hii ushindi ya Stefano beingine watu ya Ebrania habakuweze kuivumilia. Waliona Stefano kukokota taifa yao kwa imani ya Kristu. Walishirika na kisilani mingi walikimbia kumutafuta. Na wakati walimupata, walimokokota na walimupeleka mu nyumba, pahali wakubwa wao walisuburia mambo yao, nikusema ku makutano ukubwa yao. Ndani ya hii Makutano walikuwa wote wakubwa wao, wa askofu wao, walimu, wafarisayo na wanandishi ya Sheria yao. Wale wote walisanyikwa pale kusuburia na kuhukumu Stefano na kazi yake. Wale walimukokota Stefano, walilalamika mukusema:

Sisi tulimusikia kuchabulana Musa mukubwa yetu na Mungu wetu.

Tulimusikia kuchabulana Hekalu yetu na anataka kugeuza kutim na zwezo yetu ya imani yetu. Ndivyo, huyu ni adui ya Sheria yetu na ya Mungu.

Fasi wapi inafika chuki na kisilani! Walifika mpaka kumusitake, ya kama alichabulana Mungu. Nani? Huyu Stefano alimuheshimiwa Mungu na alimupenda na roho yake muzima na alikuwa tayari kutoa na uzima yake kama sandaka kwa Mungu! Tena waliripa washuhuda na waliwaweka kushuhuda ya kama kweli Stefano amechabula Mungu na Nabii Musa.

Na Stefano? Alisimama na upole na amani katikati yao. Atawajibu ninyi?

Aliwajibu uso yake takatifu na kuiyala na amani na neema ya Mungu. Ni kweli, ya kama beingine habakuweze kuona Uso yake, iliyebeba mwangaza kimungu. Tena walisema katikati yao:

Muone, namna gani Uso yake inaangaza!

Lakini wale walimuchukia, waliomba malipizi yake. Na askofu alianza kusema mbele ya Stefano:

Ukona kusema ninyi juu ya hii ma sauti yao? Ni vile, sawa hawa wanasema?

Na hii saa Stefano alifungula kinywa yake. Mara ya kwanza walisikia kinywa moja wakubwa ya Ebrania, iliyejua yote fundisho ya Agano la Kale. Sauti ilitoka ya kinywa yake kama mutoni. Alianza kusema juu ya Abrahamu na matendo ya miujiza ile walifanyikwa ile wakati yake. Namna gani Mungu aliita Abrahamu, namna gani waliishi wa patriarhe Abrahamu, Isaaki na Yakovo. Kisha aliwaambia namna gani aliishi Yosefu, mtoto ya Yakovo mu Inchi Misri, namna gani alitukuzwa na aliokoa wa nduku wake toka njaala. Kisha namna gani waliogezekwa watu ya Kabila yao Israeli mu inchi Misiri. Kisha aliwahubiri juu ya mukubwa Musa, namna gani yeye aliona muujiza ya ile muti, pahali ililugua bila kuilugua na namna gani Mungu alimuita kuwa mukubwa ya taifa yao. Kisha aliwahubiri namna gani Musa aliita Taifa yao kutoka toka Misiri na kurudia ku Inchi ya Palestina. Tena aliwambia mara ya ngapi watu ya Kabila yao mu njia ya kwenda mu Palestina walisahabu Mungu na waliwabudu ma sanamu ya watu ya pagano. Kisha alisema juu ya Yosua ya Nuni, Sanduku ya Jipya, Daudi, Solomo na namna gani ilijengwa Hekalu yao. Kisha aliwahubiri juu ya wa Nabii na namna gani taifa yao waliwafukuza wa Nabii wao.

Hii yote mafundisho ya Agano la kale alisema Stefano juu ya kuwaonyesha bintu ya mbili:

Hii ya kwanza ya kama Mungu anapenda Taifa Yake na anatuma kila wakati watu wake na anafanya daima miujiza. Na hii ya mbili: juu ya kuwaonyesha ya kama wakubwa ya Israeli daima walifukuza wa Nabii na Watakatifu ya Mungu. Na alisimama kwa Usulumbio ya Kristu, iliyeifanya wa nduku wao ya Ebrania. Lakini mbele ya kuwaambia hii kazi mubaya waliifanya kontre ya Bwana Yesu Kristu. Uso yake iligeuza. Alisuburia na namna makari na ma sauti yake walitoka ya kinywa yake kama kogoloma. Hasikuwaze ya kama mbele yake walikuwa wote wakubwa ya Taifa ya Ebrania. Ilikuja saa kuwaambia fundisho ukweli. Musikie, watoto wangu, ma sauti ya Stefano ile alisema kontre ya wakubwa ya Ebrania:

Ninyi wenye shingo gumu, musiotahiriwa katika mioyo, wala masikio, siku zote munashindana na Roho Mutakatifu: Kama baba zenu walivyofanya, na nin yi vivyo hivyo. Ni nani katika manabii asiyeteswa na baba zenu? Nao waliua wale waliotabiri habari za kuja kwake yule Mwenye Haki; ndiye ninyi sasa mumekuwa wahani wake, mukamwua. Ninyi muliopokea torati kwa amri ya malaika, wala hamukuishika».

Musikie, watoto wangu, ile saa mambo ninyi ilifanyikwa ndani ya makutano wao. Walisirika. Walifanyikwa kama ma nyama makari. Walimusagia ma meno yao kwa hasira. Walikuwa tayari kumupika na ma kofi wao.

Hii saa, wakubwa ya Makutano yao walikuwa na makari mingi na walitaka kumupika, Stefano aliyala na utukufu ya mbingu. Aliona moja vision mbele ya macho yake. Aliona utukufu wa Mungu na Yesu alisimama upande wa mukono wa kuume wa Mungu. Alisema: Tazama! ninaona mbingu zimefunguka, na Mwana wa watu amesimama mukono wa kuume wa Mungu.

Wakati walisikia wakubwa ma sauti ile ya Stefano, waliacha ma kiti yao na walifika kumusukuma inje. Walianza kumupika na maimbwe. Mbele walitosha manguo yao ile ya inje juu ya kumupika bila kuchoka mingi. Na walimwambia kwa mutu moja aliyeitwa Saulo juu ya kuchunga manguo yao. Kisha wakati kiloko huyu kijana Saulo atageuza jina na mufano ya uzima yake na atafanyika huyu Mutume Mukubwa Paulo.

Stefano anaona ya kama mwisho ya uzima yake ni karibu. Alifanya ma sala ya mbili: Moja ni hii: Ee Bwana, pokea roho yangu». Na sala yake ya mbili ni hii: « Bwana, usiwahesabie zambi hii». Ile saa alikuja mbele yake Mufano ya Bwana Yesu Kristu, mwenye yulu ya musalaba alisamehe wale walimusulumbia. Vile na yeye alisema mbele ya wale walimupika na kisilani. Maimbwe walitupa pa mwili yake wakubwa ya Ebrania kama nvula na waliizimbiria. Nafsi yake alipanda mbinguni.

Wa Kristiani busiku walienda kwa siri, walikamata maiti takatifu yake na waliimazika na heshima na mapendo mingi.

***MAELEZEO:***

Ulizo: Nani alikuwa Stefano?

Jibu: Alikuwa moja shemasi katikati ya weingine ya saba, aliyekuwa na neema ya mungu mingi na hekima takatifu.

Ulizo: Juu ya ninyi wakubwa ya Ebrania walikokota Stefano mu nyumba ya Uhukumu?

Jibu: Kwa sababu alihubiri Fundisho ya Yesu Kristu.

Ulizo: Stefano alifanya kazi moja kibaya na walimuweka pa kiti ya kumuhukumu? Jibu: Hapana. Yeye alikuwa na kuyala na mapendo na utakaso. Alisaidia wa masikini na alihubiri huu ya fundisho ukweli ya Kristu.

Ulizo: Lakini walimusimanga na walimuhukumu kama adui wao. Kisha walimwua na maimbwe. Lakini Stefano namna gani aliripa wale walimupika na walimwua? Jibu: Sawa vile Kristu aliripa wale walimusulumbia. Nikusema Stefano alipika magochi na aliomba kwa Mungu kuwasamehe wale walimwua. FUNDISHO: Inapaswa kusamehe wale wanduku walitufanyisia kazi moja kibaya. SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Bwana, usiwahesabie zambi hii» (Matendo ya Mitume 7, 60)

MATENDO KU UZIMA YETU. Mukona watu, wenye walimichukia, walimichabula na walimisimanga? Munaweza kunisema bila kusema ma jina yao.

Mtoto moja aliniuzi mbele ya watoto weingine. Mwingine mtoto alinichokoza.
Moja nduku ya ma jerani wetu aliisha kufanya kazi moja kibaya ndani ya jamaa yetu.
Moja mtoto ya hii daraja yetu alisema ma sauti ya wongo kontre kwangu na mwalimu alinilipiza bila mimi kukosa.
Hii mambo sasa mweye muliniambia shetani anafanya ninyi? Anatuonyesha hii mambo kupita munene na anawaakisha ndani ya ma roho yetu chuki na hali ya roho kibaya. Mara ya mingi tunakamata sisi mupango ya kama hatutasuburie na huyu mtoto ao mutu fulani ao tunakamata mupango kumufanyisia na sisi moja kazi kibaya kontre kwake.

Mimi, misitamusamehe huyu mutu. Misitasuburie na yeye mara ingine.
Misipende kutegeneza mapendo pamoja na yeye.

Kama tunawaza na tunafanya hivi, watoto wangu, tunaonyesha ninyi? Ya kama tusiko tena wa Kristiani wakweli. Hatufate uzima ya Kristu na ya Mtakatifu Stefano. Kristu alisamehe wale walimusulumbia. Vile alifanya na Mtakatifu Stefano. Wale watoto ao watu walituchukia, ao walituuzi, walitusulumbia? Hapana. Basi, juu ya ninyi sisi tunakatala kuwasamehe? Namna gani tutasema ya kama tuko watoto wakweli ya Yesu Kristu?

Iko namna kuniambia mtoto moja: Yesu Kristu alisamehe wa nduku wake, kwa sababu alikuwa Mungu, lakini tuko watu ya bule.
Tazama, lakini leo, tuliona na mutu moja huyu kijana Stefano, mwenye alifanya hii kazi alifanya na Yesu Kristu. Na yeye alisamehe wale walimwua na maimbwe.

Kama tusisamehe wale watu walitufanyisia kazi moja kibaya, tunasema na wongo wakati tunaomba kwa Mungu. Tunasema ninyi? « Utusamehe makosa yetu, kama sisi tunavyowasamehe waliotukosea».

Leo, watoto wangu, tutaenda kuomba hurumia toka wale watu tulipata zamani mambo moja ya sikitiko. Haina mambo kama kosa walifanya wale. Sisi tutaonyesha mapendo ya hurumia yetu na vile tutasikilizana muzuri. Vile na ma roho yao italekea na kisha na wale watatuomba hurumia na usamehe. Vile itawala amani na mapendo ukweli ndani ya ma roho yetu.

# FUNDISHO MAKUMI MBILI YA MOJA
# WATOTO YA SABA WENYE WANAITWA MAKAVEI

NAMNA YA KUKARIBIA.

Watoto wa nani mukona wa nduku yulu ya ine?

Miye! Sisi mu jamaa yetu tuko wa nduku tano, saba, mnane. .

Tunafurahi, watoto wangu, kama tunasikia ya kama weko wazazi, wenye walizala watoto ya mingi, kwa sababu watoto ni moja baraka munene ya Mungu. Wazazi wenye wekona watoto wa mingi weko wabarikiwa na kabisa, kama watoto wote weko karibu ya Mungu na ndani ya Kanisa yetu.

Hii Historia mutaisikia leo itakuwa juu ya walinzi ya ma jamaa na watoto mingi.

HISTORIA. Tuko mu wakati watu ya Ebrania walikuwa watumwa kwa mfalme Andiohos, aliyekuwa mufwasi ya Aleksandros Mukubwa. Antiohos alikuwa mfalme mugumu. Aliwachukia watu ya Ebrania, kwa sababu waliwabudu Mungu ukweli.

Wakati moja Taifa ya Ebrania aliomba uhuru yake, lakini mfalme Antiohos aliwalipiza. Aliwua makumi mnane ma elfu watu waebrania (80. 000). Tena alikamata mupango kulipiza wale waebrania ku Ndini yao.

Siku moja alimaliza moja programe yake juu ya kuwua waebrania wote.

Mbele ya wakubwa na watumishi wake alipatia hamuri yake kuleta masahani ya mingi na ndani yao manyama ya ngurumbe, juu ya kukula watu ya Ebrania. Lakini, sawa munajua na mweye, watoto wangu, taifa ya Ebrania hasikule nyama ya ngurumbe kwa sababu inawatakaza Sheria ya Musa mukubwa yao. Wa mingi watu ya Ebrania wanachakula lufu na hapana kutii kwa hamuri ya Antiohos. Lakini beingine, kwa ajili ya boka, juu ya kuokoa uzima yao, wanaichika kukula hii nyama.

Kisha saa kiloko walileta mbele yake mutu moja muzee, miaka 90. Uso yake ilikuwa upole na muheshimiwa. Richo yake ilikuwa na amani na nguvu kwa mupango yake. Jina yake ilikuwa Eleazaro.

Ee Muzee, mwenye akili ya Israeli, kuja hapa karibu, alimwambia Antiohos.

Yule anakarimbia.

Kula, basi, ya hii nyama na mitakuuhuru mara moja. Na hapana paka hii, lakini mitakupatia na ma zawandi na ma cheo ya mingi.

Eleazaro hasitii. Anasimama mbele ya mfalme bila kuogopa ma sauti matata yake.

Munilete mbio fimbo. Iko wapi fimbo, alilalamika mfalme Antiohos.

Damu inatelemusha kama mutoni toka mwili ya huyu Muzee, lakini hasiichike. Hasilekee. Ku mwisho, wakati aliona ya kama nguvu ya mwili yake ilibakia kiloko alipaza sauti na alisema mbele ya wale watu ya Ebrania walimuona:

Watoto ya Israeli, musiitii huyu muzulumu. Ni kuliko muzuri kukufa, na hapana kukatala hamuri ya Ndini yetu, hamuri ya kwarezima. Vile alinamisha kichwa yake na alitoa nafsi yake kwa Mungu.

Antiohos alishindwa toka moja muzee na ma nywele mweupe. Kisha saa kiloko atashindwa na beingine watoto wadogo. Na hasira mingi alihamuru kuleta mbele yake na beingine watu ya Israeli. Wa askari walisukuma na walipika moja kundi ya watoto ya saba. Pamoja wanakokota na mama yao, aliyeitwa Solomoni.

Musiogope, mukujeni karibu tena, aliwaambia Antiohos. Minashangaa juu ya utukufu ya mwili yenu na minatakia huyu mama, aliyemizala. Muangalie muzuri, musifate na mweye hii mufano ya

huyu muzee mumbafu Eleazaro. Kama mutanisikia, mutafanyika warafiki wangu. Mitamipatia ma sifa na ma cheo ya inchi yangu. Mutaishi na furaha na heri kabisa. Lakini kama mutakatala kukula hii nyama ya ngurumbe, hii saa ole kwenu, ole kwenu! Mutakufa wote na mateso matata kabisa.

Na, kwa sababu alitaka kuwaogopa, alihamuru na walimuletea mbele yao makisu, makoleo, mafimbo na mupeto, wenye walikuwa pembeni yao misumari. Lakini wale wanaume ya saba walibakia bila kuogopa mateso. Wanasandiki bila shaka kwa mapenzi ya Mungu, ku hamuri ya Ndini yao.

Saa inapita. Mfalme anaongolea bila uvumilia. Hii sanduku mukubwa wao alimuuliza:

Ee Muzulumu, unaongolea ninyi? Hii kazi unawaza kuifanya, fanya mbio.

Sisi wote tuko tayari na tunatakia kuliko kutoa uzima yetu sandaka kwa Mungu na hapana kukanyanga ma hamuri ya Sheria yetu.

Antiohos anafanyikwa kama nyama ya pori. Ya kwanza anaona hii nguvu ya watu wakijana. Anapaza sauti na anasema: Mumubebe huyu toka hapa. Mbio ku mateso. Na mateso inaanza. Ya kwanza walimupika bila taambu. Walimukata lunrimi yake. Na makucha ya kiuma wanatosha ngozi toka kichwa yake, wanakata mikono na mikulu yake na ku mwisho walimuweka ndani ya kiungu munene juu ya kumukalanga muzima. . .

Wa mingi katikati ya watu ya Israeli wanasikia umivu. Beingine wanahukumu huyu kijana kwa sababu alikatala kukula kiloko nyama na sasa watamukalanga ndani ya hii kiungu munene. Hii mateso waliona na mama na wa nduku wake. Lakini hawa habaogope, wanatukuza Mushahindi nduku wao. Wanapika magochi na wanaomba kwa Mungu kusaidia na nduku wao na maugu wao kisha, wakati itaanza na mateso yao. Na nduku yao, wakati alikuwa ndani ya kiungu aliangalia wa nduku wake na aliwapatia nguvu na uvumilia. Kisha saa kiloko mwili yake yote iliisha kulugua. Paka na nafsi yake alipanda yulu, kwa Mungu.

Mbio, mulete hapa mtoto mwingine, alisema mfalme na sauti makari.

Walimukamata mwingine mtoto, walimufunga na walianza kupasula mwili yake. Kisha walimutupa ndani ya hii kiungu juu ya kumukalanga muzima. Sasa inakuja mustari ya nduku ya tatu. Na yeye anatembea na nguvu mbele ya wa askari wapagano. Mbele ya mfalme alimwambia:

Unaongolea ninyi, ee muzulumu? Unapotea wakati yako, kama unaongolea kugeuza imani yangu.

Wa askari ya mfalme na ruhusa yake walimunyanganya na walimwua ndani ya mateso mingi. Kisha nduku mwingine ya ine ya tano, wanateshwa na mateso ya kuachana. Lakini ku mwisho wanaweka wote ndani ya hii kiungu juu ya kuwakalanga. Wote kama samaki wanawakalanga na hawa wanavumilia na namna ya ajaabu hii mateso ya mwisho.

Ilifika sasa na mustari ya mtoto ya sita.

Huyu mtoto mitamulekea, anawaza Antiohos. Na moja mucheko ya wongo alimuita kukuja karibu yake.

Usizanie, ee mfalme, ya kama utaweza kunishinda na ma sauti yako ya butamo ao na ma sauti ya makari. Na mimi nikona umoja imani pamoja na wa nduku wangu na minataka kufa sawa vile na hawa. Misiweze kukanyanga hamuri ya Mungu juu ya kwarezima.

Kisha saa kiloko na huyu nduku wa sita aliisha uzima yake na mateso ile ya wa nduku yake. Sasa alibakia huyu mtoto ya mwisho, muloko yao. Antiohos alimuangalia na anawaza ya kama ni teketeke kumugeuza mufano yake.

Mtoto mudogo wangu, kuja karibu yangu. Mimi minakupenda na minataka kusaidia ku uzima yako. Kula kiloko ya hii nyama muzuri. Penda maugu yako. Mitakupatia ma zawandi ya mingi. Lakini, kama usikule, angalia mateso gani wanakuongolea. Angalia wa nduku wako wote walikufa.

Mtoto mudogo hasiseme kintu. Anaangalia mfalme na richo yake ya kumuzarau. Tena anaangalia na mama yake, mwenye hii saa aliangalia mateso ya watoto wake na uvumilia na imani ya Mungu.

Kuja, alisema Antiohos kwa mama yake, kuja kusauria mtoto yako kukula kiloko nyama juu ya kuokolewa. Usisikitike kama atakufa na huyu mtoto yako ya mwisho?

Solomoni anakaribia. Alibatia mtoto yake kwa mikono yake na, kwa sababu hasipende kusikia mfalme alimusauria ninyi, alisuburia na yeye mu lugha kiebrania.

Mtoto mudogo wangu, alimwambia, mimi milikuzala na milikukomea.

Unakumbuka ngapi ma sala milikufundisha. Unakumbuka mara wa ngapi milisuburuia na weye juu ya Mungu na Hamuri yake? Unakumbuka mara ngapi uliniambia ya kama unapenda Mungu? Basi, huyu mfalme anataka kukanyanga weye hii hamuri ya Mungu juu ya kwarezima. Anataka kukuwaambia kukula na weye ya hii nyama ya ngurumbe, lakini hii nyama Ndini yetu inakatazwa kuikula sisi. Basi, usiogope huyu muzulumu. Usilete haya kwa wa nduku yako na kwa mimi. Inapaswa kuchakula kuliko lufu ya mateso na hapana kukatala hamuri ya Ndini yetu.

Mtoto mudogo alisikia ma sauria ya mama yake na alimuangalia na macho wazi kabisa. Alikarimbia mtoto mfalme Antiohos na alimwambia nguvu:

Ee muzulumu mugumu na mubaya, usiongolee. Misitatii kwa hamuri yako.

Minaitii ku Sheria ya Mungu. Lakini weye hautaweze kutoka malipizi ya Mungu.

Wakati alisema hii ma sauti yake, bila kumuzimbiria mutu mwingine, alikimbia na aliingia ndani ya hii kiugu walikalangwa na wa nduku wake weingine. Nafsi yake alienda kupumuzika pamoja na wa nduku wake ya sita.

Sasa alibakia yeye wa pekee mama yao, Solomoni. Antiohos alimufokea na alimwambia na sauti makari:

Weye unakosa ya kila mambo. Ilipaswa kulipiza weye ya kwanza. Lakini na sasa haipitishe wakati.

Mara moja aliwaambia kwa waaskari wake: Mumubebe na mumutupe ndani ya moto. Huyu mama Mutakatifu, mwenye bila taambu alipatia sandaka kwa Mungu wote watoto wake, sasa alipokea na uvumilia na furaha na mateso ku mwili yake.

Watoto wake ya saba walimutaguria na kisha aliwafata na mama yao Solomoni.

***MAELEZEO:***

Ulizo: Mfalme Antiohos aliwaambia ninyi kwa Muzee Eleazaro, kwa watoto ya saba na kwa Mama wao Solomoni?

Jibu: Aliwaambia kukula nyama ya ngurumbe.

Ulizo: Na juu ya ninyi walikatala?

Jibu: Ndini yao, Sheria ya Musa mukubwa yao ilikataza hii nyama ya ngurumbe. Nikusema ilikuwa kwa wale watu ya Israeli mambo ya imani yao na kutii kwa mapenzi ya Mungu.

Ulizo: Kwa sababu walikatala kutii kwa mfalme mambo ninyi walipata?

Jibu: Walipotesha uzima yao. Walichakula kufa na hapana kukanyanga Sheria ya Mungu.

Ulizo: Namna gani inaitwa hii hamuri, ile hababpende kuikanyanga watoto Wamakavei?

Jibu: Kifungo ya chakula ao kwarezima.

Ulizo: Sisi tukona wakati ya kwarezima?

Jibu: Ndivyo. Tukona na sisi wakati ya kifungo ya chakula, ile Kanisa yetu ilitupatia. Nikusema kwarezima ni zwezo (coutume) ya Mapokeo Takatifu yetu. FUNDISHO: Inapaswa kuchunga mafungo ya chakula yetu, ile inatuwambia Kanisa yetu.

Kama sauti ya Biblia tutabeba, watoto wangu, ile ma sauti alisema Yesu Kristu kwa Wanafunji wake, wakati wale walimuuliza juu ya ninyi habakuweze kutosha shetani toka mutu moja aliyekuwa na pepo buchafu ndani yake. Vile aliwajibu Yesu Kristu:

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Namna hii haiwezi kutoka, isipokuwa kwa kuomba na kufunga». (Matayo 17, 21).

MATENDO KU UZIMA YETU. Hii fundisho yetu tunaifanya hii wakati pahali inaanza na wakati ya kwarezima ya Ufufuo ya Kristu. Hamuri ya kwarezima ni ya zamani kabisa. Ni hamuri ya kwanza ya Mungu. Mukumbukeni wakati gani Mungu aliipatia hii hamuri?

Wakati alisema kwa watu ya kwanza juu hapana kukula ya muti moja iliyekuwa ndani ya Paradizo.

Hii hamuri yake ilikuwa sindano ya kwarezima. Na hii sindano ya kwarezima ni sindano ya utii ku sauti ya Mungu; ni sindano ya imani.

Wale wa athlete juu ya kushinda kwa masindano wao, wanatayarisha na masindano ku mbele. Na sisi, wenye tuko wa askari ya Yesu Kristu, inapaswa kusindana. Sindano ni kifungo ya chakula. Inatusaidia hii sindano kushinda ma zambi yetu. Inatusaidia kusimamisha matakio yetu ya mwili. Inatusaidia kutii kwa mapenzi ya Mungu. Inatusaidia ya makazi ya roho ya mingi. Mukumbukeni mukubwa nani ya Agano la Kale alifunga chakula?

Musa, mbele ya kubeba Sheria ya Mungu.

Na mu Agano Jipya?

Alifunga chakula Bwana Yesu Kristu. Alifunga ma siku makumi ine mu jangwa, mbele ya kuanza kazi ya Kuhubiri yake.

Basi, kifungo ya chakula ni moja bunduki kontre ya Shetani. Watu wote wanafanya kwarezima. Beingine wanafanya hii kifungo hapana juu ya kumaliza hamuri ya Kanisa yetu, lakini, kwa sababu mungaga aliwaambia. Kwa mufano mungaga anakataza ma chakula ya kuachana kwa watu, wenye wekona mambo mu afya yao. Kama mungaga atasema ya kama aipaswe kukula hii chakula fulani, sisi wote tunamutii. Lakini, juu ya ninyi, watoto wangu, hatufanye kwarezima, kama Mungu anatuwaambia?

Munajua kuniambia ma wakati ma nani Kanisa yetu inatuaambia kufunga ma chakula ya kuachana?

Ni kifungo ya chakula kila Mukazi Tatu na Mukazi Tano. Ni Kwarezima

Ukumbwa mbele ya Ufufuo ya Bwana Yesu Kristu. Ni kwarezima mbele ya Kuzaliwa Kristu na kwarezima mbele ya Kulala ya Mzazi-Mungu na kwarezima mbele ya Siku Kuu ya wa Mitume Paulo na Petro, mu tarehe 29 Mwezi ya Sita.

Tukona na ingine ma siku ya kifungo, kwa mufano: Ni Siku ya Musalaba ya Kristu, mu tarehe 14, Mwezi ya Tisa na Ile siku moja mbele ya Epifani ya Bwana Yesu na siku ya tarehe 29, mwezi ya Mnane, tunashangilia makumbusho ya kukata Kichwa ya Mtakatifu Yoane Mutangulizi.

Tunaweza kufata hii hamuri ya Mungu? Mtoto moja iko namna kutuwaambia:

Mimi, misiweze, kwa sababu wazazi wangu habaniache.

Ni mambo ya sikitiko kwa sababu ma nyumba ya mingi waaminifu wetu habachunge kwarezima. Lakini inapaswa mweye, watoto wangu, kumwambia kwa mama yenu ile ma siku Mukazi Tatu na Mukazi Tano kufanya chakula bila mafuta. Wale Watoto ya hii fundisho ya leo walichakula kufa na hapana kukanyanga Sheria ya kwarezima ya Ndini yao. Na sisi tunaweza kufata mufano yao ao hapana?

Tuko watoto ya Kanisa Orthodokse. Na ndani ya Kanisa yetu ni masindano.

Tangu leo, basi, tutakamata naziri moja. Kila wakati tukona kwarezima tutakatala kukula ma nyama na ingine ma chakula, sawa vile mazimba, samaki, mayayi na ingine.

Pamoja na hii kifungo ya chakula iko lazima kufanya na moja ingine kifungo. Ni kifungo ya zambi. Faida gani tutapata kama tunakula chakula bila mafuta, lakini tunasimanga nduku wetu, tunamuchabula ao tunamuhukumu? Ya kwanza inapaswa kufunga kinywa yetu ya kila zambi yake. Ma macho yetu ya kila zambi yao. Masikio yetu ya kila zambi yao. Vile nafsi yetu inafata kwarezima ya roho inasafishwa na inatakaswa.

## FUNDISHO MAKUMI MBILI NA MBILI
## MUTAKATIFU FILOTHEI

***NAMNA YA KUKARIBIA***

Kila fasi ya Ichi ya Grekia ikona, watoto wangu, Watakatifu yake. Kila kipimo ya inchi ya Grekia iko na kutuonyesha na moja Mtakatifu yake. Basi, leo minataka kumionyesha moja Mtakatifu Mwanamuke, mwenye ni Mulinzi ya Kapitale ya Grekia, inayeitwa Athina.

HISTORIA. Tuko ile wakati Grekia ilikuwa utumwa kwa nguvu ya wa Turki. karibu ku mwaka 1526 alizaliwa mu Athina mtoto moja mwanamuke toka wazazi watajiri. Walimubatiza na jina Regula. Wazazi yake walikuwa jina ya mbili Benizelos. Jamaa yake ilikuwa moja ukubwa kabisa katikati ya weingine ya Athina.

Tangu kipimo udogo yake huyu mtoto Regula alionyesha ya kama alikuwa na ma zawandi ya mingi. Wazazi wake waliweza kumusaidia juu ya kufunda bintu mingi, lakini ile wakati hakuna masomo. Basi, walikamata mupango kumutuma kwa moja mwalimu mwanamuke, aliyekuwa pale karibu na walimuripa juu ya kufunda mtoto wao mafundisho ya kuachana. Kila asubui waliona na watu weingine huyu mtoto Regula na moja kitunga kwa mikono yake kutambuka ma njia ya muji Athina juu ya kwenda kwa huyu mwalimu mwanamuke. Ndani ya hii kitunga mama yake alimuweka chakula yake ya kila muchana kati, kwa sababu aliikala kwa mwalimu mtoto kila siku muzima, mpaka busiku.

Regula aliendelea muzuri kwa hii mafundisho yake. Lakini kabisa aliendelea kwa ma fazila ya Kristu. Ndani ya roho yake iliisha kujipanda mawa ya mapendo na wema. Hii wema alionyesha mbele ya wamasikini na weingine watu ya Athina.

Siku moja mwalimu mwanamuke alimuona kupita bila kukula. Kitunga yake aliileta wazi. Mama yake alisahabu kumupatia chakula yake? Lakini mama yake kila siku alimuweka chakula yake ya muzuri sana.

Ee Regula, juu ya ninyi haukule? Alimuuliza mwalimu yake. Chakula yako iko wapi? Walikubeba watoto weingine mu njia?

Hapana mama, alimujibu na kiloko shaka mtoto Regula.

Leo. . . misitakule. Mitaikala kusoma ma kitabu yangu.

Unionyeshe, ilifanyika wapi hii chakula alikupatia mama yako? Uso ya mtoto iliyala na ragi nyekunda juu ya haya, kwa sababu hasikutake kufunua hii tendo, ile aliisha kuifanya.

Tazama, munajua, mu njia milipata mtoto moja. Alionekana masikini na mwenye njaala. Mimi kila siku minakula chakula ya muzuri. Lakini huyu mtoto alikuwa na njaala na ma siku mingi. Milisikia wema na milimupatia chakula yangu. . .

Wakati alisema Regula hii masauti yake, alisikia haya, kwa sababu alikuwa na unyenyekevu. Mwalimu mwanamuke alimutukuza na hasikumufokee.

Alipatia Regula hapana paka chakula, lakini na manguo yake alikabula kwa watoto wanawake wamasikini. Siku moja mama yake alimuona bila nguo ya inje.

Mtoto wangu, ulifanya ninyi hii nguo yako ya inje?

Mama wangu, misina na yo. Miliipatia kwa binti moja, mwenye alikuwa mu njia; alisikia baridi na aliisha kuchoka. Mimi nikona na manguo ingine kuvaa, lakini yule binti atavaa ninyi?

Muzuri, ulifanya, mtoto wangu. Hii tendo yako inapendeza kwa Mungu.

Lakini unaweza kuniambia miye kusona mimi moja nguo ya huyu mtoto masikini na hapana kumupatia nguo yako.

Ndivyo mama wangu, lakini vile miliwaza ya kama minaonyesha mapendo yangu kuliko muzuri kwa mutu moja.

Vile ilipita miaka ya huyu binti mudogo Regula. Wakati alikomea, walikomea na ma fazila yake. Alikuwa mtoto moja, mwenye walimutukuza watu wote, kwa agili ya matendo yake kwa wema mbele ya wa masikini na wagonjwa. Alikuwa moja binti mukristu, mwenye aliisha kupenda nguvu na roho yake muzima Yesu Kristu. Ndani yake alikuwa matakio kutumika paka kazi ya Mungu.

Wakati alikomea na aliisha masomo, wazazi yake walimuowa. Lakini hasibakie wakati mingi na bwana yake. Yule alifariki na Regula alibakia bila bwana, mbalaka. Hii mambo ya sikitiko yake aliiona kama mapenzi ya Mungu. Mungu aliisha kumutegeneza njia ingine. Njia gani? Muione!

Kama ilikuwa namna kufika ku muji Kapitale Athina karibu ya Kanisa ukubwa Cathedrale ni moja njia na jina: Ya Mutakatifu Mutawa Filothei. Ku hii njia mbele ya miaka 400 ilikuwa moja Monasteri. Ndani ya hii Monasteri walikuwa watawa wanawake, wenye walitumika kila siku ku ma kazi ya upenda-wanadamu. Busiku walisanyikwa wote pamoja na waliimba wimbo ya Mungu na walifanya ma sala yao ya Mangaribi, Asubui na ingine.

Katikati ya wale watawa wanawake alikuwa na moja, mwenye alikuwa utakaso na uzima mufazili katika Kristu. Huyu alikuwa mukubwa Igumeni wao. Yeye aliisha kukokota na weingine watawa. Yeye aliisha kujenga na hii Monasteri. Huyu nani alikuwa? (. . . ) Alikuwa huyu Regula. Sasa hasikuitwa Regula, lakini Mutawa Filothei. Aliacha uzima ya dunia na alivaa nguo ya uzima Utawa.

Wakati alikufa bwana wake na wazazi wake, alibeba mali yake na aliikabula kwa watu wa masikini na vile alijenga Monasteri. Pamoja na yeye walienda na weingine wasaidizi, wenye walitumika mu nyumba ya wazazi wake na walifanyikwa na hawa watawa. Pole-pole walifika na wakijana wanawake beingine na vile kisha wakati kiloko ilifanyikwa Kundi ya watawa wanawake.

Ndani ya hii Monasteri ilikuwa na Masomo ya kufunda kazi fulani. Tena ilikuwa masomo ya fundisho kama masomo ya Inchi ya Grekia na ingine ma nyumba ya upenda wanadamu. Watawa ya hii Monasteri na mukubwa yao Filothei walitumika kwa kila mambo na huitaji ya wale watu walikwenda pale. Ma binti ya watu waliwachunga ndani ya hii Monasteri na waliwafundisha. Tena walisaidia wazazi, wenye waliishi bila saidio ya watu weingine. Walisaidia wagonjwa. Walifundisha ma fundi ya kuachana kwa watoto wanawake. Waliwapatia chakula na kitanda juu ya kupumuzika kwa wale watu waliwafukuza WaTurki. Na vile walionyesha wema na mapendo kwa watu wote walikimbilia ku Monasteri yao.

Haina lazima kusema, watoto wangu, ya kama kuliko mingi katikati ya watawa weingine alitumika mukubwa yao mutawa Filothei. Alikuwa kama mama mwenye wema, mwenye alitoa sandaka uzima yake juu ya kusaidia wa nduku wake. Alionyesha mapendo hapana paka kwa wale watu waliingia ku Monasteri, lakini kabisa kabisa kwa wale wa masikini, wenye walikuja ya ma mukini ya pembeni ya Kapitale. Alijua ya kama, wakati watu ya ma mukini walikuja mu Athina, habakukuwe mu njia yao kisima moja kukunywa maji. Mutawa Filothei alifungula moja kisima, iliyeitwa Psihiko. Mpaka sasa iko moja quartier mu Athina na hii njia juu ya kukumbuka hii tendo kizuri ya Mutawa Filothei. Karibu ya hii quartier aliisha kujenga na moja ingine udogo Monasteri kuchunga wale waKristiani waliwafukuza wa Turki.

Siku moja ilikuwa mangaribi. Watawa ndani ya Monasteri yao waliingia mu Kanisa kusoma sala ya Mangaribi. Inje wa askeri Turki waliisha kukamata wa Greki wa mingi ile siku. Aipaswe kusahabu ya kama ile wakati Grekia ilikuwa utumwa kwa wa Turkie. Kisha saa kiloko, kimya ya Monasteri yao iliharabisha malalamiko nguvu ya watu. Mambo ninyi ilikuwa? Beingine

wanawake walikuwa inje ya Monasteri, walikokola mulango na waliongolea kuwafungula juu ya kuingia ndani.

Mutufungule, mutusaidie. Wanatufukuza. Tuko watumwa ya wa Turki na tulikimbia kwa siri. Mutufungule, mutusaidie!

Mukubwa Filothei hasiweze kukatala saidio yake. Alijua ya kama, kama atafungula Mulango ya Monasteri yake, wataingia ndani na wa askari waturki na watarabisha yoyote. Lakini mapendo na wema ile saa walimwambia ya kama inapaswa kufungula mulango. Na kweli! Ilifunguliwa mulango na wanawake beingine waliingia ndani juu ya kuokolewa toka mateso na zambi ya wa Turki.

Hii kazi na beingine, ile alifanya Mutawa Filothei ku Monasteri yake, walileta chuki kwa roho ya waTurki. Siku moja wa askari Turki waliingia ku Monasteri na, bila kusema hata sauti moja, walikamata Mukubwa Filothei na walimukokota na walimuongoza mu buloko.

Mukubwa ya wa askari alimwambia: Ao utakatala imani yako ao mitakuwua!

Minachakula hii ya mbili, alimujibu nguvu Mutawa Filothei. Lakini hasikukuje tena saa ya mateso yake. WaKristiani wakubwa walikombana na walimuuhuru. Mutawa Filothei alirudia ku Monasteri yake. Aliendelea kazi yake, kazi ya sala, mapendo, iliyefika mupaka ma kisanga ya Grekia.

Hasikupite tangu hii jabo, wakati mingi na wa Turki walionekana mara ya mbili ndani ya Monasteri yake. Hii saa lakini, walipata Filothei ku moja ingine udogo Monasteri yake, iliyekuwa mu fasi Kalogreza. Ilikuwa busiku. Mutakatifu Filothei pamoja na weingine wanawake watawa walifanya sala ya busiku. Katikati ya busiku walisikia malalamiko inje. Walikuwa wa Turki, wenye waliingia ndani juu ya kukamata Filothei. Yule Mutawa Filothei hasikukimbie.

Wa askari wa Turki walimukamata, walimukokota inje na walianza kazi yao matata kabisa. Walianza kumupika na fimbo. Damu inatoka toka mwili yake. Mtakatifu Filothei alianguka chini. Wa askari kwa sababu walichoka, walimuacha hivi chini karibu ya kufa.

Mtakatifu Filothei hakuna namna kuishi. Kisha ma siku kiloko alitoa nafsi yake kwa Mungu mu tarehe ya 19 mwezi ya mbili.

MAELEZEO: Leo, watoto wangu, tulienda hii safari mukongo, miaka 400, ile wakati Grekia ilikuwa utumuwa kwa wa Turki.

Ulizo: Mutu gani tulisikia ku hii fundisho yetu leo?

Jibu: Tulisikia uzima ya Mtakatifu Filothei.

Ulizo: Munakumbuka ninyi toka uzima ya kipimo udogo yake?

Jibu: Walimuita na jina Regula na alikuwa na mapendo na wema kwa watu ya huitaji.

Ulizo: Munaweza kusema ninyi juu ya matendo wazuri yake?

Jibu: Alijenga moja Monasteri, pahali ilikuwa fasi ya maombi kwa Mungu na fasi ya wema na mapendo. Pale wa Greki walipata kimbilio na kitumaini ku kila mateso yao.

Ulizo: Namna gani Regula alifika ku hii fasi kutoa uzima yake juu ya kusaidia wa nduku wake?

Jibu: Regula alikuwa mukristu. Mapendo yake kwa Kristu na ku Kanisa walimuongoza kutoa uzima yake kama sandaka kwa Mungu na kwa kila mukaribifu. Ulizo: Na ilikuwa paka hii Monasteri yake na paka huyu Mutawa mwanamuke, mwenye alitoa bintu mingi kwa wa nduku wake?

Jibu: Ile wakati walikuwa ma Monasteri ya mingi. Ma Monasteri na Watawa walichunga taifa ya Grekia karibu ya Imani na Kanisa ya Mungu. FUNDISHO: Kanisa inasaidia kila inchi juu ya kuchunga imani na mapendo ya Kristu.

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Kanisa ni mama yetu sisi sote» (Wa Galatia 4, 26) MATENDO KU UZIMA YETU. Kanisa yetu ikona watumishi wake, wenye weko wasaidizi yetu kwa wokovu yetu na wokovu ya watu wote ya dunia. Karibu ya moja mutawa sisi tunafundisha mapendo ya Mungu na uzima takatifu, kwa sababu watawa walitoa uzima yao kuishi moja uzima safi kwa utukufu ya Mungu na wokovu ya nafsi yao. Hii uzima yao habaweze kuishi watu ya hii dunia, kwa sababu, watu wanaishi ndani ya zambi na bila neema ya Mungu. Kila mutawa anakombana kuleta uzima wa Malaika ndani ya hii inchi yetu. Sawa vile wa Malaika wanatukuza na wanamuimba Mungu kila siku, vile na watawa wanamutukuza Mungu, wanamuimba kila siku na weko tayari kufanya kutii kwa mapenzi ya Mungu. Joo vile, pahali ni moja Monasteri iko na uzima ya roho muzuri sana, kwa sababu wa Kristiani wetu wanakimbilia kupumuzika ma roho yao, kusikia mafundisho ya utakaso ya nafsi na kufurahi furaha ya mbingu pamoja na Kundi ya watawa.

Watawa wanakombana kila siku kumuomba kwa Mungu juu ya ma nafsi yao, lakini kabisa juu ya wokovu ya wa nduku wao, wenye wanaishi ndani ya majaribu ya hii dunia. Bunduki yao munene ni sala. Na munajua sala gani wanasema kila siku kwa siri ndani ya akili na roho yao? (. . . ) Ndivyo. Ni hii: « Bwana Yesu Kristu, Mwana wa Mungu, unihurumie mimi mwenye zambi». Faida inakuja kwa roho yetu kama tunakumbuka jina ya Kristu, kama nikusema tunasema mara ya mingi kila siku jina ya Yesu Kristu. Vile ma adui yetu, nikusema ma shetani wanakimbia na kila zambi inatoka ya uzima ya akili yetu. Mungu anatusaidia daima, kwani Yeye na Baba yetu na anatuma katika mapendo yake saidio na neema yake ku uzima yetu.

Na mweye, watoto wangu, kama munataka kumupenda Mungu inapaswa kuzombelea kusema hii sala, ile wanasema na watawa, juu ya kufurahi ku uzima yenu na kuchunga neema ya Roho Mtakatifu.

Moja mutawa ni moja taa ya kuuwakisha katikati yetu, kwa sababu na uzima na mufano yake anatuonyesha namna gani na sisi tutafata uzima takatifu na safi ku uzima yetu.

Basi, aipaswe kusahabu ya kama Mungu alituita kuishi uzima ya milele mu Paradizo, lakini bila kuishi hapa uzima safi na takatifu hakuna namna kuona Uso ya Bwana Yesu Kristu.

## FUNDISHO MAKUMI MBILI NA TATU
## ALAMA YA WAKRISTIANI
## (Hesabu 21, 4-9)

***NAMNA YA KUKARIBIA***

(Mwalimu hii fundisho ataifanya mu Juma ya tatu ya Kwarezima, pahali Kanisa yetu inashangilia Usujudu ya Musalaba ya Kristu)

Leo, watoto wangu ni Juma ya kusujudu Musalaba ya Kristu. Munajua juu ya ninyi inaitwa hivi hii Juma?

Kwa sababu tunabusu na tunasujudu Musalaba.

Na juu ya ninyi ni desturi ya Kanisa yetu kutosha Musalaba katikati ya Kanisa na kuisujudu wa Kristiani?

Juu ya kubeba nguvu kwa sindano ya roho yao.

Ndivyo, hii wakati ya Kwarezima Mukubwa ni wakati ya mashindano ya roho. Sasa tuko katikati karibu ya hii wakati ya kwarezima Mukubwa. Kanisa yetu juu ya kutusaidia inatuweka mbele ya uzima yetu hii bunduki nguvu, nikusema Musalaba ya Kristu.

Wakati gani ilianza Historia ya musalaba?

Wakati ilinyanyuliwa Kristu pa Musalaba mu Kazi Tano Mukubwa.

Lakini, watoto wangu, Historia inaanza kuliko zamani. Toka Agano la Kale. Leo tutasikia moja Historia ya Musalaba toka Agano la Kale. HISTORIA. Tunaangalia mwendo ya taifa ya Israeli kutoka ya Misiri na kwenda mu Palestina. Mukubwa yao n iNabii Musa. Wanatembea ndani ya jangwa. Wekona ma zimbirio wanene, lakini wataipita. Namna gani?

Karibu yao ni na moja mwingine. Anawasidikia Mungu Mwenyezi.

Mukumbukeni ma miujiza ngapi Mungu aliwafanyisia kwa hii safari yao juu ya kufika mpaka inchi Palestina.

Na sasa moja ingine muujiza mupya. Mu jangwa ya mulima Sinaya, wakati wanatembea, walipata mbele yao moja mfalme nguvu sana, mwenye alitaka kusimamisha mwendo yao. Ku mwanzo wanaogopa. Huyu mfalme aliitwa Hananis. Alikuwa kupita nguvu ya watu ya Israeli. Lakini watu ya Isareli wekona pamoja yao na Mungu, mwenye ni kuliko mwenyezi ya kila mutu. Basi, walikimbilia kwa Mungu baba wao.

Ee Bwana wetu, wanamuomba watu wote na imani nguvu, utusaidie sisi kushinda huyu mfalme na sisi hatutakusahabu hata siku moja na tutakutoa na sandaka. Utusaidie sisi, ee Bwana wetu.

Na Bwana aliwasaidia. Na watu ya Israeli walimushinda huyu mfalme Hananis na walimukamata kama mutumwa wao.

Wakati Mungu alifanya hii muujiza mu Taifa ya Israeli, ilipasawa hii taifa kubakia karibu ya Mungu. Lakini hasikupitishe ma siku ya mingi na waligeuza sana. Ku mwendo yao walipata na ingine kizimbirio. Njia ilipitisha katikati ya jangwa na hakuna maji, hakuna chakula. Moja asubui, wakati walilamuka walikuwa na makari sana. Walifokea, walichabula na walisimanga Mukubwa yao Musa, kwa sababu yeye aliwatosha mu jangwa ya kufa kwa ajili ya njaala.

Juu ya ninyi ulitutosha toka Misiri? Sisi tuliikala pale muzuri. Sasa juu ya ninyi ulituletea hapa? Mukate hatuweze kutafuta hata ku fasi moja. Maji hata taka moja kukunywa. Juu ya ninyi ulitutosha ya Misiri? Juu ya kufa hapa? Weye uko mukosefu.

Tena walisema na ma sauti ya chabula na ugumu mbele ya Mungu. Walisema sauti ya kibego kontre ye Mungu, walilekea kwa imani yao, kwa sababu waliisha kusahabu miujiza ngapi Mungu aliwafanyisia na mara wa ngapi aliisha kuwasaidia.

Mweye munasema ninyi, watoto wangu, ilikuwa muzuri kumuchabula na kumufokea mukubwa yao Musa, huyu mtakatifu ya Mungu? Hapana! Zambi yao ilikuwa munene. Na ilipaswa kulipizwa. Na walipizwa. Asubui ya siku ingine watu wote ya Israeli walilamuka na boka mingi.

Ole kwetu! Ole kwetu! Tazama wanakuja wote kontre kwetu. Ee Mungu wetu, utusaidie, tutakufa wote!

Mambo gani ilikuwa? Inchi yao, kwa hii fasi waliikala ilisha kuyala na ma nyoka mingi. Walitembea na waliria sana na walileta boka mingi. Toka kinywa yao walitosha sumu. Walikuja toka jangwa na waliingia ndani ya ma hema ya watu ya Kabila Israeli. Walikaribia watu, walizuguluka pembeni yao na waliwalumiza nguvu. Waliwamwanga na sumu yao. Pole-pole watu walianza kuanguka chini na walikufa.

Watu ya Israeli habajue kufanya ninyi. Wanakimbia kama wa mazimu juu ya kuokolewa. Lakini ku mbele yao ingine nyoka. Wanaluka kuokoa mwili yao, lakini hakuna namna. Ma nyoka ma elfu mingi waliisha kuzuguluka fasi ya watu ya Israeli. Hakuna wokovu yao. Lufu inaonekana ma fasi yote.

Tutakufa wote, walipaza sauti na walisema watu ya Israeli. Tutafanya ninyi?

Ee Mungu wangu, alikufa mtoto wangu alifokea moja mwanamuke, wakati aliona mtoto yake kumufunga moja nyoka munene na kisha mtoto yake alikufa.

Malalamiko na ma sauti bila kitumaini wanasikiwa ma fasi yote. Watoto wanaria, ma mama wao wanapaza sauti na wanaume walipotesha kila kitumaini ya uzima yao. Mambo kibaya kabisa iliwapata.

Walipotesha kila kitumaini ya uzima yao na mara ingine sasa walikumbuka Mungu. Walisikia ya kama walipizwa juu ya hii kibego munene yao na ondoko yao toka Mungu na juu ya machabulana yao mbele ya Mungu. Utulivu yao wa pekee ni paka ya kurudia kwa Mungu. Walikimbia kwa Mukubwa yao Musa, mwenye walimuchabula mingi. Walipika magochi mbele yake na toba mingi waliomba hurumia na saidio yake.

Mukubwa Musa wetu, sisi tulikosefu mbele ya Mungu na ya hii zambi yetu yeye anatulipiza. Utusaidie na utuokoe. Tulisema, kweli, ma sauti mafumu kwa Mungu na mbele kwako. Na ma nyoka wa mingi walituzuguluka. Angalia watu ngapi tulibakia. Tutakufa wote. Utusaidie. Umuombe kwa Mungu juu ya wokovu wetu. Weye uko mutu yake na ukweli mutumishi yake. Umuombe na umuwambie kutuokoa na kusimamisha hii kazi kibaya. Ee Musa baba wetu, utusaidie.

Na Musa aliwawema tena na hii mara. Alianguka chini ku magochi na aliomba kwa Mungu juu ya wokovu ya Taifa yake. Roho yake alisikia umivu, kwani aliona watoto wake kukufa moja moja kila siku na hii lufu matata.

Na Bwana mara ingine aliwema taifa yake. Aliona toba yake na alipenda sasa kuwaokoa. Aliwapatia ndawa. Moja ndawa nguvu kabisa, ile kila mutu aliibeba, alitunzwa mara moja. Ma nyoka waliendelea kulumiza watu, lakini ule mutu alitaguria kubeba hii ndawa mara moja aliokolewa. Hasikulufe.

Ni nani ilikuwa ndawa?

Ee Musa, ilisikiwa sauti ya Mungu. Ma nyoka wanalumiza Taifa yako.

Basi, utafanya na weye moya nyoka munene toka shaba na utainyanyula yulu ku muti moja. Utaweka hii muti ku fasi moja katikati ya ma hema ya taifa yako juu ya kuona hii nyoka watu wote. Huyu nyoka ya shaba ataokoa taifa yako. Kila mutu anayelumizwa, kama anaangalia huyu nyoka ya shaba, ataokolewa.

Na Musa, mutumishi ukweli ya Mungu, alifanya vile katika sauti ya Mungu.

Alifanya moja nyoka ya shaba na aliiweka yulu ya muti moja na namna juu ya kufanyikwa musalaba. Na aliiweka yulu ya moja kilima, iliyekuwa karibu ya watu ya Israeli.

Walilamuka ile asubui watu na waliona yulu ya hii kilima pa muti moja nyoka ya shaba na walishangaa.

O, ni ninyi hii nyoka pale yulu?

Lakini habakuwa na saa ya kuuliza kwa sababu nyoka moja aliwalumiza.

Wanaumivu sana na wanaria na mara moja wanaangalia hii nyoka pa muti yulu ya hii kilima. Mara moja maumivu inasimamisha, sumu inatoka na huyu mutu aliyemulumiza nyoka anaokolewa. Muujiza munene kabisa!

Hii kavumu ya ajaabu ilizuguluka toka kinywa moja ku ingine kinywa ya kama ndawa ilipatikana! Tazama! Ni pale yulu ya muti huyu nyoka aliyefanyikwa na shaba. Kila mutu mwenye analumizwa, inapaswa mara moja kuangalia huyu nyoka ya shaba pale yulu mu hii kilima na mara moja ataokolewa.

Muwaze, watoto wangu, furaha ngapi, walisikia watu ya Israeli juu ya hii namna ya wokovu yao?

***MAELEZEO:***

Minazania na kwa mweye ilimionekana ya ajaabu hii namna ya wokovu ya watu ya Israeli! Namna gani moja nyoka toka shaba ekona hii nguvu mingi! Ao, juu ya ninyi Mungu alichakula hii namna juu ya kuokoa taifa Yake?

Lakini, watoto wangu, hii historia, sasa munasikia, inafanyikwa na leo. Na leo iko ma nyoka ya mingi. Iko wasafiri, wenye wanalumizwa toka ma nyoka ingine. Iko watu kama Musa. Iko na sumu ya ma nyoka. Lakini iko na hii nyoka ya shaba, iko mutu pahali iko kutundikwa. Iko wokovu kwa wale wanaangalia hii muti.

Sasa, mukujeni, kuangalia na mustari hii yote maana yao:

Sisi wote tuko wasafiri ndani ya hii safari ya uzima yetu. Tunatembea njia ya uzima yetu mpaka kufika ku inchi ya furaha, ku Ufalme ya mbingu. Lakini mu njia yetu iko ma nyoka. Ni shetani na watumishi wake. Nyoka munene na sumu mingi ni shetani. Yeye anataka sisi wote kutulumiza na sumu nguvu yake. Na hii sumu ni kila zambi. Watu wa mingi wanalumizwa toka ma nyoka ya zambi na wanakufa na wanapotea mu gehena. Lakini iko na huyu nyoka ya shaba, na kila mutu aliyelumizwa na anamuangalia na imani, nikusema kila mutu anayeamini kwa nguvu yake, huyu hasipotee. Anaokolewa toka ma zambi yake.

Ni ninyi maana ya huyu nyoka toka shaba? Maana yake ni Musalaba ya Kristu. Sawa vile nyoka ya shaba ilifungwa pa muti moja, vile na Kristu wetu, aliyekuja ndani ya inchi yetu, alifungwa na alipigiliwa pa muti moja ya Musalaba. Na sawa vile yule nyoka ya shaba alinyanyuliwa pa chongo ya kilima moja, vile na Musalaba ya Kristu ilinyanyuliwa na ilisimamishwa mu chongo ya kilima moja, iliyeitwa Golgota. Na sawa vile zamani kila mutu aliyeona hii nyoka ya shaba aliokolewa toka ulumizo ya ma nyoka, vile na kila mutu anaangalia na anasandiki kwa Musalaba ya Kristu, anaokolewa toka sumu ya zambi.

Musalaba, watoto wangu, ni alama ya waKristiani. Nikusema sisi wote tukona chapa (muhuli) hii alama ya Musalaba. Kwa hivi, munaona, ya kama kila mwaminifu ukweli anafanya alama ya Musalaba. Kwa sababu kama tunafanya alama ya musalaba, tunabeba nguvu ya Mungu, tunafukuza nguvu ya shetani na tunakamata kama bunduki yetu Musalaba ya Kristu.

Lakini iko na beingine wa Kristiani na watoto, wenye wanasikia haya kufanya alama ya Musalaba pa kilari yao. Kristu hasikusikie haya kusulumbiwa na kupigiliwa na misumari marefu pa Musalaba na alimwanga Damu Takatifu yake juu ya wokovu wetu. Na hawa waKristiani wanasikia haya kufanya kweli alama ya Musalaba. Kwa hivi, fundisho yetu leo ni hii:

FUNDISHO: Aipaswe kusikia haya ya kufanya alama ya Musalaba. SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: «Kila mutu anayesikia haya juu yangu na juu ya maneno yangu katika kizazi hiki cha uzini na zambi, Mwana wa watu atasikia haya juu yake wakati atakapokoja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu» (Marko 8, 38).

MATENDO KU UZIMA YETU. Juu ya ninyi tunafanya alama ya Musalaba?

Tunaifanya vile juu ya zwezo ao hapana?

Hapana juu ya zwezo. Tunafanya alama ya Musalaba kwa sababu hivi tunaonyesha ya kama tuko wa Kristiani.

Musalaba ni alama ya ufamio ya waKritiani. Wale wenye habasandiki kwa Kristu, wekona ma alama ingine: Beingine wekona nyota ya mwezi kipande, beingine mkono moja kama kofi, na beingine moja ingine alama. Musalaba ni alama ya mapendo ya Mungu, kwani yulu yake alipigiliwa kwa ajili ya mapendo Mwana wa Mungu. Ni alama ya amani, kwani Kristu yulu yake alifungula mikono yake juu ya kuungana mutu na Mungu, inchi pamoja na mbingu, kuungana mutu pamoja na kila mutu mwingine. Ni alama ya ushindi. Leo, kama wanataka kuonyesa alama ya ushindi,

wanaifanya moja herufi sawa V na bilole yao. Wa Kristiani wekona alama ya Musalaba kama alama ya ushindi, kwani na Musalaba ya Kristu ilishindwa lufu.

Tena Musalaba ni moja fundisho ya theologie ya Mungu. Kama tunafanya alama ya Musalaba, tunakikiri mafundisho ya mingi ya Kanisa yetu. Mukona kusikia Mtakatifu Kosmas wa Etolia ya Grekia?

Yeye alikuwa moja mwalimu mukubwa na musaidizi ya Inchi ya Grekia ku miaka ya Utumwa ya Grekia kwa waTurki.

Basi, Mt. Kosmas, ku kila fasi alienda alisimamisha na moja Musalaba na mbele ya hii alipanda yulu ya moja kiti na alifundisha watu. Alikabula kwa watu musalaba wadogo kama baraka ya Mungu. Alifundisha watu namna gani watafanya alama ya Musalaba. Tena aliwafundisha maana ya kila matego ya kufanya hii alama ya Musalaba pa kilari yetu. Iko muzuri sasa kumusikia namna gani alifundisha hii fundisho ya Musalaba ya Kristu:

Wa nduku wangu, musikie namna gani inapaswa sisi kufanya alama ya Musalaba:

Ya kwanza: Sawa vile Utatu Mutakatifu anatukuzwa kwa mbingu toka wa Malaika, vile na weye utaunganisha bilole yako ya tatu ya mkono yako ya kuume. Na, kwa sababu hauweze kupanda mbinguni kumusujudu Mungu, unaweka mkono yako pa sula ya kichwa yako (kwa sababu kichwa ni maana ya mbingu) na unasema: Sawa vile wa Malaika wanatukuza Utatu Mutakatifu mu mbingu, vile na mimi mutumishi minatukuza na minasujudu Utatu Mutakatifu. Na sawa vile ma bilole weko ya tatu moja moja ya kuachana lakini iko na yote ya tatu pamoja, vile na Utatu Mutakatifu ni ma Uso ya Tatu ya kuachana lakini ni Mungu Moja.

Unashusha mkono yako mu tumbo yako. Vile ni sawa kusema: Ee Bwana wangu, minakusujudu na minakuwabudu, kwa sababu ulipokelea na ulifanyika mutu mu tumbo ya Mzazi-Mungu juu ya ma zambi yetu. Kisha unaweka mkono yako ku fasi ya kuume na unasema: Ee Mungu wangu, minakuomba kunisamehe na kuniweka ku fasi ya kuume pamoja na wenye haki. Kisha unaweka mkono yako ku fasi ya kushoto na unasema: Ee Mungu wangu, minakuomba, usiniweke ku fasi ya kushoto pamoja na wenye zambi. Kisha unaangalia kiloko chini na unasema: Ee Bwana wangu, minakusujudu, kwani ulifufuka katika wafu juu ya kutupatia uzima ya milele. Hii ni maana ya Musalaba».

Sasa, watoto wangu, muweze kuniambia wakati gani inapaswa kufanya alama ya Musalaba?

Wakati tunaanza kufanya kazi moja. Wakati tunaondoka toka nyumba yetu na tunaenda mu kazi ao ku Masomo ao mu Kanisa ao fasi ingine.

Wakati tunapita inje ya Kanisa Othodokse ao inje ya moja Kanisa pahali tunamazika wafu wetu. Na tena wakati tunafanya maombi yetu kwa Mungu mu nyumba yetu.

Ndani ya Kanisa, wakati inaanza Ibada moja tunafanya alama ya Musalaba.

Wakati tunasikia Jina ya Yesu Kristu, jina ya Mzazi-Mungu, ao ya Watakatifu wetu ao tunasikia jina ya Utatu Mutakatifu hivi: Jina ya Baba na ya Mwana na ya Roho Mutakatifu ao ma fasi wakubwa ya Liturgia Takatifu.

Beingine watoto wanasikia haya juu ya kufanya alama ya Musalaba. Juu ya ninyi? Mweye munawaza ninyi? Kristu yetu alisikia haya kusulumbiwa bunji pa Musalaba? Lakini sisi juu ya ninyi tunasikia haya?

# FUNDISHO MAKUMI MBILI NA INE
# WIMBO AKATHISTE

***NAMNA YA KUKARIBIA***

Mu dunia tukona ma wimbo ya mingi. Moja mwimbo ni furaha na roho yetu.

Kama ndani ya roho iko mawazo wazuri na matendo wazuri, kisha iko namna kuimba na wimbo wazuri.

Miaka ngapi iko namna kubakia mwimbo moja?

Iko wimbo, ile inabakia miaka ya mingi mpaka na miaka 100.
Lakini mu Kanisa yetu tukona moja wimbo, ineyetunaimba sisi ya miaka kuliko mingi.

Hii Wimbo Inaitwa Wimbo Akathiste. Inaishi miaka mpaka sasa 1370.
Wale wa Kristiani wanaimba wanafurahi sana.

Ni nani huyu Wimbo Akathiste?

***HISTORIA.***

Tuko ku mwaka 626, kisha ya kuzaliwa Bwana Yesu Kristu. Ku muji Konstantinopoli, Kapitale muzuri ya njimbo Vizantion, inaanza moja makelele. Inafanyikwa moja mambo nguvu. Mfalme Iraklios jina yake, analofa ya Muji. Eko ku moja nvita kontre ya watu ya Persia. Wa askari ya Persia weko wa adui ya Vizantion. Iraklios alikamata mupango kutembea na wa askari wake mbali ya mupaka ya njimbo yake juu ua kukombana wakubwa ya Persia. Muji Konstaninopoli ni karibu wazi ya wa askari. Ma nyumba yote wekona karibu na moja askari kwa hii nvita aliifanya mfalme kontre ya waPersia. Watu wote wanatakia hii nvita kuisha muzuri na kurudia mfalme ku muji mushindi na wa askari kurudia na maharabisho wadogo.

Wakati ma macho ya watu wote walikuwa kwa hii nvita aliifanya, mfalme Iraklios mara moja ma kavumu mabaya walileta taambu na sikitiko kwa watu ya muji Konstantinopoli. Mambo gani ilifanyikwa? Mukubwa ya inchi Persia alilanda mfalme Iraklios. Na wakati Iraklios alikombana kontre ya Persia, mukubwa ya Persia alituma wa askari wake kwa siri kontre ya muji Konstantinopoli toka fasi ya magaribi. Mukubwa yao alikuwa mutu moja aliyeitwa Haganos. Lakini na ingine hatari ilionekana. Moja ingine adui aliyeitwa Avari walifania masikilizano na urafiki pamoja na wakubwa ya Persia na wale walikuja kontre ya Konstantinopoli. Vile wa askari ya Persia walikuja kuzuguluka Muji mukubwa toka inchi na Avari toka bahari; vile hatari ilikuwa munene.

Ma siku walipita na hali ya muji ilifanyikwa kupita nguvu. Pembeni ya kibabashi yake walikuwa wadogo wa askari. Mfalme Iraklios, wakati alisikia hii kavumu, alituma mara moja kundi moja ya wa askari 12. 000 juu ya kulinzi ma kibabashi ya Muji. Lakini atafanya ninyi hii Kundi ya wa askari mbele ya wa askari ma elfu ya mingi ya wa adui? Beingine waaskari ya Muji waliona hatari munene, walipotesha kila kitumaini na waliongolea kuanguka kwa mikono ya wa adui wao.

Lakini hii wakati alikuwa mu Muji moja mutu mukubwa ya Kanisa, patriarhi Sergios. Watu wote ya Muji walitumainia paka kwa huyu patriarhi. Na yule, bila kupotesha wakati, alituma ma hamuri ya mbili. Na hamuri yake ya kwanza aliita wale watu waliweza kukombana na kukamata ma bunduki na kukimbia kulinzi ma kibabashi ya Muji. Aliwaambia hivi:

Mwende, hii ma saa, musiweze kuikala ma nyumba yenu. Fasi yenu ni pale yulu ya kibabashi. Na kweli, wale waliweza kubeba bunduki mara moja walipanda pa kibabashi. Vile walipumuzika kiloko wa askari, wenye kila siku na busiku walichunga ma kibabashi na walikombana wa adui. Tena na huyu patriarhi alizuguluka pembeni ya kibabashi na moja Ikona ya Mzazi-Mungu kwa mikono yake na aliwapatia kwa askari nguvu na kitumaini ya Mungu na Mama wake Bikira Maria.

Ilikuwa mambo ya furaha kuangalia wa askari kuwatembelea patrirhi yulu ya kibabashi na kuwapatia nguvu.

Tena patriarhi aliita na wale wenye habakuweze kukombana na bunduki, nikusema watu ya wazee, wanawake na watoto. Hawa wote walianza nvita ingine nguvu, kumuomba kwa Mungu juu ya kuokoa Muji yao hii saa ya huitaji. Wa baba wao walikombana na walichunga ma kibabashi na wa mama na watoto walikuwa ndani ya ma Kanisa, walipika magochi, walinyanyula mikono yao na walimuomba kwa Mungu. Waliria sana, waliimba na waliomba kwa Mama Maria kuokoa Muji yao.

Ndani ya hii sikitiko walipita ma mwezi wadogo. Ku mwisho ilifika na tarehe ya 8 Mwezi ya mnane. WaKristiani waliisha kusikia ya kama wa adui wao wa mbili, wa Avari na wa Perse hii busiku waliisha kusikilizana juu ya kukombana pamoja kontre ya Muji Konstantinopoli. Walikuwa ma bunduki ya mingi, ma kundi wa askari wa mingi na ma chombo ya hii nvita mingi kabisa. Mukubwa ya wa askari ya Persia alisema na majivuno: « Kesho Konstantinopoli itakuwa kwa mikono yetu. Tutaingia ndani washindi.

Munasikia, watoto wangu, sikitiko ngapi na boka walikuwa waKristiani ile wakati. Wa askari walichunga ma kibabashi ma wanawake na watoto walikuwa ndani ya ma Kanisa na waliomba kwa Mungu bila masimamisho.

Walisemaka na machozi ma macho yao:

Ee Mtakatifu kamili wetu, Mzazi-Mungu Bikira Maria, saidia Muji yetu. Usitupatie kwa wa adui wetu. Umuombe kwa Mwana wako, Mungu Mwenyezi, kuokoa Muji wetu. Mtakatifu Kamili Maria, utuokoe.

Wale walikuwa ndani ya ma Kanisa, walisikia makelele ya nvita, iliyekuwa nguvu kabisa. Wa adui waliwakombana na ugumu, lakini wa Kristiani waliwafukuza mara ya mingi. Ma saa ya busiku ilipita lakini nvita inaendeleshwa. Wa askari ya Muji waliisha kuchoka na inaonekana ya kama watalekea mufano na uvumilia yao. Lakini hii saa ilifanyikwa muujiza ya Mzazi-Mungu. Ni kweli, ya kama wote mashindi ya wa Kristiani walikuwa moja muujiza. Lakini sasa inafanyikwa moja jabo ya ajaabu kabisa. Ni ninyi?

Mungu alinyanyula pepo nguvu na mu bahari ilifanyikwa zorumba na tufani nguvu. Bahari yote inatetemeka kwa ajili ya pepo nguvu na tufani. Ma chombo ya wa adui walianza kupasuka na kulobekwa ndani ya bahari. Boka mingi iliingia ndani ya ma kundi ya wa adui. Walisimama nvita na walikimbia kuokolewa. Lakini walikuwa wa mingi na walikufa mingi kabisa.

Wa Kristiani toka ma kibabashi wao waliona hii uharibifu na waliria juu ya furaha na utukufu ya Mungu. Hata mutu moja hasishake ya kama hii uharibifu ya wa adui ilikuwa moja munene muujiza ya Mzazi-Mungu. Muujiza yake. Huyu Mama wetu alisikia maombi ya wa elfu mingi waKristiani na alifanya muujiza yake.

Wakati ilifika asubui mapema, Muji ilikuwa uhuru ya kila adui. Wa Kristiani habakusahabu Mzazi-Mungu, mwenye aliwafanyisia hii muujiza. Ile busiku walikuja wote mu Kanisa ya Mzazi-Mungu ya fasi Vlahernes ndani ya Muji. Ya kwanza alikuja patriarhi Sergios, Wakubwa ya muji, wa padri wote, wa Jemadari wakubwa na ma elfu mingi ya wa Kristiani. Wote walisanyikwa mu Kanisa kumushukuru Mzazi-Mungu.

Ile busiku, watoto wangu, waliimba wote pamoja na kinywa moja hii Wimbo Akathiste, sawa na sisi tunaendelea kuimba mupaka leo. Ilikuwa kuandikwa miaka kiloko ku mbele, lakini mara ya kwanza waliimba ile busiku, bila kuikala hata mutu moja. Kwa hivi inaitwa na Akathiste, nikusema maana yake mu lugha kigreki bila kuikala hata mutu moja.

Hio Wimbo Akathiste tunaisikia na sisi kila mwaka ile wakati ya Kwarezima mbele ya Ufufuo ya Kristu. Beingine wa Kristiani waliisoma kila busiku pamoja na Sala ya Busiku (Apodipnon Kidogo).

Hii Wimbo ni ninyi? Ni, sawa vile tulisema ku mwanzo wimbo moja ya Kanisa. Ilipita wakati ya miaka 1370, lakini inaendeleshwa na itaendeleshwa kuiimba wa Kristiani ndani ya Kanisa yetu. Hakuna hata moja mukristu, mwenye hasikusikie ao hasijue hii Wimbo ya Mzazi-Mungu.

Hii Wimbo ikona ma herufi 24, nikusema sawa vile ni na ma herufi 24 ya Alphabet ya lugha kigreki. Inaanza toka herufi A na inaisha mu herufi Omega. Tena hii Wimbo ikona neno ya « Salamu» 144.

Hii Wimbo sisi tunaiisikia kila Kwarezima mbele ya Ufufuo ya Kristu, siku kila Mukazi Tano mangaribi ya ma Juma ya Tano.

***MAELEZEO:***

Ulizo: Nani alifanya hii muujiza muliisikia leo?

Jibu: Mutakatifu kamili Mzazi-Mungu. Huyu alisaidia na iliokolewa muji Konstantinopoli toka ma adui yake.

Ulizo: Na wa Kristiani walifanya ninyi juu ya kusifu na kushukuru Mzazi-Mungu?

Jibu: Walienda wote mu Kanisa ya Mzazi-Mungu ya fasi Vlahernes. Ulizo: Na leo tunaimba hii Wimbo Akathiste. Lakini mweye munasema ninyi, watu wote wanasifu na wanatukuza Mzazi-Mungu Maria Bikira? Jibu: Hapana watu wote. Wanakatala kumusifu wa eretiki, wa Protestante na waYehovai na weingine wa eretiki, wenye wanamuchabulana Mama Maria. FUNDISHO: Sisi inapaswa kusifu, kumushukuru na kumutukuza Mzazi-Mungu Bikira Maria.

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Tangu leo vizazi vyote wataniita heri» (Luka 1, 48). MATENDO KU UZIMA YETU. Mzazi Mungu Bikira Maria eko na fasi ya kuachana ndani ya Kanisa yetu. Mungu alimusifu. Paka yeye wa pekee katikati ya watu wote ya dunia alisifiwa kufanyika nyumba ya Mungu, mama ya Mungu na mutu Yesu Kristu. Na, wakati alitoka ya hii dunia, wa Malaika walimupokelea mu mbingu na walimuongoza ku fasi ya kuume ya Mwana na Mungu wake. Bile aliisha kusema na Mfalme na Nabii Daudi ku moja zaburi yake: «Kwa mukono wako wa kuume anasimama malkia amevaa zahabu ya Ofiri» (45, 9)

Mzazi-Mungu Maria ni musifiwa mu mbingu na musifiwa ku inchi yetu. Mu dunia muzima walijengwa ma Kanisa ya mingi kwa Jina yake. Ma Ikona wa Miujiza iko wa mingi kabisa mu dunia muzima. Ma Monasteri yetu ni tena ma mingi kwa Jina yake na ma elfu wa mingi kila mwaka wanaenda waKristiani wetu ma Monasteri yake.

Kwa Mzazi-Mungu anakimbilia kila mutu mwenye taambu na umivu. Tena na wale habasandiki mingi, kama watapata moja huitaji na fasi nguvu wanakimbilia Kwake kuomba saidio yake.

Mtakatifu Kamili wangu! Unisaidie, Mtakatifu Kamili wangu! Kwa saidio yako tunatumainia sisi wote na tunapika magochi mbele kwako. Fanya muujiza yako, ee Mtakatifu Kamili Mzazi-Mungu Bikira Maria!

Na Mama Maria anapokelea maombi ya Waaminifu wetu. Kwa sababu ni Musaidizi kwa mbingummbele ya Mungu Mwana wake. Kwani ni Mama ya Kristu ekona uwezo mingi mbele Kwake. Sasa tutamiambia moja mufano ya kusikia muzuri:

Mtoto moja anafanya makosa ya kuachana. Siku moja alifanya moja kosa.

Aliogopa na alienda kufuchama, kwa sababu baba yake ilikuwa namna kumupika. Na baba yake anakuja, anaona kosa ya mtoto yake na ni tayari kupika mtoto yake. lakini mtoto hakuna namna kukimbia, anaenda mbio kwa mama yake, ananguka ndani ya ubatio, ndani ya mikono yake na anamwambia:

Mama wangu, uniokoe. . .

Na mama anawema mtoto wake na anaingia katikati ya bwana yake na anamwambia kuacha mtoto yao.

Usimupike. Umuache. Hasitafanye hii kazi mara ingine. Mimi minakuambia kweli.
Na baba anaacha mtoto yake, bila kumulipiza.

Vile inafanyikwa na kwa sisi, wenye tuko watoto wakosefu ya Mungu,

mwenye ni Baba wetu na ilipaswa kutulipiza juu ya ile ma mingi makosa yetu tunaifanya kila siku. Kama tutakimbilia kwa Mama wake, mwenye ni na Mama wetu, yeye anasikia maombi yetu anamuomba kwa Mungu juu ya usamehe na saidio yetu.

Mzazi-Mungu Bikira maria ekona moja fasi yulu kabisa mbele ya weingine Watakatifu ndani ya wimbo ya Kanisa yetu.

Kila wakati tunasikia Padri kusema: « Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili,

asiye na doa, mbarikiwa kushinda, Malkia wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na

Bikira daima, pamoja na Watakatifu wote. . . « Hii inatuonyesha ya kama tunakumbuka Mama Maria ya Kristu

pamoja na Watakatifu wetu, lakini kuliko yao mu fasi yake mu mbingu na ma roho ya wa Kristiani wetu ni kupita yulu. Na mu fasi ukubwa ya Liturgia Takatifu padri anasema hivi: « Hasa Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, Malkia wetu mtukufu, Mzazi-Mungu na Maria Bikira daima». . Tena tunatoa Sandaka bila damu kwa Mzazi-Mungu. Na ndani ya Liturgia Takatifu tunakuja ku moja maungano ukubwa pamoja na Mzazi-Mungu Maria.

Mzazi-Mungu Maria ekona ma sikitiko ya mbili: Moja sikitiko yake ni kwa sababu watu wa mingi kabisa wanamuchabulana, sawa wa eretiki na sikitiko yake ya mbili ni toka beingine wanawake na wa binti kwa sababu wanavaa ma nguo bila haya. Kama sisi kweli tunamupenda Bikira Maria inapaswa na uzima na mavazi na ma sauti yetu kumusifu. Katikati ya ma roho yetu pembeni ya Yesu Kristu inapaswa kuweka Mama wake. Kwake daima tunaomba na tunasema:

Ee Mtakatifu kamili Mzazi-Mungu Bikira Maria, kwa maombi yako utuokoe sisi wenye zambi.

## FUNDISHO MAKUMI MBILI NA TANO
## MEZA UKUBWA NA TAKATIFU
## (Luka 14, 15-24, Matayo 22, 1-14)

***NAMNA YA KUKARIBIA***

Mara wa mingi, watoto wangu, watu wanakula pamoja. Munaweza kuniambia wakati gani wanashangilia na wanakula pamoja?

Kama iko Fumbo ya Ndoa ao Ubatizo.
Kama mutu moja eko na makumbusho ya Mutakatifu yake.
Kama mutu moja anashangilia ile siku ya kuzaliwa yake.
Kama sisi tutaenda ku mamukini wetu, pale watu wanasanyikwa pamoja 100, 200, 300 na wanakula pamoja, kabisa kama weko na makumbusho ya Mutakatifu ya Kanisa yao.

Mimi leo mitamiambia juu ya meza moja, pahali mukubwa ya hii meza aliita watu wa mingi.

HISTORIA. Wakati moja fulani alikuwa mfalme moja ya inchi moja munene. Alikuwa mutajiri kupita ya mutu mwingine. Nyumba yake ilikuwa ndani ya mwangaza. Na, wakati alikuwa na shangilio nyumba yake ilikuwa safi kabisa na muzuri sana.

Jabo ukubwa ya ufalme wake ilikuwa ndoa ya mtoto mwanaume wake.

Watumishi wake waliisha kutayarisha yote ma kazi juu ya hii Fumbo ya mtoto yake. Ma siku wadogo ku mbele mfalme aliita watumishi wake wote. Aliwaapatia masauria namna gani watatumika kwa hii Meza ukubwa na namna gani watapokelea watu wageni.

Aliwaambia: Mubebe hii ma jina ya watu na mwende kuwatafuta. Hawa watafika ku hii Meza. Mimi minawapenda kuwaita kwa hii shangilio yangu.

Matayarisho inaisha kuisha. Ruhusa ya mfalme ilipatiwa na waliondoka watumishi kutafuta na kutangaza wale, wenye watakuja ku hii shangilio ya mukubwa yao.

Ku masikio yao iikuwa hii sauti ya mfalme yao: Mukujeni, bintu ya chakula ni yote ytayari. Mfalme wetu anamiongolea!

Hii ma sauti ilipaswa kusema watumishi kwa warafiki na wa nduku ya mfalme. Hii sauti walimusema na mu njia juu hapana kuisahabu. Walikuwa ku mkono yao na moja muito iliyeandikwa ku moja papier.

Na tazama makutano ya kwanza. Mutumishi moja alipata nyumba ya mutu moja. Alimuona mu lupango yake kutayarisha ya safari punda yake. Alikuwa tayari kuondoka ya safari, lakini mutumishi alimupatia hii papier na alimwambia:

Mukubwa yangu alinituma. Anamiita ku Meza Ukubwa mu nyumba yake.

Bintu ya chakula ni tayari. Anamiongolea.

Unasema ninyi? Mfalme ananiita?

Ndivyo, yeye anamisifu kufika kwake.

Wakati alisema hii ma sauti mutumishi aliongolea jiba ya yule mugeni.

Lakini alimuona kusikitika. Alipindula kichwa yake fasi ingine na alionyesha ya kama hasikupende kusikia hii tangazo.

Ee bwana wangu, mfalme anamiita, hamusikie? Yeye atafanya ndoa ya mtoto wake na anamiita mu shangilio yake kukula pamoja na yeye na wa nduku wake weingine.

Uniache, mtoto wangu. Misiweze kukuja. Hakuna namna kufika hii saa.

Vile uende kusema kwa mfalme wako. Inapaswa kuondoka na punda yangu kuangalia hii shamba mupya sasa miliuza na mitaenda kuiona. . .

Wakati aliondoka na punda yake yule mugeni, mutumishi alirudia. Mu njia aliwaza:

Watumishi weingine walifanya ninyi?

Munataka kusikia? Mutumishi ya mbili alipeleka muito ya mfalme kwa mutu mwingine. Yeye alikuwa na ma shamba ya mingi. Mbulongo ya ma shamba yake ilikuwa teke-teke. Alikuwa na ngombe juu ya kurima, lakini hasikumuenee. Mbele ya ma siku wadogo aliuza na ingine ma ngombe kumi. Sasa pamoja na watumishi wake eko tayari kuwapima kama watatumika muzuri. Ile saa alisikia sauti ya mutumishi ya mfalme:

Ee bwana muzuri wangu, minakuja kwako. Mfalme munajua, ngapi anamisifu na anamipenda sana!

Na mimi, mtoto wangu, minamusifu na minamupenda. Lakini sema unataka ninyi?

Mfalme anamiita mu nyumba yake juu yakufurahi pamoja na yeye, kwa ndoa ya ntoto wake. Meza ya chakula ni tayari. Yeye anamiongolea.

Mutumishi aliongolea kuona furaha ya yule mutu. Lakini alishangaa,

wakati alimuona yule mutu kusikitika na kutupa chini kichwa yake

Oh, yeye alisema, sasa mfalme alipata saa kuniita?

Sikia mtoto wangu, uende na asema kwa mfalme wako ya kama minamushukuru sana juu ya hii mapendo na mwito yake, lakini misitaweze. Miliisha kuuza ma ngombe kumi na mitaenda ma shamba yangu kupima kama wataweza kutumika muzuri. Minasikitika kwa sababu misiweze kukuja.

Ku moja fasi ilikuwa mupandazia walijikutana wale watumishi.

Ulifanya ninyi: Alimuuliza yule ya kwanza.

Misikufanye kintu. Huyu mutu aliyemwita mfalme wetu alipenda kwenda ma shamba yake juu ya kupima ma ngombe yake. Alipotesha hii wakati muzuri kufurahi na kukula pamoja na Mfalme. Lakini weye ulifanya ninyi?

Na mimi hakuna kintu. Mfalme watu fasi wapi alipata hawa warafiki wake? Yeye aliuza shambna moja na alisema ya kama ataenda kuiona. Hasitakuje hii busiku kwetu. Na hii matayarisho ya chakula itapoteshwa. Sasa tutaangalia mfalme wetu atasema ninyi mbele ya hii mufano mubaya ya warafiki wake.

Uikala hapa kiloko; tutaongolea kufika na mwingine mutumishi ya tatu.

Tazama, yeye anakuja ya mbali. Alikarimbia, lakini uso yake hasikuonyeshe furaha. Beingine wa mbili walimuuliza habari yako nduku wetu?

Milienda kwa huyu mutu, lakini milikimbia mbio, kwa sababu alitaka kunipika. Miye na namna muzuri milimwita, vile mukusema:

Mweye muko bwana fulani?

Ndivyo, yeye alinijibu. Unataka ninyi?

Minakuja toka mfalme mukubwa wangu, mwenye alinituma na hii mwito papier juu ya kufika na mweye mu Shangilio na meza yake, kwa sababu anafanya ndoa ya mtoto wake. Mukujeni na mweye. Yeye anamiita.

Na tazama jibu yake: Uniache mtoto wangu. Mimi nikona ndoa yangu.

Nikusema, mbele ya masiku wadogo milifanya ndio yangu na misiweze sasa kukuja. Sema kwa mukubwa yako hasiniongolee.

Mfalme, wakati watumishi wake walirudia na walimwambia hii mambo yote, alishirika sana. sasa watumishi waliongolea ingine hamuri yake.

Musikie, anawaambia. Wale walikatala kukuja hanawastahili ya hii sifa ukubwa yangu. Wakati ingine watatubu, lakini itakuwa mbali ingine mwito. Sasa hatunana kupotesha wakati wetu. Meza ni tayari. Nyumba yetu ni munene na iko namna kuingia watu wa mingi kabisa. Kwa hivi mwende kuleta watu weingine.

Wa nani, ee mfalme wetu? Alimuuliza mutumishi moja.

Kila mutu, mwenye mutamupata mu njia, mu kiwanja na ku kila fasi.

Wale wa njaala, wagonjwa, wamasikini, wakipofu, watu ya kilema, wale ya umivu na wote wa nduku, wenye wekona mambo ku uzima yao, mwende kuwaita. Hawa wote wekona lazima ya mapendo na wema.

Watumishi wakle walikimbia. Ku moja fasi ya kona mutu masikini moja aliomba saidio. Mutumishi alimubeba na alimusimamisha:

Unanipeleka wapi, mtoto wangu?

Kuja mbio na usiniulize. Mfalme anakuita mu nyumba yake juu ya kula pamoja.

Anaita miye? Unafanya kosa. Unanilanda na unacheza na hali ubaya yangu.

Hapana, minakusema. Mfalme anakuita. Tuende pamoja.

Ee mtu muzuri wangu, unanipatia furaha mingi. Lakini uniache kiloko kutegeneza ma nywele yangu, kunawa kiloko uso yangu, kuvaa na moja nguo muzuri. Namna gani mitakuja na mitasimama mbele ya mfalme? . . . . . . Watu wa mingi sawa vile yule mutu waliongozwa kwa hii Meza ya mfalme. Watumishi walienda mara ya mbili katikati ya ma njia na ma fasiyote juu yakutafuta na watu weingine. Waliwaambia: Mukujeni kwa sababu hasikuyale fasi ku Meza ya mfalme wetu.

Ku mwisho nyumba ya mfalme iliyala. Kisha alikuja na mfalme.

Anakuja, anakuja ilisikiwa sauti moja. Watu wote walisimama kumupokelea.

Wafo wako. Yambo yenu, aliwasalimia na mucheko mfalme. Muikale. Hii shangilio ya leo ni shangilio yenu, ni furaha yenu. Hii chakula ni chakula yenu. Musisikie haya.

Vile ilianza furaha ukubwa. Mfalme alizuguluka kuona pembeni watu wote, wenye walikuja. Kwa kila mutu alisemaka na sauti moja. Uso yake ilikuwa butamu. Ngapi wema alikuwana hii siku! Lakini watu waliwaza ya kama mfalme atakuwa makari na matata. Lakini mbele yao waliona moja mfalme mupole na mwenye butamu.

Lakini kisha saa kilko uso ya mfalme iligeuza na ilifanyikwa makari.

Aliona mutu moja na namna makari na alimuuliza:

Namna gani weye uliingia hapa ndani? Angalia watu weingine. Weko wa masikini, lakini walikuja na heshima, walinawa, walivaa manguo kiloko kuliko wazuri na waliikala hapa. Lakini weye ulikuwa na buchafu mingi na uliingia ndani bila heshima, bila haya. Usikuweze kuvaa moja nguo kupita muzuri na mupya? Kama usikukuwe nayo, ilikuwa namna kuomba moja nguo toka watumihsi wangu. Lakini weye usikuheshimiwe hii Meza yangu. Ulifanya hivi juu ya kunileta kwangu haya na kibego.

Kisha alipindula kichwa yake, aliona watumishi wake na waliwaambia:

Mwende, kumubeba huyu mutu mbio na mutamutupa inje. Hana stahili kuikala katikati yetu. Mwende kumutupa mu buloko ya giza. Pale atabakia daima ndani ya giza. Atateswa kwa milele. . .

***MAELEZEO NA MATENDO KU UZIME YETU***

Ku hii fasi, inaisha, watoto wangu, hii Historia ya hii Meza ukubwa.

Hii Historia yote ni moja mufano (Parabole). Na wakati ingine milimielezea ni ninyi Parabole. Nikusema ni moja Historia, mukongo yake inafuchika moja maana ingine kuliko muzuri ya roho. Sasa tutaangalia maana ya hii Mufano:

Ya kwanza ni nani huyu mfalme?

Ni Mungu, hakuna mukubwa mwingine kuliko ya Mungu. Yeye ni mfalme ya wa mufalme na Bwana ya wa bwana. Yeye ni yulu ya watu na wakubwa wote. Yeye ni Bwana ya mbingu na inchi yetu.

Na Meza yake ni ninyi?

. . . . . . . . . . . . . .

Minaona ya kama hamuweze kunijibu. Mitamijibu mimi. Meza anatayarisha Mungu juu ya watu wote, ni Ufalme ya mbinguni, ni Paradizo. Ku inchi yetu Paradizo ya Mungu ni Kanisa yake. Mu mbingu ni Ufalme Takatifu.

Wa nani weko wale aliwaita mfalme juu ya kufurahi na kukula na hawa?

Tuko sisi watu wote. Weko watu wote ya dunia. Mungu anataka kuokolewa watu wote ya dunia na anatuita.

Na wa nani weko wale watumishi, wenye wanaita watu kwa hii furaha ya Meza ya Mungu?

Minazania, ya kama inapaswa kuwa wale watu wanahubiri mambo na fundisho ya Mungu, nikusema wa Nabii, wa Mitume, wa Padri Watakatifu ya kanisa yetu. Na leo weko wahubiri na walimu ya fundisho ya Mungu. . .

Ni kweli ya kama Mungu anaita watu na namna ingine, ile Yeye anajua.

Mweye munasema ninyi? Watu wote wanapokelea ma mwito ya Mungu?

Hapana. Watu wa mingi kabisa habapokelee ma mwito Yake, kwani wanaishi mbali ya Kanisa na uzima ya Mungu.

Namna gani munasikia hii mambo, watoto wangu?

Moja alama ni ya kama wale watu wanakatala kukuja mu Misa. Kila mu
Juma wanakuja watu wadogo mu Liturgia takatifu. Wa mingi wanalofa.

Ndivyo. Wanalofa. Kengele inaria na inawaita. Iko namna sawa kuwaambia, sawa walisema watumishi ya hii Parabole: « Mukujeni ku Meza ya Mungu, anamiongolea». Liturgia Takatifu ni moja Meza ya mbingu. Kwa hivi na hii fasi inafanyikwa Liturgia takatifu inaitwa Meza Takatifu!

Na mambo ninyi wanasema wale watu, wenye wanakatala kuingia mu Misa?
Moja anasema: Misina wakati, Misiweze. . . « Mwingine anasema: « Mitaenda

safari. Mitaenda ku Mukini yangu». Mwingine anasema: « Mitatayarisha

chakula mu Juma asubui juu ya kukula watu ya jamaa yangu midi»

Lakini na watoto weingine, kama mutawaita kukuja ku Masomo hii ya Kanisa yetu, wanamijibu ninyi?

Mtoto moja, anasema: « Minataka kusoma ma fundisho ya masomo yangu»
Mwingine: « Niko muzaifu, misina na nguvu. Misiweze muzuri». Mtoto mwingine: « Sasa ni saa ya muchezo». Na weingine watoto wanasema ma sauti ingine ya kuachana kwa sababu hababpende kusikia sauti ya Mungu.

Na wale watu, wenye habakukuje mu Kanisa, wanabakia na njaala. Munajua chakula gani Bwana wetu anatupatia mu Liturgia Takatifu?

Anatupatia mumoja maugu Yake: Nikusema: Komonyo Takatifu. HIi ni
Mwili na Damu Yake.

Ndivyo, watoto wangu, maana ya hii chakula ya Parabole ni Mwili na Damu ya Bwana wetu, iliyepatia kwa Wanafunji wake mangaribi ya siku Mukazi Ine Mukubwa. Inaitwa na Karamu Mistike (ya Siri), kwa sababu na namna mistike Mungu Yesu Kristu alitutoa kwa sisi wote Mwili na Damu Yake paka mara moja juu ya wokoovu wetu. Inaitwa Karamu kwani ni chakula yetu ya roho ya kila siku. Sawa vile sisi kila mangaribi, kisha chakula tunasoma Apodipnon Kidogo, nikusema Sala kisha Dipnon, (Dipnon ni chakula ya busiku), vile na waaminifu wetu ya zamani kila busiku walipewa Dipnon Takatifu, nikusema zamani walifanya Liturgia kila busiku na walipewa Mwili na damu ya Kristu kama Dipnon Takatifu. Sasa katika mapokeo yetu Liturgia inafanyikwa asubui. Na inapaswa kila mara inafanyikwa Liturgia Takatifu kupewa na Mwili na damu ya Kristu, kama tuko tayari kwa roho yetu.

Juu ya ninyi inaitwa hii Meza kwa Siri Komonyo? Mweye munasikia?

Minazania, kwa sababu sisi tunaunganishwa na Bwana Yesu Kristu. .
Komonyo, watoto wangu, ni ushirika, ungano, na Yesu Kristu. Yesu Kristu alikuwa wakati moja paka Mungu, kisha alifanyikwa na mutu. Nikusema Yeye aliunganishwa na hali kimutu yetu. Alifanyikwa mutu muzima sawa sisi, lakini bila sambi. Yeye alikuwa Mungyu na mutu pamoja. Sisi tuko watu, . lakini kama tutaunganishwa na Bwana Yesu, nikusema na Mwili na Damu yake, tunafanyikwa na sisi wa mungu katika neema ya Roho Mutakatifu. Kama tunapewa na stahili, tunaunganishwa na Yesu Kristu. Yeye anaingia kwa sisi na sisi tunaingia kwake, ndani ya uzima yake. Vile yeye anatuwambia: « Yeye anayekula mwili wangu, na kunywa damu yangu, ana uzima ya milele; na mi mitamufufua siku ya mwisho. Kwa maana mwili yangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kikunywa cha kweli. Yeye mwenye kula mwili wangu na kunywa damu yangu anakaa ndani yangu, nami ndani yake» (Yoane 6, 54-56).

Hakuna zawandi kuliko ukubwa ya Komonyo Takatifu! Lakini watu wa mingi wanakatala kukarimbia na kumubeba. Padri ndani ya Liturgia takatifu anatayarisha Hii Karamu Kistike. Na ku mwisho anatuita: « Kwa kumwogopa Mungu, na imani, na mapendo, gongeeni». Lakini watu

wadogo wanakarimbia. Juu ya ninyi? Weingine wanasema ninyi? Kama tutauliza mukristu moja ao mtoto moja: ‘ Leo juu ya ninyi usikupewe Komonyo Takatifu? Jibu gani tutasikia?

Watasema hivi karibu: Sisi vile tulizombelea kupumunika paka ma Siku
Kuu wakubwa ya Kanisa yetu.

Lakini hii zwezo kibaya! Kama kwa mufano tunakula na tunakunywa chakula paka ma Siku Kuu wakubwa, ku Siku Kuu ya Ufufuo na ya Kuzaliwa ya Kristu, tutafanya ninyi? Tutakufa. Nikusema hatuweze kuishi bila chakula ya mwili, kwa sababu tutakufa. Vile wanakufa katika roho yao, wale watu wanakatala kubeba Komonyo Takatifu ya Mungu. Chakula ya roho ni kila siku Komonyo Takatifu.

Beinmgine watu wanasema hivi: Misikufanye kifungo ya chakula na misiweze kupumunika.

Kama tunataka kupumunika mambo ya kwanza ni kuishi uzima safi, bila zambi. Hii ni kifungo ukweli. Kama tunafanya ma zambi na ma kosa fulani tutafanya Ungamo kwa padri ya roho yetu. Tunaweza kuikala kukula na mikono na buchafu? hapana. Vile na sisi hatuweze kukaribia hii Meza takatifu kubeba Komonyo ya Mungu bila kusafisha uzima na ma roho yetu na Ungamo. Vile alifanya na huyu mfalme ya Parabole ya leo. Alitafuta mutu moja mwenye buchafu na alimutosha inje na alimulipiza. Basi, ni lazima kuwa wasafi, kama iko namna. Kabisa inapaswa kusopoka kinywa na ma sauti yetu, lakini na ingine ma zambi. Kama hatunana mambo ya zambi fulani na tunakatala kupumunika hii ni zambi yetu, kwa sababu Mungu Yesu Kristu katika kinywa ya padri anatuita na sisi tunamuzarau, na tunakatala kukaribia. Basi, aipaswe kupotea Hii zawandi ya Mungu, kwani hivi tunapotea furaha na utukufu na Ufalme ya Mbingu.

FUNDISHO: Kila mu Juma inapaswa kukarimbia mu Kikombe takatifu, kama tuko wasafi na baraka ya padri wetu ya roho.

SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Twaeni, kuleni, huu ni mwili wangu. . . Nyweni ninyi wote, hii ni Damu yangu ya Agano Jipya. . . «

## FUNDISHO MAKUMI MBILI NA SITA
## YESU KRISTU ALITESWA KWA SISI

HISTORIA. Leo minataka kumiambia historia moja, watoto wangu. Ni historia ya ajaabu, lakini ni ukweli. Wakati fulani ndani ya moja muji ilifanyikwa funjo. Watu wale walikuwa ma nyumba wao, walisikia makelele na malalamiko na walitoka inje kuangalia. Watu ndani ya hii kelele walisikia sauti nguvu ya mutu moja na waliona mutu moja kukibia.

Mumukamate, Mumubabe! Alisikiwa moja sauti ya beingine watu, wenye walikimbia mbio ya kumukamata mutu moja. Mumukamate! Mumukamate! . Yeye ni mwuaji (assasin). Aliwua mutu.

Watu bado kuona na kusikia muzuri mambo gani ilikuwa, waliona kutembea mbele yao mutu moja na hali yake ilikuwa kibaya. Manguo yake walikuwa na damu, mikono yake na bilonda, ma macho yake makari na alitembea mbio juu ya kuokolewa.

Kiloko mbali ya moja fasi ingine watu ya mbili walikombana moja mwingine. Na mara moja moja alitosha kisu na aliiweka ndani ya kilari ya nduku mwingine. Huyu alilalamika, aliria na mara moja alianguka chini. Walisikia ma jerani na walikimbia pale kuona hii mambo. Hii saa huyu mwuaji alikimbia. Wajerani, wenye walimuona, waliacha huyu mutu mwenye kilonda na walikimbia kumukamata huyu mwuaji. Kisha saa kiloko waliingia kwa hii funjo na watu ya poliche, wenye walianza kumufukuza juu ya kumukamata. Wote pamoja wanapaza sauti na wanasema: Mumukamate! . . .

Na yule mwuaji? Anashindana kuokolewa. Anapindula ya njia moja ku ingine na ile nguvu ilimubakia. Jasu ya baridi ilijaza uso yake. Anakimbia na anatafuta fasi moja juu ya kufuchamwa.

Na tazama, ku dakika moja hasikuonekane. Aliingia ndani ya nyumba moja.

Ni nyumba ya nduku yake. Alifungula na haraka mulango na aliingia ndani. Nduku yake alimuona hivi na damu ku mwili yake na alishangaa. Mbele ya kumuelezea mambo gani alipata, mara moja alianguka chini mbele yake na alimuomba:

Nduku wangu, uniokoe. Mimi niko mwuaji. Wananitafuta kunibaba.
Uniokoe. Mitafanya ninyi sasa? Ole wangu, ole wangu. Watanikamata. Uniokoe.

Nduku mukubwa yake alikuwa mwema na alisikitika toka hii jabo taambu ya nduku yake. Alikamata mupango kumusaidia.

Simama, alimwambia. Usiogope. Mbio tosha manguo ile unavaa. Mitaivala mimi. Na weye beba manguo yangu. Kuja mbio, usichelewe. Wale wanakufukuza, watafika mbio inje. Tosha manguo hii yako na fanya kimya.
Wakati alisema hii ma sauti nduku mukubwa yake alibeba na alivaa manguo ya nduku yake.

Kisha saa kiloko kundi ya poliche na watu weingine walikuja inje na walimufokea kutoka inje.

Tazama, hapa ndani ya hii nyumba aliingia huyu mutu mubaya.

Mumukamate! Lufu kwa huyu mwuaji!

Alisikia mwuaji ya ndani malalamiko yao ya inje na alitetemeka kwa ajili ya boka yake. Lakini mukubwa yake alimwambia ya kama haipaswe kutetemeka.

Hazina ya watu walipomona mulango na waliingia ndani. Walimuona yule nduku na manguo ya kujaza na damu. Walimukamata na walimukokota inje.

Ee Mwuaji! Tulikukamata! Munyanganyi, mutu mubaya kabisa! sasa utaenda wapi? Utaripa sasa na damu yako hii tendo yako kibaya.

Wakati walisema watu hii ma sauti wao, walimupatia huyu nduku kwa mikono ya watu ya poliche. Hasikukuwe lazima kumuhukumu. Ma nguo yake walikuwa na kujaza na damu. Yeye hasikuseme kintu. Na wote watu walijua ya kama huyu alikuwa mwuaji mubaya.

Wakubwa walitegeneza siku ya uhukumu yake. Ile siku nyumba ya Uhukumu iliisha kujaza ya watu wa mingi. Wa nduku na wajerani ya yule mutu aliyemwua nduku yake walifokea na sauti nguvu:

Lufu! Lufu kwa mwuaji!
Na huyu nduku mukubwa aliikala bila kusema ao kutega mu kiti ya watu wakosefu. Uso yake ilikuwa upole na ya amani. Hasiseme na hesionyeshe mufano mubaya mbele ya watu weingine na mbele ya wajerani ya yule mutu aliyekufa. Anaongolea mupango ya wakubwa ya Uhukumu na amani na kinya. Lakini alikuwa musiyekosefu. Hata mutu moja hasikujue hii mambo. Hata moja? Hapana! Ndani ya nyumba ya Uhukumu alikuja na nduku yake. Yeye ni muloko yake, aliyemwua yulu mutu mugeni. Yeye ekona kichwa yake chini ya bulongo. Ndani yake anasikia tetemeko munene.

Mukubwa nduku yangu anaikala sasa kwa kitu ya mukosefu, lakini anateswa kwa ajili yangu. Juu ya mimi yeye anahukumwa sasa.
Makutano ya wakubwa ya uhukumu inaanza. Washuhuda wa mingi walisema ya kama huyu ni mwuaji ukweli. Walimukamata na manguo yake, iliwakuwa na damu mingi kwao. Kisha saa kiloko anajibu huyu mutu. Hasiseme ma sauti mingi.

Paka hii:

Mimi niko musiyekosefu! . . .
Lakini nani anamusandiki? Watu wote wanasema ya kama yeye ni na eko mustahili ya lufu. Na wote wanapaza sauti kusema:

Lufu! Yeye ni stahili ya lufu! .

Na mupango hasikuchelewe kutoka: Yeye ni mukosefu na inapaswa kufa.

Musiyekufa inapaswa kukufa. Ugumu mupango!

Mukubwa nduku anapokelea na utulivu mupango ya wakubwa ya Uhukumu.

Mapendo ukubwa alimwambia kuvaa manguo ya nduku yake na sasa kupokelea malipizi ya lufu.

Hii mupango inamalizwa. Wa askari walimubeba huyu mutu musiyekosefu na walimukokota ku fasi ya mateso na mwisho yake. Mukongo yake watu ya dunia habajue kazi ninyi mubaya na hanahaki walifanya. Wanaendelea kufokea:

Lufu! Lufu! . . .

Paka mutu moja anamufata mukubwa nduku yake na anaria. Yeye eko muloko yake, aliyekuwa mwuaji ukweli. Hazina ya watu inasimama. Saa ya lufu ilifika. Ile saa anakimbia ku mbele muloko nduku yake, alikaribia mukubwa yake, mwenye sasa eko tayari kumukata kichwa yake.

Hii makutano ya wa nduku ya mbili ilikuwa na sikitiko na machozi mingi.

Muloko mukosefu anapika magochi mbele ya mukubwa yake na anaria. Anataka kumwambia sauti moja, lakini hasiweze. Mukubwa nduku yake, alimwambia:

Simama. Mimi mitakufa kwa ajili yako. Paka minataka moja matakio ya weye. Nduku wangu, usisahabu hii tendo kizuri sasa milikufanyisia. Hii manguo yangu ulivala, sopoka usiijaze na buchafu ao na ma zambi ingine ku uzima yako. . .

Wa askari walikuwa makari. Walisimamisha makutano yao. Muloko yake alichofa kiloko. Na mukubwa ya wa askari alipatia alama. Mara moja mukubwa nduku alianguka chini mufu. Alikufa kwa mapendo ya muloko nduku yake.

Na nduku yake? Ku uzima yake yote alisikia kila saa ma sauti ya mwisho ya nduku yake:

Nduku wangu, usisahabu, hii tendo kizuri milikufanyisia. Usijaze na buchafu ya zambi hii manguo yangu mimi milikupatia kuvaa.

Na hasikusahabu hii kazi ya mukubwa yake. Kila siku alikujaka mu kaburi ya nduku yake na alimwambia hii malako: « Ee nduku wangu, misitaweze kusahabu hii tendo kizuri uliniifanyisia?

Alishindana ku uzima yake yote kuonyesha na yeye mapendo kwa watu weingine, lakini hapana hata mingi sawa alifanya nduku yake kwa huyu, lakini alisaidia na yeye wa nduku wake. . .

MAELEZEO-MATENDO KU UZIMA YETU.

Watoto wangu, minamiona na minasikia ajaabu ngapi mulipata toka hii fundisho yetu ya leo. Mutashangaa tena kuliko kama sasa mitamionyesha na picha (photo) ya yule mukubwa nduku yake.

( Hapa mwalimu atapindula mu kibabashi na ataonyesha na mufano upole na kimya Ikona Ya Bwana Yesu Kristu pa Musalaba).

Huyu, watoto wangu ni musiyesulumbiwa Bwana wetu na sisi ile ma siku tulishangilia Mateso Takatifu yake.

Ni nani eko huyu Mwenye Usulumbiwa?

Yeye ni musiyekosefu. Hasikufanye hata kazi kibaya moja. Kupindua alijaza dunia na bintu wazuri wote. Kila kintu na kiumbe sisi tunaona mu dunia ni kiumbe yake. Yeye ni nduku mukubwa yetu, Mwana wa pekee na Neno ya Mungu.

Lakini ilikuja saa, na Huyu musiyekosefu alitaambu mwuaji. Sisi wote tuko wawuji, wenye zambi na watu mabaya. Sisi wote tulianguka ndani ya kila zambi. Malipizi ya milele alituongolea. Lakini, alikuja Mwana wa Mungu alivaa manguo ya mwili wanadamu wetu, alifanyika mutu sawa sisi juu ya kuokoa kila mutu, sisi wote.

Yesu Kristu ni Musiyekosefu mukubwa. Na ku hii inchi yetu aliishi paka alisaidia watu wote. Mukumbukeni, watoto wangu, ma miujiza ngapi alifanya? Wangapi watu aliwapatia nuru ya ma macho yao? Alisimama watu ya kilema, alisafisha bilonda ya walepre, alifufuka watu, alizimba wenye njaala, alitunza wenye malari na aliuhuru, wenye walikuwa na pepo buchafu. Munataka kuandika na kusema paka na ma neno ya mbili alifanya ninyi Yesu Kristu, wakati alikuja mu dunia? Anatusema Mutume Petro: «Alipita kusaidia wote».

Lakini juu ya hii ma wema na ma saidio, juu uzima yake takatifu, namna gani aliripwa? Tazama, Musalaba ya Golgota inatuonyesha, malipo ninyi alibeba. Walimukokota kama munyanganyi ma nyumba ya kumuhukumu na alisikia ma sauti ya wa nduku wake:

Lufu! Lufu! . . . Umusulubishe, umusulubishe.

Walipika Mwili yake sana na fimbo. Walipika Uso yake mwenye mwangaza.

Pa kichwa yake walimuweka taji ya miimba. Walimutosha manguo na walimuvaa nguo nyekunda juu ya kumuchokoza. Walimupatia ku mukono simbala moja juu ya kumucheka. Walimutema na tema mingi pa uso yake. Kwa midomo yake walimupatia ya kunywa mvinyo iliyochanganyika na nyongo. Kama munyanganyi walimukokota ku lufu. Na kama munganyanyi walimupanda pa Musalaba. Na kama mwenye zambi mukubwa walimupigilia na misumari marefu.

Hii yote mateso ya Mungu wetu Yesu Kristu tutaishi hii Juma ya Mateso Takatifu Yake, ile inaanza toka mu Juma ya Matawi mangaribi. Na sisi, kwani tuko watoto wazuri na tunamupenda Yesu Kristu, tutamuuliza:

Ee Kristu mwenye usulumbiwa, juu ya ninyi ulipanda pa Musalaba, kwani

Weye uko musiyekosefu?

Na tutabeba hii jibu yake:

Mwana ya mutu alikuja kupatia uzima yake juu ya kuokolewa watu ya dunia. Na tena tutasikia toka Mutume Petro kutuwambia: Kristu aliteswa kwa sisi.

Kwa sisi aliteswa Kristu, watoto wangu. Sawa vile yule mukubwa nduku ya fundisho yetu ya leo alikufa juu ya mapendo ya muloko nduku yake vile na tena kuliko mingi alisulumbiwa Yesu Kristu mwenye bila kosa. Sisi inapaswa kupata ile mateso Yake na hapana Yeye, lakini Yeye alitoa sandaka uzima yake juu ya wokovu wetu.

Mikono yake walizambalisha paka ma baraka na ma wema. Mikono yetu wanafanya kila siku ma zambi ya mingi na mikono yetu, basi, ilipaswa kupijiliwa na misumari marefu. Lakini walipigiliwa mikono Yake, ile ya safi na takatifu.

Mikulu yake walitembea kuleta baraka na matendo wazuri, lakini mikulu yetu, ku kila fasi wataenda watafanya matendo mabaya na ma zambi mingi. Basi, mikulu yetu ilipaswa kupigiliwa na hapana mikulu takatifu ya Kristu.

Lunrimi yake alisemaka paka ma sauti takatifu na fundisho ukweli, lakini lunrimi yetu kila saa anasema ma sauti mabaya na matusi na machubulana mbele ya wa nduku wetu. Basi lunrimi yetu ilipaswa kupima ya kunywa mvinyo na nyongo na hapana lunrimi ya Bwana Yesu Kristu wetu.

Sisi tunafanya kila siku ma zambi na ilipaswa kulipizwa na hapana Kristu, mwenye hasikufanye hata zambi moja na paka Yeye ni mwenye bila zambi.

Sawa huyu nduku mukubwa, mbele ya kumwua wa askari, aliomba kintu moja ya muloko yake, vile na Kristu, aliyemwanga Damu yake pa Musalaba, anatwaambia kwa kila mukristu:

Mtoto wangu, usisahabu, hii kazi muzuri mimi milikufanyisia. Kabisa, usisahabu sasa hii Juma Takatifu. Usisahabu Mateso yangu. Usilete buchafu kwa roho yako.

Hii Juma Takatifu, watoto wangu, haina ya kucheka na kucheza na kufurahi. Yesu Kristu Mungu wetu anateswa pa Musalaba na toka watu wabaya. Akili yetu inapaswa kuwaza hii mateso yake. Mu Kanisa kila siku na mangaribi. Na pasopo mingi inapaswa kusikia hii wimbo na ma somo ya hii Kitabu inayeitwa Juma Takatifu na Mukubwa.

Wakati itakuja Mukazi Tano Mukubwa, sisi inapaswa kusimama chini ya Musalaba ya Kristu na tutamwaambia:

Ee Bwana mwenye usulumbiwa, tunakushukuru juu ya hii munene na bila kuibalula zawandi yako. Kwani sisi tuko watoto Wako, tunakulapa ya kama tutakumbuka daima hii kazi kizuri ulitufanyisia. Utustahili kuonekana wafwasi wako wenye kadiri. Utustahili kushangilia na hii Siku Kuu ya Ufufuo wako na kufufuka na sisi ku moja uzima mupya. Amina. FUNDISHO: Ee Yesu Kristu, ulisulumbiwa kwa ajili ya wokovu wangu. SAUTI YA MADIKO TAKATIFU: « Kristo aliteswa kwa ajili yetu. . . « (Barua ya kwanza ya Petro 2, 21)

## FUNDISHO MAKUMI MBILI NA SABA
## MWENDO KU MUKINI EMAU
## (Luka 24, 13-31)

***NAMNA YA KUKARIBIA***

Kristu alifufuka, watoto wangu.

Kweli alifufuka!

Misisikie kusema hii salamu na sauti yenu nguvu. Na kintu ingine tena.

Misione furaha mingi ma uso yenu. Militaka hii mufano ya furaha ku kuwa mingi kuliko ma uso yenu.

Ni kweli ya kama hii wakati ya Ufufuo ya Kristu mulifurahi na mulikula na mayayi nyekunda. Lakini juu ya ninyi tanapika mayayi na ragi mwekunda. Munajua?

Miye minajua, juu ya ninyi tunapika mayayi mwekunda. Minazania ya kama hii ragi mwekunda ni maana ya Damu ya Kristu, iliyejitoa pa Musalaba juu ya wokovu ya watu wote ya dunia.

Ni sauti ukweli hii. Lakini ingine nani atatusema? Juu ya ninyi tunapika mayayi na ragi mwekunda? . . .

Mitamijibu mimi, watoto wangu. Moja riyayi, watoto, sawa vile na bintu ingine ya dunia, ni moja symbole ya Ufufuo ya Kristu. Riyayi inafanana kama moja kaburi. Na sawa vile Kaburi ya Kristu ilikuwa ya fasi yake kufungwa muzuri, vile na riyayi moja ni ya fasi yake pembeni ya kufunga muzuri. Riyayi iko ma fasi yake pembeni ya kufunga muzuri bila kuingia hata kiloko pepo ya inje, lakini ndani yake inafuchika moja uzima. Ndani yake anaishi ndeke mtoto moja. Kaburi ya Kristu ilikuwa ma fasi yake kufungwa nguvu. Lakini ndani yake ilifuchama Uzima. Kristu ni Uzima. Yeye ni Uzima katika Kaburi.

Sawa vile, basi, sisi tunaona ragi mwekunda ku moja riyayi, vile na wa Kristiani wetu wekona mingi furaha ku roho na uzima yao. Ma roho yao inacheza toka furaha, vile na ma macho na ma uso yao wanafurahi yote. Ufufuo ya Kristu ni Jua ya furaha na hata moja mawingo ya taambu na sikitiko hasiweze kuifunika.

HISTORIA. Lakini minaona wanafunji ya mbili, wenye wekona sikitiko na taambu. Hana wanafunji wetu, toka Masomo yetu. Hawa weko wanafunji ya ingine Masomo ya kwanza. Ni nani ilikuwa Masomo ya Mungu ya Kwanza?

Ilikuwa hii iliyekuwa Mwalimu Bwana Yesu Kristu.

Waliondoka toka Yerusalema na wanaenda ku moja mukini iliyeitwa Emau.

Ma jina yao ni Luka na Kleopa. Iliopita wakati ya ma siku mbili tangu hii siku Yesu Kristu alifufuka. Ilikuja siku ya tatu. Ma roho yao ni sikitiko kama baridi. Wanatembea na kichwa yao chini na wanasuburia:

Mwalimu yetu anatoka daima. Tulimupotea. Hatutaweze kumuona mara ingine.

Tutafanya ninyi? Ni muzuri kwa sababu wakubwa wa Ebrania hasikukamate na sisi. Chuki yao ni munene sana na wanataka, kama iko namna kuharabisha na kutosha ya hii dunia kila kintu inayekumbuka Yesu Kristu na uzima yake.

Na sasa sisi tutafanya ninyi wenye wenyewe?

Misijue. . .

Vile karibu ilikuwa mazungumuzo yao. Lakini saa ya mingi mu njia wananyamaza. Wanatembea na muchoko mingi. Mawigo ya taambu ilifunika ma akili yao na hata kintu moja hasiweze kufukuza hii sikitiko yao.

Hata? Hapana, watoto wangu. Ni moja kitumaini ile itageuza hali ya roho yao. Mukongo yao walisikia mwendo ya mutu moja.

Anakuja mutu moja, alisema mwanafunji moja.

Tutasimama kiloko juu ya kupita? Alimuuliza mwingine.

Mutu mugeni anakarimbia. Anaenda pembeni yao. Anatembea pamoja na wao.

Na mara moja aliwauliza:

E, juu ya ninyi muko vile? Muniseme maneno gani munatembea na sikitiko ma uso yenu?

E bwana wetu, mambo gani iko, weye haujue? Unaikala wapi? Unaishi ndani ya Yerusalema na hausikie hata ya mutu moja mambo gani ilifanyikwa ku hii muji?

Nikusema mambo gani? Muniseme na kwangu. Misijue.

Wanafunji wale ya mbili waliona moja mwingine juu ya kuichika kumuelezea kwa huyu mugeni hii yote mambo. Na walianza kumuelezea.

Basi, haukusikie juu ya moja Yesu? Yeye ni Yesu toka Nazareti.

Kuliko muzuri kusema alikuwa, kwa sababu walimwua. Huyu, basi Yesu Kristu alionekana na nguvu munene. Alikuwa mwenyezi na ku sauti na ku matendo yake. Alihubiri kupita muzuri ya kila ingine mutu na alifanya na miujiza. Alionekena Nabi mukubwa mbele ya Mungu na mbele ya ma macho ya watu. Lakini. . .

Lakini? . . . Aliwauliza huyu mutu mugeni. Museme kisha mambo yake.

Na wote mbili wanafunji waliendelea mwendo yao na taambu mingi.

Wakuhani na weingine wakubwa ya wa Ebrania walimuchukia na walimuhukumu kukufa pa Musalaba. . .

Hata na hii tangazo haukusikie? Hakusikie ya musalaba ya tatu mu

Kilima Golgota?

Muendelee, aliwaambia yule mutu mugeni.

Namna gani tutaendelea? Sisi tupotesha kila kitumaini. Sisi tulizania ya kama Yeye ni Mwokozi, mwenye tulimuongolea, yeye atauhuru Inchi yetu na ataokoa Kabila ya Israeli wetu. Lakini sasa ilipita wakati ya masiku tatu. Alisulumbia. Bado kuona kintu moja juu ya kufufua matumaini yetu. . .

Walipenda hapa kusimama. Lakini mwingine alimwambia. Sema hii mambo juu ya wanawake.

A, ndivyo. Tena beingine wanawake, wanafunji yake na ma dada wetu katika roho, leo asubui walitwaambia ma tangazo ya ajaabu. Asubui mapema walienda mu Kaburi ya Kristu. Walitafuta ndani, lakini habakupate Mwili yake. Walirudia na walisema kwa wanafunji wanaume yake ya kama waliona wa Malaika wa mbili, wenye waliwaambia ya kama Yesu anaishi. . . Hii yote ni ma tangazo ya ajaabu!

Na wanafunji wake? Aliwauliza yule mutu mugeni.

Wanafunji wake, wakati walisikia hii ma sauti ya wanawake walikimbia mu Kaburi ya Kristu. Kweli, walipata kaburi wazi. . .

Walitembea sasa na unyamaza. Wanafunji wa mbili walisimama Historia ya hii jabo. Waliongolea kusikia atasema ninyi yule mutu mugeni. Yeye aliwajibu:

Wenye upumbafu na wenye mioyo mizito katika kuamini yote waliyoyasema manabii, Haikupasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake? (Luka 24, 25-26)

Walinyanyula ma macho yao wanafunji wa mbili na waliwaza.

Lakini, huyu mutu anajua mambo wa mingi kabisa na mpaka sasa anaonekana ya kama hasijue kintu na anatuuliza!

Utuseme, unajua ninyi juu ya Yesu Kristu?

Musikie! Wa Nabii wote ya Agano la Kale toka Musa mpaka Yoane

Mutangulizi, wote wanasema juu ya ile mateso na Ufufuo ya Kristu. Kristu alisulumbiwa, lakini sasa aliisha kufufua. . . Na alianza kuwaambia mistari toka Agano la Kale.

Wanafunji wote wa mbili walishangaa kwa hii ma sauti yake. Sikitiko na taambu ilitoka. Wanatembea sasa na furaha. Wanasikia furaha mingi kwa sababu wanasuburia pamoja na huyu mutu, mwenye bando kumufamia. Inawakumbuka sauti butamu ya Mwalimu wao Yesu Kristu.

Endelea kusema, walimwambia na hii saa waliingia ndani ya Mukini Emau.

Hapana, inapaswa kutoka. Mitamiacha. Mpaka hapa ilikuwa njia ya kutembea pamoja.

Utatoka? Hapana. Hatupende weye kutoka. Mapatano na mazungumuzo na weye ni muzuri sana. Tunakuomba kubakia pamoja na sisi. Utaenda wapi sasa? Ilikuja busiku karibu. Bakia kwa sisi. Tunafurahi pamoja na weye.

Alipima kuendelea huyu mutu mugeni njia yake, lakini wanafunji wa mbili walisimama mbele yake ya kumuzimbiria njia. Na alibakia. Aliingia ku hii nyumba na wale walienda na waliikala kukula. Yule Mugeni alikamata mukate ku mkono yake, aliangalia yulu mu mbingu, aliibariki, alikata na kipande-kipande na aliwakabula kukula.

Hii tendo ya kubariki mukate ilikuwa moja tendo ya ajaabu. Ile wakati walisuburia na Yeye walisikia ya kama Huyu Mutu Mugeni anaachana kiloko ya watu weingine. Walitaka kumuuliza, lakini habakuweze. Sasa, wakati walimuona kubariki Mukate sawa vile zamani Mwalimu yao Yesu Kristu, alitoka kila shaka ya kama Huyu Mugeni alikuwa Yesu Kristu na Uso ingine. Walikuwa tayari kumuuliza, lakini. . . Yesu Kristu alikimbia ku mbele ya ma macho yao. Wakati walifungula ma macho ya roho yao, walisikia ya kama huyu Mugeni alikuwa mwenye Ufufuo Yesu Kristu, mwenye kama Mungu alikuwa ma fasi yote.

Walifurahi na walitosha machozi kwa furaha. Walisema katikati yao:

Unaona ma roho yetu namna gani walikuwa, ili wakati yeye alisuburia na sisi? Ma roho yetu walikuwa mwangaza na moto ndani yao.

Ndivyo! Ndivyo! Alimukikiri mwanafunji mwingine. Wa mbili walisema ya kama Bwana Mwalimu wao alikuwa. Bwana wao alifufuka. Tuende, walisema, mukongo mu Yesusalema. Na furaha mingi sasa wanarudia mukongo. Walifika kwa hii nyumba waliikala wanafunji wote. Walikuwa tayari kuwaambia kwa wanafunji weingine hii yote mambo ya ajaabu yao, lakini wanafunji waliwatanguria na waliwaambia:

Munajua mambo moja? Bwana Yesu alifufuka. Alionekana kwa Petro.

Na kwa sisi alionekana, wakati sisi tulitembea hii njia ya kuenda ku

Mukini Emau. Yeye alibariki mukate yetu na kisha alikimbia. . .

***MAELEZEO:***

Ulizo: Wa nani walikuwa wanafunji, wa mbili, wenye walitembea ku Mukini Emau?

Jibu: Walikuwa Luka na Kleopa.

Ulizo: Namna gani ilikuwa hali ya mufano yao, ile wakati ku mwanzo walitembea mu njia?

Jibu: Walikuwa na taambu na sikitiko mingi ndani ya ma roho yao.

Ulizo: Juu ya ninyi?

Jibu: Kwa sababu Mwalimu wao alisulumbiwa na wale walisikia ya kama kila kitumaini juu ya Mwalimu wao ilipotesha.

Ulizo: Ku mwisho ya mwendo yao, namna gani ilikuwa hali ya ma roho yao?

Jibu: Ilijaza ma roho yao na furaha. Moja furaha kwa siri kama moto iliisha kuwaakisha ndani yao.

Ulizo: Namna gani ilifanyikwa hii mageuzo?

Jibu: Aligeuza hali ya ma roho yao Yesu Kristu mwenye ufufuo, aliyeonekana katikati ya njia yao na alisuburia na wale.

Ulizo: Mukumbukeni moja sauti ya yule mukubwa Mugeni?

Jibu: Kila sauti, iliyewalezea ilikuwa ndani ya Madiko Takatifu. Ndivyo, watoto wangu, Kristu alikuwa Yule, aliyesulubiwa na alifufuka katika Madiko Takatifu. Kwa hivi kama Fundisho yetu leo tutabeba hii sauti ya Mutume Paulo:

***FUNDISHO NA SAUTI YA MADIKO TAKATIFU***

« Kristo alikufa kwa sababu ya zambi zetu. . . akafufuka siku ya tatu kama Maandiko yanavyosema» Barua ya kwanza ya Paulo (15, 4).

MATENDO KU UZIMA YETU

Kristu alifufuka. Hii ni Jabo kuliko mukubwa mbele ya ma yoyote ma jabo ya Uzima yetu ya dunia muzima. Kama Kristu hasikufufuke, atakuwa mufu ya milele. Na moja mufu hasitaweze kuishi ndani ya ma roho ya watu mpaka sasa miaka karibu 2000. . Kristu alitoka toka Kaburi, lakini Kaburi yake ilikuwa ya kufungwa, sawa vile ma rayon ya Jua wanaingia ndani ya nyumba bila kupasuka rikalasi ya dirisha.

Hakuna namna kubakia Kristu daima mufu, kwa sababu Yeye ni Uzima ya milele. Na Uzima hasibakia ndani ya kaburi. Alifufuka na alitukuzwa. Na Lufu yake pa Musalaba alilanda Shetani. Alishuka mu Hadeze na aliuhuru wale wa Nabii na wakubwa ya Israeli, wenye waliisha kufa ya zamani na waliongolea mafikisho Yake. Mukona kuona, watoto wangu, moja picha ya Ufufuo ya Kristu? ( Hapa Mwalimu ataonyesha mioja Ikona ya Ufufuo ya Kristu na atawalezea kwa watoto).

Muione hii Ikona sasa. Kristu anaonekana na mwangaza kimungu mingi. Na mukono moja yake anakamata Adamu na mukono ingine anakamata bibi yake Eva. Anauhuru Adamu na Eva na wote wafu, wale walikufa kisha wao. Muangalieni tena. Inaonakana milango ya kupasuka na ma fungulo ya kutupa chini. Kristu aliingia mu buloko ya Gehena, alipasuka ma milango, ma fungolo na ma kofiri. Hakuna mara ingine Hedeze. Wale wanaamini kwa Ufufuo ya Kristu, wanafufua na wale pamoja na Kristu kwa milele. Wanafufua katika roho na wanaishi moja uzima mupya. Na, wakati watakufa, ma nafsi wao wanaishi furaha ya Ufufuo kwa uzima ya milele.

Na kwa sababu alifufuka Kristu, watafufuka na wate wafu. Nini wote mpaka sasa walikufa na wale watakufa itakuja saa ikubwa na wate watafufuka.

Ufufuo ya Kristu ni Jua ya uzima yetu. Inapaswa kusandiki kwa Ufufuo.

Inapaswa kusandiki ya kama wafu wote watafufuka, sawa alifufuka na Jesu Kristu toka musigishi ya lufu yake.

Basi, inapaswa kufurahi kwa Ufufuo ya Kristu, Sisi tuko watoto ya mwenye muzima Kristu. Haipaswe kusikia haya kuhubiri hii Jabo mukubwa na utukuzwa. Hii ma siku kila mwaminifu, wakati anakutana mwingine hasiseme:

Yambo, lakini anasema ninyi?

Kristu alifufuka!
Na mwingine anamujibu:

Kweli alifufuka!
Uzima wetu, watoto wangu, ni moja mwendo. Hapana njia juu ya Mukini Emau, lakini mwendo ku njia ya mbingu, ku Ufalme ya Mungu. Basi, pamoja na sisi anatembea na Kristu. Iko muzuri kusema na sisi, hii sauti walimwambia kwa Kristu wale wanafunji wake ile busiku ku Mukini Emau.

Ukae pamoja nasi! Bakia pamoja na sisi, ee Bwana! . Uzima yetu pamoja na Weye itakuwa na furaha, ee Bwana mupendwa wetu! . Amina.

( Mwalimu inapaswa kujua ya kama katikati ya hii mafundisho iko na beingine, wenye ataweza kufundisha kwa watoto wake kwa hii ma tarehe:

1. Katikati ya Mwezi ya Kumi na moja: Fundisho sa saba Yoane Murahimu.
Mwisho ya Mwezi Kumi na moja: Fundisho ya mnane Mtakatifu Ekaterini.

2. Katikati ya Mwezi Kumi na mbili: Fundisho ya Tisa na ya Kumi (Watakatifu Spiridon na Eleftherios)
3. Siku Kuu ya Kuzaliwa Kristu, Fundisho Kumi na moja.
4. Mwanzo ya Mwezi ya Kwanza: Fundisho Kumi na mbili.
5. Mwanzo ya Mwezi ya tatu: Fundisho Kumi na saba.
6. Mu Juma ya Mwana mupotevu: Fundisho Kumi na mnane.
7. Mu Juma ya Apokreo: Fundisho Kumi na Tisa.
8. Mu Juma ya Apokreo ya mbili. Fundisho Makumi mbili na moja.
9. Mwisho ya Mwezi ya tatu: Fundisho: Makumi mbili na mbili.
10. Mu Juma ya Musalaba ya Kristu. Fundisho Makumi mbili na tatu.
11. Mu Juma ya Ine ya wakati ya Kwarezima. Fundisho: Makumi mbili na Ine.
12. Mbele ya Ufufuo ya Kristu. Fundisho: Makumi mbili na sita.
13. Kisha Ufufuo ya Kristu: Fundisho Makumi mbili na saba.

Mafundisho juu ya kuogezeka imani ni hii: 2, 3, 6, 9, 11, 12, 17, 22, 24, 26, 27.

Mafundisho juu ya Ma Fumbo na ma Ibada ya Kanisa ni hii: 4, 5, 10, 18, 21, 23, 25.

Mafundisho juu ya kusaidia mufano ya watoto ku uzima yao ni hii: 1, 7, 8, 13, 14, 15, 16, 19, 20.

MONASTERI YA MUTAKATIFU GRIGORIE
KILIMA TAKATIFU
GREKIA
1998